

SURA YA 20

SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI

[SHERIA KUU]

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu

Jina

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina
2. Tafsiri.
3. Mipaka ya matumizi.
4. Taratibu ya kufuata kuendesha mashtaka.

SEHEMU YA PILI

UTARATIBU UNAOHUSIANA NA UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI

A. – Ukamataji, Utoro, Ukamataji tena, Hati ya Upekuzi na Ukamataji mali

(a) Masharti ya Utangulizi

5. Mtu akiwa kizuizini na katika mahabusu halali kisheria.
6. Matumizi ya Sehemu hii kwa maafisa polisi.
7. Wajibu wa kutoa taarifa za makosa ya jinai na vifo vya ghafla.
8. Uchunguzi wa vifo.
9. Taarifa zinazohusiana na kutendeka kwa kosa kutolewa kwa mdomo au kwa maandishi.
10. Upelelezi wa afisa polisi.

(b) Ukamataji na Hati ya Kukamata

11. Ukamataji unavyofanywa.
12. Kuzuia viziwi visivyo vya lazima.
13. Hati ya kukamata.
14. Ukamataji na afisa polisi bila hati.
15. Utaratibu endapo afisa polisi anakaimisha ukamataji bila hati
16. Ukamataji unaofanywa na watu binafsi bila hati.
17. Ukamataji unaofanywa na hakimumu.

18. Hakimu anaweza kumkamata mtu kwa kosa lolote linalotendeka mbele yake.
19. Haki ya kuingia sehemu yoyote kwa ajili ya kufanikisha ukamataji
 20. Uwezo wa kuvunja sehemu yoyote kwa ajili ya kukomboa.
 21. Utumiaji wa nguvu katika ukamataji.
 22. Baadhi ya ukamataji kutokuchukuliwa kuwa kinyume na sheria.
 23. Mtu kujulishwa sababau za kukamatwa.
 24. Upekuzi wa mtu aliyekamatwa.
 25. Uwezo wa polisi kuzuia na kukagua magari, n.k.
 26. Jinsi ya kupekuwa wanawake.
 27. Uwezo wa kutwaa silaha za hatari.
 28. Ukamataji wa wazururaji, majambazi wazoefu, n.k.
 29. Kukataa kutoa jina na makazi.
 30. Udhibiti wa watu waliokamatwa na afisa polisi.
 31. Udhibiti wa watu waliokamatwa na watu binafsi.
 32. Uzuiaji wa watu waliokamatwa.
 33. Polisi kutoa taarifa za ukamataji.

(c) Utoro na Ukamataji tena

34. Ukamataji tena wa watu waliotoroka.
35. Masharti ya vifungu vya 19 na 20 kutumika katika ukamataji chini ya kifungu cha 34.
36. Wajibu wa kumsaidia hakimu au afisa polisi katika kuzuia utorokaji wa mtu aliyekamatwa.
37. Fidia kwa maumivu, hasara au kifo kutokana na kumsaidia polisi, nk.

(d) Hati za upekuzi na ukamataji mali

38. Uwezo wa kutoa hati ya upekuzi au kuruhusu upekuzi
39. Vitu vinavyohusiana na kosa.
40. Utekelezaji wa hati ya upekuzi.
41. Upekuzi na ukamataji.
42. Upekuzi wakati wa dharura.
43. Wasimamizi na sehemu zilizofungwa kuruhusu kuingia na kutoka.
44. Kushikiliwa kwa mali iliyotwaliwa.
45. Vifungu vinavyotumika katika hati ya upekuzi.

B. – Uwezo na wajibu wa maafisa polisi wanapopeleleza makosa

(a) Masharti ya Utangulizi

46. Matakwa ya kutaja jina na anuani.
47. Polisi kuzuia kuvunjika kwa amani au kutendeka kwa makosa yanayoweza kusababisha kukamatwa

kukamatwa.

(b) Muda wa upelelezi chini ya ulinzi wa polisi

48. Mipaka katika kuhoji mtu, nk.
49. Wakati gani mtu asichukuliwe kuwa kuzuizini.
50. Muda unaotakiwa katika kumhoji mtu.
51. Pale ambapo upelelezi chini ya ulinzi hauwezi kukamilika ndani ya saa nne.

(c) Wajibu wakati wa kuwahoji watuhumiwa

52. Kuhoji watu waliotuhumiwa.
53. Watu walio kuzuizini kuelezwa haki zao.
54. Mawasiliano na mwanasheria, ndugu au rafiki.
55. Jinsi ya kuwatendea watu walio kuzuizini.
56. Wajibu maalum wakati wa kuhoji watoto.

(d) Kuweka kumbukumbu ya mahojiano

57. Kumbukumbu ya mahojiano.
58. Maelezo ya watuhumiwa.

(e) Matendo mengine ya upelelezi

59. Uwezo wa kuchukua alama za vidole, picha, nk, vya watuhumiwa
60. Gwaride la utambulisho.
61. Watu waliohukumiwa kutokana na kutambuliwa kimakosa kulipwa fidia
62. Waziri kutengeneza kanuni za gwaride la utambulisho, nk.
63. Uchunguzi wa kitabibu.

(f) Kuachiwa na Dhamana

64. Dhamana ya polisi kwa mtuhumiwa.
65. Vigezo vya kutoa dhamana ya polisi.
66. Masharti ya dhamana ya polisi.
67. Kukataa kutoa dhamana ya polisi.
68. Kutangua dhamana ya polisi.
69. Ukiukwaji wa masharti ya dhamana.

SEHEMU YA TATU
UZUIAJI WA MAKOSA

(a) Dhamana ya kutunza amani na tabia njema

70. Uwezo wa hakimu kumtaka mtu kutekeleza dhamana.
71. Dhamana ya tabia njema kutoka kwa watu wanaosambaza mambo ya uchochezi.
72. Dhamana ya tabia njema kutoka kwa watu waliotuhumiwa.
73. Dhamana ya tabia njema kutoka kwa wahalifu wazoefu.
74. Amri kutolewa.
75. Utaratibu kuhusu kuwepo mahakamani.
76. Utaratibu kuhusu kutokuwepo mahakamani.
77. Nakala ya amri kuambatanishwa na wito au hati.
78. Uwezo wa kutohitaji mahudhurio binafsi.
79. Uchunguzi wa ukweli wa taarifa.
80. Amri ya kuweka dhamana.
81. Kuachiwa kwa watu ambao taarifa imetolewa dhidi yao.

(b) Mwenendo baada ya Amri ya kuweka dhamana

82. Kuanza kwa muda ambao dhamana inahitajika.
83. Yaliyomo kwenye dhamana.
84. Uwezo wa kukataa wadhamini.
85. Utaratibu kutokana na kushindwa kuweka dhamana.
86. Uwezo wa kuwaachia watu waliofungwa kwa kushindwa kuweka dhamana.
87. Uwezo wa Mahakama Kuu kufuta dhamana.
88. Kuachiwa kwa wadhamini.

SEHEMU YA NNE
USIMAMIZI WA MWENENDO WA JINAI
A. – Mkurugenzi wa Mashtaka

89. [Imefutwa].
90. [Imefutwa].
91. Uwezo wa Mkurugenzi wa Mashtaka kuweka kufuta mashtaka
92. Ukaimishaji wa uwezo wa Mkurugenzi wa Mashtaka.
93. Taarifa za jinai za Mkurugenzi wa Mashtaka.
94. Makosa ya wageni yaliyotendeka ndani ya mipaka ya maji ya nchi kuendeshwa kwa ruhusa ya Mkurugenzi wa Mashtaka tu.

B. – Uteuzi wa Waendesha Mashtaka na Uendeshaji wa Mashtaka

95. [Imefutwa].
96. [Imefutwa].
97. Uwezo wa waendesha mashtaka.
98. Kuondolewa kwa mashitaka katika mahakama za chini.
99. Ruhusa ya kuendesha mashtaka na jina la mwenendo wa mashitaka kwa muhtasari.

SEHEMU YA TANO
UFUNGUAJI WA MASHTAKA

A. – Utaratibu wa kulazimisha mahudhurio ya watuhumiwa

(a) Wito

100. Muundo na yaliyomo kwenye wito.
101. Uwasilishaji wa wito.
102. Uwasilishaji pale mtu anayeitwa hawezi kupatikana.
103. Utaratibu pale uwasilishaji hauwezi kufanyika kwa mtu mwenyewe.
104. Uwasilishaji kwa mtumishi wa Serikali.
105. Uwasilishaji kwenye kampuni.
106. Mahudhurio kwa kampuni na kuandika kukana kosa wakati mwakilishi hajahudhuria.
107. Uwasilishaji nje ya mipaka ya mamlaka ya mahakama.
108. Uthibitisho wa uwasilishaji wakati afisa aliyepeleka hayupo.
109. Mahudhurio ya kampuni.

(b) Hati ya Ukamataji

110. Hati baada ya kutolewa wito.
111. Kutotii wito.
112. Muundo, yaliyomo na muda wa hati ya ukamataji.
113. Uwezo wa kuamuru kuwekwa kwa dhamana.
114. Hati ielekezwe kwa nani.
115. Hati inaweza kuelekezwa kwa mmiliki wa ardhi, n.k.
116. Utekelezaji wa hati inayoelekezwa kwa afisa polisi.
117. Taarifa ya kiini cha hati.
118. Mtu aliyekamatwa kupelekwa mbele ya mahakama bila kuchelewa.
119. Pale hati ya ukamataji inaweza kutekelezwa.
120. Upelekaji wa hati ya utekelezaji nje ya mipaka ya mamlaka ya mahakama.
121. Utaratibu ikiwa hati imeelekezwa kwa afisa polisi kwa utekelezaji nje ya mamlaka.
122. Utaratibu wa kukamata mtu nje ya mipaka ya mamlaka.
123. Makosa katika hati.

(c) Masharti mengine kuhusu mchakato

124. Uwezo wa kuchukua dhamana kwa ajili ya mahudhurio.
125. Ukamataji kwa kuvunja dhamana ya kuhudhuria.
126. Uwezo wa mahakama kuamuru mfungwa kuletwa mbele yake.
127. Masharti ya Sehemu hii yanayotumika kwa ujumla kwa wito na hati; na Uwezo wa mlinzi wa amani.

B. – Mashtaka

(a) Kutoa Lalamiko

- 128. Kuanzisha mashtaka.
- 129. Uwezo wa hakimu kukataa lalamiko au shtaka rasmi.
- 130. Kutolewa kwa wito au hati.

(b) Shtaka Rasmi

- 131. Watu walioshitakiwa kutahadharishwa
- 132. Makosa kuainishwa kwenye hati ya mashtaka na maelezo muhimu.
- 133. Uunganishaji wa makosa katika hati ya mashtaka au taarifa.
- 134. Uunganisha wa watuhumiwa wawili au zaidi kwenye hati ya mashtaka au taarifa.
- 135. Muundo ambao makosa yanatakiwa kuandikwa katika hati ya mashtaka.
- 136. Kesi ya watu wawili au zaidi walioshitakiwa.

(c) Kutiwa hatiani au kuachiwa kwa makosa ya zamani

- 137. Mtu aliyetiwa hatiani au kuachiwa kutoshtakiwa tena kwa kosa lilelile
- 138. Mtu anaweza kushitakiwa tena kwa makosa tofauti.
- 139. Madhara yanayozuka au ambayo hayakujulikana wakati wa kuendesha mashtaka yaliyopita.
- 140. Pale ambapo mahakama ya awali haikuwa na mamlaka ya kuendesha mashtaka yanayofuata
- 141. Jinsi ya kuthibitisha kutiwa hatiani kwa makosa ya zamani..

(d) Kulazimisha mahudhurio ya mashahidi

- 142. Wito kwa shahidi.
- 143. Hati kwa shahidi asiyetii wito.
- 144. Hati kwa shahidi katika hudhurio la kwanza.
- 145. Jinsi ya kushughulikia shahidi aliyekamatwa kwa mujibu wa hati.
- 146. Uwezo wa mahakama kuamuru mfungwa kuletwa kwa mahojiano.
- 147. Adhabu kwa kutokuhudhuria kwa shahidi.

(e) Masharti kuhusu dhamana, mdhamana na hati ya dhamana

- 148. Dhamana.
- 149. Uwezo wa Mahakama Kuu kubadilisha masharti ya dhamana yaliyotolewa na mahakama za chini.
- 150. Kubadilika kwa mazingira baada ya kutolewa dhamana.
- 151. Utekelezaji wa hati za dhamana.
- 152. Kutolewa chini ya ulinzi.
- 153. Amana badala ya hati ya dhamana.

154. Uwezo wa kuamuru dhamana inayojitosheleza baada ya ile kwanza kutojitosheleza.
155. Kuachiwa kwa wadhamini.
156. Kufa kwa mdhamini.
157. Watu waliofungwa na dhamana wakiiruka au kukiuka masharti ya dhamana wanaweza kukamatwa tena.
158. Watu wanaoruka au kukiuka masharti ya dhamana kutofikiriwa kupewa dhamana nyingine.
159. Adhabu kwa kukiuka masharti ya dhamana au kutohudhuria.
160. Kutaifishwa kwa mali iliyowekewa dhamana.
161. Rufaa na mapitio ya amri za mahakama.
162. Uwezo wa kutoza ushuru wa kiasi kinachodaiwa katika mali iliyowekewa dhamana.
163. Usuluhishi katika mazingira fulani.

SEHEMU YA SITA
USIKILIZAJI WA KESI

MASHARTI YA JUMLA KUHUSIANA NA USIKILIZAJI WA KESI

A. – Uwezo wa Mahakama

(a) Uwezo kwa Ujumla

164. Makosa chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu.
165. Makosa chini ya sheria nyingine tofauti na Sheria ya Kanuni za Adhabu.
166. Adhabu ambazo Mahakama Kuu inaweza kutoa.
167. Kuunganisha adhabu.
168. Adhabu katika hukumu ya makosa mawili au zaidi katika shtaka moja.
169. Kuachwa kwa ushahidi uliopatikana kinyume cha sheria.

(b) Mahakama za Chini

170. Adhabu ambazo mahakama za chini zinaweza kutoa.
171. Wakati ambao mahakama za chini zinaweza kupeleka shtaka Mahakama Kuu kwa kutoa adhabu..
172. Kuachiwa kwa dhamana kusubiri uthibitisho na uwezo wa mahakama inayothibitisha.

(c) Mamlaka ya Ziada ya Mahakama za Chini

173. Mamlaka ya ziada.
174. Usikilizaji wa kesi kufanywa kwa msaada wa wazee wa baraza.
175. [Imefutwa.]
176. Kumbukumbu na ripoti kupelekwa kwa Rais.

B. – Usikilizaji wa Kesi kwa Ujumla

(a) Sehemu ya Uchunguzi au usikilizaji wa kesi

177. Mamlaka ya jumla ya Mahakama za Tanzania.
178. Uwezo wa Mahakama Kuu kuchunguza na kusikiliza kesi.
179. Mahali na tarehe za vikao vya Mahakama Kuu.
180. Sehemu ya kawaida ya uchunguzi na usikilizaji wa kesi.
181. Usikilizaji wa kesi mahali kosa au mahali matokeo ya kosa yalipojitokeza.
182. Usikilizaji wa kesi pale kosa linahusiana na kosa jingine.
183. Usikilizaji wa kesi pale mahali kosa lilipotendeka hapajulikani.
184. Kosa lililotendeka safarini.
185. Mahakama Kuu inaweza kuamua mahakama inayofaa kukiwa na mashaka.
186. Mahakama kuwa mahakama ya wazi.
187. Kuzuiwa kwa watoto kuhudhuria usikilizaji wa kesi mahakamani.
188. Mahakama inaweza kuzuia kutangazwa kwa majina, nk., ya wahusika au mashahidi.

(b) Kuhamishwa kwa Kesi

189. Kuhamishwa kwa kesi pale kosa limetendeka nje ya mamlaka.
190. Kuhamishwa kwa kesi kati ya mahakimu.
191. Uwezo wa Mahakama Kuu kubadili sehemu.

(c) Usikilizaji kesi mchapuko na namna ya uendeshaji wa Kesi

192. Usikilizaji wa awali katika kuamua mambo yasiyobishaniwa.
193. Mtuhumiwa wa makosa ya kibali anaweza kukiri kosa bila kufika mahakamani.
194. Utaratibu pale mtuhumiwa anataka kukiri kosa lisilo la kibali au anatarajia kutoa utetezi wa *alibi*.

C. – Kuhojiwa kwa Mashahidi

(a) Masharti ya jumla

195. Uwezo wa kuita shahidi muhimu au kumhoji mtu aliyepo.
196. Ushahidi kuchukuliwa mbele ya mtuhumiwa.
197. Ushahidi unaweza kuchukuliwa bila kuwepo mtuhumiwa katika mazingira fulani.
198. Ushahidi kutolewa kwa kiapo.
199. Shaidi kigeugeu.
200. Utaratibu pale mtuhumiwa ni shahidi pekee aliyeitwa katika utetezi.
201. Haki ya kujibu.

- 202. Hati kuhusiana na utayarishaji wa alama za picha, nk., zinazopokelewa katika ushahidi.
- 203. Taarifa ya Mchambuzi wa Serikali.
- 204. Taarifa ya mtaalamu wa alama za vidole.
- 205. Taarifa ya mtaalamu wa maandishi.

(b) Kutolewa kwa Idhini ya Kuwahoji Mashahidi

- 206. Kutolewa kwa idhini.
- 207. Wahusika wa kesi wanaweza kuwahoji mashahidi.
- 208. Kurudishwa kwa idhini.
- 209. Kuahirishwa kwa kesi.

(c) Kuchukua na Kuweka Kumbukumbu ya Ushahidi

- 210. Jinsi ya kuweka kumbukumbu ya ushahidi mbele ya hakimu.
- 211. Tafsiri ya ushahidi kwa mtuhumiwa au wakili wake.
- 212. Maoni kuhusiana na mwonekano wa shahidi.
- 213. Utaratibu kwa makosa madogo.
- 214. Kutiwa hatiani au upelekaji wa kesi ikiwa imesikilizwa kwa sehemu na hakimu mmoja na sehemu nyingine na hakimu mwingine.
- 215. Jinsi ya kuweka kumbukumbu ya ushahidi Mahakama Kuu.

D. – Utaratibu kuhusu Mtuhumiwa mwenye Ulemavu wa Akili au Udhaifu

- 216. Mwendesha mashtaka kutoa au kuleta ushahidi kabla mahakama haijafanya uchunguzi kuhusiana na ulemavu wa akili wa mtuhumiwa.
- 217. Utaratibu wakati mtuhumiwa amethibika kuwa na uwezo wa kujitetea.
- 218. Kurudiwa kwa usikilizaji wa kesi au uchunguzi.
- 219. Utetezi wa ulemavu wa akili katika usikilizaji wa kesi.
- 220. Uwezo wa mahakama katika kuchunguza ulemavu wa akili.
- 221. Utaratibu wakati mtuhumiwa haelewi mwenendo wa kesi.

SEHEMU YA SABA

UTARATIBU WA KUENDESHA KESI MBELE YA MAHAKAMA ZA CHINI

(a) Masharti yanayohusiana na Usikilizwaji na Uamuzi wa Kesi

- 222. Kutokuhudhuria kwa mlalamikaji siku ya kusikiliza kesi.
- 223. Kuhudhuria kwa pande zote.
- 224. Kuondolewa kwa lalamiko.
- 224A. Kukoma kwa shauri katika mahakama za chini.
- 225. Kuahirishwa na kuwekwa ndani kwa mtuhumiwa.
- 226. Kutokuhudhuria kwa pande zote baada ya kuahirisha.

227. Mtuhumiwa anaweza kutiwa hatiani na kuhukumiwa adhabu hata kama hayupo.
228. Mtuhumiwa kuitwa kujibu mashitaka.
229. Utaratibu iwapo shitaka linakanwa.
230. Kuachiwa kwa mtuhumiwa kama hakuna kesi ya kujibu.
231. Utetezi.
232. Ushahidi katika majibu
233. Utaratibu wa hotuba.
234. Kutofautiana kwa mashitaka na ushahidi na kusahihishwa kwa mashitaka.
235. Uamuzi
236. Ushahidi unaohusiana na adhabu au amri muafaka.
237. Kuzingatia makosa mengine.
238. Kuandaa amri za kutiwa hatiani au kuachiwa.
239. Amri ya kuondolewa mashitaka mengine.
240. Maelezo ya mashahidi wa kitabibu.

(b) Ukomo na misamaha kuhusiana na uendeshaji wa kesi katika mahakama za chini

241. Ukomo wa muda kwa mashitaka ya muhtasari katika mazingira fulani.
242. Utaratibu kwa kosa ambalo halifai kuendeshwa kwa muhtasari.

(c) Kupeleka Watuhumiwa Kwa Ajili ya Mashtaka Mahakama za Chini kwenda Masharti Mahakama kuu kwa usikilizaji

a) Masharti yanayohusiana na kupelekwa Watuhumiwa kwa ajili ya Mashtaka Mahakama Kuu

243. Uwezo wa kupeleka shaurii
244. Mahakama kuendesha mashauri yaliyoletwa
245. Utaratibu wa kukamata
246. Kupelekwa kwa ajili ya kusilikizwa na mahakama.
247. Mashahidi wa upande wa mashitaka na upande wa utetezi.
248. Kuahirishwa kwa shauri.
249. Mtuhumiwa ana haki ya kupewa mwenendo wa kesi.
250. Mahakama inaweza kumlazimisha shahidi kuhudhuria kwenye shauri
251. Kukataa kulazimishwa.

(b) Kutunzwa kwa ushahidi katika mazingira fulani

252. Kuchukua ushahidi wa watu wanaoumwa sana na wasioweza kuhudhuria shauri.
253. Taarifa kutolewa
254. Nafasi ya kuhoji ushahidi na kuhamisha maelezo.
255. Matumizi ya maelezo katika ushahidi.

(c) Mwenendo baada ya Kuhamishwa kwa ajili ya kusikilizwai.

- 256. Kuhamisha kumbukumbu kwenda Mahakama Kuu.
- 256A. Kusikilizwa na hakimu mkazi mwenye mamlaka ya ziada.
- 257. Taarifa ya shauri.
- 258. Nakala ya habari na taarifa ya kusikilizwa kuwasilishwa.
- 259. Kurudishwa kwa uwasilishaji.
- 260. Kuahirishwa kwa shauri.
- 261. Taarifa isainiwe na Mkurugenzi wa Mashitaka.
- 262. Muundo wa taarifa.
- 263. Mashahidi kuitwa.

SEHEMU YA NANE
UTARATIBU WA KUSIKILIZA MBELE YA MAHAKAMA KUU

(a) Utendaji na jinsi ya Kusikiliza

- 264. Utendaji wa Mahakama Kuu katika mamlaka yake ya jinai.
- 265. Usikilizaji mbele ya Mahakama Kuu lazima uwe na msaada wa wazee wa baraza.

(b) Wazee wa Baraza

- 266. Wajibu wa kutumikia kama Mzee wa Baraza.
- 267. Misamaha.
- 268. Hakuna msamaha wa kijinsia au kindoa katika wajibu wa kutumikia kama Mzee wa baraza.

(c) Mahudhurio ya Wazee wa Baraza

- 269. Kuwaita Wazee wa Baraza.
- 270. Muundo wa wito.
- 271. Pingamizi kuitwa kutumikia kama Mzee wa Baraza.
- 272. Udhuru wa kutofika.
- 273. Orodha ya Wazee wa Baraza wanaohudhuria.
- 274. Adhabu kwa kutohudhuria kwa wazee wa Baraza.

(d) Tuhuma

- 275. Kujibu taarifa.
- 276. Amri za kurekebisha taarifa, usikilizaji tofauti na uahirishaji wa usikilizaji.
- 277. Kutupiliwa mbali kwa taarifa.
- 278. Utaratibu ikiwa mtuhumiwa alitiwa hatiani zamani.
- 279. Jibu la 'kukana shitaka'.
- 280. Jibu la 'autrefois acquit' na 'autrefois convict'.
- 281. Kukataa kujibu.

- 282. Jibu la 'kukubali kosa'.
- 283. Mwenendo baada ya kukana shitaka.
- 284. Uwezo wa kuahirisha mwenendo wa kesi.
- 284A. Kukoma kwa shitaka mbele ya Mahakama Kuu.

(e) Uteuzi wa Wazee wa Baraza

- 285. Uteuzi wa Wazee wa Baraza.
- 286. Kutokuwepo kwa Wazee wa Baraza.
- 287. Wazee wa Baraza kuhudhuria baada ya kesi kuahirishwa.

(f) Kesi ya Upande wa Mashitaka

- 288. Kufungua kesi ya upande wa mashitaka.
- 289. Mashahidi wa nyongeza kwa upande wa mashitaka.
- 290. Kuhojiwa mashahidi wa upande wa mashitaka.
- 291. Maelezo ya mashahidi wa kitabibu.
- 292. Maelezo ya ushahidi ya mtuhumiwa.
- 293. Kufunga kesi ya upande wa mashitaka.

(g) Kesi ya Upande wa Utetezi

- 294. Kesi ya upande wa utetezi.
- 295. Mashahidi wa nyongeza wa upande wa utetezi.
- 296. Majibu ya upande wa mashitaka.
- 297. Pale ambapo mtuhumiwa hatoi ushahidi.

(h) Kufungwa kwa Usikilizaji kesi

- 298. Wazee wa Baraza kutoa maoni yao na kutolewa kwa hukumu.
- 299. Kutiwa hatiani kama kesi ilisikilizwa na majaji wawili kwa nyakati tofauti.

SEHEMU YA TISA
KUTIWA HATIANI, HUKUMU, VIFUNGO NA UTEKELEZAJI WAKE KATIKA
MAHAKAMA ZA CHINI NA MAHAKAMA KUU

A. – Masharti mbalimbali yanayohusiana na Kutiwa Hatiani

- 300. Kama kosa lililothibitishwa limejumuishwa katika mashitaka
- 301. Mtu aliyeshitakiwa kwa kosa anaweza kutiwa hatiani kwa kujaribu kufanya kosa hilo.
- 302. Hukumu mbadala katika mashitaka mbalimbali yanayohusu mauaji ya watoto.
- 303. Hukumu mbadala katika Sheria ya Usalama Barabarani katika baadhi ya makosa ya kuua bila kukusudia.

- 304. Hukumu mbadala katika mashitaka ya ubakaji na makosa yanayofana nayo.
- 305. Mtu aliyeshitakiwa kwa uvunjaji nyumba usiku, nk, anaweza kutiwa hatiani kwa makosa yanayofanana nayo.
- 306. Hukumu mbadala kwa mashitaka ya wizi na makosa yanayofanana nayo.
- 307. Hukumu mbada katika mashitaka ya kukutwa na mali zinazodhaniwa kuwa zimepatikana kwa nia ya rushwa.
- 308. Tafsiri ya vifungu vya 300 mpaka 307.
- 309. Mtu aliyeshitakiwa kwa kosa la kibali asiachiwe kama kosa lisilo la kibali limethibitishwa.
- 310. Haki ya mtuhumiwa kutetewa.

B. – Hukumu kwa Ujumla

- 311. Jinsi ya kutoa hukumu.
- 312. Yaliyomo kwenye hukumu.
- 313. Nakala ya hukumu, n.k, kutolewa kwa mtuhumiwa au mtu mwingine mwenye maslahi ikiwa ataomba.

C. – Hukumu

(a) Kutoa Hukumu Mahakama Kuu

- 314. Kumwita mtuhumiwa.
- 315. Mwenendo katika kukamatwa kwa hukumu.
- 316. Hukumu.
- 317. Uwezo wa kuweka akiba uamuzi wa maswali yaliyojitokeza katika usikilizaji wa kesi.
- 318. Uwezo wa ya kuweka akiba maswali yaliyojitokeza katika usikilizaji wa kesi.
- 319. Pingamizi zilizowekwa kuponywa na hukumu.
- 320. Ushahidi wa kufikia hukumu sahihi.
- 321. Kutilia maanani makosa mengineyo.

(b) Hukumu ya Kifo

- 322. Hukumu ya kifo.
- 323. Mtuhumiwa kuambiwa haki ya kukata rufaa.
- 324. Mamlaka ya kumweka mtu kizuizini.
- 325. Taarifa na kumbukumbu kupelekwa kwa Rais.

(c) Hukumu nyingine

- 326. Kuachiwa kwa masharti.

(d) Kutekelezwa kwa Hukumu

- 327. Kibali kama ni hukumu ya kifungo.
- 328. Kibali kwa kulipa faini.
- 329. Pingamizi katika kukamata mali.
- 330. Kusimamishwa kwa utekelezaji wa hukumu ya kifungo kwa kushindwa kulipa faini.
- 331. Kushikiliwa endapo mtuhumiwa hana mali za kukamata ili kulipa faini.
- 332. Kushikiliwa kama mbadala wa kuuza mali za mtuhumiwa.
- 333. Malipo yote baada ya kushikiliwa.
- 334. Malipo kidogo baada ya kushikiliwa.
- 335. Nani anaweza kutoa kibali.
- 336. Mwisho wa kifungo baada ya kushikiliwa.

D. – Masharti mbalimbali katika kuwashughulikia wakosaji

(a) Wakosaji wa kwanza

- 337. Uwezo wa kumuachia kwa matazamio badala ya kuhukumu kwa adhabu.
- 338. Masharti kama mkosaji atashindwa kufuata masharti ya dhamana.
- 339. Masharti kuhusu makazi ya mkosaji.
- 339A. Kumuachia mkosaji kwa masharti ya kuitumikia jamii.
- 340. Vifungu vya 337, 338 na 339 kutotumika katika mazingira fulani.

(b) Mkosaji aliyewahi kutiwa hatiani

- 341. Uwezo wa kuamuru kuwa chini ya uangalizi wa polisi.
- 342. Matakwa kutoka kwa mtu aliyewekwa chini ya uangalizi wa polisi.
- 343. Kushindwa kukidhi matakwa chini ya kifungu 342.

(c) Dosari katika Amri au Kibali

- 344. Makosa na vitu vilivyorukwa kwenye amri na vibali.

E. – Uwezo mbalimbali wa Mahakama kuamuru Fidia, gharama, kutaifisha, n.k.

(a) Gharama na Fidia

- 345. Gharama dhidi ya mtuhumiwa.
- 346. Amri ya kulipa gharama inaweza kukatiwa rufaa.
- 347. Fidia katika mashitaka yasiyo na msingi au ya kuudhi.
- 348. Uwezo wakuamuru mtuhumiwa alipe fidia.
- 348A. Fidia katika kesi za kujamiiana.
- 349. Gharama na fidia zionyeshwe kwenye amri na jinsi ya kuzipata.
- 350. Uwezo wa mahakama kutoa gharama au fidia ndani ya faini.

(b) Kutaifisha

- 351. Uwezo wa kutaifisha mali.
- 352. Kibali cha upekuzi kwa mali iliyotaifishwa.

(c) Udhibiti wa vielelezo

- 353. Udhibiti wa vielelezo.
- 354. Udhibiti wa wa machapisho yanayodhalilisha au kashfa au vyakula vyenye madhara au visivyofaa, nk..
- 355. Mtu aliyenyang'anywa mali anaweza kurudishiwa.
- 356. Afisa wa umma anayehusiana na uuzwaji wa mali hatakiwi kununua au kuonesha nia ya kununua mali hiyo.

F. – Kukomboa Mali

- 357. Mali iliyokutwa kwa mtuhumiwa.
- 358. Mali iliyoibwa.

SEHEMU YA KUMI
RUFAA

(a) Rufaa kwa Ujumla

- 359. Rufaa kwenda Mahakama Kuu.
- 360. Hakuna rufaa katika jibu la kukubali kosa.
- 361. Kikomo
- 362. Ombi la Rufaa.
- 363. Muomba rufaa aliye gerezani.
- 364. Kukataliwa kwa rufaa kwa muhtasari.
- 365. Taarifa ya muda na mahali pa kusikiliza.
- 366. Uwezo wa Mahakama Kuu katika rufaa na haki ya mkata rufaa kuhudhuria.
- 367. Amri ya Mahakama Kuu ithibitishwe kwenda mahakama za chini.
- 368. Kusimamishwa kwa hukumu na kupatiwa dhamana kusubiri rufaa.
- 369. Ushahidi wa ziada.
- 370. Idadi ya majaji katika rufaa ya mkata rufaa.
- 371. Kuondolewa kwa rufaa.
- 371A. Kukoma kwa rufaa baada ya mkata rufaa kufariki.

(b) Mapitio

- 372. Uwezo wa Mahakama Kuu kuita kumbukumbu.
- 373. Uwezo wa Mahakama Kuu katika mapitio.
- 374. Uamuzi wa Mahakama kuwasikiliza wahusika wa kesi.
- 375. Idadi ya majaji katika mapitio.

376. Amri ya Mahakama Kuu ithibitishwe kwenda mahakama ya chini.

(c) Rufaa ya Mkurugenzi wa Mashitaka

- 377. Tafsiri.
- 378. Rufaa za Mkurugenzi wa Mashitaka.
- 379. Kikomo
- 380. Ombi la rufaa.
- 381. Taarifa ya muda na mahali pa kusikiliza kesi.
- 382. Mkurugenzi wa Mashitaka anaweza kutoa hoja mbele ya mahakama.
- 383. Kutofika kwa wahusika.
- 384. Ushahidi wa zaida.
- 385. Idadi ya majaji katika rufaa ya Mkurugenzi wa Mashitaka.
- 386. Kuondolewa kwa rufaa na Mkurugenzi wa Mashitaka.
- 386A. Kukoma kwa rufaa mjibu rufaa akifariki.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
MASHARTI YA ZIADA

(a) Mwenendo wenye Makosa

- 387. Mwenendo kwenye sehemu isiyo sahihi.
- 388. Maamuzi au hukumu, wakati gani yaweza kubadilishwa kwa sababu ya makosa au kuruka vitu kwenye mashitaka au mwenenendo.
- 389. Kukamata vitu sio kinyume na sheria wala mkamati wa vitu sio mvamizi kutokana na makosa katika mwenendo.

(b) Maelekezo katika asili ya amri ya Habeas Corpus na Writ

- 390. Uwezo wa kutoa maelekezo yenye asili ya *Habeas corpus*.
- 391. Uwezo wa Mahakama Kuu kutoa *Writ*s.

(c) Mengineyo

- 392. Watu ambao viapo vinaweza kuapwa mbele yao.
- 393. Nakala ya mwenendo wa kesi.
- 394. Fomu.
- 395. Gharama ya wazee wa baraza, mashahidi, n.k.
- 396. [Imefutwa.]

MAJEDWALI

SURA YA 20

SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI

Sheria inayotoa utaratibu wa kufuatwa katika upelelezi wa makosa ya jinai na usikilizaji wa kesi za jinai na kwa madhumuni mengine yanayo fanana na haya.

[Novemba 1, 1985]
[T.S. Na. 375 la 1985]

Sheria Na.
9 na 12 ya 1987
5 na 13 ya 1988
10 ya 1989
4 na 27 ya 1991
19 ya 1992
5 ya 1993
32 ya 1994
2, 9 na 17 ya 1996
4 na 12 ya 1998
5, 9 na 21 ya 2002
4 ya 2004
5 ya 2005
2 ya 2007
27 ya 2008

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina Kifupi

1. Sheria hii itaitwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Tafsiri

2. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maana itahitaji vinginevyo:–
"mtu mzima" maana yake ni mtu mwenye umri wa au zaidi ya miaka kumi na sita;
"kosa la kukamatwa" maana yake ni kosa ambalo afisa wa polisi anaweza, kwa kufuata Jedwali la Kwanza la Sheria hii au sheria nyingine yoyote inayotumika kwa muda huu, kukamata bila hati;
"mtoto" maana yake ni mtu ambaye hajatimiza umri wa miaka kumi na sita;
"mwenendo wa upelekaji wa kesi" maana yake ni mwenendo wa kesi unaosikilizwa na mahakama za chini kwa nia ya kumpeleka

mtuhumiwa Mahakama Kuu;

"mlalamikaji" katika mashtaka ya binafsi, maana yake mwendesha mashtaka binafsi au mtu anayelalamika mbele ya mahakama na, katika mashitaka yote ya umma, maana yake mtu anayewasilisha kesi kwa niaba ya Jamhuri mbele ya mahakama;

"lalamiko" maana yake ni shutuma kuwa mtu fulani anayejulikana au asiyejulikana, ametenda kosa;

"Kijana mdogo" maana yake ni mtu aliye chini ya umri wa miaka kumi na sita;

"Waziri" maana yake ni Waziri ambaye kwa wakati huo anahusika na mambo ya sheria;

"kosa lisilo la kibali" maana yake ni kosa ambalo afisa polisi anaweza kukamata bila hati;

"mkuu wa kituo cha polisi" inajumuisha afisa yeyote mwenye cheo kikubwa kuliko mkuu wa kituo cha polisi na vilevile inajumuisha, wakati mkuu wa kituo cha polisi hayupo katika kituo au hawezi kutokana na ugonjwa au sababu nyingine kufanya kazi zake, afisa polisi aliyepo kituoni ambaye anafuatia kwa cheo kutoka afisa huyo na ambaye ana cheo zaidi ya konstabo au, wakati Waziri ambaye kwa wakati huu, anayehusika na mambo ya ndani ataelekeza, afisa yoyote wa polisi aliyepo;

"afisa polisi" inajumuisha afisa yeyote wa jeshi la polisi na, afisa yeyote wa jeshi la mgambo anapotekeleza kazi za kipolisi kwa mujibu wa sheria zinazotumika wakati huu;

"mwendesha mashtaka" maana yake ni mtu yoyote aliyeteuliwa chini ya kifungu 22(1) cha Sheria ya Huduma za Mashtaka ya Taifa, 2008 na inajumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mwanasheria Mkuu, Mwandishi wa Sheria, Wakili wa Serikali, na mtu mwingine yeyote anayeendesha kesi za jinai kwa maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka;

"mahakama za chini" maana yake ni mahakama yoyote, isipokuwa mahakama ya kijeshi, ambayo iko chini ya Mahakama Kuu;

"Usikilizaji wa kesi kwa muhtasari" maana yake ni usikilizaji wa kesi unaofanywa na mahakama za chini, chini ya Sehemu ya VII ya Sheria hii;

"Halmashauri ya Kijiji" maana yake ni Halmashauri ya Kijiji iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 22 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya);

"kosa la kibali" maana yake ni kosa ambalo afisa polisi hawezi kukamata bila ya kuwa na hati.

Sheria Na..27
ya 2008,
kif..31

Sura ya 287

Mipaka ya Matumizi
ya Sheria Na. 5 ya
1988

3.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), hakuna kitu katika Sheria hii kitatumika na mahakama yoyote ya mwanzo au

kif. 2
Sura ya 11

hakimu wa mahakama ya mwanzo au Mahakama Kuu, mahakama ya wilaya au hakimu mkazi katika kutekeleza mamlaka yao ya rufaa, mapitio, usimamizi au mamlaka nyingine na uwezo wao chini ya Sehemu ya III ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1)–

(a) Rejeo kwa mahakama chini ya vifungu 27, 29, 30, 32 na 141 na marejeo kwa mahakama za chini katika kifungu cha 242 itajumuisha rejeo kwa mahakama ya mwanzo;

(b) Rejeo kwa hakimu chini ya kifungu 36 na vifungu vya 70 mpaka 88 itajumuisha rejeo kwa hakimu wa mahakama ya mwanzo;

(c) Mkurugenzi wa Mashtaka na mtu yeyote aliyeruhusiwa naye anaweza kutekeleza mamlaka yoyote aliyopewa na kifungu cha 90 na 91 kuhusiana na mwenendo wa kesi katika mahakama ya mwanzo na mwenendo wa kesi katika Mahakama Kuu au mahakama ya wilaya chini ya Sehemu ya III ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu; lakini hakuna kitu chini ya aya hii kitatafsiriwa kuwa kinakiuka masharti ya kifungu cha 29 cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu;

Sura ya 11

Sura ya 11

(d) Vifungu vya 137, 138, 139, 140 na 141 vitatumika kwa, na Mahakama Kuu inaweza kutekeleza mamlaka chini ya vifungu 148(3), 149, 348 na 349 kuhusiana na mahakama za mwanzo.

(3) Katika kifungu hiki maneno “mahakama ya mwanzo”, “mahakama ya wilaya” na “mahakama ya hakimu mkazi” yana maana kama yalivyopewa na Sheria ya Mahakama za Mahakimu.

Sura ya 11

Taratibu ya kufuata
kuendesha mashtaka
Sura ya 16

4.-(1) Makosa yote chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu yatachunguzwa, kusikilizwa na kushughulikiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Makosa yote chini ya sheria nyingine yoyote yatachunguzwa, yatasikilizwa au kushughulikiwa vinginevyo kwa kufuata masharti ya Sheria hii, isipokuwa pale sheria hiyo nyingine inatoa vinginevyo utaratibu wa jinsi au mahali pa upelelezi, usikilizwaji au kushughulikiwa kwa jinsi nyingine kwa makosa hayo.

SEHEMU YA PILI

UTARATIBU UNAOHUSIANA NA UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI

A. – Ukamataji, Utoro na Ukamataji tena, Hati ya Upekuzi na Ukamataji Mali

(a) Masharti ya Awali

Mtu akiwa kizuizini

5.-(1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, mtu atachukuliwa kuwa

na katika mahabusu halali kisheria

kizuizini kama anaambatana na afisa polisi kwa lengo linalohusiana na upelelezi wa kosa na afisa polisi hatamruhusu kumruhusu mtu huyo iwapo akitaka kufanya hivyo, bila kujali kuwa afisa polisi ana sababu za msingi za kuamini kuwa mtu huyo ametenda kosa, na bila kujali kama mtu huyo yuko kwenye mahabusu halali kisheria kwa kosa hilo.

(2) Kwa madhumuni ya Sheria hii, mtu atakuwa kwenye mahabusu halali kisheria iwapo atakuwa kizuizini:-

(a) kutokana na kukamatwa kihalali; au

(b) kutokana na kosa, na afisa polisi:-

(i) anaamini kwa sababu za msingi kwamba mtu huyo ametenda kosa; na

(ii) ataruhusiwa chini ya kifungu cha 14 kumkamata mtu huyo kwa kosa hilo.

(3) Mtu hatakuwa kizuizini kama anaambatana na afisa polisi pembeni mwa barabara bila kujali kama yuko kwenye gari au la, kwa madhumuni yanayohusiana na upelelezi wa kosa, lisilo kubwa, linalotokana na matumizi ya gari.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, mtu atachukuliwa kuwa ameambatana na afisa polisi kwa madhumuni yanayohusiana na upelelezi wa kosa iwapo atakuwa anasubiri mahali kwa ombi la polisi kwa dhumuni hilo.

Matumizi ya sehemu hii kwa maafisa wa polisi.

6.-(1) Kila afisa polisi anatakiwa, katika kutekeleza uwezo aliyopewa na katika kutekeleza wajibu aliopewa kama afisa polisi, kutekeleza masharti ya Sehemu hii.

(2) Pale ambapo afisa polisi anavunja au anashindwa kufuata masharti ya Sehemu hii ambayo yanatumika kwake, kuvunja au kushindwa huko hakutaadhibiwa kama kosa chini ya Sheria hii, vinginevyo adhabu iwe imetolewa waziwazi kuhusiana na kuvunja au kushindwa huko.

(3) Hakuna kitu kwenye kifungu hiki kitatafsiriwa kama ni kuvunja au kushindwa kufuata, masharti ya Sehemu hii na afisa polisi-

(a) ambacho, chini ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Jeshi Saidizi, kitu hicho kinahesabika kuwa ni utovu wa nidhamu kwa afisa polisi ambapo anaweza kushughulikiwa chini ya Sheria hiyo;

(b) ambacho kinachukulika kuwa ni sababu za kuzuilika kwa ushahidi chini ya kifungu cha 169; au

(c) kinakuwa sababu za kufungua shauri la madai.

Sura 322

Wajibu wa kutoa taarifa za makosa ya jinai na vifo vya ghafla.

7.-(1) Mtu yoyote anayejua au atakayejua:-

(a) kutendeka au kusudio la mtu yoyote kutenda kosa linaloadhibiwa chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu; au

(b) tukio lolote la kifo cha ghafla au kisicho cha asili au kifo kitokanacho na ukatili au kifo chochote kilicho katika mazingira yenye kutia shaka au mwili wa mtu yeyote

aliyekutwa amekufa bila kujua jinsi mtu huyo alivyokufa, atatakiwa wakati huohuo kutoa taarifa kwa afisa polisi au kwa mtu mwenye madaraka katika sehemu hiyo ambaye atawasilisha taarifa hiyo kwa afisa polisi msimamizi wa kituo cha polisi kilicho karibu.

(2) Hakuna shauri la jinai au madai litakalosikilizwa na mahakama yoyote dhidi ya mtu yeyote kwa ajili ya kudai fidia inayotokana na taarifa iliyotolewa na mtu huyo kwa kufuata kifungu kidogo cha (1).

(3) Pale mtu anapokufa akiwa mahabusu ya polisi au katika hospitali ya magonjwa ya akili, ukoma, makazi ya walemavu, au gerezani, afisa ambaye alikuwa amemweka mtu huyo kizuizini au aliyekuwa msimamizi wa sehemu hiyo atatakiwa wakati huohuo atoe taarifa inayohusiana na kifo kwa korona wa mahakama mwenye mamlaka ya eneo amabapo mwili umekutwa na korona huyo au mtu aliyeruhusiwa naye atatakiwa kuutazama mwili na kufanya uchunguzi kuhusiana na chanzo cha kifo, kwa kuzingatia sheria yoyote itakayokuwa inatumika kwa wakati huo inayoshughulikia uchunguzi huo.

Uchunguzi wa vifo
Sura 24

8. Uchunguzi wote kuhusiana na vifo vya ghafla au vifo vingine inavyoripotiwa chini ya kifungu cha 7 utafanywa na watu walioruhusiwa chini ya, na katika namna kama ilivyoonyeshwa na Sheria ya ya Uchunguzi wa Vifo.

Taarifa zinazohusiana
na kutendeka kwa
kosa kutolewa kwa
mdomo au kwa
maandishi
Sheria Na. 9 ya 2002
jedwali.

9.-(1) Taarifa zinazohusiana na kutendeka kwa kosa inaweza kutolewa kwa mdomo au kwa maandishi kwa afisa polisi au kwa mtu mwingine yeyote mwenye mamlaka katika eneo husika.

(2) Taarifa yoyote chini ya kifungu kidogo (1) itatakiwa kuwekwa kumbukumbu kwa namna iliyoonyeshwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 10.

(3) Pale katika kufuatilia taarifa iliyotolewa chini ya kifungu hiki shauri limefunguliwa kwenye mahakama za mahakimu, hakimu atatakiwa, kama mtu anayetoa taarifa ametajwa kuwa shahidi, kuhakikisha nakala ya taarifa na maelezo mengine aliyoyatoa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 10, kupelekwa kwa mtuhumiwa mara moja.

(4) Taarifa yoyote iliyotolewa chini ya kifungu hiki na mtu yeyote inaweza kutumika kama ushahidi kwa kufuata masharti ya sheria iliyopo wakati huo inayohusiana na utaratibu wa utoaji na upokelewaji wa ushahidi kuhusiana na shauri linalotokana na kosa husika.

Upelelezi wa afisa
polisi
Sheria Na. 9 ya 2002
jedwali.

10.-(1) Iwapo kutokana na taarifa zilizopokelewa au kwa njia nyingine yoyote afisa polisi ana sababu za kushuku utendekaji wa kosa au kuhisi uvunjwaji wa amani atatakiwa, pale inapobidi, kwenda yeye mwenyewe katika sehemu hiyo kupeleleza ukweli na mazingira ya kesi

na kuchukua hatua zitakazokuwa zinafaa kutambua na kukamata kwa mhalifu pale kosa ni lile ambalo anaweza kukamata bila hati.

(2) Afisa polisi yeyote baada ya kufanya upelelezi anaweza kwa amri ya maandishi kumtaka kufika mbele yake mtu yoyote anayeishi ndani ya mipaka ya kituo cha polisi cha afisa polisi huyo au kituo chochote cha karibu, ambaye, kutokana na taarifa zilizotolewa au katika njia nyingine inaonekana anajua mazingira ya kesi, au mtu ambaye anamiliki waraka au kitu kingine kinachohusiana na upelelezi wa kesi, kuhudhuria au kuleta waraka huo au kitu kingine, na mtu huyo atalazimika kuhudhuria na kuleta nakala iliyothibitishwa ya waraka huo au kitu kingine kama ilivyotakiwa:

Isipokuwa kwamba pale afisa polisi amepokea nakala iliyothibitishwa ya waraka au kitu kingine atalazimika kutoa risiti kwa mtu ambaye kwayo anapokea waraka huo au hicho kitu kingine.

(2A) Mtu yeyote aliyeitwa kuhudhuria au kuleta waraka au kitu kingine kinachohusiana na upelelezi wa kesi chini ya kifungu kidogo cha (2), ambaye anakataa au kwa makusudi anazembea kufanya hivyo au ambaye ni shahidi kwenye upelelezi husika anakataa kujibu swali lolote analoulizwa au kutoa waraka wowote au kitu chochote kingine kinachohusiana na upelelezi atakuwa anatenda kosa na atawajibika kama akitiwa hatiani kulipa faini isiyoziidi shilingi laki tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu au vyote.

(3) Afisa polisi yeyote anayefanya upelelezi anaweza, kwa kuzingatia masharti mengine ya Sehemu hii, kumhoji kwa mdomo mtu yeyote anayeaminika kujua ukweli na mazingira ya kesi na atayaweka kwenye maandishi maelezo yote yatakayotolewa na mtu huyo anayehojiwa. Maelezo yote, ikijumuiisha swali lolote la ufafanuzi lililoulizwa na afisa polisi na jibu lake, yatarekodiwa kwa ukamilifu kwa Kiswahili au Kiingereza au katika lugha nyingine yoyote ambayo mtu huyo anahojiwa, na kumbukumbu hizo zitapaswa kuonyeshwa au kusomwa kwa mtu huyo au kama haelewi lugha ambayo maelezo yameandikwa yatatafsiriwa kwake katika lugha anayoiwelewa na atakuwa huru kuelezea au kuongeza kitu kwenye maelezo yake. Baada ya hapo atasaini maelezo hayo mara tu baada ya mstari wa mwisho wa kumbukumbu ya maelezo hayo na anaweza kumuita mtu yoyote aliyepo kusaini kama shahidi kwa saini yake. Afisa polisi baada ya kuweka kumbukumbu maelezo ataambatanisha uthibitisho ufuatao kwa chini katika kila maelezo atakayokuwa ameyaweka kumbukumbu:

"Mimi....., natamka kwamba kwa uaminifu na usahihi nimeweka katika kumbukumbu maelezo ya mtajwa hapo juu....."

(4) Utakuwa ni wajibu wa afisa polisi kabla ya kumhoji mtu kumweleza mtu huyo kuwa anawajibika kuyajibu kwa ukweli maswali yote yanayohusiana na kesi atakayoulizwa naye na kwamba hawezi kukataa kujibu swali lolote kwa sababu tu swali hilo lina mwelekeo wa kumhatarisha wazi katika shitaka la jinai, adhabu au kunyang'anywa

mali yake.

(5) Afisa polisi au mtu aliye kwenye mamlaka hatatakiwa kutoa ahadi au kutoa au kusababisha kutolewa ushawishi, vitisho au ahadi kwa mtu yoyote aliyeshitakiwa kwa kosa kumshawishi mtu huyo kutoa maelezo yanayohusiana na mashitaka dhidi yake. Lakini hakuna afisa polisi au mtu aliye kwenye mamlaka atazuia, au kukatisha tamaa kwa njia ya onyo au kwa njia nyingine mtu yoyote kutoa, katika harakati ya upelelezi wowote, maelezo yoyote ambayo yuko tayari kutoa kwa hiari yake mweyewe.

(6) Maelezo ya mtu yeyote kwa afisa polisi katika harakati ya upelelezi wowote yanaweza kutumika kwa mujibu wa masharti ya sheria iliyopo kwa wakati huo inayohusiana na utaratibu wa kuchukua na kupokea ushahidi, lakini sio kwa madhumuni ya kuongezea ushuhuda wa mtu huyo mahakamani.

(7) Katika shauri lolote chini ya Sheria hii, kutolewa kwa nakala iliyothibitishwa ya taarifa inayotajwa katika kifungu cha 9 au maelezo yoyote yaliyowekwa katika kumbukumbu chini ya kifungu hiki yatakuwa ni uthibitisho tosha kuwa taarifa ilitolewa au kwamba maelezo hayo yaliyotolewa kwa afisa polisi aliyeyaweka katika kumbukumbu; na bila kujali masharti ya sheria ingine yoyote, haitakuwa lazima kumwita afisa polisi kama shahidi kwa ajili tu ya kuleta nakala iliyothibitishwa.

(b) Ukamataji na Hati ya Kukamata

Ukamataji
unavyofanywa

11.-(1) Katika kufanya ukamataji afisa polisi au mtu mwingine anayefanya ukamataji atalazimika hasa kugusa au kuzuia mwili wa mtu anayekamatwa isipokuwa kama mtu huyo atakubali kwa mdomo au vitendo kwenda mahabusu.

(2) Iwapo mtu anayekamatwa anakataa kwa nguvu jitihada za kumkamata, au anajaribu kutoroka kukamatwa, afisa polisi au mtu mwingine anaweza kutumia njia zote muhimu kufanikisha ukamataji .

Kuzuia vizuizi
visivyo vya lazima

12. Mtu aliyekamatwa hatatakiwa kuwa kwenye kizuizi kikubwa zaidi ya kile cha lazima kuzuia asitoroke.

Hati ya kukamata

13.-(1) Pale taarifa iliyo chini ya kiapo imepelekwa mbele ya hakimumu, Katibu Kata au Katibu wa Halmashauri ya Kijiji, ikituhumu kuwa kuna sababu za msingi za kuamini kuwa mtu ametenda kosa–

(a) hakimumu, Katibu Kata au Katibu wa Halmashauri ya Kijiji, kama itakavyokuwa, iwapo mtu huyo hayuko kwenye kizuizi, lakini kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), anaweza kutoa hati cha kukamatwa kwa mtu huyo na kupelekwa mbele ya mahakama iliyoonyeshwa kwenye hati hiyo kujibu taarifa na kushughulikiwa zaidi kwa mujibu wa Sheria; au

(b) Hakimu, Katibu Kata au Katibu wa Halmashauri ya Kijiji, kama itakavyokuwa, anaweza kutoa wito unaomtaka mtu huyo kuhudhuria mbele ya mahakama kujibu taarifa.

(2) Muda wowote baada ya hakimu, Katibu Kata au Katibu wa Halmashauri ya Kijiji kutoa wito unaomtaka mtu kuhudhuria mbele ya mahakama kujibu taarifa chini ya kifungu kidogo cha (1) na kabla ya wito haujapelekwa rasmi kwa mtu huyo, Hakimu, Katibu Kata, au Katibu wa Halmashauri ya Kijiji, kama itakavyokuwa, kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), anaweza kutoa waraka wa kukamatwa mtu huyo na kupelekwa mbele ya mahakama iliyoonyeshwa kwenye hati ili kujibu taarifa na kushughulikiwa zaidi kwa mujibu wa sheria.

(3) Hati haitatolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) au (2) kuhusiana na taarifa mpaka hapo–

(a) Hati ya kiapo kimeletwa kikieleza sababu ambazo utolewaji wa kibali unahitajiwa;

(b) mtoa taarifa au mtu mwingine anayetoa taarifa zaidi kadri Hakimu, Katibu Kata, au Katibu wa Halmashauri ya Kijiji anavyotaka kuhusiana na sababu ambazo utolewaji wa hati unahitajika; au

(c) Hakimu, Katibu Kata, au Katibu wa Halmashauri ya Kijiji ameridhika kwamba kuna sababu za msingi kwa hati kutolewa.

(4) Pale mtoa taarifa anatoa taarifa kwa Hakimu, Katibu Kata, au Katibu wa halmashauri ya Kijiji kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3)(b) atatoa taarifa chini ya kiapo.

(5) Pale Hakimu, Katibu Kata, au Katibu wa Halmashauri ya Kijiji anatoa hati chini ya kifungu kidogo cha (1), atalazimika kueleza kwenye hati ya kiapo alichopelekwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) kuwa ni sababu zipi (kama zipo) zilizoonyeshwa katika hati ya kiapo na maelezo ya sababu nyingine yoyote ambayo ametumia kuhalalisha utoaji wa hati.

Ukamataji na afisa
polisi bila hati

14. Afisa polisi anaweza bila ya hati kumkamata:–

(a) mtu yeyote ambaye anafanya uvunjifu wa amani mbele yake;

(b) mtu yeyote ambaye kwa makusudi anamzuia afisa polisi aliye katika utekelezaji wa majukumu yake, au mtu ambaye ametoroka au anajaribu kutoroka kutoka mahabusu halali kisheria;

(c) mtu yeyote ambaye atakutwa na kitu chochote kinachodhaniwa kwa sababu za msingi kuwa ni kitu kilichoibwa au mtu anayedhamiria kutenda kosa kuhusiana na kitu hicho;

(d) mtu yeyote atakayemkuta amelala au kuzurura katika barabara kuu, yadi, bustani au sehemu nyingine wakati wa usiku na ambaye anamdhanika kwa sababu za msingi

kuwa ametenda kosa au anataka kutenda kosa au ambaye amebeba bila ya ruhusa halali silaha ya hatari au kifaa cha kuvunjia nyumba;

- (e) mtu yeyote ambaye ana sababu za msingi za kuamini kuwa hati ya ukamataji imeshatolewa;
- (f) mtu yeyote anayemdhanika kwa sababu za msingi kuwa amehusika katika kitendo kilichotendeka sehemu yoyote nje ya Tanzania ambacho, kama kingetendeka Tanzania, kingeadhibiwa kama kosa, na ambacho, kwa mujibu wa Sheria ya Kubadilishana Watuhumiwa, au vinginevyo, anawajibika kukamatwa na kuzuiwa Tanzania;
- (g) mtu yoyote anayefanya tendo lolote linaloazimia kutusi nembo ya taifa au bendera ya taifa;
- (h) mtu yeyote anayemdhanika kuwa ni mzururaji.

(3) Pale mtu ambaye amekamatwa kwa kosa kwa mujibu wa wa kifungu kidogo cha (1) au (2) anashikiliwa kizuizini kuhusiana na upelelezi wa kosa lakini hajashitakiwa kwa kosa, itakuwa halali kisheria kuendelea kumshikilia mtu huyo chini ya kizuizi kwa muda wote ambao afisa polisi msimamizi anayehusika na upelelezi anaamini kwa sababu za msingi kwamba ni lazima kuendelea kumshikilia mtu huyo chini ya kizuizi kwa sababu moja au nyingine au zozote zilizoainishwa katika vifungu vidogo vya (1) na (2).

Utaratibu endapo afisa polisi anakaimisha ukamataji bila hati

15. Wakati afisa msimamizi yeyote wa kituo cha polisi atamtaka afisa aliye chini yake kukamata bila hati (zaidi ya kosa lilitokea mbele ya afisa huyo) mtu yeyote ambaye anaweza kukamatwa kihalali bila ya hati chini ya kifungu cha 14, atalazimika kutoa kwa afisa anayetakiwa kufanya ukamataji amri kwa maandishi akiainisha mtu anayetakiwa kukamatwa na kosa au sababu nyingine ambazo ukamataji unahitajika kufanyika.

Ukamataji unaofanywa na watu binafsi bila hati.

16.-(1) Mtu yeyote binafsi anaweza kumkamata mtu yeyote ambaye mbele yake anafanya kosa mojawapo kati ya makosa yaliyotajwa katika kifungu cha 14.

(2) Mtu atakayekutwa anatenda kosa linaloambatana na uharibifu wa mali anaweza kukamatwa bila ya hati na mmiliki wa mali hiyo au watumishi wake au mtu aliyeruhusiwa na mmiliki wa mali.

Ukamataji unaofanywa na hakim.

17. Hakim yeyote anaweza wakati wowote kumkamata au kutoa hati akielekeza kukamatwa kwa mtu yeyote ambaye anaamini kwa sababu za msingi kuwa ametenda kosa ndani ya mipaka ya mamlaka yake.

Hakimu anaweza kumkamata mtu kwa kosa lolote

18. Wakati kosa lolote limetendeka mbele ya hakim ndani ya mipaka ya mamlaka yake anaweza yeye mwenyewe kukamata au

linalotendeka mbele yake

kumuamuru mtu yeyote kumkamata mkosaji na anaweza, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii yanayohusiana na utoaji wa dhamana, kumpeleka mkosaji mahabusu.

Haki ya kuingia sehemu yoyote kwa ajili ya kufanikisha ukamataji

19.-(1) Iwapo mtu yeyote anatekeleza hati ya ukamataji au afisa polisi yeyote mwenye mamlaka ya kukamata, ana sababu za msingi za kuamini kuwa mtu anayetakiwa kukamatwa ameingia au yuko ndani ya nyumba yoyote au mahali popote, mtu huyo au afisa polisi atamtaka mtu anayeishi ndani au msimamizi wa nyumba husika au mahali hapo kumruhusu kuingia kwenye nyumba hiyo au mahali hapo, na mtu anayeishi ndani au msimamizi wa nyumba hiyo atalazimika kumruhusu bila vipingamizi kuingia ndani na kumuwezesha kwa njia zozote kufanya upekuzi, ndani ya nyumba hiyo au mahali hapo.

(2) Iwapo uingiaji kwenye nyumba hiyo au mahali hapo hauwezi kupatikana chini ya kifungu kidogo cha (1), itakuwa halali kisheria kwa jinsi yoyote kwa mtu anayetekeleza hati ya ukamataji, na kwa jinsi yoyote ambayo hati inaweza kutolewa lakini haiwezekani kupatikana kabla ya mtu anayekamatwa kupata nafasi ya kutoroka, kwa afisa polisi, kuingia kwenye nyumba au mahali hapo na kupekua ndani yake na, ili kufanikisha kuingia, kuvunja mlango wowote wa nje au ndani au dirisha la mtu huyo anayepaswa kukamatwa au la mtu mwingine yeyote au vinginevyo kufanikisha kuingia kwenye nyumba au mahali hapo, ikiwa baada ya taarifa ya mamlaka yake na madhumuni na mahitaji ya kuingia yamefanywa, hawezi kwa njia nyingine kuingia, kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3)

(3) Iwapo nyumba hiyo au mahali hapo ni makazi yanayomilikiwa na mwanamke (sio mtu anayekamatwa) ambaye, kwa mujibu wa mila, hatoki mahali pa uma, mtu au afisa polisi atalazimika kabla ya kuingia kwenye makazi hayo, kutoa taarifa kwa mwanamke huyo kuwa ana uhuru wa kuondoka, na atatakiwa kutoa nafasi muhimu kumwezesha mwanamke huyo kuondoka na baada ya hapo anaweza kuvunja makazi, kufungua na kuingia ndani yake.

Uwezo wa kuvunja sehemu yoyote kwa ajili ya kukomboa.

20. Afisa polisi yeyote au mtu mwingine aliyeruhusiwa kufanya ukamataji anaweza kuvunja sehemu yoyote kwa ajili ya kujikomboa mwenyewe au mtu mwingine ambaye, baada ya kuingia kihalali kisheria kwa ajili ya kufanya ukamataji, amezuiwa ndani ya sehemu hiyo.

Utumiaji wa nguvu katika ukamataji

21.-(1) Afisa polisi au mtu mwingine hatatakiwa, wakati wa kumkamata mtu, kutumia nguvu zaidi au kuvunja utu wa mtu huyo zaidi ya ilivyo lazima kufanikisha ukamataji au kumzuia utorokaji wa mtu baada ya kukamatwa.

(2) Bila kupunguza matumizi ya kifungu kidogo cha (1), afisa polisi hatatakiwa, wakati wa kumkamata mtu, kufanya kitendo

kinachoweza kusababisha kifo kwa mtu huyo, isipokuwa kama afisa polisi anaamini kwa sababu za msingi kwamba kufanya kitendo hicho ni muhimu katika kulinda maisha au kuzuia madhara makubwa kwa mtu mwingine.

Baadhi ya ukamataji kutokuchukuliwa kuwa kinyume cha sheria

22. Pale mtu anayemkamata mtu mwingine kwa kosa zaidi ya lile lililo kwenye hati lakini katika mazingira yaliyotajwa katika kifungu cha 16, ukamataji hautachukuliwa kuwa ni kinyume cha sheria kwa sababu tu hapo baadaye itaonekana, au itaamuliwa na mahakama, kwamba mtu huyo hakutenda kosa.

Mtu kujulishwa sababu za ukamatwa

23.-(1) Mtu anayemkamata mtu mwingine atalazimika kisheria, wakati wa ukamataji, kumwambia mtu huyo kosa ambalo anakamatwa kwalo.

(2) Mtu anayemkamata mtu mwingine atachukuliwa kuwa ametimiza masharti ya kifungu kidogo cha (1) iwapo atamwambia mtu huyo kiini cha kosa ambalo anakamatwa kwalo; na sio lazima kufanya hivyo katika lugha sahihi kabisa au ya kitaalamu.

(3) Kifungu kidogo cha (1) hakitumiki kwa au kuhusiana na ukamataji wa mtu-

- (a) Iwapo, kwa sababu za mazingira ambayo anakamatwa, mtu huyo anapaswa kujua kiini cha kosa ambalo anakamatwa kwalo; au
- (b) Iwapo, kwa sababu ya vitendo vyake mtu anayekamatwa anasababisha kushindikana kuelezwa kosa analokamatwa nalo na mtu anaye mkamata.

Upekuzi wa mtu aliyekamatwa

24. Wakati ambapo mtu anakamatwa:-

- (a) na afisa polisi chini ya hati ambayo hairuhusu utoaji wa dhamana, au chini ya hati ambayo inaruhusu dhamana lakini mtu anayekamatwa hawezi kutimiza masharti ya dhamana; au
- (b) bila ya hati, au anakamatwa na mtu binafsi chini ya hati, na mtu anayekamatwa hawezi kisheria kupewa dhamana, au hawezi kutimiza masharti ya dhamana, afisa polisi anayekamata, au kama ukamataji unafanywa na mtu binafsi, afisa polisi anayepolekewa mtu huyo aliyekamatwa, anaweza kumpekua mtu huyo aliyekamatwa na kuweka mahali pa usalama vitu vyote, atakavyokutwa navyo isipokuwa vile ambavyo ni mavazi muhimu.

Uwezo wa polisi kuzuia na kukagua magari, nk.

25.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya vifungu vya 50 na 51 vya Sheria hii, afisa polisi yeyote anaweza kufanya chochote au vyote

vifuatavyo yaani, kusimamisha, kupekua au kuzuia–

- (a) chombo chochote, meli, ndege au gari ikiwa kuna sababu za msingi kutilia shaka kuwa kuna–
 - (i) mali yoyote iliyoibwa;
 - (ii) vitu vyovyote vilivyotumika au vinavyokusudiwa kutumika katika kutenda kosa;
 - (iii) bila ya udhuru kisheria, silaha yoyote ya hatari, kitu cha ulaghai au kitu chochote kilichokatazwa chini ya sheria yoyote;
- (b) Mtu yeyote ambaye kwa sababu za msingi anadhaniwa kuwa anamiliki au anasafirisha kwa njia yoyote kitu chochote kilichotajwa katika aya ya (a)

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3), iwapo baada ya kumalizika kwa muda uliotajwa katika kifungu cha 50 kwa ajili ya kumhoji mtu hakuna maombi yoyote ya kuongeza muda yamefanyika au maombi yamefanyika na yamekataliwa, chombo, meli ndege, gari, au mtu, kama itakavyokuwa, vitaachiliwa au mtu huyo ataachiliwa na kwa suala la mtu, bidhaa zozote zilizokamatwa kutoka kwake zitarejeshwa kwake.

(3) Pale muda wa kumhoji mtu umeongezwa kufuatia maombi sawia yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2), hakimumu atalazimika, kama ni muhimu, kuamuru kuwa chombo, meli, ndege au gari vishikiliwe ili kufanikisha upelelezi zaidi au kwa ajili ya kutumika kama kielelezo katika shauri mahakamani.

Jinsi ya kupekua wanawake

26. Wakati ambapo ni muhimu kwa mwanamke kupekuliwa, upekuzi lazima ufanyike na mwanamke mwingine kwa heshima zaidi.

Uwezo wa kutwaa silaha za hatari

27. Afisa polisi au mtu mwingine anayefanya ukamataji anaweza kuchukua kutoka kwa mtu anayekamatwa silaha yoyote ya hatari ambayo anayo, na atapeleka mahakamani au kwa afisa ambaye au ambako afisa polisi au mtu yeyote anayefanya ukamataji anatakiwa kisheria kumpeleka mtu aliyekamatwa na silaha zote zilizochukuliwa.

Ukamataji wa wazururaji, majambazi wazoefu, n.k.

28. Afisa yeyote msimamizi wa kituo cha polisi anaweza kwa njia kama hiyo kukamata au kuamuru kukamatwa:-

- (a) mtu yeyote atakayekutwa anachukua tahadhari kujificha ndani ya mipaka ya kazi ya kituo hicho katika mazingira yanayotosheleza kuamini kwamba anachukua tahadhari hizo akiwa na nia ya kutenda kosa lisilo la kibali;
- (b) mtu yeyote ndani ya mipaka ya kituo ambaye hana njia ya kipato inayomwezesha kuishi au ambaye hawezi kujielezea yeye mwenyewe;
- (c) mtu yeyote ambaye kwa sifa ni jambazi mzoefu, mvunjaji nyumba, au mwizi au mzoefu wa kupokea vitu

vilivyoibwa akijua kuwa vimeibiwa, au ambaye kwa sifa anafanya kughusubu au katika kufanya ughusubu anamuweka au anajaribu kumuweka mtu katika hali ya kuogopa kudhuriwa.

Kukataa kutoa jina na makazi.

29.-(1) Wakati mtu yeyote ambaye mbele ya afisa polisi ametenda au ametuhumiwa kutenda kosa la kibali anakataa baada ya kuombwa na afisa polisi kutaja jina lake na makazi yake, au anataja jina na makazi ambayo afisa ana sababu za msingi za kuamini kuwa ni uongo, anaweza kukamatwa na afisa huyo ili jina lake na makazi yake yaweze kuhakikiwa.

(2) Wakati jina la kweli na makazi ya kweli ya mtu huyo yamehakikiwa ataachiwa baada ya kutoa dhamana, akiwa na wadhamini au bila wadhamini, na kutakiwa kuhudhuria mbele ya mahakama kama itahitajika hivyo; lakini kama mtu huyo si mkazi wa Tanzania dhamana italazimika kuambatana na mdhamini au wadhamini wakazi wa Tanzania

(3) Ikiwa jina la kweli na makazi ya huyo mtu hayatahakikiwa ndani ya saa ishirini na nne kuanzia muda wa kukamatwa, au kama atashindwa kuweka dhamana, au iwapo itahitajika, kuwaleta wadhamini, wanaotosheleza atapelekwa moja kwa moja kwenye mahakama yenye mamlaka.

Udhibiti wa watu waliokamatwa na afisa polisi.

30. Afisa polisi anayefanya ukamataji bila hati atalazimika, bila kuchelewa kusiko muhimu na kwa kuzingatia masharti yaliyomo humu ndani yahasuyo utoaji dhamana kumchukua au kumpeleka mtu aliyekamatwa mbele ya mahakama yenye mamlaka katika eneo la kituo cha polisi.

Udhibiti wa watu waliokamatwa na watu binafsi Sheria Na. 5 ya 1998, kif. 3

31.-(1) Mtu yeyote binafsi anayemkamata mtu bila ya hati atalazimika bila ya kuchelewa kusiko muhimu kumkabidhi mtu aliyekamatwa kwa afisa polisi au kwenye kituo cha polisi kilicho karibu, au kama hakuna ama, kwa Katibu Kata au Katibu wa Halmashauri ya Kiji ambako ukamataji umefanyika.

(2) Iwapo kuna sababu za kuamini kwamba masharti ya kifungu cha 14, hayatumiki kwa mtu aliyekamatwa, afisa polisi atamkamata mtu huyo tena .

(3) Iwapo kuna sababu za kuamini kuwa mtu aliyekamatwa ametenda kosa la kibali, na anakataa baada ya kuombwa na afisa polisi kutaja jina lake na makazi, au akataja jina na makazi ambayo afisa ana sababu za kuamini kuwa ni uongo, atalazimika kumshughulikia chini ya masharti ya kifungu cha 29; lakini kama hakuna sababu za kutosha kuamini kuwa ametenda kosa lolote atalazimika kumuachia mara moja.

Uzuiaji wa watu waliokamatwa

32.-(1) Wakati mtu yeyote amewekwa mahabusu kwa kosa bila

kibali, isipokuwa kwa kosa linaloadhibiwa kwa kifo, afisa msimamizi wa kituo cha polisi ambako ameletwa, katika jinsi yoyote, na kama inaonekana haiwezekani kumpeleka mbele ya mahakama inayofaa ndani ya saa ishirini na nne kuanzia alipowekwa mahabusu, anaweza kuichunguza kesi na, isipokuwa kama kosa linaonekana na afisa huyo kuwa ni kubwa, kumwachia mtu huyo baada ya kuweka dhamana kwa kiasi cha kutosha akiwa na wadhamini au bila ya wadhamini, na kumtaka kuhudhuria mbele ya mahakama katika muda na mahali palipotajwa kwenye dhamana; lakini kama atashikiliwa mahabusu atalazimika kupelekwa mbele ya mahakama haraka iwezekanavyo.

(2) Pale mtu yeyote amewekwa mahabusu bila hati kwa kosa linaloadhibiwa kwa kifo, atatakiwa kupelekwa mbele ya mahakama haraka iwezekanavyo.

(3) Pale mtu yeyote atakamatwa chini ya hati ya ukamataji atatakiwa kupelekwa mbele ya mahakama haraka iwezekanavyo.

(4) Bila kujali chochote kilichopo katika vifungu vidogo vya (1), (2) na (3), afisa msimamizi wa kituo cha polisi anaweza kumwachia mtu aliyekamatwa kwa kudhaniwa kutenda kosa lolote iwapo baada ya uchunguzi wa kina wa polisi, kwa maoni yake hakuna ushahidi uliojitosholeza, kuendelea na shtaka.

Polisi kutoa taarifa za kukamataji

33. Afisa msimamizi wa kituo cha polisi atatoa taarifa kwa hakimu aliye karibu, ndani ya saa ishirini na nne au mapema iwezekanavyo, kesi za watu wote waliokamatwa bila hati ndani ya mipaka ya kituo chake, hata kama watu hao wamepewa dhamana au la.

(c) Utoro na ukamataji tena

Ukamataji tena wa watu waliotoroka

34. Iwapo mtu aliye katika mahabusu halali ya kisheria anatoroka au kutoroshwa, mtu ambaye katika mahabusu yake mtu huyo ametoroka au kutoroshwa anaweza kwa haraka kuanza kumtafuta mtu huyo na kumkamata mahali popote Tanzania.

Masharti ya vifungu vya 19 na 20 kutumika katika ukamataji chini ya kifungu cha 34

35. Masharti ya vifungu vya 19 na 20 yatatumika katika ukamataji chini ya kifungu cha 34 ingawaje mtu anayefanya ukamataji huo hafanyi chini ya hati na si afisa polisi mwenye mamlaka ya kukamata.

Wajibu wa kumsaidia hakimu au afisa polisi katika kuzuia utorokaji wa mtu aliyekamatwa

36. Kila mtu anawajibika kumsaidia hakimu au afisa polisi ambaye kimsingi anahitaji msaada wake:-

- (a) katika kumkamata au kuzuia kutoroka kwa mtu yeyote ambaye hakimu au afisa polisi anaruhusiwa kumkamata; au
- (b) katika kuzuia au kukomesha uvunjifu wa amani, au katika kuzuia madhara yoyote yanayotaka kutendeka

katika reli yoyote, njia, telegrafu au mali nyingine ya umma.

Fidia kwa maumivu, hasara au kifo kutokana na kumsaidia polisi, nk.

37.-(1) Pale mtu yeyote anapata hasara ya mali au maumivu ya mwili, au anakufa kutokana na kuchukua hatua au katika harakati za kumsaidia hakimu, afisa polisi au afisa mwingine wa sheria kuzuia utendekaji wa kosa au katika kumkamata mtu ambaye ametenda au anadhaniwa kwa sababu za msingi kuwa ametenda kosa, atatakiwa kupata fidia kwa ajili ya hasara au maumivu na kama atakufa, wategemezi wake au wawakilishi wake kisheria watakuwa na haki ya kupokea fidia ambayo mtu huyo angepokea kama asingekufa.

(2) Kiwango cha fidia kitakacholipwa chini ya kifungu kidogo cha (1) kitakadiriwa, na mambo mengine yote yahusuyo malipo ya fidia yatashughulikiwa, kulingana na masharti ya sheria iliyopo kwa wakati huo kuhusiana na malipo ya fidia kwa waathirika wa makosa ya jinai.

(3) Fidia yoyote itakayolipwa chini ya kifungu hiki italazimika kulipwa katika namna na katika fungu la fedha kama litakavyoelezwa na sheria iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2).

(d) Hati za upekuzi na ukamataji mali

Uwezo wa kutoa hati ya upekuzii au kuruhusu ukaguzi Sheria Na. 5 ya 1988 kif. 4; 5 ya 1994 jedwali

38.-(1) Iwapo afisa polisi msimamizi wa kituo cha polisi ataridhishwa kwamba kuna sababau za msingi kutuhumu kuwa ndani ya nyumba, chombo, chombo cha uchukuzi, sanduku, kipokezi au mahali kuna:-

- (a) kitu chochote kuhusiana na kosa lililotendeka;
- (b) kitu chochote ambacho kuna sababu za msingi kuamini kuwa kitasaidia kama ushahidi kuhusu utendekaji wa kosa;
- (c) kitu chochote ambacho kuna sababu za msingi kuamini kwamba kinakusudiwa kutumika kwa madhumuni ya kutenda kosa,

na afisa ameridhika kuwa uchelewaji utasababisha kuondolewa au kuharibiwa kwa kitu hicho au kitahatarisha maisha au mali, anaweza kufanya upekuzi au kutoa idhini kwa maandishi kwa afisa polisi yeyote aliye chini yake kupekua nyumba, chombo, sanduku, kipokezi au mahali hapo kama itakavyokuwa.

(2) Wakati idhini iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) inatolewa, afisa polisi anayehusika atalazimika, mapema iwezekanavyo, kutoa taarifa ya kutolewa kwa idhini hiyo, sababu ambazo idhini imetolewa na matokeo ya upekuzi wowote uliofanywa chini ya idhini hiyo kwa hakimu.

(3) Pale kitu chochote kitakamatwa kufuatia uwezo uliotolewa na kifungu kidogo cha (1) afisa anayekamata kitu hicho atatakiwa kutoa risiti ya kukubali kukamata kitu hicho, ikiwa na saini ya mmiliki

au mkazi wa makazi hayo au ndugu yake wa karibu au mtu mwingine ambaye kwa muda huo anashikilia au anadhibiti makazi hayo, na saina za mashahidi walioshuhudia upekuzi, kama wapo.

(4) Mtu yeyote, aliyepewa uwezo na sheria kuamuru, kuruhusu au kufanya upekuzi kwa mtu yoyote, mahali, jengo, chombo, chombo cha usafirishaji au kipokezi, kwa nia mbaya na bila ya sababu zozote za msingi za kufanya hivyo, akaamuru, akaruhusu au akafanya upekuzi atakuwa anatenda kosa na kama akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

(5) Hakuna mashitaka yoyote dhidi ya mtu kwa kosa chini ya kifungo kidogo cha (4) yatafunguliwa isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashitaka.

Vitu vinavyohusiana na kosa

39. Kwa madhumuni ya Sehemu hii:-

- (a) kitu chochote ambacho kinahusiana na utendekaji wa kosa au kinadhaniwa kwa sababu za msingi kuwa kosa limetendeka;
- (b) kitu chochote ambacho kuna sababu za msingi za kuamini kuwa kinaweza kusaidia kama ushahidi kuhusiana na utendaji wa kosa; na
- (c) kitu chochote ambacho kuna sababu za msingi za kuamini kuwa kinakusudiwa kutumika kwa ajili ya utendekaji wa kosa lolote.

Kitahesabika kuwa ni kitu kinachohusiana na kosa.

Utekelezaji wa hati ya upekuzi

40. Hati ya upekuzi inaweza kutolewa na kutekelezwa siku yoyote (ikiwemo jumapili) na inaweza kutekelezwa kati ya muda wa jua kuchomoza na jua kuchwa lakini mahakama inaweza, kwa maombi ya afisa polisi au mtu mwingine ambaye imeelekezwa, kumruhusu kutekeleza katika muda wowote.

Upekuzi na ukamataji.

41. Afisa polisi anaweza kumpekua mtu au nguo iliyovaliwa, au mali ambayo inathibitiwa na mtu na anaweza kukamata kitu chochte kinachohusiana na kosa kitakachokutwa katika harakati za upekuzi, iwapo upekuzi na ukamataji wa mali unafanywa na afisa polisi:-

- (a) kufuatia hati kilichotolewa chini ya Sehemu hii;
- (b) kwa mujibu wa kifungo cha 24 baada ya kumuweka mtu katika mahabusu halali ya kisheria kuhusiana na kosa;
- (c) baada ya kumzuia mtu kwa mujibu wa kifungo kidogo cha (2) cha kifungo cha 42;
- (d) kufuatia amri iliyotolewa na mahakama.

Upekuzi wakati wa dharura.

42.-(1) Afisa polisi anaweza:-

- (a) kumpekua mtu anayemshuku kubeba kitu chochote kinachohusiana na kosa; au
- (b) kuingia kwenye ardhi yoyote, au katika jengo lolote, chombo au gari, ambamo anaamini kwa sababu za msingi kuwa kitu chochote kinachohusiana na utendekaji wa kosa kimo,

na anaweza kukamata kitu hicho ambacho amekipata katika harakati za upekuzi huo, au kwenye ardhi au katika jengo, chombo au gari kama itakavyokuwa–

- (i) iwapo afisa polisi anaamini kwa sababu za msingi kwamba ni muhimu kufanya hivyo kwa ajili ya kuzuia hasara au uharibifu wa kitu chochote kinachohusiana na kosa; na
- (ii) Upekuzi au uingiaji unafanyika katika mazingira ambayo ni mazito na ya haraka yanayohitaji na kuhalalisha upekuzi au uingiaji wa haraka bila mamlaka ya amri ya mahakama au hati kilichotolewa chini ya Sehemu hii.

(2) Afisa polisi anayeamini kwa sababu za msingi kwamba mtu amebeba silaha ya hatari au kitu chochote kinachohusiana na kosa anaweza kumsimamisha mtu huyo na kukamata silaha hiyo au kitu chochote kitachokutwa kwa mtu huyo.

(3) Afisa polisi anayeamini kwa sababu za msingi kuwa silaha ya hatari, au kitu chochote kinachohusiana na kosa kimebebwa katika chombo au gari, anaweza kusimamisha na kukamata silaha hiyo au kitu chochote kitakachokutwa kwenye chombo au gari.

Wasimamizi wa sehemu zilizofungwa kuruhusu kuingia na kutoka

43.-(1) Wakati ambapo jengo lolote au mahali pengine panapotakiwa kupekuliwa pamefungwa, mtu yoyote anayeishi ndani au msimamizi wa nyumba au mahali husika atalazimika, akitakiwa na afisa polisi au mtu mwingine anayetokeleza hati cha upekuzi, na baada ya kuonyeshwa hati, kumruhusu kuingia bila vikwazo, kumpatia mazingira yote muhimu kwa upekuzi ndani na kumruhusu bila vikwazo kutoka.

(2) Iwapo kuingia au kutoka kwenye jengo au sehemu nyingine hakuwezi kupatikana, afisa polisi au mtu mwingine anayetokeleza hati ya upekuzi anaweza kuendelea katika namna iliyoonyeshwa na kifungu cha 19 au kifungu cha 20.

(3) Pale mtu yeyote aliye ndani au karibu na jengo au mahali anatumia kwa sababu za msingi kuficha katika mwili wake kitu chochote ambacho upekuzi unatakiwa kufanyika au unafanyika, anaweza kupekuliwa na kama mtu huyo ni mwanamke, masharti ya kifungu cha 26 yatafuatwa.

Kushikiliwa kwa mali iliyotwaliwa

44.-(1) Wakati kitu kimekamatwa na kimeletwa mbele ya

mahakama kinaweza, kwa kuzingatia kifungu cha 353, kuzuiliwa mpaka kuhitimishwa kwa kesi au upelelezi, uangalifu wa kutosha uchukuliwe katika kukitunza kisiharibike.

(2) Iwapo rufaa imekatwa au kama mtu yeyote anashikiliwa kwa ajili ya kesi yake kusikilizwa na mahakama, mahakama inaweza kuamuru kitu hicho kiendeleo kushikiliwa kwa ajili ya rufaa au kusikilizwa kesi.

(3) Iwapo hakuna rufaa iliyokatwa, au ikiwa hakuna mtu ambaye anasubiri kesi yake kusikilizwa na mahakama, mahakama itaelekeza kitu hicho kurudishwa kwa mtu kilipochukuliwa, isipokuwa kama mahakama inaona ni vizuri au inaruhusiwa au inatakiwa na sheria kukidhibiti kwa njia nyingine.

Vifungu
vinavyotumika
katika hati za
upekuzi

45.-(1) Masharti ya vifungu vidogo vya (1) na (3) ya kifungu cha 112, vifungu vya 114, 116, 119, 120 na 121 vitatumika kama itakavyokuwa kwa hati zote za upekuzi zinazotolewa chini ya kifungu cha 38.

(2) Kila hati ya upekuzi italazimika kurudishwa mahakamani ikiwa na uthibitisho unaonyesha muda na jinsi ilivyotekelezwa na kitu gani kimefanyika chini yake.

B. – Uwezo na Wajibu wa Maafisa Polisi wanapopeleleza makosa

(a) Masharti ya Utangulizi

Matakwa ya kutaja
jina na anuani

46.-(1) Palea afisa polisi anaamini kwa sababu za msingi kuwa mtu ambaye jina lake na anuani yake havijulikani kwake anaweza kumsaidia katika uchunguzi wake kuhusiana na kosa ambalo limetendeka linaweza kuwa limetendeka au linaweza kutendeka, afisa polisi anaweza kumuomba mtu huyo ataje jina na anuani yake

(2) Pale afisa polisi amemuomba mtu, chini ya kifungu kidogo cha (1), kutaja jina na anuani na akamarifu mtu huyo sababu za kumuomba, mtu huyo-

- (a) hatapaswa kukataa au kushindwa kutekeleza maombi hayo;
- (b) hatapaswa kutoa kwa afisa wa polisi jina au anuani ambayo ni ya uongo katika hali yoyote ; na
- (c) anaweza kumuomba afisa polisi kutaja jina lake, cheo chake na sehemu yake ya kawaida ya kazi.

(3) Pale afisa polisi ambaye anamuomba mtu chini ya kifungu kidogo cha (1) ameombwa na mtu, kulingana na aya ya (c) ya kifungu kidogo cha (2) kutaja jina lake, cheo na sehemu ya kazi, afisa polisi–

- (a) hatapaswa kukataa au kushindwa kutekeleza maombi hayo;
- (b) atalazimika kutotoa kwa mtu huyo jina au cheo ambacho ni cha uongo katika hali yoyote; na

- (c) atalazimika kutotaja kwa mtu huyo kama sehemu yake ya kazi anuani tofauti na anuani yake kamili na sahihi ya sehemu yake ya kazi ya kila siku.

(4) Mtu yeyote anayevunja kifungu hiki anatenda kosa, akitiwa hatiani, atawajibika kufungwa kwa kipindi kisichozidi miezi sita au kulipa faini isiyozidi shilingi elfu mbili au vyote.

Polisi kuzuia kuvunjika kwa amani au kutendeka kwa makosa yanayoweza kusababisha kukamatwa.

47. Kila afisa polisi yeyote anaweza kuingilia kwa madhumuni ya kuzuia na atalazimika kwa uwezo wake kuzuia, uvunjaji wa amani au utendekaji wa kosa lolote la kukamatwa.

(b) Muda wa upelelezi chini ya ulinzi wa polisi

Mipaka katika kuhoji mtu, nk

48.-(1) Pale mtu yuko au alikuwa, kizuizini kuhusiana na kosa, afisa polisi anaweza:-

- (a) kumuuliza maswali; au
(b) kuchukuwa hatua nyingine za kiupelelezi,

Kuhusiana na upelelezi wa kosa, katika kipindi kinachoruhusiwa kwa kumuhoji mtu na si vinginevyo.

(2) Masharti ya Sheria hii kuhusiana na muda unaoruhusiwa kumuhoji mtu hautachukuliwa:-

- (a) kuweka halali kisheria kushikiliwa kwa mtu chini ya kizuizi katika kipindi chochote ambacho kingekuwa, isipokuwa kwa masharti hayo, kinyume na sheria kumshikilia chini ya kizuizi; au
(b) kuhalalisha uulizwaji wa maswali au uchukuliwaji wa hatua zingine za upelelezi kuhusiana na mtu katika kipindi ambacho kingekuwa, isipokuwa kwa masharti hayo, kinyume na sheria kumshikilia chini ya kizuizi.

Wakati gain mtu asichukuliwe kuwa kizuizini.

49. Afisa polisi hatatakiwa kumuweka kizuizini kuhusiana na kosa lolote mtu ambaye alikuwa chini ya kizuizi kuhusiana na hilo kosa:-

- (a) isipokuwa kama anafanya hivyo kutokana na mambo ambayo yamejulikana na afisa polisi msimamizi wa upelelezi wa kosa hilo mara tu baada ya mtu huyo kuacha kuwa chini ya kizuizi; au
(b) isipokuwa kama muda wa kutosha umepita tangu mtu huyo alipoacha kuwa chini ya ulinzi.

Muda unaotakiwa katika kumuhoji mtu

50.-(1) Kwa madhumuni ya sheria hii, kipindi kinachoruhusiwa cha kumuhoji mtu ambaye yuko kizuizini kuhusiana na kosa utakuwa:-

- (a) kwa kuzingatia aya ya (b), kipindi cha msingi

kinachoruhusiwa kumuhoji mtu ambacho ndio kusema, ni kipindi cha saa nne kuanzia muda alipochukuliwa kuwa chini ya kizuizi kuhusiana na kosa hilo;

(b) iwapo kipindi cha msingi kilichoruhusiwakumhoji mtu kimeoongezwa chini ya kifungu cha 51, kipindi cha msingi kama kilivyoongezwa.

(2) Katika kuhesabu kipindi kinachoruhusiwa cha kumuhoji mtu ambaye yuko kizuizini kuhusiana na kosa, kutahesabika kuwa ni sehemu ya kipindi hicho muda wowote ambao afisa polisi anayepeleleza kosa ameacha kumuhoji mtu au anasababisha mtu huyo kufanya kitendo chochote kinachohusiana na upelelezi wa kosa-

(a) wakati mtu huyo, baada ya kuchukuliwa chini ya kizuizi, anasafirishwa kwenda kituo cha polisi au sehemu nyingine kwa madhumuni yoyote yanayohusiana na upelelezi;

(b) kwa madhumuni ya:-

(i) kumwezesha mtu kupanga, au kujaribu kupanga, kuhudhuria kwa mwanasheria;

(ii) kumwezesha afisa polisi kuwasiliana, au kujaribu kuwasiliana na mtu yeyote ambaye anatakiwa na kifungu cha 54 kuwasiliana naye kuhusiana na upelelezi wa kosa;

(iii) kumwezesha mtu huyo kuwasiliana, au kujaribu kuwasiliana, na mtu yeyote ambaye, chini ya Sheria hii, ana haki ya kuwasiliana naye; au

(iv) kupanga au kujaribu kupanga, kuhudhuria kwa mtu ambaye, chini ya masharti ya Sheria hii anatakiwa kuwepo wakati wa kumuhoji mtu aliye chini ya kizuizi au wakati mtu aliye chini ya kuzuizi anafanya jambo linalohusiana na upelelezi;

(c) wakati wa kusubiri kufika kwa mtu aliyetajwa chini ya aya ndogo ya (iv) ya aya (b); au

(d) wakati mtu aliye chini ya kizuizi anawasiliana na mwanasheria.

Pale ambapo upelelezi chini ya ulinzi hauwezi kukamilika ndani ya saa nne

51.-(1) Pale mtu akiwa katika mahabusu halali kisheria kutokana na kosa wakati wa kipindi cha msingi kinachoruhusiwa kumuhoji mtu, lakini bado hajashitakiwa na kosa, na inaonekana kwa afisa polisi msimamizi wa upelelezi wa kosa, kwa sababu za msingi, kwamba ni muhimu mtu huyo ahojiwe zaidi, anaweza:-

(a) kuongeza kipindi cha kuhoji kisichozidi saa nane na kumtaarifu mtu anayehusika ipasavyo; au

(b) aidha kabla ya kuisha kwa kipindi cha awali au ule ulioongezwa, kufanya maombi kwa hakimumuhoji kwa ajili ya kuongeza muda zaidi.

(2) Afisa polisi atalazimika kutoongeza kipuuzi au kwa nia ya kuleta maudhi kipindi cha msingi kinachoruhusiwa cha kumhoji mtu, lakini mtu yeyote ambaye kipindi cha kuhojiwa ameongezwa kufuatia aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (1), anaweza kudai fidia dhidi ya uongezaji wa kipindi cha msingi uliofanywa kipuuzi au kwa nia ya kuudhi, lakini jukumu la kuthibitisha litakuwa kwake.

(3) Pale hakimu ambaye maombi yameletwa na afisa polisi chini ya kifungu kidogo cha (1), na baada ya kumpa mtu huyo, au mwanasheria anayemwakilisha, nafasi ya kuwasilisha utetezi kuhusiana na maombi hayo, ameridhika–

- (a) kwamba mtu huyo yuko katika mahabusu halali kisheria;
- (b) kwamba upelelezi wa kosa unaofanywa na afisa polisi umeendeshwa au unaendeshwa kwa haraka iwezekanavyo; na

(c) kwamba itakuwa ni sawa, katika mazingira yote, kuongeza kipindi husika,

hakimu anaweza kuongeza kipindi hicho zaidi kwa jinsi atakavyoona kimsingi inafaa.

(c) Wajibu Wakati wa Kuwahoji Watuhumiwa

Kuhoji watu waliotuhumiwa.

52.-(1) Pale afisa polisi anashuku kuwa mtu ametenda kosa kubwa, au anaamini kuwa taarifa zilizopokelewa na polisi zinaweza kumwingiza mtu katika utendekaji wa kosa kubwa, lakini shuku hiyo au imani hiyo sio ile ambayo, chini ya kifungu cha 14, inahalalisha ukamataji wa mtu huyo bila hati, afisa polisi atalazimika kutomuuliza swali lolote, isipokuwa kama amemjulisha kwamba anaweza kukataa kujibu swali lolote atakaloulizwa na afisa polisi.

(2) Afisa polisi ambaye amemjulisha mtu kama ilivyolekezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) atamtaka mtu huyo kusaini au kuweka alama ya dole gumba, kwa kufuata fomu iliyowekwa, kama uthibitisho kuwa amejulishwa hivyo na tarehe ambayo, na muda ambao, amejulishwa hivyo.

(3) Pale inapokuwa muhimu kwa mahakama, katika mwenendo wowote, kuamua kama afisa polisi alimjulisha mtu kama inavyotakiwa na kifungu kidogo cha (1) na uthibitisho uliotajwa katika kifungu kidogo cha (2) na kusainiwa na mtu huyo hautatolewa katika ushahidi, mahakama itasadiki, isipokuwa kama imethibitishwa vinginevyo, kwamba mtu huyo hakujulishwa hivyo.

(4) Bila kujali masharti ya vifungu vidogo vya (1) hadi (3), pale afisa polisi katika harakati za kumhoji mtu yeyote chini ya kifungu hiki anaamini kwamba kuna ushahidi wa kutosha kuhalalisha mtu huyo kushakwa kwa kosa, ataendelea kumfungulia shtaka mtu huyo kama inavyohitajika na kumuonya kwa maandishi na kama inawezekana kwa mdomo kama utaratibu ulivyowekwa, na kumuarifu kuwa inaweza kudhaniwa vinginevyo kutokana na kushindwa au kukataa

kujibu swali lolote au kutokana na yeye kushindwa au kukataa kufafanua katika hatua hiyo jambo lolote ambalo ni la muhimu katika shitaka.

Watu walio kizuizini kuelezwa haki zao.

53. Pale mtu anakuwa kizuizini, afisa polisi hatamuuliza maswali yoyote, au kumtaka kufanya chochote, kwa madhumuni yanayohusiana na upelelzi wa kosa, isipokuwa kama:-

- (a) afisa polisi amemwambia jina na cheo chake;
- (b) mtu huyo amejulishwa na afisa polisi, katika lugha ambayo anaielewa, kwa maandishi na, kama inawezekana, kwa mdomo, kwamba yuko kizuizini na kosa ambalo kwalo yupo kizuizini; na
- (c) mtu huyo ameonywa na afisa polisi katika hali ifuatayo, yaani, kwa kumjulisha au kusababisha kujulishwa, katika lugha anayoielewa, kwa maandishi kwa kufuata fomu iliyowekwa na, iwapo inawezekana, kwa mdomo kwamba –

(i) halazimiki kujibu swali lolote atakaloulizwa na afisa polisi, tofauti na swali linalotafuta habari kuhusiana na jina na anuani yake; na

(ii) kwa kuzingatia Sheria hii, anaweza kuwasiliana na mwanasheria, ndugu au rafiki.

Mawasiliano na mwanasheria, ndugu au rafiki

54.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), afisa polisi atatakiwa, baada ya kuombwa na mtu aliye kizuizini, kuruhusu kutolewa kwa nyenzo muhimu kumwezesha mtu huyo kuwasiliana na mwanasheria, ndugu au rafiki yake atakayemchagua.

(2) Afisa polisi anaweza kukataa kutokana na kifungu kidogo cha (1) kutolewa kwa nyenzo kwa ajili ya kuwasiliana na mtu aliye ndugu au rafiki wa mtu aliye kizuizini, iwapo afisa polisi anaamini kwa sababu za msingi kwamba ni muhimu kumzuia mtu aliye kizuizini kuwasiliana na mtu kwa ajili ya kuzuia-

- (i) utorokaji wa mshiriki wa mtu aliye kizuizini; au
- (ii) upotevu, uharibifu au kughushiwa kwa ushahidi unaohusiana na kosa.

Jinsi ya kuwatendea watu walio kizuizini.

55.-(1) Mtu akiwa kizuizini, atatakiwa kutendewa kiubinadamu na kwa kufuata utu wa binadamu.

(2) Mtu, akiwa kizuizini, hatapaswa kutendewa ukatili, kinyume na ubinadamu au kudhalilishwa.

(3) Pale mtu aliye kizuizini:-

- (a) anamwomba afisa polisi kupatiwa matibabu, ushauri au msaada kuhusiana na ugonjwa au majeraha; au

(b) anaonekana kwa afisa polisi kuwa anahitaji matibabu, ushauri au msaada kuhusiana na ugonjwa au majeraha, afisa polisi atalazimika mara moja kuchukuwa hatua zinazostahili kama itakavyokuwa muhimu kuhakikisha kwamba mtu huyo anapatiwa matibabu, ushauri au msaada.

Wajibu maalum wakati wa kuhoji watoto.

56.-(1) Afisa polisi msimamizi wa upelelezi wa kosa ambalo mtoto amewekwa kizuizini atalazimika, bila kuchelewa baada ya mtoto kuwekwa kizuizini, kuhakikisha mzazi au mlezi wa mtoto anataarifiwa kwamba mtoto wake yuko kizuizini na kosa ambalo kwalo yuko kizuizini.

(2) Katika kifungu hiki “mtoto” maana yake ni mtu ambaye hajafikisha umri wa miaka kumi na sita.

(d) Kuweka kumbukumbu ya mahojiano

Kumbukumbu ya mahojiano.

57.-(1) Afisa polisi ambaye anamhoji mtu kwa madhumuni kujua kama mtu huyo ametenda kosa atalazimika, isipokuwa kama kutokana na mazingira haiwezekani kufanya hivyo, kuhakikisha mahojiano yanarekodiwa.

(2) Kama mtu anayehojiwa na afisa polisi kwa madhumuni ya kujua kama mtu huyo ametenda kosa, wakati wa mahojiano akakiri kosa, aidha kwa mdomo au kwa maandishi, afisa polisi atalazimika kurekodi au kufanikisha kurekodiwa kwa maandishi, wakati mahojiano yakiendelea au mapema iwezekanavyo baada ya mahojiano kumalizika, akiainisha–

- (a) kwa jinsi itakavyowezekana, kufanya hivyo, maswali aliyoulizwa mtu wakati wa mahojiano na majibu aliyotoa mtu huyo kuhusiana na maswali hayo;
- (b) maelezo mengine aliyoyasema mtu huyo kwa mdomo wakati wa mahojiano tofauti na majibu kwa maswali aliyoulizwa;
- (c) kama mtu aliandika maelezo yoyote wakati wa mahojiano na, kama ndivyo, muda alioanza kuandika maelezo hayo;
- (d) kama onyo lilitolewa kwa mtu kabla hajakiri na, ikiwa ndivyo, namna ambavyo onyo lilitolewa, muda ambao lilitolewa na majibu yoyote yaliyotolewa na mtu kuhusu onyo hilo;
- (e) muda ambao mahojiano yalianza na kumalizika; na
- (f) iwapo mahojiano yalisimamishwa, muda ambao yalisimamishwa na kuanza tena.

(3) Afisa polisi anayerekodi mahojiano na mtu kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atalazimika kuandika, au kuhakikisha kuandikwa, kwa mujibu wa fomu iliyowekwa na baada ya hapo mwishoni mwa rekodi hiyo aina ya uthibitisho, isipokuwa kama mtu

huyo hawezi kusoma:–

- (a) kuonyesha rekodi kwa mtu huyo na kumtaka–
 - (i) kusoma rekodi na kufanya masahihisho au marekebisho kwenye rekodi hiyo kama anapenda kufanya na kuongeza maelezo mengine kwenye rekodi hiyo na kama atakavyopenda kufanya;
 - (ii) kusaini uthibitisho uliowekwa mwishoni mwa rekodi; na
 - (iii) iwapo rekodi inaendelea kwa zaidi ya ukurasa mmoja, kuandika herufi za mwanzo za jina lake kama saini, katika kila ukurasa ambao hajasaini; **na**
- (b) kama mtu anakataa, anashindwa au anaonekana kushindwa kutekeleza ombi hilo, kuthibitisha kwenye rekodi kwa mkono wake yale aliyofanya kuhusiana na mambo mtu aliyokataa, kushindwa au kuonekana kushindwa kuyatekeleza kuhusiana na ombi hilo.

(4) Pale ambapo mtu anayehojiwa na afisa polisi hawezi kusoma rekodi ya mahojiano au anakataa kusoma, au anaonekana kwa afisa polisi kutokusoma rekodi pale anaponyeshwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) afisa polisi atalazimika:–

- (a) kumsomea rekodi, au kuhakikisha anasomewa rekodi;
- (b) kumuuliza kama angependa kusahihisha au kuongeza chochote kwenye rekodi;
- (c) kumruhusu kusahihisha, kurekebisha au kuongeza kwenye rekodi, au kufanya marekebisho yoyote, masahihisho yoyote au nyongeza kwenye rekodi ambayo amemwomba afisa polisi kufanya;
- (d) kumtaka asaini uthibitisho mwishoni mwa rekodi; na
- (e) kuthibitisha kwa mkono wake, mwishoni mwa rekodi, kile alichofanya kuhusiana na kifungu hiki kidogo.

Maelezo ya
watumiaji.

58.-(1) Pale mtu aliye kizuizini anamuarifu afisa polisi kuwa angependa kuandika maelezo, afisa polisi atalazimika–

- (a) kuhakikisha anapatiwa vifaa anavyovihitaji kwa ajili ya kuandika maelezo; na
- (b) kumtaka, kama ameonywa kwa mujibu wa aya ya (c) ya kifungu cha 53, kuweka bayana mwanzoni mwa maelezo yake jinsi onyo lilivyotolewa kwake, na kwa jinsi anavyolikumbuka.

(2) Pale mtu aliye kizuizini anampatia afisa polisi maelezo aliyoyaandika, afisa polisi atalazimika kuandika, au kuhakikisha kuandikwa, mwishoni mwa maelezo uthibitisho kwa kufuata fomu iliyowekwa, na baada ya hapo atalazimika:–

- (a) kuonyesha maelezo kwa mtu na kumtaka:–

- (i) kusoma maelezo na kufanya masahihisho au marekebisho kwenye maelezo hayo kama atakavyopenda kufanya na kuongeza maelezo mengine kwenye maelezo hayo kama atakavyopenda kufanya;
- (ii) kusaini uthibitisho uliowekwa mwishoni mwa maelezo; na
- (iii) iwapo maelezo yanaendelea kwa zaidi ya ukurasa mmoja, kuandika herufi za mwanzo za jina lake kama saini katika kila ukurasa ambao hajasaini; na

(b) iwapo mtu anakataa, anashindwa au anaonekana kushindwa kutekeleza ombi hilo, kuthibitisha kwenye maelezo kwa mkono wake yale aliyofanya kuhusiana na mambo mtu aliyokataa, kushindwa au kuonekana kushindwa kuyatekeleza kuhusiana na ombi hilo.

(3) Pale ambapo mtu anahojiwa na afisa polisi anakataa kusoma maelezo au anaonekana kwa afisa polisi kutokusoma maelezo pale anapoonyeshwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) afisa polisi atalazimika:-

- (a) kumsomea maelezo, au kuhakikisha anasomewa maelezo;
- (b) kumuuliza kama angependa kusahihisha au kuongeza chochote kwenye maelezo;
- (c) kumruhusu kusahihisha, kurekebisha au kuongeza kwenye maelezo, au kufanya marekebisho, masahihisho au nyongeza yoyote kwenye maelezo ambayo amemwomba afisa polisi kufanya;
- (d) kumtaka asaini uthibitisho mwishoni mwa maelezo; na
- (e) kuthibitisha kwa mkono wake, mwishoni mwa maelezo, kile alichofanya kuhusiana na kifungu hiki kidogo.

(e) Matendo mengine ya upelelezi

Uwezo wa kuchukua alama za vidole, picha, nk, vya watuhumiwa

59.-(1) Afisa polisi yeyote msimamizi wa kituo au afisa polisi yeyote anayepeleleza kosa anaweza kuchukua au kuhakikisha kuchukuliwa vipimo, alama za mikono, vidole vya mikono, nyayo au miguu, au kurekodi sauti au, picha ya, au sampuli ya mwandiko wa mtu yeyote anayeshitakiwa kwa kosa, bila kujali kuwa mtu huyo yuko kwenye mahabusu halali ya kisheria au vinginevyo kama hivyo vipimo, alama, rekodi, picha au sampuli, kama itakavyokuwa, zinaaminika kwa sababu za msingi kuwa ni muhimu kwa ajili ya kumtambua mtu kwa ajili ya, au kufanikisha ushahidi kuhusiana na utendaji wa kosa ambalo limemfanya awe kizuizini au ashitakiwe.

(2) Afisa polisi yeyote msimamizi wa kituo au afisa polisi yeyote anayepeleleza kosa anaweza kuchukua au kuhakikisha

kuchukuliwa vipimo, alama za mikono, vidole vya mikono, nyayo, au vidole vya miguu, au rekodi ya sauti, picha ya au sampuli ya mwandiko, ya mtu yeyote ambaye hajashitakiwa kwa kosa lolote la jinai kama hivyo vipimo, alama, rekodi, picha au sampuli, kama itakavyokuwa, inaaminika kwa sababu za msingi kuwa ni muhimu kwa ajili ya kuwezesha upelelezi wa kosa lolote.

(3) Hakuna mtu anayeshitakiwa au ambaye hajashitakiwa kwa kosa lolote ataruhusiwa kukataa au kupinga kuchukuliwa vipimo, alama, rekodi, picha au sampuli, na kama anakataa au kupinga, afisa polisi anayehusika anaweza kuchukuwa hatua stahili, ikijumuisha kutumia nguvu kiasi, kama itakavyokuwa muhimu kuhakikisha kuwa vipimo, alama, rekodi, picha au sampuli, kama itakavyokuwa, vinachukuliwa.

(4) Mtu yoyote anayekataa kuchukuliwa vipimo, alama, rekodi, picha au sampuli kama inavyotakiwa chini ya vifungu vidogo vya (1) na (2) ana hatia ya kosa na atawajibika akitiwa hatiani kulipa faini isiyoziidi shilingi elfu kumi au kufungwa kipindi kisichozidi miezi ishirini na nne au kwa vyote.

(5) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (10), mtu anayetunza vipimo, alama, rekodi, picha au sampuli na mtu yeyote anayetunza nakala za vipimo, alama, rekodi, picha au sampuli atatakiwa kuziharibu–

(a) kuhusiana na mtu ambaye yuko kwenye mahabusu halali ya kisheria kufuatia mashitaka ya kutenda kosa–

(i) iwapo mashitaka dhidi ya mtu huyo hayataendelea ; au

(ii) pale mashitaka yakiendelea, lakini mtu huyo ameachiwa huru;

(b) kwa mtu aliyetajwa katika kifungu kidogo cha (2), ikiwa hivyo vipimo, alama, rekodi, picha au sampuli, kama itakavyokuwa, havihitajiki tena kwa madhumuni ya kumwezesha upelelezi.

(6) Kutaamishwa na sehemu itakayoidhinishwa na Waziri anayehusika na upelelezi wa makosa ya jinai, ofisi itakayojulikana kama Ofisi ya Rekodi ya Makosa ya Jinai kwa ajili ya kutunza, kufananisha na kufaharisha alama za vidole au fomu.

(7) Ofisi ya Rekodi ya Makosa ya Jinai italazimika, kwa kufuata usimamizi wa jumla wa Inspekta Jenerali wa Polisi, kuwa chini ya usimamizi wa afisa mwandamizi wa polisi, mtaalamu wa kufananisha alama za vidole ambaye atakuwa anateuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa taarifa itakayotangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

(8) Fomu za alama za vidole zilizokamilika zitatumwa na kutunzwa katika Ofisi ya Rekodi ya Makosa ya Jinai.

(9) Fomu zote za alama za vidole zitakuwa katika mfumo maalumu.

Sura 39

(10) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (5), itakuwa ni halali kubakisha kumbukumbu zote zilizopatikana kwa mujibu wa vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki kuhusiana na mtu yoyote ambaye amri ya kufukuzwa chini ya Sheria ya Ufukuzaji watu Wasiofaa imefutwa au imesitishwa.

Gwaride la utambulisho.

60.-(1) Afisa polisi yeyote msimamizi wa kituo cha polisi au afisa polisi yeyote anayepeleleza kosa anaweza kuendesha gwaride la utambulisho kwa dhumuni la kuhakikisha kama shahidi anaweza kumtambua mtu anayetuhumiwa kutenda kosa.

(2) Afisa polisi yeyote msimamizi wa kituo cha polisi au afisa polisi yeyote anayepeleleza kosa anaweza kumtaka mtu yeyote ambaye ushiriki wake ni muhimu katika upelelezi wa kosa kuhudhuria na kushiriki katika gwaride la utambulisho.

(3) Hakuna mtu ambaye atatakiwa chini ya kifungu kidogo cha (2) kuhudhuria na kushiriki katika gwaride la utambulisho atakuwa na haki ya kukataa au kupinga kuhudhuria na kushiriki katika gwaride la utambulisho.

(4) Mtu yeyote ambaye, bila sababu halali au za msingi, anakataa kuhudhuria na kushiriki katika gwaride la utambulisho atakuwa na hatia ya kosa na atawajibika akitiwa hatiani kulipa faini isiyoziidi shilingi elfu mbili au kifungu kisichozidi miezi sita au vyote viwili.

Watu waliohukumiwa kutokana na kutambuliwa kimakosa kulipwa fidia

61.-(1) Pale ambapo imethibitika katika ushahidi kwamba mtu ametiwa hatiani kwa kutambuliwa kimakosa na kusababisha kushitakiwa, kuadhibiwa au kupata hasara yoyote au maumivu, mtu huyo au mwakilishi wake kisheria kama mtu huyo atakufa, atakuwa na haki fidia kama vile alikuwa muathirika wa makosa ya jinai.

(2) Fidia itakayolipwa chini ya kifungu hiki na mambo mengine yote yatakayofuatwa kuhusianana na kiasi cha fidia, jinsi ya kukokotoa kiasi na namna ya malipo itapaswa kufuata kifungu cha 37.

Waziri kutengeneza kanuni za gwaride la utambulisho,nk.

62. Waziri atatakiwa kutengeneza kanuni kutoa utaratibu utakaofuatwa katika kufanya gwaride la utambulisho, na katika kuchukua alama za vidole na picha za watuhumiwa au washtakiwa.

Uchunguzi wa kitabibu

63.-(1) Hakimumu anaweza, baada ya maombi ya afisa polisi, kuruhusu afisa tabibu kumchunguza mtu aliye katika kizuizi halali kisheria kuhusiana na kosa au kuruhusu afisa tabibu kuchukuwa na kuchanganua sampuli yoyote kutoka kwa mtu huyo kama ana sababu za msingi za kuamini kuwa uchunguzi utaleta ushahidi kuhusiana na kosa.

(2) Baada ya afisa tabibu kufanya uchunguzi na kuchanganua kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atatakiwa kupeleka ripoti ya maandishi ya huo uchunguzi Mahakamani.

(3) Katika mwenendo wowote wa kesi, mahakama inaweza kuamuru kwamba mtu yeyote ambaye ni mshiriki katika kesi au ni shahidi kwenye mwenendo wa kesi ajipeleke mwenyewe kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu na mtu huyu atalazimika kujipeleka mwenyewe.

(4) Afisa tabibu atalazimika, baada ya kumchunguza mtu ambaye mahakama imeamuru kwamba ajipeleke mwenyewe kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (3) kupeleka kwenye mahakama iliyoamuru uchunguzi, ripoti ya maandishi kuhusu uchunguzi huo.

(f) Kuachiwa na Dhamana

Dhamana ya polisi
kwa mtuhumiwa.

64.-(1) Bila kuathiri masharti ya sheria yoyote inayotumika kwa wakati huu kuhusiana na kutolewa kwa dhamana na afisa polisi, mtu aliyewekwa chini ya ulinzi wa polisi kwa mashaka ya kimsingi kuwa ametenda kosa atalazimika kuachiwa mara moja, iwapo—

- (a) afisa polisi aliyemkamata anaamini kuwa mtu huyo kweli hajatenda kosa lolote au hana sababu za msingi za kuendelea kumshikilia mtu huyo chini ya ulinzi;
- (b) Afisa polisi aliyemkamata anaamini kuwa alimkamata mtu ambaye siye; au
- (c) Baada ya saa ishirini na nne baada ya mtu kukamatwa, hakuna mashitaka rasmi yaliyoelekezwa dhidi ya mtu huyo isipokuwa kama afisa polisi anayehusika anaamini kwa sababu za msingi kwamba kosa linalodhaniwa kutendeka ni kosa kubwa.

(2) Pale mashitaka rasmi yameelekezwa dhidi ya mtu aliye chini ya ulinzi wa polisi, afisa polisi msimamizi wa kituo cha polisi anaweza, baada ya mtu huyo kuweka dhamana, akiwa na au bila ya kuwa na wadhamini, kuhudhuria mbele ya mahakama kama atahitajika, kumwachia mtu huyo pale:—

- (a) mtu huyo, ingawa anatakiwa kushitakiwa, alikamatwa bila kibali;
- (b) maada ya uchunguzi wa kina, kwa maoni yake, imeonekana kuwa hakuna ushahidi unaojitosheleza kuendelea na mashitaka;
- (c) kosa lenyewe, ingawaje ni la kibali, sio kosa kubwa; au
- (d) inaonekana kwamba uchunguzi zaidi utatakiwa kufanywa, na hauwezi kukamilika ndani ya muda mfupi wa kawaida.

(3) Pale mtu aliyekamatwa ni wa chini ya umri wa miaka kumi na tano, mtu huyo anaweza kuachiwa baada ya mzazi wake, mlezi wake, ndugu yake au mtu mwingine wa kuaminika amechukuwa dhamana kwa niaba yake.

(4) Bila kujali sheria nyingine inayotumika kwa wakati huu kuhusiana na kutolewa kwa dhamana kunakofanywa na afisa polisi, hakuna ada au ushuru utakaotozwa kwa ajili ya dhamana katika makosa ya jinai, dhamana ya kushitaki au kutoa ushahidi au dhamana kwa ajili ya mtu kuhudhuria au itolewavyo vinginevyo kutolewa au kuchukuliwa na afisa polisi.

(5) Kila afisa polisi anayemkamata mtu anayetiliwa shaka kwa sababu za msingi kuwa ametenda kosa lolote atalazimika kumuarifu mtu huyo haki yake ya dhamana chini ya kifungu hiki.

Vigezo vya kutoa dhamana ya polisi.

65. Mambo ya kuzingatia katika utoaji wa dhamana unaofanywa na afisa polisi kwa mtu anayeshitakiwa kwa kosa ni:-

- (a) uwezekano wa mtu kuhudhuria mahakamani kuhusiana na kosa kama atapewa dhamana, hii ni kusema:-
 - (i) historia yake na mshikamano wake na jamii au makazi, ajira na hali ya kifamilia na rekodi yake ya polisi, kama inajulikana, na
 - (ii) mazingira ambao kosa lilitendeka, asili na ukubwa wa kosa, uzito wa ushahidi dhidi ya mtu huyo na taarifa nyingine zinazohusiana na uwezekano wake wa kutoroka;
- (b) maslahi ya mtu huyo, hii ni kusema-
 - (i) kipindi ambacho mtu huyo anaweza kulazimika kuwa mahabusu kama dhamana itakataliwa, na masharti ambayo atashikiliwa mahabusu;
 - (ii) mahitaji ya mtu kuwa huru akijitayarisha kuhudhuria mbele ya mahakama, kupata ushauri wa kisheria na kwa madhumuni mengine; au
 - (iii) umuhimu wa mtu huyo kupata hifadhi ya mwili, hata kama umuhimu huo unajitokeza kwa sababu ya kutojiweza kutokana na ulevi, maumivu au matumizi ya madawa au unatokana na sababu zingine; na
- (c) hifadhi ya jamii, hii ni kusema, uwezekanao wa mtu huyo kuingilia ushahidi kwa kuwatisha mashahidi au kuzuia uchunguzi wa polisi kwa jinsi yoyote ile.

Masharti ya dhamana ya polisi.

66. Mtu atakuwa na haki ya kupata dhamana ya polisi kama:-

- (a) anaahidi kwa maandishi kuhudhuria mbele ya mahakama iliyotajwa katika muda na mahali palipotajwa, au katika muda mwingine na mahali kama atakavyoarifiwa na afisa polisi;
- (b) anaahidi kwa maandishi kuzingatia masharti yatakayotajwa kuhusiana na mwenendo wake wakati ameachiwa kwa dhamana, masharti yasiyohusiana na utoaji wa dhamana, kuweka fedha au kutaifisha fedha;

- (c) mtu mwingine anayekubalika na afisa polisi anakiri kwa maandishi, kwamba anamfahamu mtu anayeshitakiwa na anamtambua kuwa ni mtu anayewajibika ambaye anaweza kuhudhuria mahakamani kujibu mashitaka;
- (d) mtu anayeshitakiwa, au mtu mwingine anayekubalika kwa afisa polisi, anaingia kwenye makubaliano, akiwa na dhamana au bila dhamana, kutaifishwa kiasi cha fedha iliyotajwa iwapo mtu aliyeshitakiwa atashindwa kuhudhuria mahakamani kujibu mashitaka; au
- (e) mtu anayeshitakiwa, au mtu mwingine anayekubalika kwa afisa polisi, anaweka kwa afisa polisi, kiasi Fulani cha fedha kilichotajwa kitakachotaifishwa iwapo mtu aliyeshitakiwa atashindwa kuhudhuria mahakamani kujibu mashitaka.

Kukataa kutoa dhamana ya polisi.

67.-(1) Pale afisa polisi anakataa kutoa dhamana atalazimika kurekodi kwa maandishi sababu za kukataa huko.

(2) Pale afisa polisi anakataa, chini ya kifungu cha 64, kutoa dhamana kwa mtu aliyeshitakiwa kwa kosa, au anatoa dhamana lakini mtu huyo hawezi au hataki kufuata, au kupanga mtu mwingine kufuata, masharti yoyote ambayo dhamana imetolewa kwayo, mtu huyo atalazimika kupelekwa mbele ya hakimu kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria mapema iwezekanavyo na si zaidi ya kikao cha kwanza cha mahakama katika sehemu ambayo inawezekana kumpeleka mtu huyo kwa dhumuni hilo.

(3) Mtu anayesubiri kwenye mahabusu kupelekwa mbele ya hakimu kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) anaweza, katika muda wowote, kumuomba afisa polisi kumpatia nyenzo kwa ajili ya kufanya maombi ya dhamana kutoka kwa hakimu na, kama anafanya hivyo, afisa polisi atalazimika, ndani ya saa ishirini na nne, au katika muda mwingine wa kutosha kadri inavyowezekana baada ya kufanya maombi, kumpeleka mbele ya hakimu.

Kutengua dhamana ya polisi
Sheria Na. 5 ya 1988
kif.5

68. Pale afisa polisi msimamizi wa kituo cha polisi anaamini kwa sababu za msingi kwamba mtu aliyeachiwa kwa dhamana chini ya kifungu cha 64:-

- (a) anatoroka; au
- (b) ameshindwa kufuata, au anataka au anaweza kushindwa kufuata ahadi aliyoitoa kama sharti la kuachiwa,

afisa polisi anaweza kufuta dhamana na baada ya hapo mtu huyo anaweza kukamatwa tena na afisa polisi.

Ukiukwaji wa masharti ya dhamana
Sheria Na. 9 ya 1996
jedwali

69.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2) pale mtu aliyeachiwa kwa dhamana iliyotolewa na afisa polisi kwa makusudi na bila sababu ya msingi anashindwa kutekeleza ahadi aliyoitoa kama sharti la kuachiwa kwake, atakuwa anatenda kosa na atawajibika, kama

akitiwa hatiani, kwa adhabu isiyoziidi adhabu ya juu ambayo angeweza kupewa iwapo angetiwa hatiani kwa kosa linalohusiana na kukamatwa kwake na kisha kuachiwa kwa dhamana.

(2) Pale mtu aliyeachiwa kwa dhamana iliyotolewa na afisa polisi kuhusiana na makosa mawili au zaidi kwa makusudi au bila ya sababu ya msingi anashindwa kutimiza ahadi aliyoitoa kama sharti la kuachiwa kwake, kifungu kidogo cha (1) kitatumika kama vile kosa ambalo aliachiwa kwa dhamana ni kosa ambalo ameshindwa kutimiza ahadi au kama ameshindwa kutimiza ahadi kuhusiana na makosa mawili au zaidi, kwa kosa ambalo ni zito au kubwa zaidi.

SEHEMU TATU
UZUIAJI WA MAKOSA

(a) Dhamana kwa kulinda amani na kwa tabia njema

Uwezo wa hakimu
kumtaka mtu
kutekeleza dhamana

70.-(1) Wakati ambapo hakimu anataarifiwa kwa kiapo kwamba mtu yeyote anaweza kutenda kosa la uvunjifu wa amani au kuvuruga utulivu wa umma au kufanya jambo lolote baya ambalo linaweza kusababisha uvunjifu wa amani au kuvuruga utulivu wa umma, hakimu anaweza, kwa jinsi ilivyoonyeshwa kwenye sehemu hii, kumtaka mtu huyo kuonyesha sababu kwa nini asiamuriwe kuweka dhamana, akiwa na au bila wadhamini, kwa kulinda amani kwa muda, usiozidi mwaka mmoja, kama hakimu atakavyoona inafaa.

(2) Mashtaka hayatafunguliwa chini ya kifungu hiki isipokuwa kwamba aidha mtu aliyetolewa taarifa au sehemu ambayo uvunjifu wa amani au vurugu inategemewa ni ndani ya eneo la mipaka ya mamlaka ya hakimu.

Dhamana ya tabia
njema kutoka kwa
watu wanaosambaza
mambo ya
uchochezi.
Sheria Na. 5 ya 1998
kif. 6

71. Wakati wowote ambapo hakimu anataarifiwa kwa kiapo kwamba kuna mtu yupo ndani ya mipaka ya mamlaka yake na kwamba mtu huyo, anasambaza au anajaribu kusambaza au kwa njia nyingine anasaidia kusambaza, ndani au nje ya mipaka hiyo kwa mdomo au kwa maandishi au kwa njia nyingine:-

- (a) jambo lolote za uchochezi, hii ni kusema, jambo lolote ambalo uchapishaji wake unaadhibiwa chini ya kifungu cha 32 cha Sheria ya Magazeti;
- (b) jambo lolote linalomhusu jaji au hakimu ambalo ni kashfa chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu;

Sura 16

hakimu anaweza, kwa utaratibu uliowekwa katika sehemu hii, kumtaka mtu huyo kuonyesha sababu kwanini asiamuriwe kuweka dhamana akiwa na au bila ya wadhamini kuonyesha tabia njema kwa muda fulani, usiozidi mwaka mmoja, kama hakimu atakavyoona inafaa.

Dhamana ya tabia
njema kutoka kwa
watu waliotuhumiwa

72. Wakati ambapo hakimu anataarifiwa chini ya kiapo kwamba mtu yeyote anachukua tahadhari kujificha asionekane ndani ya mipaka ya mamlaka ya hakimu, na kwamba kuna sababu kuamini

kwamba mtu huyo anachukua tahadhari hizo kwa nia ya kutenda kosa, hakimumu anaweza, kwa utaratibu uliotolewa kwenye sehemu hii, kumtaka mtu huyo kuonyesha sababu kwanini asiamuriwe kuweka dhamana akiwa na wadhamini kuonyesha tabia njema kwa muda fulani, usiozidi mwaka mmoja, kama hakimumu atakavyoona inafaa

Dhamana ya tabia njema kutoka kwa wahalifu wazoeifu.

73. Wakati ambapo hakimumu anataarifiwa kwa kiapo kwamba mtu yeyote ndani ya mipaka ya mamlaka yake—

- (a) kitabia ni jambazi, mvunja nyumba au mwizi;
- (b) kitabia ni mpokeaji vitu vilivyoibwa, akijua kuwa vimeibwa;
- (c) kitabia anawalinda au anawahifadhi wezi, au anasaidia katika kuficha au kuuza vitu vilivyoibwa;
- (d) kitabia anatenda au anajaribu kutenda, au anasaidia au anashiriki katika kutenda, kosa lolote linaloadhibiwa chini ya Sura za XXX, XXXIII na XXXIV za Sheria ya Kanuni za Adhabu;
- (e) kitabia anatenda au anajaribu kutenda, au anasaidia au anashiriki katika kutenda, kosa linalohusiana na uvunjifu wa amani; au
- (f) ni mzururaji au kibaka; au
- (g) yuko tayari kufanya lolote na ni hatari kumruhusu kumwacha huru bila ya kujulikana alipo na bila ya kuweka dhamana itakuwa ni hatari katika jamii,

hakimumu anaweza, kwa utaratibu uliowekwa katika Sehemu hii, kumtaka mtu huyo kuonyesha sababu kwanini asiamuriwe kuweka dhamana akiwa na wadhamini kuonyesha tabia njema kwa muda fulani, usiozidi mwaka mmoja, kama hakimumu atakavyoona inafaa.

Sura 16

Amri kutolewa.

74. Wakati ambapo hakimumu anatenda chini ya vifungu vya 70, 71, 72 au 73 vya Sheria hii anaona ni muhimu kumtaka mtu yeyote kuonyesha sababu chini ya vifungu hivyo, atalazimika kutoa amri kwa maandishi akiainisha bayana:—

- (a) kiini cha taarifa iliyopokelewa;
- (b) kiasi cha dhamana kitakachotolewa;
- (c) kipindi ambacho dhamana inatumika; na
- (d) idadi, tabia na daraja la wadhamini, kama wapo, wanaohitajika.

Utaratibu kuhusu mtu kuwepo mahakamani.

75. Iwapo mtu ambaye amri inatolewa dhidi yake yupo mahakamani, italazimika kusomwa kwake au kama atahitaji hivyo, kiini cha amri hiyo kitaelezwa kwake.

Utaratibu kuhusu kutokuwepo mahakamani.

76.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), iwapo mtu ambaye amri imetolewa dhidi yake hayupo mahakamani, hakimumu atalazimika kutoa wito kumtaka kuhudhuria au, kama mtu huyo yupo

kizuizini, hati itatolewa ikimtaka afisa ambaye mtu huyo yupo chini ya kizuizini chake kumleta mbele ya mahakama.

(2) Wakati ambapo inaonekana kwa hakimu, kufuatia ripoti ya afisa polisi au kufuatia taarifa iliyotolewa kwa kiapo (kiini cha ripoti au taarifa kitalazimika kurekodiwa na hakimu), kwamba kuna sababu za kuhisi uvunjifu wa amani, na kwamba uvunjifu huo wa amani hauwezi kuzuilika kwa njia yoyote isipokuwa kwa kumkamata haraka mtu huyo, hakimu anaweza katika muda wowote kutoa hati ya kumkamata.

Nakala ya amri kuambatanishwa na wito au hati.

77. Kila wito au hati itakayotolewa chini ya kifungu cha 76 itaambatana na nakala ya amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 74, na kwamba nakala hiyo itapelekwa na afisa anayepeleka au anayetokeleza wito au hati kwa mtu aliyepelekeka au aliyekamatwa chini ya hati.

Uwezo wa kutohitaji mahudhuria binafsi.

78. Hakimu tofauti na hakimu wa mahakama ya mwanzo anaweza, iwapo anaona kuna sababu ya kutosha, kuacha kumtaka kuhudhuria binafsi kwa mtu yoyote aliyeitwa kuonyesha sababu kwanini asiamuriwe kuweka dhamana ya kulinda amani na anaweza kumruhusu kuhudhuria kupitia wakili wake.

Uchunguzi wa ukweli wa taarifa.

79.(1) Pale amri chini ya kifungu cha 74 imesomwa au kufafanuliwa chini ya kifungu cha 75 kwa mtu aliyepo mahakamani, au wakati mtu yeyote amehudhuria au ameletwa mbele ya hakimu kufuatana na au katika kutekeleza wito au hati iliyotolewa chini ya kifungu cha 76, hakimu atalazimika kuendelea kuchunguza kuhusu ukweli wa taarifa ambayo imesababisha hatua kuchukuliwa, na kuchukua ushahidi mwingine kama itakavyoonekana ni muhimu.

Sura 11

(2) Uchunguzi chini ya kifungu kidogo cha (1) utafanywa, kwa karibu kadri inavyowezekana, katika namna iliyoelezwa na au chini ya Sheria hii au Sheria ya Mahakimu wa Mahakama, kwa usikilizaji wa mashitaka na kurekodi ushahidi katika usikilizaji mashitaka mbele ya mahakama za chini au mahakama za mwanzo.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki kuhusu kwamba masharti ya kifungu cha 73 yanatumika kwa mtu fulani unaweza kuthibitishwa na ushahidi wa hadhi ya mtu kwa ujumla au kwa ushahidi mwingine wowote.

(4) Kama watu wawili au zaidi wamehusishwa kwa pamoja katika jambo lililo chini ya uchunguzi, wanaweza kushughulikiwa katika uchunguzi wa pamoja au uchunguzi tofauti kama hakimu atakavyoona ni haki.

Amri ya kuweka dhamana.

80.(1) Iwapo baada ya uchunguzi imethibitika kwamba ni muhimu kulinda amani au kuonyesha tabia njema, kama itakavyokuwa, mtu ambaye anafanyiwa uchunguzi atatakiwa kuweka

dhamana, akiwa na au bila ya wadhamini, na hakimu atatoa amri mara moja, isipokuwa kwamba:–

- (a) hakuna mtu atakayelazimika kutoa dhamana ya aina tofauti na, au ya kiasi kikubwa kuliko, au kwa kipindi kirefu kuliko kile kilichotajwa kwenye amri liliyotolewa chini ya kifungu cha 74;
- (b) kiasi cha dhamana yoyote kitawekwa kwa kuzingatia mazingira ya kesi na hakitapaswa kuwa kikubwa mno;
- (c) pale ambapo mtu anayechunguzwa ni mtoto, dhamana itatolewa na wadhamini wake tu.

(2) Mtu yoyote aliyeamuriwa kutoa dhamana kulinda amani au kuonyesha tabia njema chini ya kifungu hiki anaweza kukata rufaa Mahakama Kuu au Mahakama ya Wilaya, na masharti ya Sehemu ya X ya Sheria hii (kuhusiana na rufaa) au Shemu ya III ya Sheria ya Mahakimu wa Mahakama, kama itakavyokuwa, yatatumika katika kila rufaa hiyo.

Sura 11

Kuachiwa kwa watu ambao taarifa imetolewa dhidi yao.

81. Iwapo baada ya uchunguzi chini ya kifungu cha 79, haijathibitika kwamba ni muhimu kwa kulinda amani au kuonyesha tabia njema, kama itakavyokuwa, kwamba mtu anayechunguzwa atoe dhamana, hakimu atalazimika kuingiza katika rekodi yake hali hiyo, na kama mtu yuko mahabusu kwa madhumuni hayo tu, atamtoa, au kama hayuko mahabusu, atamwachia.

(b) Mwenendo baada ya Amri ya kuweka dhamana

Kuanza kwa muda ambao dhamana inahitajika.

82.-(1) Iwapo mtu ambaye amri ya kutoa dhamana imetolewa dhidi yake chini ya kifungu cha 74 au kifungu cha 80 atakuwa, wakati amri inatolewa, amehukumiwa kifungo au anatumikia adhabu ya kifungo, muda ambao dhamana inahitajika utanza baada ya kuisha kwa kifungo.

(2) Wakati mwingine kipindi ambacho dhamana inahitajika utanza katika tarehe ya amri isipokuwa kama hakimu, kwa sababu za kutosha, ameweka tarehe ya baadaye,

Yaliyomo kwenye dhamana.

83. Dhamana itakayotolewa na mtu yeyote itambana mtu huyo kulinda amani au kuonyesha tabia njema, kama itakavyokuwa, kama ni kuonyesha tabia njema kutendo au kujaribu kutenda au kusaidia, kushiriki, kutoa ushauri au kupanga kutenda kosa lolote linaloadhibiwa kwa adhabu ya kifungo, popote litakapotendeka, itakuwa ni uvunjaji wa dhamana.

Uwezo wa kukataa wadhamini.

84. Hakimu anaweza kumkataa mdhamini yeyote anayetolewa chini ya kifungu chochote kilichopita kwa msingi kwamba, kwa sababu zitakazorekodiwa na hakimu, mdhamini huyo ni mtu asiyefaa.

Utaratibu kutokana na kushindwa dhamana.

85.-(1) Iwapo mtu yeyote aliyeamriwa kutoa dhamana hatatoa dhamana hiyo katika tarehe au kabla ya tarehe ya kipindi ambacho dhamana inayotakiwa kutolewa kuanza, atalazimika, isipokuwa katika mazingira yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2), kuchukuliwa kwenda gerezani au, kama tayari yuko gerezani, kushikiliwa kwenye hilo gereza mpaka muda utakapoisha au ndani ya kipindi hicho anaweza dhamana mahakamani au kwa hakimu aliyetoa amri kutaka dhamana hiyo.

(2) Pale mtu ameamriwa na hakimu kutoa dhamana kwa muda unaozidi mwaka mmoja, hakimu atalazimika, iwapo mtu hatatoa dhamana, kutoa hati kuelekeza kwamba ashikiliwe gerezani akisubiri amri ya Mahakama ya Wilaya au Mahakama Kuu, kama itakavyokuwa, na italazimika ndani ya kipindi cha mwezi mmoja kuwasilisha mwenendo haraka iwezekanavyo mbele ya mahakama hiyo.

(3) Mahakama ya Wilaya au Mahakama Kuu kama itakavyokuwa, baada ya kuchunguza mwenendo na kutaka kutoka kwa hakimu taarifa yoyote nyingine au ushahidi ambao itaona ni muhimu, inaweza kutoa amri yoyote kadri itakavyoona inafaa.

(4) Kipindi ambacho, ambao mtu amefungwa kwa kushindwa kutoa dhamana hakitazidi miaka mitatu.

(5) Iwapo dhamana itapelekwa kwa afisa msimamizi wa gereza, atalazimika mara moja kupeleka suala hilo mahakamani au kwa hakimu aliyetoa amri na kusubiri amri ya mahakama hiyo au hakimu.

Uwezo wa kuwaachia watu waliofungwa kwa kushindwa kuweka dhamana.

86. Wakati ambapo hakimu wa wilaya ana maoni kuwa mtu yeyote aliyefungwa kwa kushindwa kutoa dhamana anaweza kuachiwa bila madhara mabaya kwa jamii, atatakiwa kutoa taarifa ya haraka kuhusiana na kesi kwa ajili ya amri ya Mahakama Kuu, ambayo inaweza, kama itaona inafaa, kuamuru mtu huyo kuachiwa.

Uwezo wa Mahakama Kuu kufuta dhamana.

87. Mahakama Kuu inaweza, katika muda wowote, kwa sababu za kutosha zitakazorekodiwa kwa maandishi, kufuta dhamana yoyote kwa ajili ya kutunza amani au kuonyesha tabia njema iliyowekwa chini ya Sehemu hii kwa amri ya mahakama yoyote.

Kuachiwa kwa wadhamini.

88.-(1) Mdamini yeyote aliyeweka dhamana kwa ajili ya mtu mwingine kulinda amani au kuonyesha tabia njema anaweza katika muda wowote kuomba kwa hakimu kufuta dhamana yoyote iliyowekwa chini ya vifungu vilivyotangulia ndani ya mipaka ya mamlaka yake.

(2) Kufuatia maombi yaliyofanywa, hakimu atalazimika kutoa wito wake au hati, kama atakavyoona inafaa, kumtaka mtu ambaye mdhamin anawajibika kwake kuhudhuria au kuletwa mbele yake.

(3) Pale ambapo mtu anahudhuria au analetwa mbele ya hakimu, hakimu atafuta dhamana na atalazimika kumwamuru kutoa, kwa sehemu ya muda uliobaki wa dhamana, dhamana mpya ya aina ileile na dhamana ya mwanzo, na kila amri kwa madhumuni ya vifungu vya 83, 84, 85 na 86 itahesabika kuwa ni amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 80.

SEHEMU YA NNE
USIMAMIZI WA MWENENDO WA JINAI

A. – Mkurugenzi ya Mashtaka

Imefutwa

89. [Imefutwa na Sheria Na.5 ya 2005, Jedwali.].

Imefutwa

90. [Imefutwa na Sheria Na.27 ya 2008, Kifungu cha 31].

Uwezo wa
Mkurugenzi wa
Mashtaka kufuta
mashtaka.

91.-(1) Katika kesi yoyote ya jinai na katika hatua yoyote ile kabla ya hukumu au uamuzi, kama itakavyokuwa, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuweka *nolle prosequi*, aidha kwa kueleza mahakamani au kwa kuiambia mahakama husika kwa maandishi kwa niaba ya Jamhuri kuwa mwenendo hautaendelea; na baada ya hapo mtuhumiwa ataachiwa mara moja kuhusiana na shtaka ambalo *nolle prosequi* imewekwa na kama amepolekwa gerezeni atatakiwa kuachiwa, au kama yuko chini ya dhamana wadhamini wake watakoma kuwa wadhamini; lakini kuachiwa huko kwa mtuhumiwa hakutachukuliwa kama kizuizi kwa mashtaka mengine ya baadaye dhidi yake kwa kutumia maelezo hayo hayo.

(2) Iwapo mtuhumiwa hayupo mbele ya mahakama wakati *nolle prosequi* inawekwa, msajili au karani wa mahakama atatakiwa mara moja kuhakikisha notisi ya maandishi ya kuwekwa kwa *nolle prosequi* inapelekwa kwa mtunzaji wa gereza ambamo mtuhumiwa anaweza kuwa anazuiwa na kama mtuhumiwa amepolekwa kwa kusikiliza shauri, kwa mahakama ya chini ambako ndiko alikosikilizwa na mahakama hiyo italazimika mara moja kuhakikisha notisi kama hiyo ya maandishi anapewa shahidi yeyote anayewajibika kutoa ushahidi na kwa wadhamini wake (kama wapo) na vilevile kwa mtuhumiwa na wadhamini wake kama alishatolewa kwa dhamana.

Ukaimishaji wa
uwezo wa
Mkurugenzi wa
Mashtaka.

92.-(1) Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuamuru kwa maandishi kwamba mamlaka yote au mamlaka yoyote uliotwikwa kwake na kifungu cha 91 na Sehemu ya VII ya Sheria hii inaweza kutekelezwa na Maafisa Sheria, Wakili wa Serikali, au Mwandishi wa Sheria na utekelezaji wa mamlaka hayo na yeyote kati yao utachukuliwa kama vile umetekelezwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza, kwa maandishi, kufuta amri yoyote aliyoitoa chini ya kifungu hiki.

Taarifa za jinai za
Mkurugenzi wa
Mashtaka Sheria Na.
5 ya 1988 kif. 7

93.-(1) Bila kujali kitu chochote kilichopo katika Sheria hii, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza, kwa ruhusa ya Rais, kuonyesha Mahakama Kuu, dhidi ya watu walio kwenye mamlaka hiyo taarifa kwa madhumuni ambayo Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuonyesha taarifa kwa niaba ya Jamhuri katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

(2) Mwenendo huo unaweza kuchukuliwa kwa taarifa yoyote itakayoonyeshwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

(3) Mahakama Kuu inaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya kutekeleza masharti ya kifungu hiki.

Makosa ya wageni
yaliyotendeka ndani
ya mipaka ya maji ya
nchi kuendeshwa
kwa ruhusa ya
Mkurugenzi wa
Mashtaka tu

94.-(1) Kwa kuzingatia masharti mengine ya kifungu hiki, mashtaka ya mtu yeyote ambaye si raia wa Jamhuri ya Muungano kwa kosa lililotendeka baharini kwa kipimo cha maji maili mia mbili za pwani ya Jamhuri ya Muungano zikipimwa kutoka kina cha chini cha maji hayatafunguliwa katika mahakama yoyote isipokuwa kwa idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kwa kibali chake kwamba ni muhimu mashtaka hayo yafunguliwe.

(2) Mwenendo mbele ya mahakama za chini kabla ya kuhamishwa kwa ajili ya kusikilizwa kwa mtuhumiwa na mahakama za juu au kuamuliwa na mahakama kwamba mtuhumiwa anatakiwa kuwekwa kwenye shauri la kusikilizwa hautachukuliwa kuwa ni usikilizwaji wa mashtaka ya kosa lililotendwa na mtuhumiwa kwa madhumuni ya ridhaa na kibalichini ya kifungu hiki.

(3) Haitakuwa lazima kueleza kwenye shitaka lolote kuwa ridhaa au kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka kinachotakiwa na kifungu hiki kimetolewa, na ukweli kwamba ridhaa au kibali vimetolewa atadhaniwa hivyo isipokuwa kama vitapingwa na mtuhumiwa wakati wa kusikiliza shauri.

(4) Utoaji wa nyaraka unayodhaniwa kuwa umesainiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ukiwa na ridhaa na kibali vitakuwa ni ushahidi wa kutosha, kwa madhumuni ya kifungu hiki, kuwa ni ridhaa na kibali vinachotakiwa na kifungu hiki.

(5) Kifungu hiki hakitaathiri au kudhuru usikilizaji wa mashtaka ya kitendo chochote cha uharamia kama kilivyofafanuliwa na Sheria za Kimataifa.

(6) Neno “kosa” kama lilivyotumika kwenye kifungu hiki maana yake ni kitendo, uzembe au kushindwa kwa aina iliyotajwa ambako, iwapo kingetendeka katika sehemu yoyote ya nchi ya Jamhuri ya Muungano, vitaadhibiwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania zinazotumika kwa wakati huu.

B. – Uteuzi wa Waendesha Mashtaka na Uendeshaji Mashtaka

Imefutwa

95. [Ilifutwa na Sheria Na. 27 ya 2008].

Imefutwa

96. [Ilifutwa na Sheria Na. 27 ya 2008].

Uwezo wa
Waendesha mashtaka

97. Mwendesha mashtaka wa Serikali anaweza kwenda na kuongea bila idhini yoyote ya maandishi mbele ya mahakama yoyote ambako kesi yoyote anayoismamia ipo katika uchunguzi, kusikilizwa au rufaa; na kama mtu binafsi amemweka wakili kuendesha mashtaka katika kesi ya aina hiyo mwendesha mashtaka wa Serikali anaweza kuendesha mashtaka na wakili aliyewekwa atatakiwa kufuata maelekezo yake.

Kuondolewa kwa
mashtaka katika
mahakama za chini.

98. Katika shtaka lolote lililopo mbele ya mahakama ya chini mwendesha mashtaka wa Serikali anaweza kwa idhini ya mahakama au kwa maelezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka, katika muda wowote kabla hukumu haijasomwa, kumuondolea mashtaka mtu yeyote aidha kwa ujumla au kuhusiana na kosa moja au zaidi ambalo mtu huyo ameshitakiwa kwalo; na baada ya kuondolewa huko–

- (a) Iwapo kutafanywa kabla mtuhumiwa hajaitwa kutoa utetezi wake, atatakiwa kuachiwa huru, lakini kuachiwa huko kwa mtuhumiwa hakutahesabika kuwa ni kuzuizi kwa mashtaka mengine baadaye kuhusiana na maelezo yale yale;
- (b) Iwapo kutafanywa baada ya mtuhumiwa kuitwa kutoa utetezi wake, ataachiwa huru.

Ruhusa ya kuendesha
mashtaka na na jina
la mwenendo wa
mashtaka kwa
muhtasari.

99.-(1) Hakimu yeyote anayechunguza undani au anayesikiliza kesi yoyote anaweza kuruhusu mashtaka kuendeshwa na mtu yeyote, lakini hakuna mtu zaidi ya mwendesha mashtaka wa Serikali au afisa mwingine ambaye kwa ujumla au mahususi ameruhusiwa na Rais kwa niaba hiyo atakuwa na haki ya kuendesha mashtaka bila ya kibali hicho.

(2) Mtu yeyote au afisa aliyerejewa katika kifungu kidogo cha (1) atakuwa na uwezo sawa wa kuondoa mashtaka kama ilivyotolewa katika kifungu cha 98, na masharti ya kifungu hicho yatatumika kwa kila ondoleo lililofanywa na mtu huyo au afisa.

(3) Mtu yeyote anayeendesha mashtaka anaweza kufanya hivyo yeye mwenyewe au kwa kutumia wakili.

(4) Katika shauri la muhtasari, iwapo mwendesha mashtaka ni mtu binafsi, jina lake litaonekana kwenye kichwa cha mwenendo kama mwendesha mashtaka na, iwapo mwendesha mashtaka ni afisa polisi, itatosheleza iwapo, katika kichwa cha mwenendo, mwendesha mashtaka ametajwa kama Inspekta Jenerali wa Polisi.

SEHEMU YA TANO

UFUNGUAJI WA MASHTAKA

A. – Utaratibu wa kulazimisha mahudhurio kwa watuhumiwa

(a) Wito

Muundo na yaliyomo
kwenye wito

100.-(1) Kila wito unaotolewa na mahakama chini ya Sheria hii utatakiwa kuwa kwa maandishi, katika nakala mbili, zilizosainiwa na kugongwa mhuri na afisa wa mahakama au na afisa mwingine yeyote kama Mahakama Kuu itakavyoweza, anayeongoza usikilizaji wa kesi mara kwa mara kuelekeza kwa kanuni.

(2) Kila wito utaelekezwa kwa mtu anayeitwa na utamtaka kuhudhuria katika muda na mahali ilivyoonyeshwa katika wito mbele ya mahakama yenye mamlaka ya kuchunguza, kusikiliza kosa linalosemekama kuwa limetendwa na utaeleza kwa ufupi kosa ambalo kwalo mtu ambaye wito unatolewa dhidi yake anashitakiwa.

Uwasilishaji wa
wito.

101.-(1) Kila wito utawasilishwa na afisa polisi au na afisa wa mahakama iliyotoa wito huo au mtumishi mwingine wa umma au mtu yeyote mwingine kama mahakama itakavyoelekeza na, kama inawezekana, kuwasilishwa binafsi kwa mtu anayeitwa kwa kupeleka au kufikisha kwake nakala mojawapo ya wito.

(2) Kila mtu ambaye wito umewasilishwa kwake, kama atatakiwa na afisa anayempelekea, atasaini kukiri kupokea nyuma ya nakala nyingine.

Uwasilishaji pale
mtu anayeitwa hawezi
kupatikana.

102. Iwapo mtu aliyetwa hawezi kupatikana hata kwa kufanya jitihada zote, wito unaweza kuwasilishwa kwa kuacha nakala moja ya wito kwa ajili yake kwa mwanafamilia ambaye ni mtu mzima au kwa mfanyakazi mtu mzima anayeishi naye au mwajiri wake; na mtu atakayeachiwa wito huo, iwapo atatakiwa na afisa aliyempelekea, atasaini kukiri kupokea nyuma ya nakala nyingine.

Utaratibu pale
uwasilishaji hauwezi
kufanyika kwa mtu
mwenyewe.

103. Iwapo uwasilishaji kwa njia iliyotajwa na kifungu cha 101 au 102 hauwezi kufanyika kwa jitihada zote, afisa anayewasilishisha atabandika nakala moja ya wito katika sehemu yoyote ya wazi ya nyumba au makazi ambapo mtu anayeitwa kwa kawaida anaishi na baada ya hapo wito utachukuliwa kuwa umewasilishwa sawasawa.

Uwasilishaji kwa
mtumishi wa
Serikali.

104. Iwapo mtu aliyetwa yupo kwenye utumishi wa idara ya Serikali au shirika la umma, mahakama inayotoa wito italazimika wakati wote kupeleka nakala kwa mkuu wa idara au shirika la umma, kama itakavyokuwa, ambako mtu huyo ameajiriwa, na mkuu atahakikisha wito umewasilishwa kwa namna iliyowekwa na kifungu cha 101 na atairudisha mahakamani chini ya saini yake pamoja na idhinisho kama inavyohitajika na kifungu hicho.

Uwasilishaji kwenye kampuni

105. Kuwasilishwa kwa wito kwenye kampuni iliyosajiliwa unaweza kufanywa kwa kupeleka kwa katibu, meneja mwenyeji au afisa mwingine mwandamizi wa kampuni katika ofisi iliyosajiliwa ya kampuni hiyo au kwa barua iliyosajiliwa iliyoelekezwa kwa afisa mtendaji mkuu wa kampuni na katika suala la barua iliyosajiliwa, uwasilishwaji utachukuliwa kuwa umefanyika wakati barua imefika katika njia ya kawaida ya posta.

Mahudhurio kwa kampuni na kuandika kukana kosa wakati mwakilishi hajahudhuria.

106. Pale, katika shauri la shirika, mwakilishi hakuhudhuria katika muda ulitotajwa na wito au taarifa au kama mwakilishi huyo amehudhuria lakini ameshindwa kujibu shtaka, mahakama itaamuru jibu la ‘kukana kosa’ kuandikwa na shauri litaendelea kama vile shirika limetoa jibu la kukana kosa.

Uwasilishaji nje ya mipaka ya mamlaka ya mahakama.

107. Iwapo mahakama itataka kwamba wito uliotolewa na mahakama uwasilishwe katika sehemu yoyote nje ya mipaka ya mamlaka yake, itapeleka wito katika nakala mbili kwa hakimu mwenye mamlaka katika mpaka ambako mtu anayeitwa anaishi au atakaewasilishiwa.

Uthibitisho wa uwasilishaji wakati afisa aliyepeleka hayupo.

108. Pale afisa aliyewasilisha wito hayupo mahakamani wakati wa kusikiliza kesi, na wakati wowote ambapo wito uliotolewa na mahakama uliwasilishwa nje ya mipaka ya mamlaka yake, kiapo kinachodhaniwa kufanywa mbele ya hakimu kuwa wito huo umewasilishwa, na nakala ya wito inayodhaniwa kuidhinishwa, kwa namna iliyowekwa na Sheria hii, na mtu aliyepelekewa au kupokea au ambaye aliachiwa, kitakubaliwa kama ushahidi na maelezo yaliyotolewa ndani yake yatachukuliwa kuwa ni sahihi isipokuwa ikithibitishwa vinginevyo.

Mahudhurio ya kampuni.

109.-(1) Mahudhurio mbele ya mahakama kwa shirika yatakuwa kwa njia ya wakili au afisa yeyote wa shirika.

(2) Bila ya kujali kitu chochote kilichoko kwenye ibara za usajili, sheria ndogo au nyaraka nyingine zinazotawala kuundwa kwa shirika, na bila ya kujali kitu chochote katika sheria nyinginezo zilizoko, afisa wa shirika anayehudhuria mbele ya mahakama kwa niaba ya shirika chini ya masharti ya kifungu hiki atachukuliwa kuhudhuria hivyo akiwa na madaraka kamili ya shirika na kuwa na madaraka yote kuiwakilisha shirika.

(3) Katika kifungu hiki na katika kifungu cha 111, “afisa” kuhusiana na shirika inamaanisha mkurugenzi yeyote, mjumbe yeyote wa bodi ya utawala kwa jina lolote au staili iliyowekwa, meneja mwenyeji au afisa mwandamizi wa shirika na katibu.

(b) Hati ya Ukamataji

Hati baada ya kutolewa wito.

110. Bila ya kujali utolewaji wa wito, hati inaweza kutolewa katika muda wowote kabla au baada ya muda ulioonyeshwa kwenye wito wa kuhudhuria kwa mtuhumiwa lakini hakuna hati itakayotolewa isipokuwa kama malalamiko yametolewa kwa kiapo au na afisa polisi au afisa aliyeidhinishwa wa mamlaka ya serikali za mitaa.

Kutotii wito.

111.-(1) Iwapo mtuhumiwa, tofauti na shirika, hatahudhuria katika muda na mahali palipotajwa kwenye wito na kuhudhuriwa kwake binafsi hakujasamehewa chini ya kifungu cha 193, mahakama inaweza kutoa hati ya kukamatwa kwake na kuhakikisha anapelekwa mbele ya mahakama.

(2) Iwapo mtuhumiwa, akiwa ni shirika, hajahudhuria kwa namna iliyowekwa na kifungu cha 109, mahakama inaweza kuamuru afisa yoyote wa shirika kuletwa mbele yake kwa namna iliyowekwa na Sheria hii ya kulazimisha mahudhurio ya mashahidi.

(3) Hakuna hati ya kukamatwa itakayotolewa chini ya kifungu hiki isipokuwa kama malalamiko yamefanywa kwa kiapo au na afisa polisi au mtu mwingine aliyeidhinishwa wa mamlaka ya serikali za mitaa.

(4) Hakuna kitu katika kifungu hiki kitaathiri uwezo wa mahakama kushughulikia kesi yoyote bila ya kuwepo kwa mtuhumiwa, kwa namna iliyowekwa na kifungu cha 193, bila kujali mtuhumiwa ni mtu binafsi au shirika.

Muundo, yaliyomo na muda wa hati ya ukamataji.

112.-(1) Kila hati ya kukamatwa itatolewa chini ya mkono wa jaji au hakimu aliyetoa hati hiyo na itakuwa na mhuri wa mahakama.

(2) Kila hati ya kukamatwa itaeleza kwa ufupi kosa ambalo kwalo mtu ambaye hati inatolewa dhidi yake anashitakiwa na itataja au kumuelezea mtu huyo, na itaamuru mtu au watu ambao imeelekezwa kwao kumkamata mtu ambaye imetolewa dhidi yake na kumleta mbele ya mahakama iliyotoa hati au mbele ya mahakama nyingine yenye mamlaka na kesi hiyo kujibu shtaka lililotajwa katika hati na kushughulikiwa zaidi kwa mujibu wa sheria.

(3) Kila hati itaendelea kutumika muda wote mpaka itakapotekelezwa au mpaka itakapofutwa na mahakama ambayo iliitoa.

Uwezo wa kuamuru kuwekwa kwa dhamana.

113.-(1) Mahakama yoyote inayotoa hati ya kumkamata mtu yeyote kuhusiana na kosa lolote tofauti na mauaji au uhaini inaweza, kwa hiari yake, kuelekeza kwa idhinisho katika hati kwamba, kama akiweka dhamana akiwa na wadhamini wa kutosha kuhudhuria kwake mbele ya mahakama katika muda uliotajwa na baada ya hapo mpaka itakavyoelekezwa vinginevyo na mahakama, afisa ambaye hati imeelekezwa kwake atampa dhamana na kumuachia kutoka kizuizini.

(2) Idhinisho litaeleza;

(a) Idadi ya wadhamini;

- (b) Kiasi ambacho watatoa na watu ambao hati ya kukamatwa imetolewa dhidi yao watabanwa nayo; na
- (c) muda ambao anatakiwa kuhudhuria mbele ya mahakama.

(3) Wakati ambapo dhamana inachukuliwa chini ya kifungu hiki afisa ambaye hati imeelekezwa kwake atatakiwa kupeleka dhamana mahakamani.

Hati ielekezwe kwa nani.

114.(1) Hati ya kukamatwa inaweza kuelekezwa kwa afisa polisi mmoja au zaidi, au kwa afisa polisi mmoja au kwa maafisa polisi wengine wote wa eneo ambalo mahakama ina mamlaka, au kwa maafisa polisi wote kwa ujumla wa eneo hilo; lakini mahakama yoyote inayotoa hati hiyo inaweza, kama utekelezaji wa haraka ni muhimu, na na hakuna afisa wa polisi aliyepo karibu, kuelekeza kwa afisa aliyeruhusiwa wa serikali za mitaa ndani ya mamlaka yake, au kwa mtu mwingine yeyote au watu, na mtu huyo au watu hao watatekeleza hati hiyo mara moja.

(2) Wakati hati imeelekezwa kwa maafisa wengi au mtu zaidi ya mmoja, inaweza kutekelezwa na yeyote kati ya wale au zaidi ya mmoja wao.

Hati inaweza kuelekezwa kwa mmiliki wa ardhi, etc.

115.(1) Hakimu yeyote wa wilaya au mkazi anaweza kuelekeza hati kwa mmiliki wa ardhi yoyote, meneja wa ardhi au mkulima ndani ya mipaka ya mamlaka yake ya kukamatwa kwa mfungwa yeyote aliyetoroka au mtu ambaye anatuhumiwa kwa kosa la kukamatwa na amepuka ufuatiliwaji.

(2) Mmiliki wa ardhi, meneja au mkulima atakiri kwa maandishi kupokea hati na ataitekeleza kama mtu ambaye kwayo hati imetolewa yupo au ataingia kwenye ardhi yake au shamba au ardhi iliyo chini yake.

(3) Wakati mtu ambaye kwayo hati imetolewa amekamatwa, atakabidhiwa pamoja na hati kwa afisa polisi aliye karibu, ambaye atahakikisha anapeleka mbele ya hakimu mwenye mamlaka isipokuwa kama dhamana imechukuliwa chini ya kifungu cha 113.

Utekelezaji wa hati inayoelekezwa kwa afisa polisi.

116. Hati iliyoelekezwa kwa afisa polisi yeyote inaweza kutekelezwa na afisa polisi mwingine ambaye jina lake limeidhinishwa kwenye hati na afisa ambaye hati ilielekezwa au kuidhinishwa kwenye hati.

Taarifa ya kiini cha hati.

117. Afisa polisi au mtu yeyote anayetekeleza hati ya kukamata atamjulisha mtu anayepaswa kukamatwa, kiini cha hati na kama itahitajika, atamuonyesha hati hiyo.

Mtu aliyekamatwa kupeleka mbele ya mahakama bila

118. Afisa polisi au mtu mwingine anayetekeleza hati ya kukamata, bila kuchelewa kusiko na sababu, na kwa kuzingatia

kuchelewa.

masharti ya kifungu cha 113 kuhusiana na dhamana, atampeleka mtu aliyekamatwa mbele ya mahakama ambayo anatakiwa na sheria kumpeleka mtu huyo na atarudisha hati mahakamani ikiwa na idhinisho kuonyesha muda na namna ya utekelezaji.

Pale hati ya ukamataji inaweza kutekelezwa.

119. Hati ya kukamatwa inaweza kutekelezwa katika sehemu yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Upelekaji wa hati ya utekelezaji nje ya mipaka ya mamlaka ya mahakama.

120.-(1) Wakati hati ya kukamatwa inatakiwa kutekelezwa nje ya mipaka ya mamlaka ya mahakama inayoitoa, mahakama hiyo inaweza, badala ya kuielekeza hati hiyo kwa afisa polisi, kuipeleka kwa posta au vinginevyo kwa hakimu yeyote ndani ya mipaka ya mamlaka ambako inatakiwa kutekelezwa.

(2) Hakimu ambaye hati hiyo imepelekwa kwake ataidhinisha jina lake kwenye hati na, kama inawezekana, kuhakikisha inatekelezwa kwa namna iliyotolewa chini ya Sheria hii ndani ya mipaka ya eneo la mamlaka yake.

Utaratibu ikiwa hati imeelekezwa kwa afisa polisi kwa utekelezaji nje ya mamlaka.

121.-(1) Wakati hati ya ukamataji iliyoelekezwa kwa afisa polisi inatakiwa kutekelezwa nje ya mipaka ya eneo la mamlaka ya mahakama iliyoitoa, afisa polisi ataipeleka kwa ajili ya kuidhinishwa na hakimu aliye ndani ya mipaka ya eneo ambalo kwalo hati hiyo itatekelezwa.

(2) Hakimu ataidhinisha kwa kuandika jina lake katika hati na idhinisho litakuwa mamlaka ya kutosha kwa afisa polisi ambaye hati imeelekezwa kwake kuitekeleza ndani ya mipaka hiyo na maafisa polisi wenyeji watalazimika, kama watahitajika, kumsaidia afisa huyo katika kutekeleza hati hiyo.

(3) Wakati ambapo kuna sababu za kuamini kwamba uchelewaji utakaotokea wa kupata idhinisho la hakimu ndani ya mipaka ya eneo ambalo kwalo hati inatakiwa kutekelezwa utazuia utekelezaji wake, afisa polisi ambaye hati imeelekezwa anaweza kutekeleza hati hiyo bila idhinisho katika sehemu yoyote nje ya mipaka ya eneo la mamlaka ya mahakama iliyoitoa.

Utaratibu wa kukamata mtu nje ya mipaka ya mamlaka.

122.-(1) Wakati hati ya kukamatwa imetekelezwa nje ya mipaka ya eneo la mamlaka ya mahakama iliyoitoa, isipokua kama mahakama iliyoitoa hati iko ndani ya maili ishirini kutoka kwenye eneo la kukamata au iko karibu kuliko mipaka ya eneo la hakimu mwenye mamlaka ambako ukamataji ulifanyika au isipokuwa kama dhamana imechukuliwa chini ya kifungu cha 113, mtu aliyekamatwa atapelekekwa mbele ya hakimu ndani ya mipaka ya eneo la mamlaka ambako ukamataji ulifanyika.

(2) Hakimu atalazimika, kama mtu aliyekamatwa anaonekana

kuwa ni mtu aliyekusudiwa na mahakama iliyotoa hati, kuelekeza kuondolewa chini ya ulinzi na kupelekwa kwenye mahakama hiyo.

(3) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2) iwapo mtu amekamatwa kwa kosa tofauti na la mauaji au uhaini na yuko tayari na anataka kuweka dhamana kwa kiwango cha kumridhisha hakimu au kama maelekezo yameshaidhinishwa chini ya kifungu cha 113 kwenye hati na mtu huyo yupo tayari na anataka kutoa dhamana inayotakiwa kutokana na maelekezo, hakimu atachukua dhamana hiyo, kama itakavyokuwa, na atapeleka dhamana kwenye mahakama iliyotoa hati.

(4) Hakuna kitu katika kifungu hiki kitachukuliwa kumzuia afisa polisi kuchukua dhamana chini ya kifungu cha 113.

Makosa katika hati.

123. Kutofuata utaratibu wowote au kosa lolote kuhusiana na kiini au fomu ya hati ya kukamata na tofauti yoyote kati yake na malalamiko ya maandishi au kati ya malalamiko hayo na ushahidi uliotolewa kwa upande wa mashitaka katika shauri la uchunguzi, hautoathiri uhalali wa mwenendo katika au baada ya kusikilizwa kwa kesi, lakini iwapo utofauti unaonekana mbele ya mahakama kuwa mtuhumiwa amedanganywa au kupotoshwa, mahakama inaweza, kwa maombi ya mtuhumiwa, kuahirisha usikilizaji wa kesi hadi tarehe za baadaye na wakati huo huo kumweka mtuhumiwa rumande au kumtoa kwa dhamana.

(c) Masharti mengine kuhusu mchakato

Uwezo wa kuchukua dhamana kwa ajili ya mahudhuria.

124. Wakati mtu yeyote ambaye kuhudhuria au kukamatwa kwake afisa anayeongoza katika mahakama ana mamlaka ya kutoa wito au hati yupo mahakamani, afisa anaweza kumtaka mtu huyo kuweka dhamana, akiwa na au bila ya kuwa na wadhamini, kwa kuhudhuria kwake kwenye mahakama hiyo.

Ukamataji kwa kuvunja dhamana ya kuhudhuria.

125. Pale ambapo mtu yeyote ambaye anabanwa na dhamana iliyochukuliwa chini ya Sheria hii kuhudhuria mbele ya mahakama na hajahudhuria, afisa anayeongoza kwenye mahakama hiyo anaweza kutoa hati akielekeza kwamba akamatwe na aletwe mbele yake.

Uwezo wa mahakama kuamuru mfungwa kuletwa mbele yake.

126.-(1) Wakati mtu ambaye kuhudhuria au kukamatwa kwake mahakama ina mamlaka ya kutoa wito au hati amefungwa kwenye gereza lolote ndani ya mipaka ya eneo la mamlaka ya mahakama, mahakama inaweza kutoa amri kwa afisa msimamizi wa gereza kumtaka kumleta mfungwa katika ulinzi sahihi, katika muda utakaotajwa katika amri, mbele ya mahakama.

(2) Afisa msimamizi huyo, baada ya kupokea amri, atafanya kwa kufuata amri hiyo na atatoa ulinzi wa kutosha kwa mfungwa wakati wa

kutoka gerezani kwa malengo yaliyotajwa hapo juu.

Masharti ya Sehemu hii yanayotumika kwa ujumla kwa wito na hati; na uwezo wa mlinzi wa amani.

127. Masharti yaliyomo kwenye Sehemu hii kuhusiana na utolewaji uwasilishaji na utekelezaji wa wito na hati, kama itakavyowezezana, yatatumika kwa kila wito na kila hati ya kukamata iliyotolewa chini ya Sheria hii au kutolewa na mlinzi wa amani na, isipokuwa kama au; hiyo inaweza kuwa kinyume na sheria yoyote nyingine, uwezo wa hakimu au mahakama kuhusiana na kutoa au kuidhinisha wito au hati unaweza kutekelezwa na mlinzi wa amani.

B. – Mashtaka

(a) Kutoa lalamiko

Kuanzisha Mashtaka.

128.-(1) Shtaka linaweza kuanzishwa aidha kwa kutoa malalamiko au kwa kumleta mbele ya hakimu mtu aliyekamatwa kwa hati au bila hati.

(2) Mtu yeyote anayeamini kwa sababu za msingi na za kuaminika kwamba kosa limetendeka na mtu yeyote anaweza kutoa malalamiko ya kosa kwa hakimu mwenye mamlaka.

(3) Pale malalamiko yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (2) yamefanywa kwa hakimu asiye na mamlaka ya kuchukua dhamana ya kosa atalazimika:–

(a) Iwapo lalamiko liko kwenye maandishi, atarudisha kwa ajili ya kupelekwa kwenye mahakama sahihi ikiwa na idhinisho kuonyesha hivyo; au

(b) iwapo lalamiko halipo katika maandishi, atamuelekeza mlalamikaji kupeleka lalamiko kwenye mahakama sahihi.

(4) Lalamiko linaweza kutolewa kwa mdomo au kwa maandishi lakini, iwapo litatolewa kwa mdomo, litatakiwa kuandikwa na hakimu na, katika hali yoyote, litatakiwa kusainiwa na mlalamikaji na hakimu.

(5) Hakimu, baada ya kupokea lalamiko lolote, kwa kuzingatia kifungu cha 129, atandaa au kuhakikisha inaandaliwa na atalazimika kusaini hati rasmi ya mashtaka likiwa na maelezo ya kosa ambalo mtuhumiwa anashitakiwa, isipokuwa kama shtaka limesainiwa na kuwasilishwa na afisa polisi.

(6) Wakati mtuhumiwa ambaye amekamatwa bila ya hati ameletwa mbele ya hakimu, mashitaka rasmi yakiwa na maelezo ya kosa ambalo mtuhumiwa anashitakiwa, yatasainiwa na kuwasilishwa na afisa polisi aliyeleta mashitaka.

Uwezo wa hakimu kukataa lalamiko au shtaka rasmi.

129. Pale hakimu ana maoni kuwa malalamiko au mashtaka rasmi yaliyofanywa au yaliyoletwa chini ya kifungu cha 128 hayafichui kosa lolote, hakimu atatoa amri akikataa kukubali

malalamiko au mashtaka na atarekodi sababu za kutoa amri hiyo.

Kutolewa kwa wito au hati.

130. Baada ya kupokea lalamiko na baada ya kusaini shtaka kwa mujibu wa kifungu cha 128, hakmu anaweza, kwa hiari yake, kutoa aidha wito au hati kulazimisha mahudhurio ya mtuhumiwa mbele ya mahakama ya chini yanye mamlaka ya kuchunguza au kusikiliza kosa linalolalamikiwa kuwa limetendwa; isipokuwa kwamba hati haitatolewa kwa mara ya kwanza isipokuwa tu kama lalamiko umefanywa kwa kiapo ama na mlalamikaji au shahidi au mashahidi.

(b) Shtaka Rasmi

Watu walioshtakiwa kutahadharishwa

131. Mara baada ya afisa polisi kumshitaki mtuhumiwa kwa kosa, afisa polisi atalazimika kumtahadharisha mtu kwa maandishi na kama inawezekana kwa mdomo, katika utaratibu uliowekwa.

Makosa kuainishwa kwenye hati ya mashtaka na maelezo muhimu.

132. Kila shtaka au taarifa itakuwa na, na itajitosheleza kama itakuwa na, maelezo ya kosa maalumu au makosa ambayo mtuhumiwa anashitakiwa, pamoja na maelezo mengine kama yatakavyokuwa muhimu kwa kutoa taarifa za msingi kuhusiana na asili ya kosa aliloshitakiwa nalo.

Uunganishaji wa makosa katika hati ya mashtaka au taarifa.

133.-(1) Makosa yoyote yanaweza kuwekwa kwa pamoja katika hati ya mashtaka au taarifa iwapo makosa hayo yanatokana na taarifa zilezile au kama yanaundwa au ni sehemu ya mfululizo wa makosa ya ya aina moja au yanayofanana.

(2) Pale makosa zaidi ya moja yamewekwa kwenye hati moja ya mashtaka au taarifa, maelezo ya kila kosa lililoshtakiwa yataonyeshwa katika aya tofauti katika hati ya mashtaka au taarifa na kuitwa shitaka.

(3) Pale ambapo, kabla ya shauri au katika hatua yoyote ya shauri, mahakama ina maoni kuwa mtu anayetuhumiwa anaweza kuaibika au kuathirika katika utetezi wake kutokana na kushtakiwa kwa makosa zaidi ya moja katika hati moja ya mashtaka au taarifa, au kwa sababu nyingine yoyote ni vizuri kuelekeza kwamba ashitakiwe katika shauri tofauti kwa kila kosa au makosa aliyoshitakiwa nayo katika hati ya mashtaka au taarifa, mahakama inaweza kuamuru shauri tofauti la kila shtaka au mashtaka ya hati hiyo mashtaka au taarifa.

Uunganishaji wa watuhumiwa wawili au zaidi kwenye hati ya mashtaka au taarifa.

134.-(1) Watu wafuatao wanaweza kuunganishwa katika hati moja ya mashtaka au taarifa na wanaweza kushtakiwa pamoja, yaani–

- (a) watu wanaotuhumiwa kwa kosa moja lilitotendwa katika mlolongo mmoja;
- (b) watu wanaotuhumiwa kwa kosa na watu wanaotuhumiwa kusaidia au kujaribu kutenda kosa hilo;
- (c) watu wanaotuhumiwa kwa makosa tofauti yaliyotendwa

- Cap.16
- (d) katika mlolongo mmoja; watu wanaotuhumiwa kwa kosa lolote chini ya sura ya ishirini na tano mpaka thelathini na moja ya Sheria ya Kanuni za Adhabu na watu wanaotuhumiwa kupokea na kutunza mali, umilikaji ambao unatuhumiwa kuhamishwa kutokana na kosa lililotendwa na watu waliotajwa awali, au watu walio saidia au kujaribu kutenda kosa mojawapo ya hayo ya mwisho yaliyotajwa;
- Cap.16
- (e) watu wanaotuhumiwa kwa kosa lolote linalohusiana na fedha bandia chini ya Sura ya thelathini na sita ya Sheria ya Kanuni za Adhabu, na watu wanaotuhumiwa kwa kosa lingine lolote chini ya sura hiyo kuhusiana na fedha hiyo, au kusaidia au kujaribu kutenda kosa kama hilo; au
- Cap.200
- (f) watu wanaotuhumiwa kwa kosa lolote la uhujumu uchumi chini ya Sheria ya Kudhibiti Uhujumu Uchumi na Makosa ya Kupanga.

(2) Kwa ajili ya kuondoa mashaka, inatamkwa hapa kuwa hakuna kitu katika kifungu hiki au katika Sheria hii kitatafsiriwa kuzuia watu ambao wameshtakiwa tofauti kuunganishwa katika hati moja ya mashtaka au taarifa na kushtakiwa kwa pamoja kama ni watu wanaoangukia katika makundi yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1).

Muundo ambao makosa yanatakiwa kuandikwa katika hati ya mashtaka.

135. Masharti yafuatayo ya kifungu hiki yatumika kwa hati zote za mashitaka na taarifa na, bila kujali kanuni yoyote ya sheria au mazoea, hati ya mashitaka au taarifa haitapingwa kuhusiana na, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, muundo wake au yaliyomo kama imeandaliwa kwa kufuata masharti ya kifungu hiki:–

- (i) shtaka katika hati ya mashtaka au taarifa itaanza kwa maelezo ya kosa, lilishtakiwa itakayoitwa maelezo ya kosa;
- (ii) maelezo ya kosa yatafafanua kosa kwa ufupi kwa lugha ya kawaida na kwa jinsi inavyoweza kuepuka kutumia maneno ya kitaalamu na kutaja vigezo muhimu vya kosa, na kama kosa linaundwa kwa sheria, itatakiwa kurejea kifungu cha sheria kinachounda kosa hilo;
- (iii) baada ya maelezo ya kosa, taarifa kuhusiana na kosa hilo utafanywa katika lugha ya kawaida, ambapo matumizi ya maneno ya kitaalamu hayatakuwa muhimu, isipokuwa kama kanuni yoyote ya sheria inaweka mipaka ya taarifa kuhusiana na kosa ambayo inatakiwa kutolewa kwenye hati ya mashitaka au taarifa, hakuna kitu katika aya hii kitahitaji taarifa zaidi kutolewa zaidi ya zile zinazohitajika;
- (iv) fomu zilizotolewa kwenye jedwali la pili la Sheria hii,

- au fomu zinazofanana na hizo kwa karibu, zitatumika katika mazingira ambayo zinapaswa kutumika; na katika mazingira mengine fomu za aina hiyo, au zinazofanana na hizo kwa karibu zitatumika, taarifa kuhusiana na kosa na taarifa kuhusiana na kosa zikibadilishwa kulingana na mazingira ya kila jambo;
- (v) pale hati ya mashtaka au taarifa ina shtaka zaidi ya moja, mashtaka yatatakiwa kupewa namba kwa mtiririko;
- (b) (i) pale sheria inayounda kosa inataja kosa kuwa ni kutenda au kushindwa kutenda mojawapo kati ya matendo hayo tofauti, au kutenda au kushindwa kutenda kitendo katika mojawapo ya nafasi tofauti, au kwa mojawapo ya nia tofauti, au inataja sehemu ya kosa katika njia mbadala, matendo, kushindwa kutenda, nafasi au nia, au vitu vingine vilivyotajwa katika sheria inaweza kutajwa kwa njia ya mbadala katika shtaka linalounda kosa;
- (ii) haitakuwa muhimu, katika shtaka lolote linalounda kosa ambalo linashtakiwa na sheria, kukanusha kinzano au msamaha kutoka, au sifa juu ya, matumzi ya sheria inayounda kosa;
- (c) (i) ufafanuzi wa mali katika hati ya mashitaka au taarifa itakuwa katika lugha ya kawaida na kiasi cha kuonyesha kwa ufasaha mali inayotajwa, na, kama mali inafafanuliwa hivyo, haitakuwa muhimu (isipokuwa kama inatakiwa kwa dhumuni la kufafanua kosa kufuatana na umiliki maalum wa mali hiyo au thamani maalum ya mali) kumtaja mtu anayemiliki mali hiyo au thamani ya mali husika;
- (ii) pale mali inamilikiwa na mtu zaidi ya mmoja, na wamiliki wa mali wametajwa kwenye hati ya mashitaka au taarifa, itatosheleza kueleza kuwa mali inamilikiwa na mmoja wa watu hao kwa jina na wengineo, na kama watu wanaomiliki mali ni umoja wa watu wakiwa na jina la pamoja, kama vile kampuni ya pamoja, au “wakazi”, “wadhamini”, “makamishina”, au “klabu” au jina lingine, itajitosheleza kutumia jina la pamoja bila kutaja mtu binafsi;
- (iii) mali inayomilikiwa na au iliyotolewa kwa matumizi ya, asasi yoyote ya umma, huduma au idara inaweza kutajwa kama mali ya Jamuhuri ya Muungano;
- (iv) sarafu, noti za benki na noti za fedha zinaweza kutajwa

kama fedha, na madai yoyote kuhusu fedha, ili mradi zinahusiana na ufafanuzi wa mali, zitajitosheleza kwa uthibitisho wa kiasi chochote cha sarafu au wa noti za benki au fedha (ingawaje aina maalumu ya sarafu ambayo inaunda jumla hiyo, au noti za aina fulani za benki au fedha, hazitadhibitishwa); na katika mambo ya kuiba au kufanya udanganyifu, kwa uthibitisho kuwa mtuhumiwa kwa kutokuwa mwaminifu alijipatia, sarafu yoyote au noti ya benki au fedha, au sehemu yoyote ya thamani yake, ingawaje sarafu hiyo au noti hiyo ya benki au fedha inaweza kuwa imepeleka kwake kwa dhumuni kuwa baadhi au sehemu ya thamani hiyo inatakiwa irudishwe kwa mtu aliyepeleka au kwa mtu yoyote mwingine, na sehemu hiyo itakuwa imerudishwa ipasavyo;

- (v) pale mtu anashitakiwa kwa kuiba fedha au kitu kingine chochote, itatosheleza kuainisha jumla yake, au idadi yake au kiasi cha vitu, kama itakavyokuwa, kufuatana na kosa linalodaiwa kutendeka na kati ya tarehe ambazo kosa linadaiwa kutendeka, bila kutaja kitu halisi au tarehe halisi;
- (d) ufafanuzi au cheo katika hati ya mashitaka au taarifa kumhusu mtuhumiwa, au mtu yeyote mwingine ambaye anatajwa kwenye hati ya mashitaka au taarifa, utakuwa kwa kiasi kinachojitosheleza kuweza kumtambua mtu huyo bila ya kutaja jina lake kamili, makazi yake, mtindo, hadhi au kazi, na, iwapo jina la mtu halijulikani au kwa sababu nyingine yoyote, haiwezekani kutoa ufafanuzi au cheo chake, basi ufafanuzi huo au cheo kitatolewa kama itakavyowezekana kutokana na mazingira, au mtu huyo anaweza kutajwa kama “mtu asiyejulikana”;
- (e) pale ni muhimu kurejea waraka wowote au hati yoyote katika hati ya mashitaka au taarifa, itatosheleza kufafanua waraka huo au hati hiyo kwa jina au cheo ambacho hujulikana, au kwa mfano wake, bila kuonyesha nakala yake yoyote;
- (f) kwa kuzingatia masharti mengine ya kifungu hiki, itatosheleza kufafanua sehemu yoyote, muda, kitu, suala, tendo au kutokutenda kwa aina yoyote ambako ni muhimu kurejea katika hati ya mashitaka au taarifa kwa lugha ya kawaida katika namna ya kuonyesha kwa ufasaha mahali, muda, kitu, suala, tendo au kutokutenda kulikorejewa;
- (g) haitakuwa ni muhimu katika kueleza nia yoyote ya kughilibu kudanganya au kudhuru kutaja nia yoyote ya

kughilibu, kudanganya au kudhuru mtu yoyote kama sheria inayounda kosa hilo haifanyi nia ya kughilibu, kudanganya au kudhuru mtu kuwa ni kigezo muhimu cha kosa;

- (h) pale kutiwa hatiani kwa zamani kumewekwa kwenye hati ya mashitaka au taarifa, itaelezwa mwishoni mwa hati ya mashitaka au taarifa kwa njia ya maelezo kwamba mtuhumiwa amewahi kutiwa hatiani kwa kosa hilo katika muda na mahali fulani bila ya kutoa maelezo kuhusu kosa;
- (i) tarakimu na vifupisho vinaweza kutumika kwa kueleza kitu chochote ambacho huwa kwa kawaida huelezwa kwa njia hiyo.

Kesi ya watu wawili au zaidi walioshitakiwa.

136. Ikiwa hati ya mashitaka yoyote watu wawili au zaidi wanashitakiwa kwa pamoja kwa kutenda kosa, haitakuwa ni lazima kueleza kuwa “wote wawili na kila mmoja”, au “mmoja au wengine” au kwamba “wote na kila mmoja” au “mmoja au zaidi” ame/wametenda kosa, au ali/walifanya au ali/walishindwa kufanya tendo lolote; lakini huo mbadala utadhaniwa katika mashitaka yote.

(c) Kutiwahatiani au kuachiwa kwa makosa ya zamani

Mtu aliyetiwa hatiani au kuachiwa kutoshtakiwa tena kwa kosa lilelile

137. Mtu ambaye ameshawahi kushtakiwa na mahakama yenye mamlaka halali kwa kosa na kutiwa hatiani au kuachiwa kwa kosa hilo hataweza, wakati kutiwa huko hatiani au kuachiwa huko hakujabadilishwa au kutupiliwa mbali, kushtakiwa tena kwa maelezo yale yale na kwa kosa lile lile.

Mtu anaweza kushitakiwa tena kwa makosa tofauti.

138. Mtu aliyetiwa hatiani au kuachiwa kwa kosa lolote anaweza baadaye kushitakiwa kwa kosa lingine lolote ambalo angeweza kushtakiwa kwalo katika shauri la kwanza chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 134.

Madhara yaliyozuka au ambayo hayakujulikana wakati wa kuendesha mashtaka yaliyopita.

139. Mtu aliyetiwa hatiani au aliyeachiwa kwa tendo lolote linalosababisha matokeo ambayo kwa pamoja na tendo lingine linaunda kosa lingine tofauti na lile ambalo alitiwa hatiani au kuachiwa, anaweza baadaye kushitakiwa kwa kosa hilo la mwisho lililotajwa iwapo madhara hayakutokea au hayakujulikana na mahakama kuwa yalitokea wakati alipotiwa hatiani au kuachiwa.

Pale ambapo mahakama ya awali haikuwa na mamlaka ya kuendesha mashtaka yanayofuata.

140. Mtu aliyetiwa hatiani au aliyeachiwa kwa kosa lolote linaloundwa na tendo lolote, bila kujali kutiwa huko hatiani au kuachiwa huko anaweza, baadaye kushitakiwa kwa kosa lingine lolote linaundwa na matendo yaleyale ambalo linaweza kuwa limetendwa,

kama mahakama ambayo mwanzo alishitakiwa haikuwa na uwezo wa kusikiliza kesi ambayo baadaye anashitakiwa.

Jinsi ya kuthibitisha kutiwa hatiani kwa makosa ya zamani.

141.-(1) Katika uchunguzi wowote, shtaka au mwenendo mwingine chini ya Sheria hii, kutiwa hatiani kulikopita kunaweza kuthibitishwa, zaidi ya namna nyingine kama zilivyowekwa na sheria yoyote kwa wakati sheria hiyo inatumiaka:-

- (a) kwa nakala iliyothibitishwa, kwa mkono wa afisa anayetunza kumbukumbu za mahakama ambako kutiwa hatiani kulifanyika, kuwa ni nakala ya hukumu inayotoa adhabu au amri;
- (b) kwa cheti kilichosainiwa na afisa msimamizi wa gereza ambako adhabu au sehemu ya adhabu ilitumikiwa;
- (c) kwa kuwasilisha hati ya kufungwa ambayo adhabu ilitumikiwa, au
- (d) kwa kuwasilishwa hukumu ya mwisho ya mahakama yenye mamlaka iliyotamka kwa mara ya mwisho mtu kutiwa hatiani,

Pamoja na, katika kila jambo hilo, ushahidi kuhusiana na utambulisho wa mtuhumiwa na mtu aliyetiwa hatiani.

(2) Cheti katika muundo uliowekwa na Mkurugenzi wa Mashitaka kilichotolewa kwa mkono wa afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka kwa niaba hiyo, ambaye alifanananisha alama za vidole za mtuhumiwa na zile za mtu aliyetiwa hatiani hapo awali, kitakuwa ushahidi wa dhahiri wa yale yote yaliyoelezwa mle ndani mwake kama kitatolewa na mtu aliyechukua alama za vidole vya mtuhumiwa.

(3) Kuhukumiwa kwa zamani katika sehemu yoyote nje ya Tanzania kunaweza kuthibitishwa kwa kutoa cheti kinachoonekana kutolewa kwa mkono wa afisa polisi katika nchi ambako kutiwa hatiani huko kulifanyika, kikiwa na nakala ya hukumu inayotoa adhabu au amri na alama za vidole au picha za alama za vidole za mtu aliyetiwa hatiani, pamoja na ama:-

- (a) ushahidi kwamba alama za vidole, au picha, za mtu aliyetiwa hatiani awali ni za mtuhumiwa; au
- (b) cheti kilichotolewa chini ya mkono wa afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi wa Mashitaka chini ya kifungu kidogo cha (2) kwamba amefanananisha alama za vidole, au picha, ya mtu aliyetiwa hatiani hapo awali na alama za vidole au picha za mtuhumiwa na kwamba ni za mtu mmoja.

(4) Cheti kinachoonekana kutolewa chini ya mkono wa afisa polisi katika nchi ambako kutiwa hatiani kulifanyika na cheti kilichotolewa kwa mujibu ya masharti ya aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (3) kitalazimika, iwapo ni katika sula la cheti cha mwisho kinatolewa na mtu ambaye alichukua alama za vidole vya mtuhumiwa, kuwa ushahidi wa dhahiri wa yale yote yaliyoyomo humo bila

uthibitisho kwamba afisa anayeonekana kuisaini ni kweli aliisaini na alipewa uwezo wa kufanya hivyo.

(d) Kutolazimisha mahudhurio ya mashahidi

Wito kwa shahidi.

142.-(1)Iwapo imefanywa kuonekana kwamba ushahidi wa muhimu unaweza kutolewa na au unahodhiwa na mtu yoyote, itakuwa ni halali kisheria kwa mahakama kutoa wito kwa mtu huyo kumtaka ahudhurie mbele ya mahakama au kumtaka kuleta na kutoa mahakamani kwa dhumuni la ushahidi nyaraka zote na maandiko yote anayohodhi au yaliyo katika mamlaka yake ambayo yanaweza kutajwa au vinginevyo kufafanuliwa kwenye wito.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki kishachukuliwa kuathiri masharti ya kifungu cha 132 cha Sheria y Ushahidi.

Cap.6

Hati kwa shahidi
asiyetii wito.

143. Iwapo, bila udhuru wa kutosha, shahidi hatahudhuria kuitikia wito wa mahakama, na ikithibitishwa uwasilishaji sahihi wa wito umefanywa katika muda wa kutosha kabla hajatakiwa kuhudhuria mahakama inaweza kutoa hati ya kumleta shahidi huyo mbele ya mahakama katika muda na mahali hapo kama itakavyoelekezwa kwenye hati.

Hati kwa shahidi
katika hudhurio la
kwanza.

144. Iwapo mahakama inaridhishwa na ushahidi wa kiapo kwamba shahidi hatahudhuria mpaka alazimishwe kufanya hivyo, inaweza mara moja kutoa hati ya kumkamata na kumleta shahidi mbele ya mahakama katika muda na mahali kama itakavyoelekezwa kwenye hati ya ukamataji.

Jinsi ya
kushughulikia
shahidi
aliekamatwa kwa
mujibu wa hati.

145. Pale shahidi amekamatwa chini ya hati mahakama inaweza, kama atatoa dhamana kupitia wadhamini kwa kiwango cha kuiridhisha mahakama kwamba atahudhuria siku ya kusikiliza kesi, kumuamuru kuachiliwa kutoka chini ya ulinzi, au kama atashindwa kutoa dhamana, kuamuru kuwekwa kizuizini kwa kuletwa siku ya kusikiliza kesi.

Uwezo wa
mahakama kuamuru
mfungwa kuletwa
kwa mahojiano.

146.-(1) Mahakama yoyote yenye nia ya kumhoji mtu kama shahidi, katika kesi yoyote inayoendelea mbele yake, mtu yoyote aliyezuiwa gereza ndani ya mipaka ya mamlaka yake inaweza kutoa amri kwa afisa msimamizi wa gereza kumtaka kumleta mfungwa huyo katika ulinzi sahihi, katika muda utakaotajwa kwenye amri, mbele ya mahakama kwa mahojiano.

(2) Afisa msimamizi, baada ya kupokea amri, atatakiwa kutenda kwa mujibu wa amri hiyo na atalazimika kutoa ulinzi wa kutosha kwa mfungwa huyo wakati akiwa nje ya gereza kwa madhumuni yaliyoelekezwa kwenye amri.

Adhabu kwa
kutohudhuria kwa
shahidi.

147.-(1) Mtu yeyote aliyeitwa kuhudhuria kama shahidi ambaye, bila sababu ya msingi, anashindwa kuhudhuria kama alivyotakiwa na wito au ambaye, baada ya kuhudhuria, anaondoka bila kupata ruhusa ya mahakama au anashindwa kuhudhuria baada ya kuahirishwa kwa mahakama baada ya kuamuriwa kuhudhuria, atawajibika kwa amri ya mahakama kulipa faini isiyoziidi shilingi elfu tano.

(2) Faini iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) inaweza kutozwa kwa kushika na kuuza mali yoyote inayohamishika inayomilikiwa na shahidi ambayo iko ndani ya mipaka ya eneo la mamlaka ya mahakama.

(3) Ikishindana kupata faini kwa kushika mali na kuuza shahidi anaweza, kwa amri ya mahakama, kufungwa kama mfungwa wa madai kwa kipindi cha siku kumi na tano isipokuwa kama faini imelipwa kabla ya kuisha kwa kipindi hicho.

(4) Kwa sababu nzuri itakayoonyeshwa, Mahakama Kuu inaweza kusamehe au kupunguza faini yoyote iliyotolewa chini ya kifungu hiki na mahakama ya chini.

(e) Masharti kuhusu dhamana, wadhamini n na bondi

Dhamana Sheria Na.
12 of 1987; 13 ya
1988; 10 ya 1989 kif.
2; 27 ya 1991 kif. 2;
12 ya 1998 Jedwali.;
9 ya 2002 Jedwali.

148.-(1) Wakati ambapo mtu yoyote amekamatwa au ameshikiliwa bila hati na afisa msimamizi wa kituo cha polisi au amehudhuria au ameletwa mbele ya mahakama na yuko tayari katika muda wowote wakati yuko chini ya ulinzi wa afisa huyo au katika hatua yoyote ya mwenendo mbele ya mahakama hiyo kutoa dhamana afisa au mahakama, kama itakavyokuwa, wanaweza, kwa kuzingatia masharti yafuatayo ya kifungu hiki, kutoa dhamana kwa mtu huyo; isipokuwa kwamba afisa au mahakama wanaweza, badala ya kuchukua dhamana kutoka kwa mtu huyo, kumwachia baada ya kuweka dhamana akiwa na au bila ya wadhamini kwa kuhudhuria kama iliyowekwa katika kifungu hiki.

(2) Kiasi cha dhamana kitawekwa kwa kuzingatia uzito na mazingira mengine ya kesi, lakini hakitapaswa kuzidi sana.

(3) Mahakama Kuu inaweza, kwa kuzingatia vifungu vidogo vya (4) na (5) vya kifungu hiki, katika kesi yoyote kuelekeza kwamba mtu yoyote apewe dhamana au kwamba dhamana inayotakiwa na mahakama ya chini au afisa polisi ipunguzwe.

(4) Bila kujali kitu chochote kilichoko katika kifungu hiki, hakuna afisa polisi ataweza au mahakama itaweza, baada ya mtu kukamatwa na wakati anasubiri shauri au rufaa, kumwachia mtu huyo kwa dhamana iwapo Mkurugenzi wa Mashtaka, anathibitisha kwa maandishi kwamba kuna uwezekano kwa usalama au maslahi ya Jamhuri kuathirika, na cheti kilichotolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kifungu hiki kitaanza kutumika kuanzia tarehe kitakapowasilishwa mahakamani au kutaarifiwa kwa afisa msimamizi

wa kituo cha polisi na kitaendelea kutumika hadi mwenendo unaohusika utakapohitimishwa au Mkurugenzi wa Mashitaka atakapokiondoa.

(5) Afisa polisi msimamizi wa kituo cha polisi au mahakama ambako mtuhumiwa ameletwa au amehudhuria, haitatoa dhamana kwa mtu huyo iwapo:-

- (a) mtu huyo anashitakiwa kwa:-
 - (i) mauaji, uhaini, ujambazi wa kutumia silaha, au unajisi wa mtoto;
 - (ii) usafirishaji haramu wa madawa ya kulevya kinyume cha Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya, lakini haihusu mtu aliyeshitakiwa kwa kosa la kukutwa na madawa ambayo kwa kuzingatia mazingira yote ambako kosa lilitendeka, haikuwa kwa makusudi ya usafirishaji au kibiashara;
 - (iii) kosa linalohusisha heroini, kokeini, opiamu iliyotayarishwa opiamu popi (papava setijeramu), majani ya popi, mmea wa koka, majani ya koka, kanibisi sativa au kanibisi resini (Heipu ya India), methakvolani (mandraksi), kata edulisi (khati) au dawa nyingine ya kulevya au kitu cha saikotropiki kilichoreshwa kwenye jedwali la Sheria hii ambayo ina thamani iliyothibitishwa na Kamishina wa Kamisheni ya Taifa ya Uratibu wa Uthibiti wa Madawa, inayozidi shilingi milioni kumi;
 - (iv) ugaidi dhidi ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002;
 - (v) usafirishaji fedha haramu kinyume na Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Fedha ya mwaka 2006;
- (b) inaonekana kwamba mtuhumiwa hapo awali aliwahi kuhukumiwa kwa kifungo cha miaka inayozidi mitatu;
- (c) inaonekana kuwa mtuhumiwa hapo awali aliwahi kupewa dhamana na mahakama na alishindwa kutiia masharti ya dhamana au alitoroka;
- (d) inaonekana na mahakama kwamba ni muhimu kwa mtuhumiwa kuwekwa chini ya ulinzi kwa ajili ya ulinzi au usalama wake;
- (e) kosa ambalo mtu anashitakiwa nalo linahusisha fedha halisi au mali yenye thamani inayozidi shilingi milioni kumi isipokuwa kama mtu huyo ataweka dhamana ya fedha taslim au mali nyingine inayolingana na nusu ya kiasi au thamani ya fedha halisi au mali iliyohusika na

Kurasa 95

Sheria Na.21
ya 2002,
2 ya 2007
kif.19

inayobaki imewekewa dhamana:

Isipokuwa kwamba pale mali inayowekwa dhamana ni mali isiyohamishika, itatosha kuweka hati miliki, au iwapo hati miliki haipo ushahidi mwingine wowote utakaoiridhisha mahakama kuthibitisha uwepo wa mali; isipokuwa masharti haya hayatumika kwa dhamana ya polisi.

(6) Pale mahakama itaamua kumwachia mtuhumiwa kwa dhamana, italazimika kutoa masharti yafuatayo kwenye dhamana, yaani—

- (a) mtuhumiwa kusalimisha pasipoti yake polisi au nyaraka nyingine za kusafiria; na
- (b) kizuizi katika matembezi ya mtuhumiwa kwenye eneo la mji, kijiji au eneo lingine la makazi yake.

(7) Mahakama inaweza, kwa kuongeza kwenye masharti ya lazima yaliyoorodheshwa katika kifungu kidogo cha (6), kuweka mojawapo au zaidi ya masharti yafuatayo ambayo yanaonekana na mahakama yanaweza kumfanya mtuhumiwa kuhudhuria katika shauri au kuja tena mahakamani katika muda na mahali unaotakiwa au kama itakavyokuwa muhimu kwa masilahi ya haki au kwa kuzuia makosa ya jinai, yaani:—

- (a) kumtaka mtuhumiwa kuripoti katika muda tofauti utakaowekwa katika kituo cha polisi au mamlaka nyingine ndani na eneo la makazi yake;
- (b) kumtaka mtuhumiwa kutokuzuru eneo lililotajwa au majengo, au kuambatana na watu fulani waliotajwa;
- (c) sharti lingine lolote ambalo mahakama itaona ni muhimu na haki kuweka kwa kuongezea kwenye masharti yaliyopita.

Uwezo wa Mahakama Kuu kubadilisha masharti ya dhamana yaliyotolewa na mahakama za chini.

149. Pale inapohusiana na mwenendo wowote wa jinai mahakama ya chini ina uwezo wa kumwachia mtu yeyote kwa dhamana lakini kama inakataa kufanya hivyo au inafanya hivyo au inataka kufanya hivyo kwa masharti yasiyokubalika kwa mtu huyo, Mahakama Kuu inaweza kumpa dhamana au kuelekeza apewe dhamana au, kama amechiwa kwa dhamana, inaweza kubadili masharti yoyote ambayo kwayo alipewa dhamana au kupunguza kiasi ambacho yeye au mdhamini yoyote anatakiwa kutimiza katika dhamana.

Kubadilika kwa mazingira baada ya kutolewa dhamana.

150. Pale ambapo mtuhumiwa amepewa dhamana na mazingira yamejitokeza ambayo, iwapo mtuhumiwa asingekuwa amepewa dhamana, kwa maoni ya mwendesha mashitaka au afisa polisi, yange halalisha mahakama kukataa dhamana au kutaka dhamana ya kiasi kikubwa, jaji au hakimu, kama itakavyokuwa, akijulishwa hali hiyo na mwendesha mashitaka au afisa polisi, atatoa hati ya kumkamata mtuhumiwa na, baada ya kumpa mtuhumiwa nafasi ya kusikilizwa, anaweza ama kumpeleka gerezani kusubiri usikilizwaji au

kumpa dhamana kwa masharti yaleyale au kwa kiasi kikubwa zaidi kama jaji au hakimumu atakavyoona inafaa.

Utekelezaji wa hati za dhamana.

151. Kabla mtu yeyote hajaachiwa kwa dhamana, au kwa kujidhamini yeye mwenyewe, dhamana ya kiasi fulani cha fedha kama mahakama au afisa polisi, jinsi itakavyokuwa, akiona inafaa itatakiwa kuwekwa na mtu huyo, na wakati atakapoachiwa kwa dhamana, akiwa na mdhamini mmoja au wengi wa kutosha, itaweka sharti kwamba atalazimika kuhudhuria katika muda na mahali palipotajwa katika dhamana na atalazimika kuendelea kuhudhuria mpaka itakapoelekezwa vinginevyo na mahakama au afisa polisi.

Kutolewa chini ya ulinzi.

152.-(1) Mara baada ya utekelezaji wa dhamana, mtu ambaye kuhudhuria kwake dhamana imetekelezwa, ataachiwa, na kama yupo gerezani mahakama inayomwachia kwa dhamana itatakiwa kutoa amri ya kutolewa kwa afisa msimamizi wa gereza, na afisa baada ya kupokea amri, atalazimika kumwachia.

(2) Hakuna kitu katika kifungu hiki au kifungu cha 146 kitachukuliwa kutaka kuachiwa kwa mtu yeyote anayewajibika kushikiliwa kwa mambo mengine nje ya yale ambayo dhamana imetekelezwa.

Amana badala ya hati ya dhamana.

153. Wakati mtu anatakiwa na mahakama au afisa yeyote kutekeleza dhamana akiwa na au bila ya wadhamini, mahakama au afisa, isipokuwa katika suala la dhamana ya kuonyesha tabia njema, kumruhusu kuweka jumla ya fedha ya kiasi ambacho mahakama au afisa anaweza kukipanga badala ya kutekeleza dhamana.

Uwezo wa kuamuru dhamana inayojitosheleza baada ya ile kwanza kujitosheleza

154. Iwapo, kwa kosa, udanganyifu au kwa sababu nyingine yoyote, wadhamini wasiojitosheleza wamekubaliwa, au iwapo baada ya muda wameonekana hawatoshelezi, mahakama inaweza kutoa hati ya ukamataji ikielekeza kuwa mtu aliyeachiwa kwa dhamana aletwe mbele yake na inaweza kumuamuru kutafuta wadhamini na kama akishindwa kufanya hivyo inaweza kumpeleka gerezani.

Kuachiwa kwa wadhamini.

155.-(1) Wote au yeyote kati ya wadhamini kwa ajili ya kuhakikisha mtu aliyeachiwa kwa dhamana anahudhuria na kuonekana mahakamani anaweza wakati wowote kuomba kwa hakimumu kufuta dhamana aidha yote au inayomhusu yeye muombaji au waombaji.

(2) Baada ya maombi kufanywa hakimumu atatakiwa kutoa hati ya ukamataji ikielekeza kuwa mtu aliye katika dhamana aletwe mbele yake.

(3) Baada ya mtu huyo kuhudhuria kwa mujibu wa hati, au kwa kujisalimisha kwa hiari yake, hakimumu atatoa amri ya kufutwa kwa dhamana aidha yote au kama inavyomhusu mwombaji au waombaji, na itamtaka mtu huyo kutafuta wadhamini wengine wanaojitosheleza,

na kama anashindwa kufanya hivyo anaweza kumpeleka gerezani.

Kufa kwa mdhamini.

156. Pale ambapo mdhamini aliyeweka dhamana anakufa kabla dhamana haijatiwa, mali zake zitasamehewa kutumika kuhusiana na dhamana, lakini mtu aliyewekewa dhamana anaweza kutakiwa kutafuta mdhamini mpya.

Watu waliofungwa na dhamana wakiiruka au kukiuka masharti ya dhamana wanaweza kukamatwa

157.-(1) Afisa polisi anaweza kumkamata bila hati mtu yeyote aliyeachiwa kwa dhamana:-

- (a) iwapo afisa polisi ana sababau za msingi za kuamini kuwa mtu huyo anaweza kuvunja sharti kwamba atahudhuria katika muda na mahali anapotakiwa au sharti lolote jingine ambalo kwalo alipewa dhamana, au iwapo afisa polisi ana sababu za kuhisi kuwa mtu huyo anavunja au amevunja sharti jingine; au
- (b) baada ya kutaarifiwa kwa maandishi na mdhamini yeyote wa mtu huyo kwamba mdhamini anaamini kuwa mtu huyo anaweza kuvunja sharti la kwanza lililotajwa na kwa sababu hiyo mdhamini anataka kujiondoa kutoka wajibu wake kama mdhamini.

(2) Mtu aliyekamatwa chini ya kifungu kidogo cha (1)-

- (a) atatakiwa, isipokuwa kama anakamatwa ndani ya saa ishirini na nne kabla ya wasaa ambao anatakiwa kwa mujibu wa sharti la dhamana yake kuhudhuria mbele ya mahakama yoyote, kuletwa haraka iwezekanavyo, na kwa hali yoyote ndani ya saa ishirini na nne baada ya kukamatwa, mbele ya hakim mwenye mamlaka kwenye eneo ambalo amekamatwa; na
- (b) isipokuwa katika hali ya kipekee atatakiwa kupelekwa mbele ya mahakama ambayo anatakiwa kwa ajili ya kuendelea na shauri.

Watu wanaoruka au kukiuka masharti ya dhamana kutofikiriwa kupewa dhamana nyingine.

158. Mtu yoyote aliye chini ya dhamana na anayekamatwa kwa kushukiwa kimisingi kuwa anajiandaa kuvunja au yuko kwenye harakati za kuvunja masharti ya dhamana yake, iwapo mahakama itaridhika kwamba alikamatwa kwa haki, hatafikiriwa tena kwa dhamana nyingine katika kesi hiyo.

Adhabu kwa kukiuka masharti ya dhamana au kutohudhuria

159. Pale mtu anatoroka wakati akiwa kwenye dhamana au, hayuko kwenye dhamana, atashindwa kuhudhuria mbele ya mahakama katika tarehe iliyowekwa na anajificha ili hati ya ukamataji isiweze kutekelezwa:-

- (a) kiasi cha mali yake, inayohamishika au isiyohamishika, kwa kadri inavyolingana na kiasi cha thamani ya fedha ya mali yoyote inayohusika katika kesi inaweza

- kutaifishwa kwa kushikiliwa; na
- (b) shauri kuhusiana na mtu huyo litaendelea bila kujali hatua ya shauri lilipofikia wakati mtuhumiwa anatoroka, baada ya jitihada za kutosha kufanywa kumtafuta na kumlazimisha ahudhurie.

Kutaifishwa kwa mali iliyowekewa dhamana.

160.-(1) Wakati ambapo inathibitika kwa kiwango cha kuiridhisha mahakama ambapo dhamana chini ya Sheria hii au Sheria ya Kanuni ya Adhabu imechukuliwa au wakati dhamana inapokuwa imechukuliwa na afisa polisi kwa kuhudhuria mbele ya mahakama kuwa dhamana hiyo imetwaliwa, mahakama itarekodi sababu za uthibitisho huo na inaweza kumwita mtu yeyote anayebanwa na dhamana hiyo kulipa adhabu inayohusika au kuonyesha sababu kwa nini isilipwe.

(2) Iwapo sababu za kutosha hazijaonyeshwa na adhabu haijalipwa, mahakama inaweza kuendelea kutoza adhabu kwa kutoa hati ya kukamatwa na kuuzwa mali inayohamishika inayomilikiwa na mtu huyo au mali zake kama amefariki.

(3) Hati inaweza kutekelezwa ndani ya mipaka ya eneo la mamlaka ya mahakama iliyoitoa na itaruhusu kushikiliwa na kuuzwa mali inayohamishika inayomilikiwa na mtu huyo nje ya mipaka hiyo kama inaidhinishwa na hakimumu yeyote ndani ya mipaka ya eneo la mamlaka ambalo kwato mali hiyo inapatikana.

(4) Iwapo adhabu haitalipwa na haiwezi kupatikana kwa kushikiliwa na kuuza mali, mtu anayetakiwa kulipa atawajibika, kwa amri ya mahakama iliyotoa hati, kutumikia kifungo cha miezi sita.

(5) Mahakama inaweza kwa hiari yake kusamehe sehemu ya adhabu na kudai malipo kwa sehemu tu.

(6) Pale ambapo mdhamini kwenye dhamana atakufa kabla ya dhamana kutwaliwa, mali zake zitasamehewa kutumika kuhusiana na dhamana.

(7) Pale mtu yeyote aliyetoa dhamana atafungwa kwa kosa ambalo utendekaji wake ni kuvunja masharti ya dhamana yake, nakala ya hukumu ya mahakama iliyothibitishwa ambayo mtu huyo alitiwa hatiani kwa kosa hilo inaweza kutumika kama ushahidi katika mwenendo chini ya kifungu hiki dhidi ya mdhamini au wadhamini wake na iwapo nakala iliyothibitishwa inatumika hivyo mahakama itachukulia kwamba kosa lilitendwa na mtu huyo isipokuwa kama itathibitishwa vinginevyo.

Rufaa na mapitio ya amri za mahakama.

161. Amri zote zitakazotolewa chini ya vifungu vya 148 mpaka 160 na hakimumu yeyote zinaweza kukatiwa rufaa au kupitiwa na, Mahakama Kuu.

Uwezo wa kutoza ushuru wa kiasi kinachodaiwa katika

162. Mahakama Kuu inaweza kuelekeza hakimumu yeyote kutoza kiasi kinachotakiwa kwenye dhamana ya kuonekana na kuhudhuria

mali iliyowekewa dhamana. Usuluhishi katika mazingira fulani.

Mahakama Kuu.

163. Katika suala la mwenendo unaohusu kuumizwa au kosa lingine lolote kumhusu mtu mwenyewe au binafsi mahakama inaweza iwapo inafikiri kwamba maslahi ya umma hayahitaji kutolewa kwa adhabu, kukuza maelewano na kuhimiza na kurahisisha maelewano, katika njia ya amani, juu ya mwenendo au masharti ya malipo ya fidia au masharti mengine yatayokubaliwa na mahakama, na inaweza baada ya hapo kuamuru mwenendo kusimamishwa.

SEHEMU YA SITA
USIKILIZAJI WA KESI
MASHARTI YA JUMLA KUHUSIANA NA USIKILIZAJI WA KESI
A. – Uwezo wa Mahakama
(a) Uwezo kwa Ujumla

Makosa chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu.

164.-(1) Kwa kuzingatia masharti mengine ya Sheria hii, kosa lolote chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu linaweza kusikilizwa na Mahakama Kuu au, pale ambapo kosa limeonyeshwa katika kolamu ya tano ya Sehemu A ya Jedwali la Kwanza la Sheria hii, na mahakama za chini.

Cap.16

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), pale ambapo hakuna sharti ililowekwa katika Sehemu A ya Jedwali la Kwanza la Sheria hii kuhusiana na kosa lolote chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, kosa hilo litasikilizwa, na litachukuliwa siku zote kuwa limekuwa likisikilizwa na Mahakama Kuu pamoja na mahakama ya chini.

Makosa chini ya sheria nyingine tofauti na Sheria ya Kanuni za Adhabu.

165.-(1) Kosa lolote chini ya sheria yoyote isipokuwa Sheria ya Kanuni ya Adhabu pale mahakama yoyote imetajwa kwa niaba hiyo kwenye sheria hiyo, litasikilizwa na mahakama hiyo.

(2) Pale ambapo hakuna mahakama iliyotajwa, kosa linaweza, kwa kuzingatia masharti mengine ya Sheria hii, kusikilizwa na Mahakama Kuu au, pale ambapo kosa limeonyeshwa katika kolamu ya tano ya Sehemu B ya Jedwali la Kwanza kwenye Sheria hii kuwa ni kosa linalosikizwa na mahakama za chini, litasikilizwa na mahakama za chini.

Adhabu ambazo Mahakama Kuu inaweza kutoa

166. Mahakama Kuu inaweza kupitisha adhabu au kutoa amri yoyote nyingine inayoruhusiwa na sheria.

Kuunganisha adhabu Sheria Na. 5 ya 2002 Jedwali

167.-(1) Mahakama yoyote inaweza kupitisha adhabu halali kisheria ikijumuisha adhabu yoyote ambayo inaruhusiwa na sheria kupitisha; lakini pale ambapo mahakama ya chini inayoongozwa na hakimumu tofauti na hakimumu mkazi au hakimumu mfawidhi wa wilaya, itatoa adhabu ya viboko kama nyongeza kwenye adhabu ya kifungu, adhabu hiyo ya viboko haitaweza kutekelezwa mpaka iwe imethibitishwa na

Mahakama Kuu.

(2) Katika kuamua uwezo wa mamlaka ya Mahakama chini ya kifungu cha 164 kupitisha adhabu ya kifungo, mahakama itachukuliwa kuwa na mamlaka ya kupitisha adhabu yote iliyotajwa kwenye kifungu hicho zaidi ya kipindi cha kifungo ambacho kinaweza kutolewa kama akishindwa kulipa faini.

(3) Pale ambapo mahakama inapitisha adhabu chini ya kifungu kidogo cha (1), inaweza kuzuia kutolewa kwa paroli kwa mfungwa na italazimika kuonyesha sababu za kuzuia huko.

Adhabu katika
hukumu ya makosa
mawili au zaidi
katika shtaka moja.
Sheria. Na. 4 ya 1998
kif. 22

168.-(1) Pale mtu, katika shauri moja la Mahakama Kuu, anatiwa hatiani kwa makosa mawili au zaidi, Mahakama Kuu inaweza kumuadhibu kwa makosa hayo kwa adhabu mbalimbali zilizoainishwa kwa makosa hayo; na wakati zinahusu kifungo, adhabu hizo zitaanza moja baada ya kuisha kwa nyingine katika mpangilio ambao Mahakama Kuu inaweza kuelekeza isipokuwa kama Mahakama Kuu inaelekeza kwamba adhabu hizo zitekelezwe kwa pamoja.

(2) Pale mtu anatiwa hatiani katika shauri moja kwa makosa mawili au zaidi na mahakama ya chini mahakama inaweza, kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3), kumuadhibu kwa makosa hayo kwa adhabu mbalimbali zilizoainishwa kwa makosa hayo na ambazo mahakama ina mamlaka ya kuzitoa; na endapo adhabu hizo zinahusu kifungo, zitaanza moja baada ya kuisha kwa nyingine katika mpangilio ambao mahakama itaelekeza, isipokuwa kama mahakama itaelekeza kwamba adhabu zitatumikiwa kwa pamoja.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2), mahakama ya chini, katika yoyote ambayo imemtia hatiani mtu katika shauri moja kwa makosa mawili au zaidi, haitakuwa na mamlaka—

(a) pale mahakama inatoa adhabu halisi ya kifungu tu, kutoa adhabu za kifungo za kufuatana zinazidi kwa ujumla:—

(i) katika kesi yoyote ambayo katika kosa lolote ambalo mtuhumiwa ametiwa hatiani ni kosa ambalo mahakama ya chini inaweza kisheria kupitisha adhabu ya kifungo kwa kipindi kinachozidi miaka mitano, kipindi cha kifungo kwa miaka kumi; au

(ii) katika kesi yoyote nyingine, kipindi cha kifungo kwa miaka minane;

(b) pale ambapo mahakama itatoa adhabu ya faini tu, kutoa adhabu ya faini ambayo inazidi kwa ujumla —

(i) katika kesi yoyote ambayo katika kosa lolote ambalo mtuhumiwa ametiwa hatiani ni kosa ambalo mahakama ya chini inaweza kisheria kutoza faini inayozidi shilingi elfu kumi, kiasi ambacho ni sawasawa na mara tatu ya kiasi

ambacho mahakama ya chini inaweza kisheria kutoza;

(ii) katika kesi yoyote nyingine, kiasi cha shilingi elfu thelethini:

Isipokuwa kwamba kwa kushindwa kulipa faini jumla ya vifungo vinavyofuatana havitazidi muda wa kifungo cha miaka minane;

(c) pale ambapo mahakama inapitisha muunganiko wa adhabu halisi au adhabu za kifungo na faini, kutoa adhabu zinazozidi–

(i) jumla ya adhabu za vifungo vinavyofuatana iwapo ni adhabu za kifungo halisi au adhabu za kifungo kwa kushindwa kulipa faini, kwa miaka kumi; na

(ii) jumla ya faini ya shilingi elfu thelathini au kama kosa lolote kati ya makosa ambayo mtuhumiwa ametiwa hatiani ni kosa ambalo mahakama ya chini inaweza kisheria kutoza faini inayozidi shilingi elfu kumi, kiasi ambacho ni sawa sawa na mara mbili ya kiasi cha faini ambacho mahakama ya chini inaweza kisheria kutoza.

(4) Kwa madhumuni ya rufaa au kuthibitisha, jumla iliyotolewa chini ya kifungu hiki katika kesi za kutiwa hatiani kwa makosa mawili au zaidi katika shauri moja zitachukuliwa kuwa ni adhabu moja.

(5) Bila kujali kifungu kidogo cha (4), pale adhabu mbili au zaidi za kifungo zinaelekezwa kutumikiwa kwa pamoja, ni kipindi kirefu tu cha adhabu za vifungo hivyo kitatiliwa maanani katika ukokotoaji wa jumla ya adhabu ya kifungo kwa lengo la kifungu hiki.

(6) Pale ambapo mahakama imemtia hatiani mtu katika kesi ambayo inahusisha kosa la kujamiiana chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, mahakama itapitisha adhabu kama ilivyotajwa katika Sheria hiyo na kwa mujibu wa Sheria ya Adhabu za Chini.

Cap.16

Cap.19

Kuachwa kwa ushahidi uliopatikana kinyume cha sheria.

169.-(1) Iwapo, katika mwenendo wowote mahakamani kuhusiana na kosa, pingamizi linawekwa dhidi ya upokeaji ushahidi wa kukiri kwa misingi kwamba ushahidi ulipatikana kinyume na au kwa matokeo ya kukiuka, au kwa kushindwa kufuata masharti ya Sheria hii au Sheria nyingine yoyote, kuhusiana na mtu, mahakama itatakiwa, kwa hiari yake, kutopokea ushahidi isipokuwa kama, kwa kupima uwezekano, itaridhika kuwa kupokelewa kwa ushahidi ni dhahiri na kimsingi utafaidisha maslahi ya umma bila kuathiri haki na

uhuru wa mtu yoyote.

(2) Mambo ambayo mahakama inaweza kuyaangalia katika kuamua iwapo, katika mwenendo kuhusiana na kosa, itaridhishwa kama inavyotakiwa na kifungu kidogo cha (1) yanahusisha–

- (a) uzito wa kosa wakati wa upelelezi ambao masharti yalikiukwa, au hayakufuatwa, uharaka na ugumu wa kumtambua mtuhumiwa na uharaka au umuhimu wa kuhifadhi ushahidi wa jambo hilo;
- (b) asili na uzito wa ukiukwaji au kushindwa; na
- (c) kiwango ambacho ushahidi uliopatikana kwa kukiuka au kwa matokeo ya kukiuka au kwa matokeo ya kushindwa kufuata masharti ya sheria yoyote, ungeweza kupatikana kihalali kisheria.

(3) Wajibu wa kuithibitishia mahakama kwamba ushahidi uliopatikana kwa kukiuka au kwa matokeo ya kukiuka, au kwa matokeo ya kushindwa kufuata masharti ya Sheria hii upokelewe kwenye mwenendo utakuwa kwa upande ambao unataka ushahidi upokelewe.

(4) Kifungu hiki ni nyongeza katika, na si uvunjaji wa, sheria yoyote nyingine au kanuni ambayo mahakama inaweza kukataa kupokea ushahidi katika mwenendo.

(b) Mahakama za Chini

Adhabu ambazo mahamakama za chini zinaweza kutoa.
Sheria Na. 4 ya 1998 kif. 23; 9 ya 2002 jedwali.
Kurasa 90

170.-(1) Mahakama ya chini inaweza, katika kesi ambazo adhabu zake zimeruhusiwa kisheria, kupitisha adhabu mojawapo kati ya hizi zifuatazo:–

- (a) kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano; isipokuwa kwamba pale ambapo mahakama inamtia mtu hatiani kwa kosa lililotajwa katika jedwali lolote kwenye Sheria ya Adhabu za Chini ambayo mahakama ina mamlaka ya kusikiliza, itakuwa na mamlaka ya kupitisha adhabu ya chini ya kifungo;
- (b) faini isiyozidi shilingi milioni ishirini;
- (c) adhabu ya viboko kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Adhabu ya Viboko;

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1):–

- (a) adhabu ya kifungo:–
 - (i) kwa kosa la kwenye jedwali (kama ilivyofafanuliwa katika kifungu kidogo cha (5)), ambalo linazidi kipindi cha chini cha kifungo kilichotajwa kwa ajili hiyo na Sheria ya Adhabu za Chini;
 - (ii) kwa kosa lingine lolote ambalo linazidi miezi kumi na mbili ;
- (b) adhabu ya viboko inayozidi viboko kumi na mbili;

Cap.17

Cap.90

Cap.90

- (c) adhabu ya faini au kwa malipo ya fedha (nje ya malipo ya fidia chini ya Sheria ya Adhabu za Chini), inayozidi shilingi elfu sita,

haitatekelezwa au kutozwa mpaka rekodi ya kesi, au nakala yake iliyothibitishwa, imepelekwa Mahakama Kuu na adhabu au amri imethibitishwa na Jaji.

Isipokuwa kwamba kifungu hiki hakitatumika kuhusiana na adhabu yoyote itakayopitishwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa daraja au cheo chochote.

(3) Masharti ya kifungu kidogo cha (1) hayataathiri masharti ya sheria yoyote inayoruhusu mahakama ya chini kutoa adhabu kuhusiana na kosa lolote lililotajwa katika sheria hiyo, inayozidi adhabu iliyotolewa katika kifungu hicho kidogo.

(4) Masharti ya kifungu kidogo cha (2) yatatumika kuhusiana na adhabu ya kifungo hata kama adhabu hiyo ni adhabu ya msingi ya kifungo kwa kushindwa kulipa faini au ni muunganiko wa adhabu mbili.

Cap.90

(5) Katika kifungu hiki “kosa la kwenye jedwali” litakuwa na maana iliyopewa neno hilo katika Sheria ya Adhabu za Chini.

(6) Afisa polisi msimamizi wa kituo cha polisi anaweza, kama atajiridhisha kuwa mtu yeyote ametenda kosa ambalo adhabu yake haizidi shilingi laki mbili kwa amri chini ya mkono wake kumaliza kosa hilo kwa kumtaka mtu huyo kufanya malipo ya jumla ya fedha:

Isipokuwa kwamba–

- (a) jumla hiyo ya fedha itakuwa ni nusu ya adhabu ya juu inayotolewa kwa kosa hilo;
- (b) uwezo unaotolewa na kifungu hiki kidogo utatumika tu pale mtu anakiri kwa maandishi kwamba ametenda kosa;
- (c) afisa polisi atatoa risiti kwa mtu ambaye amepokea kiasi hicho cha fedha yake

Wakati ambao mahakama za chini zinaweza kupeleka shtaka Mahakama Kuu kwa kutoa adhabu.

171.-(1) Pale ambapo chini ya masharti ya Sheria hii mahakama ya chini inayoongozwa na Hakimu wa Wilaya itamtia hatiani mtu mzima yeyote kwa kosa iwapo, baada ya kupata taarifa kuhusiana na tabia yake na mengineyo kuhusu mtu huyo mzima au kuhusiana na mazingira ya kosa, mahakama ina maoni kuwa adhabu kubwa inatakiwa kutolewa kwa kosa zaidi ya ile ambayo mahakama ina mamlaka ya kutoa, mahakama inaweza, badala ya kumshughulikia kwa namna nyingine yoyote, kumweka mhalifu chini ya ulinzi wa Mahakama Kuu kwa adhabu kufuatana na masharti yafuatayo ya kifungu hiki.

(2) Pale ambapo mhalifu anapelekwa Mahakama Kuu kwa adhabu chini ya masharti ya kifungu hiki, Mahakama Kuu itachunguza mazingira ya kesi na itamshughulikia mhalifu kwa namna ambayo mtuhumiwa huyo angeshughulikiwa na Mahakama Kuu iwapo angetiwa hatiani na Mahakama Kuu kwa kosa hilo.

(3) Iwapo Mahakama Kuu itatoa adhabu kwa mtuhumiwa, masharti ya Sheria hii kuhusiana na rufaa dhidi ya kutiwa hatiani tu yatatumika kama ilivyo kwenye kesi nyingine inayosikilizwa na mahakama ya chini.

(4) Mahakama Kuu inaweza kwa hiari yake kuahirisha uchunguzi wake chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki mpaka mwisho wa muda wa kufungua taarifa ya rufaa dhidi ya kutiwa hatiani, na kama taarifa hiyo imefunguliwa mbele ya Mahakama Kuu itaanza uchunguzi huo mpaka uamuzi wa mwisho wa rufaa hiyo au rufaa zitakazofuata au kwa muda wowote mfupi kama mahakama itakavyoona inafaa.

(5) Pale mtu, ambaye amepolekwa Mahakama Kuu kwa adhabu kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1), atafungua taarifa ya rufaa dhidi ya kutiwa kwake hatiani, Mahakama Kuu au mahakama ya chini ambayo ilimtia hatiani inaweza, kwa sababu zitakazorekodiwa na mahakama kwa maandishi, ikatoa dhamana akiwa na au bila ya wadhamini akisubiri kusikilizwa kwa rufaa.

(6) Masharti ya kifungu hiki yatatafsiriwa kuiwezesha Mahakama Kuu katika uamuzi wake katika kesi yoyote iliyo chini yake kutumia uwezo wake wa marejeo chini ya kifungu cha 373 cha Sheria hii katika namna ileile kama vile rekodi ya mwenendo chini ya kifungu hicho imeripotiwa Mahakama Kuu kwa ajili ya amri.

Kuachiwa kwa dhamana kusubiri uthibitisho au uwezo wa mahakama inayothibitisha.

172.-(1) Wakati ambapo mahakama ya chini inapitisha adhabu ambayo inahitaji kuthibitishwa, mahakama inayotoa adhabu inaweza kwa hiari yake kumtoa mtu aliyeadhibiwa kwa dhamana ikisubiri kuthibitishwa au amri nyingine kama mahakama inayothibitisha inavyoweza kutoa.

(2) Pale:-

- (a) mtu emepolekwa mahabusu kwa adhabu ya Mahakama Kuu;
- (b) mtu amewekwa mahabusu akisubiri kuthibitishwa kwa adhabu yake na mahakama ya juu; au
- (c) mtu amekuwa mahabusu kwa kipindi akisubiri shauri lake,

adhabu yake hata kama ipo chini ya Sheria ya Adhabu za Chini, au katika sheria yoyote nyingine, itaanza kuhesabiwa pale adhabu hiyo itakapothibitishwa, kama itakavyokuwa, na adhabu hiyo itatilia maanani muda ambao mtu huyo amekuwa mahabusu.

(4) Iwapo mtu aliyeadhibiwa, wakati adhabu inapitishwa, anatumikia adhabu ya kifungo kwa kosa lingine kipindi cha kifungo ambacho ameadhibiwa kitalazimika, isipokuwa kama mahakama itaamuru vinginevyo, kuanza kutoka tarehe ya kuisha kwa adhabu ya kosa hilo lingine, kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (5).

(5) Mahakama Kuu inaweza kutumia uwezo uleule katika kuthibitisha kama ilivyopewa kwake katika marejeo na Sehemu ya X

ya Sheria hii.

(6) Mahakama inayothibitisha inaweza, kwa hiari yake, pale ambapo hakuna amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na mahakama iliyomtia hatiani, kumwachia kwa dhamana mtu aliyedhibiwa akisubiri amri katika marejeo na Mahakama Kuu katika kutumia uwezo wake chini ya kifungu cha 385 cha Sheria hii.

(7) Pale mtu anatiwa hatiani kwa kosa lililotajwa katika jedwali lolote katika Sheria ya Adhabu za Chini, masharti ya kifungu hiki yatatumika kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 8 cha Sheria hii.

Cap.19

(c) Mamlaka ya Ziada ya Mahakama za chini

Mamlaka ya ziada
Sheria Na. 32 ya
1994 jedwali.; 17 ya
1996 Jedwali.

173.-(1) Waziri baada ya kushauriana na Jaji Mkuu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa amri itakayotangazwa kwenye gazeti:-

- (a) kumpa hakimu mkazi yoyote uwezo wa kusikiliza kosa la aina yoyote ambalo, isipokuwa kwa masharti ya kifungu hiki tu, kwa kawaida yangesikilizwa na Mahakama Kuu na anaweza kuainisha eneo ambalo anaweza kutumia uwezo huo wa nyongeza; au
- (b) kumpa hakimu huyo yeyote uwezo wa kusikiliza kila, kesi iliyotajwa au kesi za makosa hayo na hakimu huyo atakuwa na, kwa mujibu wa amri, uwezo wa kutoa, kuhusiana na makosa yaliyotajwa kwenye amri hiyo, adhabu yoyote ambayo kisheria ingetolewa na Mahakama Kuu.

(2) Hakuna kitu katika kifungu hiki kitaathiri uwezo wa Mahakama Kuu kuamuru kuhamishwa kwa kesi.

(3) Kwa madhumuni ya rufaa yoyote kutoka au marejeoya uamuzi wake katika kutumia mamlaka hayo, hakimu mkazi huyo atachukuliwa kuwa ni jaji wa Mahakama Kuu, na mahakama anayoiongoza naye wakati akitumia mamlaka hayo itachukuliwa kuwa ni Mahakama Kuu.

Uendeshaji uwe kwa
msaada wa wazee
wa baraza.

174. Makosa yote yatakayosikilizwa chini ya kifungu cha 173 yatalazimika kusikilizwa kwa msaada wa wazee wa baraza wawili au zaidi na katika namna ilivyowekwa ya **usikilizaji wa makosa** na Mahakama Kuu.

Imefutwa

175. [Imefutwa na Sheria Na. 32 ya 1994 Jedwali.]

Kumbukumbu na
ripoti kupelekwa
kwa Rais.

176. Katika kila kesi ambayo adhabu ya kifo imethibitishwa na Mahakama Kuu, jaji anayethibitisha adhabu atalazimika, haraka kama itakavyokuwa, kupeleka rekodi ya kesi au nakala yake ya kweli

iliyothibitishwa kwa Rais pamoja na ripoti kwa maandishi aliyoisaini ikiambatanisha pendekezo lolote au maoni yoyote ambayo ataona vema kuweka na kupeleka kwa pamoja na pendekezo lolote au maoni yaliyotolewa na mahakama iliyomuadhibu mtuhumiwa; na baada ya hapo hilo suala litashughulikiwa chini ya kifungu cha 325 cha Sheria hii.

B. – Mashauri kwa ujumla
(a) Mahali pa Uchunguzi au Kusikilizwa

Mamlaka ya ujumla ya Mahakama za Tanzania.

177. Kila Mahakama ina mamlaka ya kuamuru kuletwa mbele yake mtu yeyote ambaye yupo kwenye eneo la mipaka ya mamlaka yake na anashitakiwa kwa kosa lililotendwa Tanzania au ambalo kwa mujibu wa sheria linaweza kushughulikiwa kama vile limetendwa ndani ya Tanzania na kumshughukia mtuhumiwa kwa mujibu wa mamlaka yake.

Uwezo wa Mahakama Kuu kuchunguza na kuendesha makosa

178. Mahakama Kuu inaweza kuchunguza au kusikiliza kosa lolote kwa kuzingatia mamlaka yake katika mahali popote ambapo ina uwezo wa kuitisha vikao; na, isipokuwa kama iliyotolewa chini ya kifungu cha 93, hakuna kosa la jinai litakalopelekwa chini ya mamlaka ya Mahakama Kuu isipokuwa kama limechunguzwa kwanza na mahakama ya chini na mtuhumiwa amepelekwa Mahakama Kuu kwa kusikilizwa.

Mahali na tarehe ya kikao cha Mahakama Kuu.

179.-(1) Katika kutekeleza mamlaka yake ya **kwanza** ya jinai Mahakama Kuu itaitisha vikao mahali na katika siku zile kama Jaji Mkuu atakavyoelekeza.

(2) Msajili ya Mahakama Kuu atalazimika kama kawaida kutoa taarifa kabla ya vikao vyote.

Sehemu ya kawaida ya uchunguzi na uendeshaji mashitaka.

180. Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 178 na kwa uwezo wa kuhamisha unayotolewa na vifungu vya 189,190 na 191, kila kosa litalazimika kuchunguzwa na kusikilizwa, kama itakavyokuwa, na mahakama yenye mamlaka ndani ya mipaka ya eneo ambalo kosa limetendwa au ndani ya mipaka ya eneo ya mamlaka ambamo mtuhumiwa alikamatwa, au akiwa katika ulinzi kwa mashitaka ya kosa, au amehudhuria kujibu wito ulitolewa kisheria ukimshitaki kwa kosa.

Uendeshaji mashitaka sehemu kosa lilipotendeka au sehemu matokeo ya kosa yalijitokeza.

181. Wakati mtu anatuhumiwa kwa kutenda kosa kwa sababu ya kitu chochote kilichotendeka au kwa matokeo yoyote ambayo yametokea, kosa linaweza kuchunguzwa kwa undani au kusikilizwa, kama kesi itakavyokuwa, na mahakama iliyo ndani ya mipaka yenye mamlaka ambako kitu chochote hicho kimefanyika au matokeo yoyote hayo yametokea.

Uendeshaji wa shitaka iwapo kosa

182. Wakati tendo ni kosa kwa kulihusisha na tendo lolote

linahusiana na kosa lingine.

lingine ambalo vilevile ni kosa au ambalo litakuwa ni kosa kama mtendaji angekuwa na uwezo wa kutenda kosa, shtaka la kosa lililotajwa linaweza kuchunguzwa kwa undani au kusikilizwa na mahakama ndani ya mipaka yenye mamlaka ambapo kosa mojawapo lilitendwa

Uendeshaji wa shitaka kama mahali pa kosa hapana uhakika

183. Wakati hakuna uhakika ni wapi kati ya maeneo mengi kosa lilitendeka au kama kosa limetendwa kwa sehemu katika mipaka ya eneo moja na kwa sehemu katika mipaka ya eneo lingine au kama inajumuisha matendo mengi yaliyotendwa katika maeneo mbalimbali, litaweza kuchunguzwa au kusikilizwa na mahakama yenye mamlaka katika moja ya mipaka ya maeneo hayo.

Kosa lililotendeka safarini.

184. Kosa lililotendwa wakati mshitakiwa akiwa katika safari linaweza kuchunguzwa au kusikilizwa na mahakama ndani ya mipaka ya eneo lenye mamlaka ambamo mshitakiwa au dhidi ya mtu ambaye au kitu kinachohusiana na utendaji wa kosa kilipita wakati wa safari.

Mahakama Kuu inaweza kuamua mahakama inayofaa kukiwa na mashaka.

185. Wakati wowote mashaka yanajitokeza kuhusiana na mahakama ambayo kosa litatakiwa kuchunguzwa au kusikilizwa mahakama yoyote yenye mashaka hayo inaweza, katika utashi wake, kuripoti mazingira hayo Mahakama Kuu na Mahakama Kuu italazimika kuamua ni mahakama ipi kosa litalazimika kuchunguzwa au kusikilizwa; na uamuzi wa Mahakama Kuu utakuwa wa mwisho na unaohitimisha isipokuwa itakuwa wazi kwa mtuhumiwa kuonyesha kuwa hakuna mahakama katika Tanzania yenye mamlaka katika kesi hiyo.

Mahakama kuwa mahakama ya wazi Sheria Na. 4 ya 1998 kif. 24

186 (1) Mahali ambapo mahakama yoyote imekaa kwa ajili ya kuchunguza au kusikiliza kosa lolote patalazimika, isipokuwa kama kinyume chake kimeelezwa wazi katika sheria yoyote, kuchukuliwa kuwa ni mahakama ya wazi ambayo watu wote watakuwa na fursa ya kuhudhuria kwa kiasi ambacho pataweza kuwachukua, isipokuwa kwamba hakimumu au jaji **aliyekaa** anaweza, kama ataona ni muhimu au itaharakisha–

- (a) katika **shauri ya katikati ya shauri**; au
- (b) katika mazingira ambayo kutangazwa kutakuwa na madhara kwa maslahi ya–
 - (i) haki, ulinzi, usalama wa umma, amani ya umma au maadili ya umma; au
 - (ii) maslahi ya watu walio chini ya umri wa miaka kumi na nane au kulinda maisha binafsi ya watu wanahusika katika shauri,

kuamuru katika hatua yoyote ya uchunguzi au usikilizwaji wa kesi yoyote mojawapo kwa watu kwa ujumla au mtu fulani nje

ya wahusika ambao si wenye kesi au wawakilishi wao wa kisheria hawatakuwa na fursa ya kuingia au kuwa au kubaki katika chumba au jengo linalotumika na mahakama.

(2) Mahakama yoyote inaweza, kwa lengo la kuchunguza au kusikiliza kosa lolote, kukaa jumapili au siku ya mapumziko na hakuna uamuzi, adhabu au amri itakayopitishwa na mahakama yenye mamlaka halali kubadilishwa kwa sababu ya ukweli kuwa ilitolewa au ilipitishwa jumapili au siku ya mapumziko; lakini mahakama haitalazimika kukaa jumapili au siku ya mapumziko isipokuwa kama ni maoni ya mahakama kwamba kutokufanya hivyo kutasababisha kuchelewesha, gharama au usumbufu ambao katika mazingira ya kesi hautakuwa wa busara.

(3) Bila kujali masharti ya sheria nyingine yoyote, ushahidi wa watu wote katika mashauri yote yanayohusisha makosa ya kujamiiana yatapokelewa na mahakama katika mahakama ya siri, na ushahidi na mashahidi waliohusika katika shauri hawatatangazwa na au katika gazeti lolote au chombo kingine cha habari, lakini kifungu hiki kidogo hakitazuia kuchapisha au kutangaza jambo lolote kwa nia njema katika ripoti za sheria au gazeti au jarida la kitaalamu ambalo kwa nia njema linatarajiwa kusambazwa kati ya wajumbe wa fani ya sheria au udaktari.

Kuzuiwa kwa watoto kuhudhuria usikilizaji wa kesi mahakamani

187. Hakuna mtoto atakayeruhusiwa kuwa mahakamani wakati wa shauri la mtu yoyote mwingine anayeshitakiwa kwa kosa au wakati wa mwenendo wa mwanzo wa shauri hilo isipokuwa katika muda huo ambapo uwepo wake utahitajika kama shahidi au vinginevyo kwa madhumuni ya haki; na mtoto yeyote aliye mahakamani wakati chini ya kifungu hiki haruhusiwi kuwepo ataamuriwa kuondolewa; lakini hiki kifungu hakitatumika kwa wahudumu, maafisa sheria, makarani au watu wengine wanaotakiwa kuhudhuria mahakamani kwa madhumuni yanayohusiana na ajira zao.

Mahakama inaweza kuzuia kutangazwa kwa majina, nk., ya wahusika au mashahidi.

188. Mahakama inaweza kuzuia utangazaji wa majina au utambulisho wa wahusika kwenye kesi au mashahidi kwa ajili ya kuen deleza kwa au kwa manufaa ya usimamizi wa haki.

(b) Kuhamishwa kwa kesi

Kuhamishwa kwa kesi ikiwa kosa lilitendeka nje ya mamlaka.

189.-(1) Iwapo baada ya kusikiliza lalamiko lolote itaonekana kwamba chanzo cha lalamiko kilitokea nje ya mipaka ya eneo la mamlaka ya mahakama ambayo lalamiko limepelekwa, mahakama inaweza kwa utashi wake yenyewe kuelekeza kesi ihamishiwe kwenye mahakama yenye mamlaka katika eneo ambalo chanzo cha lalamiko kilitokea.

(2) Iwapo mtuhumiwa yuko chini ya ulinzi, na mahakama

inayoelekeza uhamisho inafikiri ni kwa haraka mtu huyo aendelee kushikiliwa au kama hayuko chini ya ulinzi, kwamba awekwe chini ya ulinzi huo, mahakama italazimika kumwelekeza mtuhumiwa kuchukuliwa na afisa polisi mbele ya mahakama yenye mamlaka mahali ambapo chanzo cha lalamiko kilitokea na italazimika kutoa hati kwa dhumuni hilo kwa afisa, na atalazimika kumpa lalamiko na wadhamini, kama wapo, iliyochukuliwa na mahakama, itakayopelekewa kwenye mahakama ambayo mtuhumiwa atapelekwa, na malalamiko na dhamana, vitalazimika kuchukuliwa kwa nia na madhumuni yote kama vile vimechukuliwa na mahakama iliyotajwa mwisho.

(3) Iwapo mtuhumiwa haendelei au hajawekwa chini ya ulinzi kama ilivyotajwa, mahakama itamtaarifu kwamba imeelekeza kuhamishwa kwa kesi na baada ya hapo masharti ya kifungu kidogo cha (2) kuhusiana na kuhamisha na uhalali wa nyaraka katika kesi utatumika.

Kuhamisha kesi kati ya mahakimu.

190. Hakimu yeyote wa wilaya–

- (a) anaweza kuhamisha kesi yoyote ambayo ameichukua kwa uchunguzi au usikilizaji kwenda mahakama yoyote ya chini ambayo ina mamlaka ya kuichunguza au kuisikiliza kesi hiyo ndani ya mipaka ya eneo la mamlaka ya hakimu huyo; na
- (b) anaweza, kama kwa ujumla nafasi ya wahusika au mashahidi inahitaji, kuhamisha kesi yoyote ambayo ameichukua kwa uchunguzi au usikilizaji kwenda mahakama yoyote ya chini nje ya mipaka ya mamlaka yake ambayo ina uwezo wa kuchunguza au kusikiliza kesi hiyo.

Uwezo wa Mahakama Kuu kubadili sehemu ya kuendeshea kesi

191.-(1) Wakati wowote itakapofanywa kuonekana na Mahakama Kuu–

- (a) kwamba uchunguzi au usikilizaji wa haki na usio wa upendeleo hauwezi kufanyika katika mahakama yoyote ya chini yake;
- (b) kwamba maswali fulani ya kisheria yenye ugumu usio wa kawaida yanaweza kujitokeza;
- (c) kwamba kuona sehemu ile au karibu na ambapo kosa lilitendeka unaweza kuhitajika kwa ajili ya uchunguzi au usikilizaji wa kosa wa kuridhisha ;
- (d) kwamba amri chini ya kifungu hiki kwa ujumla itakiwa ni kwa manufaa ya wahusika au mashahidi ; au
- (e) kwamba amri chini ya kifungu hiki ni kwa kuharakisha kutendeka kwa haki au kama inavyotakiwa na masharti yoyote ya Sheria hii;

inaweza kuamuru:–

- (i) kwamba kosa lolote lichungunzwe au kusikilizwa na mahakama yoyote isiyo na mamlaka chini ya vifungu vya 164 hadi 190 lakini kwa jinsi nyingine ina mamlaka ya kuchunguza au kusikiliza kosa hilo;
- (ii) kwamba kesi fulani ya jinai au daraja la kesi lihamishwe kutoka kwenye mahakama ya chini kwenye mamlaka yake kwenda mahakama yoyote nyingine yenye mamlaka sawa au mamlaka kubwa zaidi;
- (iii) kwamba mtuhumiwa aletwe mbele yake kwa kusikilizwa.

(2) Mahakama Kuu inaweza kutenda aidha kwa mujibu wa ripoti ya mahakama ya chini au kwa maombi ya mhusika mwenye maslahi au kwa uamuzi wake yenyewe.

(3) Kila maombi kwa ajili ya kutekeleza uwezo unaotolewa na kifungu hiki utalazimika kufanywa kwa maombi ambayo yatalazimika, isipokuwa kama mwombaji ni Mkurugenzi wa Mashitaka, yakiambatana na hati ya kiapo.

(4) Kila mtuhumiwa anayefanya maombi atalazimika kutoa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka taarifa kwa maandishi ya maombi, pamoja na nakala ya sababu ambazo yanaombewa na hakuna amri italazimika kufanywa kuhusiana na maombi isipokuwa mpaka masaa ishirini na nne yamepita kati ya kutoa hiyo taarifa na kusikilizwa kwa maombi.

(5) Pale mtuhumiwa amefanya maombi Mahakama Kuu inaweza kumuelekeza kutoa dhamana, na au bila wadhamini, kwa masharti kwamba, kama atatiwa hatiani, atalipa gharama za mwendesha mashitaka..

(c) Shauri Liliongezwa na Kumalizwa kwa Kesi

Kusikilizwa kwa utangulizi kuamua mambo yanayobishaniwa. Sheria Na. 19 ya 1992 kif. 2

192.-(1) Bila kujali masharti ya kifungu cha 229, iwapo mtuhumiwa atakiri kutokuwa na kosa mahakama italazimika kwa haraka iwezekanavyo, kuendesha usikilizaji wa awali katika mahakama ya wazi katika uwepo wa mtuhumiwa au wakili wake (kama anawakilishwa na wakili) na mwendesha mashitaka wa umma kuzingatia mambo ambayo hayabishaniwi kati ya wahusika na ambayo yataongeza shauri la haki na kwa haraka.

(2) Katika kuchambua mambo hayo ambayo hayabishaniwi mahakama itaeleza kwa mtuhumiwa ambaye hawakilishwi na wakili kuhusiana na asili na madhumuni ya usikilizaji wa awali na inaweza kuuliza maswali kwa wahusika kama itakavyoona inafaa; na majibu ya maswali hayo yanaweza kutolewa bila kiapo au uthibitisho.

(3) Katika kuhitimisha usikilizaji wa awali iliofanywa chini ya kifungu hiki, mahakama itaandaa **maandiko ya kumbukumbu** ya mambo yaliyokubaliwa na kumbukumbu italazimika kusomwa na

kufafanuliwa kwa mtuhumiwa katika lugha anayoilewa, iliyosainiwa na mtuhumiwa na wakili wake (kama yupo) na mwendesha mashitaka wa umma, na halafu itahifadhiwa kwenye faili.

(4) Jambo lolote au waraka uliokiriwa au kukubaliwa (kama hilo jambo au waraka umetajwa kwenye muhtasari wa ushahidi au hapana) katika kumbukumbu iliyofailiwa chini ya kifungu hiki itachukuliwa kama vile imethibitishwa ipasavyo, isipokuwa kama, wakati wa mwenendo wa usikilizaji, mahakama ina maoni kwamba maslahi ya haki yanahitaji hivyo, mahakama inaweza kuelekeza kwamba jambo au waraka wowote uliokiriwa au kukubaliwa katika kumbukumbu iliyofailiwa chini ya kifungu hiki iweze kuthibitishwa rasmi.

(5) Pale ambapo inawezekana, mtuhumiwa atalazimika kushauriwa mara moja baaada ya usikilizaji wa awali na kama kesi inatakiwa kuahirishwa kutokana na kutokuwepo kwa mashahidi au sababu nyingine, hakuna kitu katika kifungu hiki kitatafsiriwa kikimtaka jaji au hakimu huyohuyo ambaye aliendesha usikilizaji wa awali chini ya kifungu hiki kuendesha shauri.

(6) Waziri anaweza, baada ya kuwasiliana na Jaji Mkuu, kwa amri itakayotangazwa kwenye gazeti kutengeneza kanuni kwa ajili utendaji mzuri wa madhumuni ya kifungu hiki na bila kuathiri kwa ujumla kilichoelezwa, kanuni zinaweza kutoa:-

- (a) ucheleweshwaji wa kuwaita mashahidi mpaka itakapojulikana kama watahitajika kutoa ushahidi kwenye shauri au hapana;
- (b) utolewaji wa taarifa kwa mashahidi ukiwaonya kwamba wanaweza kuhitajika kuhudhuria mahakamani kutoa ushahidi wakati wa shauri.

Mtuhumiwa wa
makosa ya hati
anaweza kukiri kosa
bila kufika
mahakamani

193.-(1) Mtu ambaye awali alishitakiwa kwa kosa la hati ambalo linaadhibiwa tu kwa faini au kwa kifungu kisichozidi miezi sita au kwa muungano wa hizo adhabu anaweza, kwa maandishi au kwa kupitia kwa wakili, kukiri makosa kwenye mashtaka kama mtu huyo ameitwa au hakuitwa na hakimu atalazimika kutohitaji mtuhumiwa kuhudhuria yeye mweyewe isipokuwa kama kuhudhuria yeye mwenyewe kunahitajika kwa sababu yoyote nyingine ambapo anaweza kuelekeza mtuhumiwa kuhudhuria yeye mwenyewe.

(2) Iwapo hakimu ametoa faini kwa mtuhumiwa ambaye kuhudhuria yeye mwenyewe hakuhitajiki chini ya kifungu hiki, na faini hiyo haijalipwa ndani ya muda uliotolewa kwa malipo hayo hakimu anaweza hapohapo **kutoa wito** kumuita mtuhumiwa kutoa sababu kwanini asipelekwe jela kwa muda huo ambao hakimu atautaja; lakini kama mtuhumiwa hatahudhuria baada ya kurudishwa kwa wito hakimu anaweza hapohapo kutoa hati na kumpeleka jela kwa kipindi ambacho hakimu anaweza kuamua.

(3) Iwapo, katika kesi yoyote ambayo chini ya kifungu hiki

kuhudhuria kwa mtuhumiwa hakuhitajiki, kutiwa hatiani kulikopita kukatajwa dhidi yake na hakujakiriwa kwa maandishi au kwa kupitia wakili wa mtu huyo hakimu anaweza kuahirisha mwenendo na kuelekeza kuhudhuria binafsi kwa mtuhumiwa na, kama inahitajika, kuhakikisha anahudhuria kwa namna iliyotolewa chini ya Sheria hii.

(4) Wakati wowote kuhudhuria kwa mtuhumiwa kunapokuwa hakuhitajiki na kuhudhuria baadaye kunahitajika, gharama za kila kuahirishwa kwa madhumuni hayo zitalazimika kubebwa katika kila tukio na mtuhumiwa.

Utaratibu kama mtuhumiwa anataka kukiri kosa lisilo la hati au anataka kujitetea kuwa hakuwepo eneo la tukio.

194.-(1) Pale mtuhumiwa anashitakiwa kwa kosa lisilo la hati, tofauti na kosa linaloadhibiwa kwa kifo au kifungu cha maisha, anakusudia kukiri kuwa na hatia kwenye kosa na anataka kesi yake imalizwe mara moja anaweza, kutoa taarifa ya maandishi kwa lengo hilo kwa hakimu ambaye kesi itasikilizwa mbele yake, na itakuwa ni halali kisheria kwa hakimu kumpelekea mtuhumiwa mashitaka rasmi na taarifa ya kuhudhuria mahakamani, sio pungufu ya siku nne kamili, mbele ya hakimu kwa dhumuni la kukiri kuwa na hatia kwenye makosa na kumalizwa kabisa kwa kesi.

(2) Iwapo mtuhumiwa kufuatia taarifa iliyopelekwa kwake chini ya kifungu kidogo cha (1) atahudhuria na kukiri kuwa na hatia kwenye shitaka, hakimu atalazimika kuishughulikia kesi kwa namna inayofanana na pale ambapo mtuhumiwa amekiri kuwa na hatia chini ya kifungu cha 229 isipokuwa kwamba kama ni kesi ambayo inatakiwa kusikilizwa Mahakama Kuu tu au ni kubwa kwa asili hakimu anafikiri kwamba suala la adhabu likaamuliwe na mahakama hiyo, hakimu atampeleka mtuhumiwa kwenye mahakama hiyo kwa adhabu, na kupelekwa huko kutakuwa ni hati inayojitosheleza kumleta mtuhumiwa, bila ya taarifa ya ziada, mbele ya Mahakama Kuu kwa adhabu; na hati ya awali ya kupelekwa kwa muda huo mpaka atakapoachiliwa katika mwenendo wa sheria utalazimika kubaki ukitumika hadi atakapoletwa mbele ya Mahakama Kuu kwa adhabu.

(3) Iwapo mtuhumiwa aliyeletwa mbele ya hakimu kwa ajili ya kukiri kuwa na hatia hataki kuwa na hatia kwenye shitaka au akakiri kuwa na hatia kwa sehemu tu ya shitaka, hakimu hata kubali ukiri huo wa masharti, na kukiri kutalazimika kumalizwa kwa *pro loco et tempore*, na baada ya hapo taratibu dhidi ya mtuhumiwa zitalazimika kuendelea kwa kufuata masharti mengine ya Sheria hii.

(4) Pale mtuhumiwa anakusudia kutumia utetezi wa kutokuwepo eneo la tukio la kosa katika utetezi wake, atalazimika kutoa taarifa kwa mahakama na upande wa mashitaka kwa lengo la kutumia utetezi huo kabla ya kusikilizwa kwa kesi.

(5) Pale mtuhumiwa hajatoa taarifa ya nia ya kutumia utetezi wa kutokuwepo kwenye eneo la tukio la kosa kabla kuanza kusikilizwa kwa kesi, atalazimika kuupatia upande wa mashitaka maelezo ya kutokuwepo huko muda wowote kabla ya kesi ya upande wa mashitaka

haijafungwa.

(6) Iwapo mtuhumiwa atajitetea kuwa hakuwepo katika eneo la tukio la kosa bila kwanza kuwataarifu upande wa mashitaka kwa mujibu wa kifungu hiki, mahakama inaweza kwa uamuzi wake, kutoupa uzito wowote kwenye utetezo huo.

C. – Kuwahoji Mashahidi

(a) Masharti ya jumla

Uwezo wa kuita shahidi muhimu au kuhoji mtu aliyepo

195.-(1) Mahakama yoyote inaweza, katika hatua yoyote ya shauri au mwenendo mwingine chini ya Sheria hii, kumuita mtu yeyote kama shahidi au kumhoji mtu yeyote aliyehudhuria, ingawaje hakuitwa kama shahidi, kumuita tena na kumhoji tena mtu yoyote ambaye tayari amehojiwa; na mahakama italazimika kumwita na kumhoji au kumuita tena na kumhoji tena mtu yeyote huyo kama ushahidi wake unaonekana kuwa ni muhimu kwa uamuzi wa haki wa kesi.

(2) Mwendesha mashitaka au mtuhumiwa au wakili wake, atalazimika kuwa na haki ya kumhoji tena mtu huyo, na mahakama italazimika kuahirisha kesi kwa dhumuni hilo kama itaona kuwa ni muhimu.

Ushahidi uchukuliwe mbele ya mtuhumiwa

196. Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo, ushahidi wote utakaochukuliwa kwenye shauri lolote chini ya Sheria hii utalazimika kuchukuliwa mbele ya mtuhumiwa, isipokuwa kama kuhudhuria kwake binafsi hakuhitajiki.

Ushahidi waweza kuchukuliwa bila kuwepo mtuhumiwa katika mazingira fulani.
Sheria Na 5 ya 1988 kif. 8

197. Bila kujali masharti ya kifungu cha 196, ushahidi unaweza kuchukuliwa katika shauri lolote chini ya Sheria hii pasipokuwepo mtuhumiwa iwapo:–

(a) jaji au hakimu anayehoji anaona kwamba kwa sababu ya matendo yake ya hovyoyote mbele yake haiwezekani kwa ushahidi kutolewa mbele yake; au

(b) hawezi kuwepo kwa sababu za kiafya lakini anawakilishwa na wakili na amekubali kuwa ushahidi utolewe bila yeye kuwepo,

na itakuwa ni halali kisheria kwa mahakama kuendelea na shauri na kutoa hukumu bila ya kuwepo mtuhumiwa.

Ushahidi utolewe kwa kiapo

Sura ya .334

198.-(1) Kila shahidi kwenye jambo au kesi ya jinai atalazimika, kwa kuzingatia masharti ya sheria nyingine yoyote zinazoelezea vinginevyo, kuhojiwa kwa kiapo au uthibitisho kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Viapo na Matangazo ya Kisheria.

(2) Pale mtuhumiwa, baada ya kuhojiwa, ataamua kukaa kimya mahakama itakuwa na haki ya kuona kuwa anayoulizwa ni kweli na mahakama na upande wa mashitaka unaweza kutoa maoni kuhusiana

na kushindwa kwa mtuhumiwa kutoa ushahidi.

Shaidi anayegeuka.

199.-(1) Wakati wowote mtu yeyote, anayehudhuria aidha kwa kuheshimu wito au kwa mujibu wa hati, au akiwepo mahakamani na akatakiwa na mahakama kutoa ushahidi wa mdomo:-

- (a) anakataa kuapishwa au kuthibitishwa;
- (b) baada ya kuapishwa au kuthibitishwa, anakataa kujibu swali lolote analoulizwa;
- (c) anakataa au anadharau kutoa waraka wowote au kitu ambacho anatakiwa kukitoa; au
- (d) anakataa kusaini ushahidi wake,

bila, katika kesi yoyote, kutoa sababu za msingi kwa kukataa huko au kuzembea, mahakama inaweza kuahirisha kesi kwa muda usiozidi siku nane na inaweza katika muda huo kumpeleka mtu huyo jela, isipokuwa kama baada ya hapo atakubali kufanya kile anachotakiwa kufanya.

(2) Iwapo mtu huyo, baada ya kuletwa mbele ya mahakama siku ya au kabla ya kusilizwa kulikoahirishwa, anakataa tena kufanya kile anachotakiwa kufanya mahakama inaweza, kama itaona inafaa, kuahirisha tena kesi na kumpeleka mtu huyo jela kwa muda kama ule; na hivyo tena mara kwa mara hadi atakapokubali kufanya kile anatakiwa kukifanya.

Utaratibu kama mtuhumiwa ni shahidi pekee aliyetitwa katika utetezi

200. Pale shahidi pekee kwenye ukweli wa kesi aliyetitwa kwa utetezi ni mtu aliyeshitakiwa, atalazimika kuitwa kama shahidi baada ya kufungwa kwa ushahidi wa upande wa mashitaka, lakini itakuwa halali kisheria kwa mahakama kwa uamuzi wake yenyewe kuahirisha usilikizaji wa kesi mpaka muda na wakati fulani palipoteuliwa na kutajwa wakati mtuhumiwa akiwepo na akisikia.

Haki ya kujibu Sheria Na. 27 ya 2008 kif.31

201. Katika mambo ambayo haki ya kujibu chini ya kifungu cha 296 kunategemea suala kama ushahidi umeitwa kwa ajili ya utetezi, ukweli kwamba mtu aliyeshitakiwa ameitwa kama shahidi hautalazimika kama sababu pekee ya kutoa haki kwa upande wa mashitaka haki ya kujibu isipokuwa kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mshitaka wanapohudhuria kama wakili wa upande wa mashitaka watalazimika katika mambo yote kuwa na haki ya kujibu.

Cheti kuhusiana na alama za picha, nk., zinazopokelewa katika ushahidi

202.-(1) Katika uchunguzi wowote, usikilizaji au mwenendo mwingine chini ya Sheria hii cheti katika muundo ulio katika Jedwali la Tatu la Sheria hii, kilichotolewa chini ya mkono wa afisa aliyeteuliwa kwa amri ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa dhumuni hilo, ambaye atakuwa ametayarisha picha za kuchapisha au picha za kukuzwa kutoka katika mkanda ulio wazi pamoja na picha za kuchapishwa zozote, picha za kukuzwa na viambatanisho vingine vilivyorejewa humo ndani, utakuwa ni ushahidi wa ukweli ulioelezwa

kwenye cheti.

(2) Mahakama inaweza kudhania kuwa sahihi kwenye cheti hicho ni halisi.

(3) Wakati cheti hicho kinatumika katika shauri lolote au mwenendo chini ya Sheria hii nje ya uchunguzi mahakama inaweza, kama inafikiri inafaa, kumwita na kumhoji mtu aliyetoa cheti.

Taarifa ya
Mchambuzi wa
Serikali.

203.-(1) Waraka wowote unaochukuliwa kuwa ni taarifa chini ya mkono wa mchambuzi wa serikali juu ya suala au kitu chochote kilichowasilishwa rasmi kwake kwa majaribio au uchambuzi na taarifa katika harakati za mwenendo chini ya Sheria hii, vinaweza kutumika kama ushahidi katika uchunguzi wowote, shauri au mwenendo chini ya Sheria hii.

(2) Mahakama inaweza kudhania kwamba sahihi kwenye waraka wowote huo ni halali na kwamba mtu aliyeisaini alishika wadhifa katika ofisi anayosema kuwa aliishikilia wakati anasaini waraka huo.

(3) Wakati taarifa yoyote itatumika hivyo katika mwenendo wowote nje ya uchunguzi mahakama inaweza, kama itaona inafaa kumwita na kumhoji mchambuzi kuhusiana na kilichomo kwenye taarifa hiyo.

(4) Katika kifungu hiki “mchambuzi wa serikali” inajumuisha mwanapatholojia mwandamizi, mwanapatholojia na mtu yoyote aliyeteuliwa na Waziri anayehusika na mambo ya afya kufanya kazi za mchambuzi wa serikali chini ya kifungu hiki.

Taarifa ya mtaalamu
wa alama za vidole.

204.-(1) Waraka wowote chini ya mkono wa afisa aliyeteuliwa kwa dhumuni hilo kwa amri ya Mkurugenzi wa Mashitaka, ambayo inachukuliwa kuwa ni taarifa juu ya alama zozote za vidole, au picha zozote za alama za vidole vilivyolewa kwake kwa uchunguzi au ulinganisho, utalazimika kupokelewa katika ushahidi katika uchunguzi wowote, shauri la mwenendo mwingine chini ya Sheria hii na utakuwa ni ushahidi wa ukweli wote ulioelezwa kwenye waraka huo.

(2) Mahakama inaweza **kudhania** kwamba sahihi kwenye taarifa yoyote ni halisii.

(3) Wakati taarifa yoyote inapokelewa kama ushahidi katika shauri au mwenendo wowote chini ya Sheria hii nje ya uchunguzi mahakama inaweza, kama itaona inafaa, na italazimika kama ikiombwa hivyo na mtuhumiwa au wakili wake, kumwita na kumuhoji au kumuweka tayari kwa kuhojiwa tena mtu aliyetoa taarifa hiyo.

(4) Katika kifungu hiki “alama za vidole” zinajumuisha alama za kiganja, alama za vidole vya miguu na alama za unyayo..

Taarifa ya mtaalamu
wa mwandiko.

205.-(1) Katika kila **mwenendo wa kuhamisha**, shauri au mwenendo mwingine na au mbele ya hakimumu au jaji chini ya Sheria hii,

taarifa katika muundo uliowekwa katika Jedwali la Tatu kwenye Sheria hii, iliyotolewa chini ya mkono wa afisa aliyeteuliwa kwa amri ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa madhumuni hayo, ikiwa ni taarifa juu ya mwandiko wowote, au picha zinazoonyesha za mwandiko wowote, zilizoletwa kwake kwa ajili ya uchunguzi au ufananisho, pamoja na kila alama za picha, zilizokuzwa au viambatanisho vingine vilivyorejewa ndani yake na vilivyosainiwa na afisa huyo, vitalazimika kupokelewa kwenye ushahidi na vitalazimika kuwa ushahidi wa mambo yaliyoelezwa humo ndani.

(2) Mahakama inaweza **kudhania** kwamba sahihi kwenye taarifa yoyote chini ya kifungu hiki, alama, vilivyokuzwa au viambatanisho ni halisi.

(3) Wakati taarifa yoyote chini ya kifungu hiki inapokelewa kama ushahidi katika shauri lolote au mwenendo chini ya Sheria hii nje ya uchunguzi, mahakama italazimika, kama mtuhumiwa au wakili wake ameomba hivyo na inaweza kama itaona inafaa kumwita na kumhoji mtu aliyetoa taarifa hiyo au kuweka tayari kwa ajili ya kuhojiwa tena.

(b) Kutolewa kwa Kamisheni kwa Kuwahoji Mashahidi

Kutolewa kwa kamisheni.

206.-(1) Wakati wowote katika harakati za mwenendo wowote chini ya Sheria hii, Mahakama Kuu au hakimu wa wilaya ikiridhika kwamba kumuhoji shahidi ni muhimu kwa ajili ya utendekaji wa haki, na kwamba kuhudhuria kwa shahidi huyo hakuwezi kupatikana bila ucheleweshwaji, gharama au usumbufu ambao, katika mazingira ya kesi, utakuwa hauna msingi, mahakama au hakimu anaweza kutoa kamisheni kwa hakimu yeyote ndani ya mipaka ya eneo la mamlaka anakoishi shahidi kuchukua ushahidi wa huyo shahidi.

(2) Hakimu ambaye kamisheni imetolewa kwake atalazimika kuendelea hadi sehemu shahidi aliko au atalazimika kumwita shahidi mbele yake na atalazimika kuchukua ushahidi wake kwa namna ileile na anaweza, kwa dhumuni hili, kutumia uwezo uleule kama vile kwenye shauri.

Wenye kesi wanaweza kuwahoji mashahidi.

207.-(1) Wahusika katika kila mwenendo chini ya Sheria hii ambapo kamisheni imetolewa watalazimika kuarifiwa na mahakama au hakimu anayetoa kamisheni kwamba wanaweza vilevile kupeleka maswali kwa maandishi ambayo mahakama au hakimu anayeelekeza kamisheni anaweza kufikiri yanaendana na jambo, na hakimu ambaye kamisheni inaelekezwa kwake atalazimika kumhoji shahidi kwa kutumia maswali hayo.

(2) Mhusika yeyote anaweza kuhudhuria mbele ya hakimu kwa kutumia wakili au, kama hayuko chini ya ulinzi, yeye mwenyewe na anaweza kumhoji, kumuuliza maswali na kumhoji tena, kama itakavyokuwa, shahidi.

Kurudishwa kwa kamisheni.

208.-(1) Baada ya kamisheni iliyotolewa chini ya kifungu cha 206 imetekezwa ipasavyo italazimika kurudishwa, pamoja na yale aliyosema shahidi aliyehojiwa chini yake, kwenda Mahakama Kuu au kwa hakimu aliyetoa, kama itakavyokuwa, na kamisheni, kurudishwa kwake na ushahidi vitalazimika kuwa wazi wakati wote kwa ukaguzi wa pande husika na vinaweza, isipokuwa kwa sababu za haki, kusomwa kama ushahidi katika kesi na upande wowote na vitafanywa sehemu ya kumbukumbu.

Sura ya 6

(2) Ushahidi wowote uliochukuliwa hivyo, kama unakidhi masharti ya kifungu cha 132 cha Sheria ya Ushahidi, unaweza pia kupokelewa kama ushahidi katika hatua za baadaye za kesi mbele ya mahakama nyingine.

Kuahirishwa kwa mwenendo.

209. Katika kila kesi ambayo kamisheni imetolewa chini ya kifungu cha 206 mwenendo unaweza kuahirishwa kwa muda utakaotajwa unaotosheleza kutekeleza na kurudishwa kwa kamisheni.

(c) Kuchukua na Kurekodi Ushahidi

Jinsi ya kurekodi ushahidi mbele ya hakimu.

210.-(1) Katika mashauri, isipokuwa mashauri chini ya kifungu cha 213, na au mbele ya hakimu, ushahidi wa mashahidi utalazimika kurekodiwa katika mfumo ufuatao:-

- (a) ushahidi wa kila shahidi utalazimika kuchukuliwa kwa maandishi katika lugha ya mahakama na hakimu au wakati akiwepo na akisikia na chini ya maelekezo yake na usimamizi wake na utalazimika kusainiwa na yeye na utalazimika kufanywa sehemu ya kumbukumbu; na
- (b) ushahidi hautakiwi kikawaida kuchukuliwa katika muundo wa maswali na majibu lakini, kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), katika muundo wa simulizi.

(2) Hakimu anaweza, kwa uamuzi wake, kuandika au kuamuru kuandikwa kwa baadhi ya maswali na majibu.

(3) Hakimu atalazimika kumuarifu kila shahidi kwamba ana haki ya ushahidi kusomwa mbele yake na kama shahidi atasema ushahidi usomwe mbele yake, hakimu atalazimika kurekodi kila maoni ambayo shahidi anaweza kutoa kuhusiana na ushahidi wake.

Kutafsiriwa kwa ushahidi kwa mtuhumiwa au wakili wake.

211.-(1) Wakati wowote ushahidi wowote unapotolewa katika lugha isiyoeleweka kwa mtuhumiwa na akiwepo mwenyewe, utalazimika kutafsiriwa kwake katika mahakama ya wazi kwa lugha inayoeleweka kwake.

(2) Iwapo amewakilishwa na wakili na ushahidi unatolewa katika lugha nje ya lugha ya mahakama, na haieleweki kwa wakili,

utalazimika kutafsriwa kwa wakili huyo katika lugha ya mahakama.

(3) Wakati nyaraka zinapotolewa kwa dhumuni la kuthibitishwa rasmi itakuwa ni kwa uamuzi wa mahakama kutafsri kama itakavyoonekana muhimu.

Maoni kuhusiana na mwonekano wa shahidi.

212. Wakati hakimu amerekodi ushahidi wa shahidi atalazimika vilevile kurekodi maoni yoyote, kama yapo, kama atavyofikiri yanafaa kuhusiana na mwonekano wa shahidi wakati wa kuhojiwa.

Utaratibu katika makosa madogo.

213.-(1) Bila kujali kitu chochote kilichomo kwenye Sheria hii kila hakimu anaweza, kama anafikiri inafaa, kusikiliza kosa lolote lililotajwa katika kifungu kidogo cha (1) bila kurekodi ushahidi kama ilivyotolewa hapo mbele, lakini katika kila kesi hiyo atalazimika kuingiza katika muundo ambao Mahakama Kuu inaweza kuelekeza, maelezo yafuatayo:-

- (a) namba ya mfululizo;
- (b) tarehe ya kutendeka kwa kosa;
- (c) tarehe ya lalamiko;
- (d) jina la mlalamikaji;
- (e) jina, ukoo na makazi ya mtuhumiwa;
- (f) kosa ulilolalamikiwa na kosa (kama lipo) lililothibitishwa, na, katika kesi chini ya aya za (c), (d) au (e) za kifungu kidogo cha (2), thamani ya mali ambayo kosa lilitendeka kwake;
- (g) majibu ya mtuhumiwa;
- (h) maoni na, kama ushahidi umeshachukuliwa, hukumu inayounda kilichomo kwenye huo ushahidi;
- (i) adhabu au amri nyingine ya mwisho; na
- (j) tarehe ambayo mwenendo ulisitishwa.

(2) Makosa yaliyorejewa katika kifungu kidogo cha (1) ni kama yafuatayo:-

Sura ya .16

- (a) makosa yanayoadhibiwa kwa kifungu kwa kipindi kisichozidi miezi sita au faini isiyozidi shilingi elfu moja;
- (b) majeruhi ya kawaida chini ya kifungu cha 240 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu;

Sura ya.16

- (c) wizi chini ya **Sura ya XXVII** ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu pale thamani ya mali iliyoibiwa haizidi shilingi mia moja;

Sura ya 16

- (d) kupokea au kushikilia mali iliyoibiwa chini ya Sura ya XXXII ya Sheria ya kanuni ya Adhabu pale thamani ya mali hiyo haizidi shilingi mia moja;
- (e) madhara ya makusudi kwa mali pale thamani ya mali hiyo haizidi shilingi mia moja;
- (f) kusaidia, kufanikisha, kushauri au kuleta utendekaji wa kosa lolote kati ya makosa yaliyotajwa katika kifungu hiki

kidogo;

- (g) kujaribu kutenda moja ya kosa lilitotajwa katika kifungu hiki kidogo;
- (h) kosa lolote lingine ambalo Jaji Mkuu anaweza, kwa amri itakayotangazwa kwenye gazeti, kuelekeza kusikilizwa kwa kufuata masharti ya kifungu hiki.

(3) Wakati wa harakati za shauri chini ya masharti ya kifungu hiki itaonekana kwa hakimu kwamba kesi ni ya aina ambayo inafanya kuwa si vizuri kusikilizwa hivyo, hakimu atalazimika kumwita tena shahidi yoyote na kuendelea kusikiliza tena kesi kwa namna tofauti na ilivyotolewa na Sehemu hii.

(4) Hakuna adhabu ya kifungu kwa kipindi kinachozidi miezi sita au ya faini ya kiasi kinachozidi shilingi elfu moja kitatozwa katika kutiwa hatiani chini ya kifungu hiki.

Kutiwa hatiani au kuhamishwa kama kesi imesikilizwa na mahakimu wawili kila mmoja sehemu yake Sheria Na. 5 ya 1988 kif. 9; 9 ya 2002 Jedwali.

214.-(1) Pale hakimu yoyote, baada ya kusikiliza na kurekodi ushahidi wote au sehemu ya ushahidi katika shauri lolote au lililoendeshwa lote au kwa sehemu ya mwenendo wowote wa kuhamishwa ni kwa sababu yoyote hawezi kumaliza shauri au mwenendo wa kuhamishwa ndani ya muda wa kawaida, hakimu mwingine ambaye ana mamlaka na anatekeleza mamlaka hayo anaweza kuichukua na kuendeleza shauri au mwenendo wa kuhamishwa, kama itakavyokuwa, na hakimu anayechukuwa hivyo anaweza kufanyia kazi ushahidi na mwenendo uliorekodiwa na hakimu aliyekuwa anasikiliza na anaweza, katika suala la shauri na kama ataona ni muhimu, kuwaita tena mashahidi na kuanza tena shauri au mwenendo wa kuhamishwa.

(2) Wakati wowote kama masharti ya kifungu kidogo cha (1) yatatumika Mahakama Kuu inaweza, kama kuna rufaa au hakuna, kufutilia mbali kutiwa hatiani kokote kulikopitishwa kwa kutumia ushahidi ambao si wote ulichukuliwa na hakimu aliyetoa hiyo hukumu, iwapo ina maoni kuwa mtuhumiwa ameathirika katika hilo na inaweza kuamuru shauri lianzwe upya.

(3) Hakuna kitu katika kifungu kidogo cha (1) kitatafsiriwa kumzuia hakimu aliyerekodi ushahidi wote katika shauri lolote na ambaye, kabla ya kupitisha hukumu hawezi kumaliza shauri, kutoka katika kuandika hukumu na kupeleka rekodi ya mwenendo pamoja na hukumu kwa hakimu aliyemrithi ili hukumu isomwe na katika suala la kutiwa hatiani, kwa adhabu kupitishwa na huyo hakimu mwingine.

Jinsi ya kurekodi ushahidi Mahakama Kuu.

215. Mahakama Kuu inaweza, mara kwa mara, kwa kanuni kuweka utaratibu ambao ushahidi utarekodiwa katika kesi zinazokuja mbele ya mahakama na ushahidi au kilichomo ndani yake utalazimika kuchukuliwa kwa kufuata kanuni hizo.

D. -Utaratibu katika Masuala ya Ulemavu wa akili au Kutoweza kwa Mtuhumiwa

Mwendesha
mashitaka kutoa au
kuonyesha ushahidi
kabla mahakama
hajifanya
uchunguzi
kuhusiana na
ulemavu wa akili wa
mtuhumiwa Sheria
Na. 9 ya 2002
Jedwali.

216.-(1) Wakati shauri likiendelea mahakama ina sababu ya kuamini kwamba mtuhumiwa hana akili timamu na matokeo yake hawezi kutengeneza utetezi wake italazimika, kabla ya kufanya uchunguzi juu ya ukosefu wa akili timamu na bila kujali ukweli kwamba mtuhumiwa anaweza kuwa hajajibu mashitaka, kuita upande wa mashitaka kutoa au kuleta ushahidi kuthibitisha hilo shitaka.

(2) Iwapo wakati wa kufunga ushahidi wa kuthibitisha hayo shitaka itaonekana kwa mahakama kwamba hakuna kesi dhidi ya mtuhumiwa mahakama italazimika kutupilia mbali mashitaka na kumwachia huru mtuhumiwa na inaweza baada ya hapo kumshughulikia chini ya Sheria ya Magonjwa ya Akili.

(3) Iwapo wakati wa kufunga ushahidi katika kuthibitisha shitaka inaonekana kwa mahakama kwamba kuna kesi dhidi ya mtuhumiwa, italazimika baada ya hapo kuchunguza juu ya ukosefu wa akili timamu wa mtuhumiwa na, kwa dhumuni hili, inaweza kumwamuru kuwekwa kizuizini katika hospitali ya magonjwa ya akili kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu au, katika mazingira ambayo dhamana inaweza kutolewa, inaweza kumwachia kwa dhamana kama kukiwa na ulinzi wa kutosha juu ya usalama wake na ule wa umma na kwa sharti kuwa atajipeleka mwenyewe kwenye uchunguzi wa kitabibu au uangalizi na afisa tabibu kama itakavyoelekezwa na mahakama.

(4) Afisa tabibu msimamizi wa hospitali ya magonjwa ya akili ambayo mtuhumiwa ameamuriwa kuzuiliwa au afisa tabibu ambaye ameamuriwa atajipeleka mwenyewe kwa ajili ya uchunguzi wa akili au uangalizi kufuatia kifungu kidogo cha (3) italazimika, ndani ya siku arobaini na mbili za huo uzuiliwaji au kujipeleka, kutayarisha na kupeleka kwenye mahakama iliyoamuru huo uzuiliwaji au kujipeleka, taarifa iliyoandikwa juu ya hali ya akili ya mtuhumiwa ikieleza kama kwa maoni yake mtuhumiwa hana akili timamu na matokeo yake hawezi kujitetea.

(5) Baada ya kupokelewa na mahakama taarifa iliyoandikwa iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (4) italazimika kuendelea na uchunguzi wake katika suala la kutokuwa na akili timamu kwa mtuhumiwa na inaweza kupokea kama ushahidi kwa dhumuni hilo taarifa yoyote hiyo inayoonekana kusainiwa na afisa tabibu aliyeitayarisha isipokuwa kama itathibitisha kuwa afisa tabibu anayeonekana kuisaini kwa ukweli hakuisaini.

(6) Pale mahakama imeifanyia kazi taarifa yoyote iliyoandikwa iliyopokelewa katika ushahidi chini ya kifungu kidogo cha (5) na ushahidi wowote mwingine ambao unaweza kupatikana juu yake kuhusiana na hali ya akili ya mtuhumiwa ina maoni kuwa mtuhumiwa hana akili timamu na matokeo yake hawezi kujitetea italazimika kurekodi ilichokiona juu ya hilo, kuahirisha mwenendo mwingine

Sura ya .98

katika kesi, kuamuru mtuhumiwa azuiliwe kama mhalifu asiye na akili katika hospitali ya magonjwa ya akili au sehemu nyingine inayofaa ya kizuizi hadi atakapoachiwa au kushughulikiwa vinginevyo kwa namna iliyotolewa katika kifungu cha 217 au 218.

(7) Pale taarifa iliyoandikwa inatakiwa na kifungu kidogo cha (4) inasema kuwa mtuhumiwa ana akili timamu na anaweza kujitetea, mwenendo utalazimika kuendelea kama ilivyotolewa na kifungu cha 218.

Utaratibu kama mtuhumiwa amethibika kuwa na uwezo wa kujitetea Sheria Na. 9 ya 2002 Jedwali.

217.-(1) Pale mtuhumiwa aliyezuiliwa kufuatia hati iliyotolewa chini ya kifungu cha 216 au kifungu cha 281 anaonekana na afisa tabibu aliyekuwa akimwangalia kuwa amepona ugonjwa wa akili kutosheleza kuweza kujitetea, afisa tabibu atalazimika hapohapo kupeleka kwenye mahakama inayohusika cheti kinachoeleza ndani yake vilevile kama mtuhumiwa anaweza, lakini kwa shitaka dhidi yake, kuwa mzima kusimama shaurini, na nakala iliyothibitishwa ya cheti hicho kwa Mkurugenzi wa Mashitaka.

(2) Pale Mkurugenzi wa Mashitaka anakusudia kuendelea na mashitaka dhidi ya mtuhumiwa, anaweza ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kupokea nakala iliyothibitishwa ya cheti kilichotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), kuitaarifu mahakama iliyotoa hati chini ya kifungu cha 216 au 218 kwamba anataka kuendelea na mwenendo dhidi ya mtuhumiwa.

(3) Pale mahakama inapokea cheti kilichotolewa katika kifungu kidogo cha (1), au kama mahakama inataarifiwa na Mkurugenzi wa Mashitaka kwamba Jamhuri inakusidia kuendelea na mwenendo dhidi ya mtuhumiwa, itaamuru kuondolewa kwa mtu huyo kutoka sehemu ambayo anazuiliwa na kuamuru aletwe mbele yake kwa utaratibu uliotolewa na kifungu cha 218.

(4) Pale mahakama inataarifiwa na Mkurugenzi wa Mashitaka kuwa Jamhuri haikusudii kuendelea na mwenendo dhidi ya mtuhumiwa, mahakama italazimika:-

- (a) katika kesi ambazo cheti kilichotolewa katika kifungu kidogo cha (1) kinaeleza kwamba mtuhumiwa ana uwezo wa kuachiwa bila masharti hapo hapo, kutoa amri ya kuachiwa kwake; au
- (b) katika kesi zingine zozote, kurekodi kwamba mwenendo umesimamishwa, kumwachia mtuhumiwa dhidi ya mashitaka na baada ya hapo kuendelea kumshughulikia chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Magonjwa ya akili kama mtu anayedhaniwa kuwa ameletwa mbele yake chini ya Sheria hiyo.

(5) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (4), kuachiliwa kokote kwa mtuhumiwa kufuatia kifungu hiki hakutazuia mashitaka mengine ya baadaye dhidi yake kwa kutumia mazingira au ukweli

Sura ya .98

uleule.

Kurudiwa kwa usikilizwaji wa shauri au uchunguzi.

218.-(1) Wakati wowote taarifa ya maandishi chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu cha 216 au taarifa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 217 inapokelewa na mahakama, italazimika, kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (4) kuendelea na shauri na kumtaka mtuhumiwa kuhudhuria au kuletwa mbele yake.

(2) Pale mwenendo unaendelea chini ya kifungu kidogo cha (1) mahakama italazimika, katika kesi zote ambazo mwenendo unaendelea kwa kufuata kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 217, kuendelea kusikiliza kesi **upya**, na katika mazingira mengine yoyote inaweza kwa uamuzi wake kuifanya kesi iwe imesikilizwa kwa sehemu na baada ya hapo inaweza kuendelea kusikiliza ushahidi mwingine katika kesi.

(3) Taarifa yoyote ya maandishi iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu cha 216 au kutolewa kwa cheti kilichotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 217, inaweza, kama hairidhiki kuwa mtuhumiwa ana akili timamu na anaweza kujitetea kurekodi uamuzi juu ya hilo na kuendelea kutoa amri mpya chini ya kifungu kidogo cha (6) cha kifungu cha 216.

Kinga ya ulemavu wa akili katika shauri Sheria Na. 9 ya 2002 Jedwali.

219.-(1) Pale kitendo chochote au kushindwa kutenda kumeshitakiwa dhidi ya mtu yeyote kama kosa na inakusudiwa wakati wa shauri la mtu huyo kutoa utetezi wa ulemavu wa akili, kwamba utetezi utalazimika kutolewa wakati ambao mtu ameitwa kujibu mashitaka.

(2) Iwapo, kwa ushahidi ulio kwenye rekodi, inaonekana na mahakama kwamba mtuhumiwa alifanya kitendo au alishindwa kufanya kitendo alichoshitakiwa lakini hakuwa na akili timamu kwa hiyo kutowajibika kwa matendo yake katika muda ambapo kitendo kilifanyika au alishindwa kutenda, mahakama italazimika kutoa uamuzi maalumu kwamba mtuhumiwa alifanya kitendo au alishindwa kufanya kitendo alichoshitakiwa lakini kwa sababu ya ulemavu wa akili, hatakuwa na hatia ya kosa.

(3) Wakati uamuzi maalumu kufuatia kifungu kidogo cha (2), umetolewa na mahakama italazimika–

(a) pale mtu ambaye uamuzi maalumu umetolewa dhidi yake alishitakiwa kwa kosa chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu linalohusisha ukatili wa mwili au uharibifu wa mali ambao, isipokuwa kwa ugonjwa wake wa akili, wakati wa kufanya kitendo au kushindwa kufanya kitendo wakati wa kutiwa hatiani angewajibika kwa adhabu ya kifo au kuwajibika kufungwa kwa kipindi kisichopungua miaka saba, kuamuru mtu huyo kuwekwa kwenye hospitali ya magonjwa ya akili, jela au sehemu nyingine inayofaa kuwekwa kama mgonjwa wa akili mhalifu ; au

Sura ya 16

(b) katika kesi yoyote nyingine, kwa uamuzi wake, aidha kuendelea kumshughulikia mtu huyo chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Magonjwa ya Akili au kumwachia au kumshughulikia vinginevyo, kwa kuzingatia masharti kama kubaki chini ya uangalizi katika mahali popote au na mtu yoyote na kwa masharti hayo mengine kwa kuhakikisha usalama na ustawi wake na ule wa umma kama mahakama itakavyoona inafaa.

(4) Mkuu wa hospitali ya magonjwa ya akili, jela au sehemu nyingine ambayo mgonjwa wa akili mhalifu anazuiliwa kwa amri ya mahakama chini ya kifungu kidogo cha (3)(a), atalazimika kupeleka taarifa kwa maandishi kwa Waziri juu ya hali, historia na mazingira ya huyo mgonjwa wa akili baada ya kuisha kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya amri ya mahakama na baada ya hapo baada ya kuisha miaka miwili kutoka tarehe ya taarifa ya mwisho.

(5) Baada ya kuingalia taarifa chini ya kifungu kidogo cha (5) Waziri anaweza kuamuru kwamba mgonjwa wa akili mhalifu aachiliwe huru au ashughulikiwe vinginevyo, kwa kuzingatia masharti kama kubaki chini ya uangalizi katika mahali popote au na mtu yoyote na kwa masharti hayo mengine kwa kuhakikisha usalama na ustawi wake na ule wa umma kama Waziri atakavyoona inafaa.

(6) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, mtu yoyote aliyeruhusiwa na Waziri, anaweza wakati wowote, baada ya mgonjwa wa akili mhalifu kuwekwa kizuizini, kutoa taarifa kwa Waziri juu ya hali, historia na mazingira ya mgonjwa wa akili mhalifu na Waziri, baada ya kuiangalia taarifa, anaweza kuamuru kwamba mgonjwa wa akili mhalifu aachiliwe huru au ashughulikiwe vinginevyo, kwa kuzingatia masharti kama kubaki chini ya uangalizi katika mahali popote au na mtu yoyote na kwa masharti hayo mengine kwa kuhakikisha usalama na ustawi wake na wa umma kama mahakama itakavyoona inafaa.

(7) Mahakama inaweza, katika muda wowote, kuamuru kwamba mgonjwa wa akili mhalifu ahamishwe kutoka hospitali ya magonjwa ya akili kwenda jela au kutoka sehemu yoyote anayozuiliwa au abaki chini ya uangalizi wa ama jela au hospitali ya magonjwa ya akili.

Uwezo wa mahakama kuchunguza ulemavu wa akili

220.-(1) Pale kitendo au kushindwa kufanywa kitendo chochote kimeshitakiwa dhidi ya mtu yoyote kama kosa na inaonekana kwa mahakama wakati wa shauri la mtu huyo kwa kosa hilo kwamba mtu huyo anaweza kuwa hakuwa na akili timamu kwa hiyo kutowajibika kwa kitendo chake wakati kitendo kilipotendeka au kitendo kiliposhindwa kutendeka, mahakama inaweza, bila kujali kwamba hakuna ushahidi uliochukuliwa au kutolewa juu ya huo ugonjwa wa akili, kuahirisha mwenendo na kuamuru mtuhumiwa kuzuiliwa katika hospitali ya magonjwa ya akili kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu.

(2) Afisa tabibu msimamizi wa hospitali ya magonjwa ya akili ambamo mtuhumiwa ameamuriwa kuzuiliwa kufuatia kifungu kidogo cha (1) atalazimika, ndani ya siku arobaini na mbili za kuzuiliwa kutayarisha na kupeleka mbele ya mahakama iliyoamuru kuzuiliwa taarifa iliyoandikwa juu ya hali ya akili ya mtuhumiwa ikiainisha kama, kwa maoni yake, wakati ambapo kosa lilitendekea mtuhumiwa hakuwa na akili timamu kwa hiyo kutowajibika kwa kitendo chake na taarifa hiyo iliyoandikwa inayodhaniwa kusainiwa na afisa tabibu aliyeitayarisha inaweza kupokelewa kama ushahidi isipokuwa kama itathibitishwa kwa afisa tabibu anayedhaniwa kusaini kwa ukweli hakuisani.

(3) Pale mahakama imepokea taarifa iliosainiwa na afisa tabibu msimamizi wa hospitali ya magonjwa ya akili ambamo mtuhumiwa alizuiliwa mtuhumiwa na waendesha mashitaka watalazimika kuwa na haki ya kutoa ushahidi wowote unaohusiana na suala la ugonjwa wa akili kama watakvyoona inafaa.

(4) Iwapo, kwa ushahidi uliorekodiwa, inaonekana kwa mahakama kuwa mtuhumiwa alifanya kitendo au alishindwa kufanya kitendo alichoshitakiwa lakini hakuwa na akili timamu kwa hiyo kutowajibika kwa kitendo chake wakati kitendo kilipofanyika au aliposhindwa kufanya kitendo, mahakama italazimika kutoa uamuzi maalumu kwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 219 na masharti yote ya kifungu cha 219 yatalazimika kutumika kwa kila kesi kama hiyo.

Utaratibu kama
mtuhumiwa haelewi
mwenendo wa kesi.

221.-(1) Iwapo mtuhumiwa, ingawaje hana ugonjwa wa akili, hawezi kufanywa kuelewa mwenendo–

- (a) katika kesi zinazoshauriwa na mahakama za chini, mahakama italazimika kuendelea kusikiliza ushahidi na, kama wakati wa kufunga ushahidi wa upande wa mashitaka na, kama utetezi umeshaitwa tayari, wakati wa kufunga ushahidi wa utetezi, mahakama ina maoni kwa ushahidi ambao umesikilizwa unaweza kuhalalisha kutiwa hatiani, italazimika kumwadhibu mtuhumiwa kwa kuwekwa kizuizini kwa ridha ya Rais; lakini kama ushahidi hauhalalishi kutiwa hatiani italazimika kumwachia na kumruhusu mtuhumiwa;
- (b) katika kesi ambazo zinatakiwa kuhamishwa na mahakama ya chini na inasikilizwa na Mahakama Kuu, mahakama ya chini, italazimika kumuhamisha mtuhumiwa kwa kusikilizwa na Mahakama Kuu na ama kumuachia kwa dhamana au kumpeleka jela kwa kumtunza kwa usalama, na Mahakama Kuu italazimika, kama Mkurugenzi wa Mashitaka ameleta taarifa, kuendela kusikiliza ushahidi wote uliopo kwa wote upande wa mashitaka na utetezi, kama itaridhika kwamba mtuhumiwa ana hatia ya kosa

aliloshitakiwa italazimika kumuadhibu kwa kuwekwa kizuizini kwa ridhaa ya Raisi; au

- (c) iwapo Mkurugenzi wa Mashitaka ameeleza kwa mahakama inayohamisha kwamba hokusudii kuleta taarifa, mtuhumiwa atalazimika mara moja kuachiwa kuhusiana na shitaka dhidi yake na, kama amepelekwa jela, ataachiwa au, kama yuko kwenye dhamana, dhamana yake italazimika **kuachiwa**; lakini kuachiwa huko kwa mtuhumiwa hakutatumika kama kuzuizi kwa mwenendo wa baadaye dhidi yake kwa kutumia mazingira au ukweli uleule.

(2) Mtu aliyeadhibiwa kwa kuwekwa kizuizini kwa ridhaa ya Rais atawajibika kuzuiliwa katika sehemu hiyo na chini ya masharti hayo kama Waziri anavyoweza, kwa amri mara kwa mara, kuelekeza na wakati amewekwa kizuizini atachukuliwa kuwa chini ya ulinzi kisheria.

(3) Waziri anaweza katika muda wowote, kwa kuanzisha mwenyewe au baada ya kupokea taarifa kutoka kwa mtu yoyote aliyeruhusiwa na yeye, kuamuru kwamba mtu aliyewekwa kizuizini kwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (2) kuachiliwa au kushughulikiwa vinginevyo, kwa kuzingatia masharti kama kubaki chini ya uangalizi mahali popote au na mtu yoyote na kwa masharti hayo mengine kwa kuhakikisha usalama na ustawi wake na wa umma kama Waziri atakavyoona inafaa.

(4) Wakati mtu amewekwa kizuizini kwa ridhaa ya Raisi chini ya aya ya (a) au (b) ya kifungu kidogo cha (1), jaji au hakimumu anayesikiliza atalazimika kupeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali nakala ya rekodi ya ushahidi uliochukuliwa wakati wa shauri, na taarifa ya maandishi iliyosainiwa na yeye ikijumuisha mapendekezo au maoni yoyote juu jambo ambalo ataona yanafaa.

SEHEMU YA SABA

TARATIBU KATIKA MASHAURI MBELE YA MAHAKAMA ZA CHINI

(a) Masharti Yanayohusiana na Kusikiliza na Kuamuliwa kwa Kesi

Kutokuhudhuria
kwa mlalamikaji
siku ya kusikiliza
kesi

222. Iwapo, katika kesi yoyote ambayo mahakama ya chini ina mamlaka kusikiliza na kuamua, mtuhumiwa amehudhuria kwa kutii wito aliopolekewa katika muda na mahali palipoteuliwa katika wito kwa ajili ya kusikilizwa kwa kesi, au ameletwa mbele ya mahakama akiwa amekamatwa, kwa hiyo, kama mlalamikaji, baada ya kupewa taarifa ya muda na mahali palipoteuliwa kwa ajili ya kusikiliza **shitaka** hatahudhuria, mahakama italazimika kutupilia mbali shitaka na kumwachia huru mtuhumiwa, isipokuwa kama kwa sababu fulani, italazimika kufikiri ni vema kuahirisha usikilizaji, wa kesi mpaka tarehe nyingine na, wakati akisubiri usikilizaji ulioahirishwa, ama

kumuachia mtuhumiwa kwa dhamana au kumweka rumande au kuchukua **dhamana** kwa ajili ya kuhudhuria kwake kama mahakama itakavyoona inafaa.

Kuhudhuria kwa pande zote.

223. Iwapo muda ulioteuliwa kusikiliza kesi mlalamikaji na mtuhumiwa wote wamehudhuria mbele ya mahakama ambayo inatakiwa kusikiliza na kuamua mashitaka, au kama mlalamikaji amehudhuria na kuhudhuria binafsi kwa mtuhumiwa kumesimamishwa chini ya kifungu cha 193, mahakama italazimika kuendelea kusikiliza kesi.

Kuondolewa kwa lalamiko.

224. Iwapo mlalamikaji, muda wowote kabla ya amri ya mwisho haijapitishwa katika kesi yoyote chini ya Sehemu hii, anairidhisha mahakama kuwa kuna sababu za msingi za kumruhusu kuondoa lalamiko lake, dhidi ya mtuhumiwa au, kama kuna watuhumiwa zaidi ya mmoja, au mmoja kati yao, mahakama inaweza kumruhusu kuyaondoa malalamiko na italazimika baada ya hapo kumuachia huru mtuhumiwa dhidi ya malalamiko yalioondolewa; isipokuwa kwamba kifungu hiki **kitalazimika kutumika** tu kwa makosa madogo. .

Kukoma kwa shauri katika mahakama za chini Sheria Na 9 ya 2002 Jedwali.

224A. Kila shauri chini ya Sehemu hii litalazimika kukoma baada ya kifo cha mtuhumiwa.

Kuahirishwa na kuwekwa rumande kwa mtuhumiwa Sheria Na. 5 ya 1988 kif. 10

225.-(1) **Kwa kuzingatia** vifungu vidogo vya (3) na (6), kabla au wakati wa kusikiliza kesi yoyote, itakuwa halali kisheria kwa mahakama kwa uamuzi wake kuahirisha usikilizaji mpaka muda na mahali fulani patakapoteuliwa hapo na kuelezwa mbele ya na kusikilizwa na mhusika au wahusika au mawakili wao watakao kuwepo hapo, na katika muda huo mahakama inaweza kuamuru mtuhumiwa kuachiliwa bila masharti, au inaweza kumpeleka jela, au inaweza kumuachia baada ya kutoa dhamana bila au na wadhamini kwa uamuzi wa mahakama, kwa masharti ya kuhudhuria kwake katika muda na mahali ambapo kusikilizwa huko au kusikilizwa zaidi kutaahirishwa.

(2) Bila kuajli masharti ya kifungu kidogo cha (1), hakuna kuahirishwa kutakuwa kwa zaidi ya siku thelathini za wazi au, kama mtuhumiwa amepelekwa jela, kwa zaidi ya siku kumi na tano za wazi, ile siku, inayofuatia siku ya kwanza itahesabika kama ni siku ya kwanza.

(3) Mahakama inaweza kumpeleka mtuhumiwa kwenda mahabusu ya polisi:–

(a) kwa siku zisizozidi tatu za wazi kama hakuna jela ndani ya maili tano za jengo la mahakama na inaweza mara kwa

mara kumpeleka tena mtuhumiwa kwenye mahabusu ya polisi kwa kipindi kisichozidi siku kumi na tano kwa ujumla;

- (b) kwa siku zisizozidi saba za wazi kama hakuna jela ndani ya maili tano za jengo la mahakama na mahakama haikusudii kukaa tena katika jengo la mahakama hiyo ndani ya siku tatu, na inaweza mara kwa mara kumpeleka tena mtuhumiwa kwenye mahabusu ya polisi kwa kipindi kisichozidi siku kumi na tano kwa ujumla;
- (c) kwa maombi ya mtuhumiwa, kwa siku zisizozidi kumi na tano za wazi.

(4) Isipokuwa kwa kesi zinazohusu makosa chini ya vifungu vya 39, 40, 41, 43, 45, 48(a) na 59, vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu ikihusisha udanganyifu, njama za kudanganya au kughushi, italazimika kuwa si halali kwa mahakama kuahirisha kesi kuhusiana ma makosa yaliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria hii chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kwa jumla inayozidi siku sitini isipokuwa kwa mazingira yafuatayo–

Sura ya.16

- (a) pale ambapo cheti cha Afisa Jinai kimeletwa mahakamani kikieleza umuhimu na sababu za kuahirisha kesi, mahakama inaweza kuahirisha kesi kwa kipindi kingine kisichozidi siku sitini kwa ujumla kuhusiana na makosa yaliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria hii;
- (b) pale ambapo cheti kimeletwa mahakamani na Mwanasheria wa Serikali kikieleza umuhimu na sababu za kuomba kuahirisha tena zaidi ya kuahirisha kulikofanyika chini ya aya ya (a), mahakama italazimika kuahirisha kesi kwa kipindi kingine kisichozidi, kwa ujumla, siku sitini;
- (c) pale ambapo cheti kimeletwa mahakamani na Mkurugenzi wa Mashitaka au mtu aliyeidhinishwa na yeye kwa niaba yake kikieleza umuhimu na sababu za kuahirisha tena zaidi ya kuahirisha kulikofanyika chini ya aya ya (b), mahakama italazimika kutoahirisha kesi hiyo kwa kipindi kinachozidi kwa ujumla miezi ishirini na nne kuanzia tarehe ya mwanzo ya kuahirisha kesi kulikotolewa chini ya aya ya (a).

(5) Pale ambapo hakuna cheti kilicholetwa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (4), mahakama italazimika kuendelea kusikiliza kesi au, kama upande wa mashitaka hawako tayari kuendelea na usikilizaji kumuachia huru mtuhumiwa mahakamani isipokuwa kwamba kuachiliwa huru kokote chini ya kifungu hiki hakitatumika kama kizuizi kwa shitaka la baadaye litakaloletwa dhidi ya mtuhumiwa kwa kosa lilelile.

(6) Hakuna kitu katika kifungu hiki kitatafsriwa kutoa utumikaji wa kifungu hiki kwa mwenendo wowote katika mahakama ya chini kuhusiana na kosa lolote linalosikilizwa tu na Mahakama Kuu chini ya

Sura ya .200

Sheria ya Makosa ya Uchumi na Uhalifu wa Kupanga.

Kutokuhudhuria
kwa pande zote
baada ya kuahirisha.

226.-(1) Iwapo wakati au mahali ambapo kusikiliza au kusikiliza zaidi kumeahirishwa, mtuhumiwa hakuhudhuria mbele ya mahakama ambayo ilitoa amri ya kuahirishwa, itakuwa ni halali kisheria kwa mahakama kuendelea na kusikiliza au kusikiliza zaidi kama vile mtuhumiwa alikuwepo; na kama mlalamikaji hatahudhuria, mahakama inaweza kutupilia mbali mashitaka na kumuachilia huru mtuhumiwa na au bila gharama kama mahakama itakavyoona inafaa.

(2) Iwapo mahakama imemtia hatiani mtuhumiwa akiwa hayupo, inaweza kutengua kutiwa hatiani, baada ya kuridhika kwa kutokuwepo kwake kulitokana na sababu ambazo asingeweza kuzithibiti na kwamba alikuwa na utetezi wa msingi juu ya kesi

(3) Adhabu yoyote iliyopitishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) itachukuliwa kuanza tarehe ya kukamatwa na mtu aliyepelekea kukamatwa huko, atalazimika kuandika tarehe hiyo nyuma ya hati ya kuhamishwa.

(4) Mahakama, kwa uamuzi wake, inaweza kuacha kumtia hatiani mtuhumiwa wakati hayupo, na katika kila kesi kama hiyo mahakama italazimika kutoa hati kwa ajili ya kumkamata mtuhumiwa na kuamuru kuletwa mbele ya mahakama.

Mtuhumiwa
anaweza kutiwa
hatiani na
kuhukumiwa adhabu
hata kama hayupo.

227. Pale katika kesi yoyote ambapo kifungu cha 226 hakitumiki, mtuhumiwa baada ya kusikilizwa na mahakama ya chini anashindwa kuhudhuria katika tarehe iliyopangwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa baada ya kufungwa kwa kesi ya upande wa mashitaka au katika tarehe iliyopangwa ya kupitishwa kwa adhabu, mahakama inaweza, iwapo inaridhika kuwa kuhudhuria kwa mtuhumiwa hakuwezekani bila ya kuchelewa kusiko na msingi au gharama, itaendelea kumaliza kesi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 231 kama vile mtuhumiwa akiwepo, ameshindwa kutoa maelezo yoyote au kutoa ushahidi wowote au, kama itakavyokuwa, , kutoa maelezo ya ziada au kutoa ushahidi wa ziada kuhusiana na adhabu ambayo mahakama inaweza kupitisha. :

Isipokuwa kwamba:—

- (a) pale mtuhumiwa anashindwa kuhudhuria lakini wakili wake anahudhuria, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, wakili atakuwa na haki ya kuita shahidi yeyote wa utetezi na kuihutubia mahakama kama vile mtuhumiwa alikuwa **amehukumiwa au anahukumiwa**, na wakili atakuwa na haki ya kuita shahidi yoyote na kuihutubia mahakama katika mambo yanayohusiana na adhabu yoyote ambayo mahakama inaweza kuipitisha; na
- (b) pale mtuhumiwa anahudhuria katika tarehe itakayofuata ambayo mwenendo unaweza kuwa umeahirishiwa, mwenendo chini ya kifungu hiki katika siku ile au siku zile

ambazo mtuhumiwa hakuwepo hazitakuwa si halali kwa sababu tu ya kutokuwepo kwake.

Mtuhumiwa kuitwa kujibu mashitaka Sheria Na. 4 ya 1991 kif. 2

228.-(1) Kiini cha **shtaka** kitaelezwa kwa mtuhumiwa na mahakama, na ataulizwa kama anakubali au anakataa ukweli wa shtaka..

(2) Iwapo mtuhumiwa anakiri ukweli wa shtaka, kukiri kwake kutalazimika kurekodiwa kwa karibu iwezekanavyo katika maneno anayotumia na hakimumu atalazimika kumtia hatiani na kupitisha adhabu juu yake au kutoa amri dhidi yake, isipokuwa kama kutatokea kuwa na sababu za msingi kinyume chake.

(3) Iwapo mtuhumiwa hataki ukweli wa shtaka, mahakama italazimika kuendelea kusikiliza kesi kama ilivyoelezwa baada ya hapa.

(4) Iwapo mtuhumiwa anakataa kujibu shtaka, mahakama italazimika kuamuru majibu ya kutokuwa na hatia kuingizwa kwa ajili yake.

(5)(a) Iwapo mtuhumiwa anajibu:-

(i) kwamba alishawahi kuachiliwa kwa kosa hilo; au

(ii) amepata msamaha **katika** sheria kwa kosa lake,

mahakama italazimika kwanza kuendesha shauri kujua kama jibu hilo ni kweli.

(b) Iwapo mahakama inaamua kuwa ushahidi uliotolewa kuunga mkono jibu hilo hautoshelezi, au kama itagundua kuwa jibu hilo ni la uongo, mtuhumiwa atatakiwa kujibu shtaka.

(6) Baada ya mtuhumiwa kujibu shtaka lililosomwa kwake mahakamani chini ya kifungu hiki, mahakama italazimika kupata kutoka kwake anuani yake ya kudumu na italazimika kurekodi na kuitunza.

Utaratibu iwapo **shtaka** linakanwa."

229.-(1) Iwapo mtuhumiwa hataki ukweli wa mashitaka, upande wa mashitaka utafungua kesi dhidi ya mtuhumiwa na utalazimika kuita mashahidi na kutoa ushahidi unaounga mkono mashitaka.

(2) Mtuhumiwa au wakili wake anaweza kuuliza maswali kwa kila shahidi aliyeletwa dhidi yake.

(3) Iwapo mtuhumiwa hatatumia wakili, mahakama italazimika, baada ya kufungwa kwa mahojiano ya kila shahidi wa upande wa mashitaka, kumuuliza mtuhumiwa kama anataka kuuliza maswali yoyote kwa shahidi huyo au kutoa maelezo yoyote.

(4) Iwapo mtuhumiwa atauliza swali lolote, hakimumu atalazimika kurekodi majibu na, kama atatoa maelezo hakimumu atalazimika, kama anafikiri inahitajika kwa maslahi ya mtuhumiwa, kuweka kiini cha maelezo hayo kwa shahidi kwa njia ya swali na kurekodi jibu lake.

Kuachiwa kwa mtuhumiwa kama

230. Iwapo wakati wa kufunga ushahidi unaounga mkono

hakuna kesi ya kujibu.

shtaka, inaonekana na mahakama kwamba hakuna kesi iliyojengwa dhidi ya mtuhumiwa kutosholeza kumtaka kutoa utetezi aidha kuhusiana na kosa ambalo anashtakiwa au kuhusiana na kosa lolote ambalo, chini ya masharti ya vifungu vya 300 mpaka 399 vya Sheria hii, anawajibika kutiwa hatiani mahakama italazimika kutupilia mbali mashitaka na kumuachilia huru mtuhumiwa.

Utetezi.

231.-(1) Wakati wa kufunga ushahidi unaounga mkono shtaka, kama inaonekana kwa mahakama kwamba kesi imejengwa dhidi ya mtuhumiwa kutosheleza kumtaka kutoa utetezi ama kuhusiana na kosa analoshtakiwa au kuhusiana na kosa lolote lingine ambalo, chini ya masharti ya kifungu cha 300 hadi 309 vya Sheria hii, anawajibika kutiwa hatiani mahakama italazimika tena kueleza kiini cha shtaka kwa mtuhumiwa na kumtaarifu haki yake:-

(a) ya kutoa ushahidi kwa kiapo au la kwa uthibitisho, kwa niaba yake;

(b) ya kuita mashahidi katika ushahidi wake,

na atalazimika baada ya hapo kumuuliza mtuhumiwa au wakili wake kama inakusudiwa kutekeleza mojawapo ya haki zilizotajwa hapo juu na atalazimika kurekodi jibu; na mahakama baada ya hapo itamuita mtuhumiwa kutoa utetezi wake isipokuwa kama mtuhumiwa hatapenda kutumia mojawapo ya haki hizo.

(2) Bila ya kujali kwamba mtuhumiwa amechagua kutoa ushahidi bila kiapo au uthibitisho, atalazimika kuhojiwa na upande wa mashtaka.

(3) Iwapo mtuhumiwa, baada ya kutaarifiwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), anachagua kubaki kimya mahakama atakuwa na haki ya **kudhania** kinyume dhidi ya mtuhumiwa na mahakama vilevile na upande wa mashitaka watalazimika kuruhusiwa kutoa maoni kutokana na kushindwa kwa mtuhumiwa kutoa ushahidi.

(4) Iwapo mtuhumiwa anaeleza kwamba ana mashahidi wa kuwaita lakini wakati huo hawapo mahakamani, na mahakama inaridhika kwamba ukosefu wa hao mashahidi si kwa sababu ya kosa au uzembe wowote wa mtuhumiwa na kwamba kuna uwezekano kwamba wanaweza, kama wangukwepo, kutoa ushahidi mzito kwa niaba ya mtuhumiwa, mahakama inaweza kuahirisha **shauri** na kutoa wito au kuchukua hatua nyingine kulazimisha mahudhurio ya mashahidi hao.

Ushahidi katika jibu

232. Iwapo mtuhumiwa anamuuliza maswali shahidi yeyote au anatoa ushahidi tofauti na tabia yake kwa ujumla, mahakama inaweza kutoa ruhusa kwa mwendesha mashitaka kutoa au kuwasilisha **ushahidi kwa kujibu**.

Utaratibu wa kuwasilisha hoja

233. Mwendesha mashtaka au mtuhumiwa au wakili wake wana haki ya kuongea mahakamani kwa namna na mpangilio

unaofanana kama kwenye shauri chini ya masharti ya Sheria hii mbele ya Mahakama Kuu.

Kutofautiana kwa shtaka na ushahidi na kusahihishwa kwa shtaka

234.-(1) Pale ambapo katika hatua yoyote ya shauri, inaonekana na mahakama kwamba shtaka lina kasoro, ama katika yaliyomo au muundo wake, mahakama inaweza kutoa amri ya kusahihisha shtaka ama kwa njia ya kurekebisha shtaka au kwa kubadilisha au kwa kuongeza shtaka jipya kama mahakama itakavyoona muhimu kulingana na mazingira ya kesi isipokuwa, kwa kuzingatia **uzito** wa kesi, marekebisho yanayohitajika hayawezi kufanyika bila uvunjaji wa haki; na marekebisho yote yatakayofanyika chini ya masharti ya kifungu kidogo hiki yatalazimika kufanywa kwa masharti ambayo mahakama itaona ni ya haki.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), pale shtaka limerekebisha chini ya kifungu kidogo hicho:-

- (a) mahakama italazimika baada ya hapo kumwita mtuhumiwa kujibu shtaka lililorekebisha;
- (b) mtuhumiwa anaweza kuhitaji kwamba mashahidi au mmoja wao waitwe tena na watoe ushahidi upya au kuhojiwa upya na mtuhumiwa au wakili wake na, katika tukio hilo la mwisho, mwendesha mashtaka atakuwa na haki ya kuwahoji tena mashahidi hao katika mambo yatakayojitokeza kutokana na kuhojiwa huko; na
- (c) mahakama inaweza kumruhusu mwendesha mashtaka kumwita na kumuuliza tena, kuhusiana na marekebisho yoyote ya au nyongeza katika shtaka yanayoweza kuruhusiwa, shahidi yoyote ambaye amehojiwa isipokuwa kama mahakama kwa sababu yoyote zitakazorekodiwa kwa maandishi itaona kwamba maombi yanafanywa kwa nia ya kukashifu, kuchelewesha au kwa kuzuia kutendeka kwa haki.

(3) Kutofautiana kati ya shtaka na ushahidi uliotolewa kutetea shtaka hilo kuhusiana na muda ambao kosa linalolalamikiwa lilitendeka sio muhimu na shtaka halitakiwi kurekebisha kwa tofauti hiyo kama itathibitishwa kwamba mwenendo ulifunguliwa ndani ya muda, kama upo, uliowekwa na sheria kwa kufunguliwa kwake.

(4) Pale marekebisho ya shtaka yamefanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) au kuna tofauti kati ya shtaka na ushahidi kama ilivyofafanuliwa katika kifungu kidogo cha (2) mahakama italazimika, kama ina maoni kuwa mtuhumiwa kutokana na hayo amedanganywa au ameongopewa, kuahirisha shauri kwa muda fulani kama itakavyokuwa muhimu.

(5) Pale marekebisho ya shtaka yamefanyika chini ya kifungu kidogo cha (1), mwendesha mashtaka anaweza kuomba kwamba mashahidi au mmoja wao waitwe tena na kutoa ushahidi upya au wahojiwe zaidi na mwendesha mashtaka na mahakama italazimika

kumwita shahidi huyo au mashahidi hao isipokuwa kama mahakama, kwa sababu zitakazorekodiwa kwa maandishi, itaona kuwa ombi linafanywa kwa dhumuni la kukashifu, kuchelewesha au kuzuia kutendeka kwa haki.

Uamuzi
Sheria Na. 10 ya
1989 kif. 2

235.-(1) Mahakama, baada ya kuwasikiliza wote mlalamikaji na mtuhumiwa na mashahidi wao na ushahidi, atamtia hatiani mtuhumiwa na kutoa adhabu au kutoa amri dhidi yake kwa mujibu wa sheria au itamwachia huru au itatupilia mbali shtaka chini ya kifungu cha 38 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu.

Sura ya.16

(2) Iwapo mahakama itamwachia huru mtuhumiwa, itamtaka kutoa anuani yake ya kudumu kwa ajili ya kupelekewa nyaraka kama kutakuwa na rufaa dhidi ya kuachiwa kwake na mahakama itarekodi au kuhakikisha inarekodiwa.

Ushahidi
unaohusiana na
adhabu au amri
muafaka

236. Mahakama inaweza, kabla ya kutoa adhabu, kupokea ushahidi wowote kama itakavyoona inafaa, kwa ajili ya kujiridhisha yenyewe kuhusiana na adhabu sahihi ya kutoa.

Kuzingatia makosa
mengine

237. Bila kuathiri ujumla wa kifungu cha 236, mahakama ya chini inayoendeshwa na hakimu mkazi inaweza, kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, dhumuni la kujua adhabu sahihi ya kupitisha, utazingatia kosa lingine lolote lililotendwa na mtuhumiwa:-

- (a) **iwapo imefafanuliwa na mahakama kwa mtuhumiwa katika lugha ya kawaida kwamba adhabu itakayotolewa dhidi yake kwa kosa ambalo ametiwa hatiani katika mwenendo huo inaweza kuwa kubwa kama kosa jingine utazingatiwa; na**
- (b) **baada ya ufafanuzi mtuhumiwa:-**
 - (i) **anakubali kuwa alitenda kosa hilo lingine; na**
 - (ii) **anaiomba mahakama kuzingatia kosa hilo jingine.**

(3) Hakuna kitu katika kifungu hiki, kitaruhusu mahakama ambayo imezingatia kosa lingine katika kupitisha adhabu yoyote kwa mtuhumiwa inayozidi adhabu ya juu ambayo inaweza kutolewa na mahakama hiyo kwa kosa ambalo mtu huyo alitiwa hatiani katika mwenendo huo.

Kuandaa amri za
kutiwa hatiani au
kuachiwa

238. Kutiwa hatiani au kuachiwa huru au amri nyingine zinaweza, kama zitahitajika, ziandaliwe na zisainiwe na mahakama au na karani au afisa mwingine wa mahakama.

Amri ya
kuondolewa
mashtaka mengine

239. Kutolewa kwa nakala ya amri ya kuachiwa iliyothibitishwa na karani au afisa mwingine wa mahakama italazimika,

bila uthibitisho mwingine, kuwa kuzuizi kwa mashtaka lingine litakalofunguliwa katika suala hilo dhidi ya mtuhumiwa huyohuyo.

Maelezo ya
mashahidi wa
kitabibu

240.-(1) Katika mwenendo wa kesi yoyote iliyo mbele ya mahakama ya chini, waraka wowote unaodhaniwa kuonyesha kuwa ni taarifa iliyosainiwa na shahidi tabibu katika suala ambalo moja kwa moja ni suala la taaluma ya utabibu au upasuaji litapokelewa katika ushahidi.

(2) Mahakama inaweza **kudhania** kwamba sahihi iliyowekwa katika waraka wowote wa maandishi ni halali na kwamba mtu aliyesaini waraka huo alikuwa na wadhifa wa ofisi hiyo au alikuwa na sifa za kitaaluma zilizomwezesha kushikilia nafasi au kuwa nazo wakati anaweka saini katika waraka huo.

(3) Wakati taarifa iliyorejewa katika kifungu hiki inapokelewa kama ushahidi mahakama inaweza kama inafaa, na kama ikiombwa na mshtakiwa au wakili wake, kumwita kufanya awepo kwa kuhojiwa zaidi mtu huyo aliyeandaa taarifa na mahakama itamtaarifu mshtakiwa kuhusu haki yake ya kumtaka mtu aliyeandaa taarifa kuitwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki kidogo.

(b) Ukomo Na Mambo Ya Pেকে Yanayohusiana Na Mashauri Yaliyo Mbele Ya Mahakama Za Chini

Ukomo wa muda
kwa mashitaka ya
haraka katika
mazingira fulani

241. Isipokuwa tu pale ambapo muda mrefu zaidi unaruhusiwa na sheria, hakuna kosa, ambalo adhabu ya juu kabisa haizidi kifungo cha miezi sita au faini ya shillingi elfu tano au vyote litasikilizwa na au kuendeshwa na mahakama ya chini isipokuwa kama shtaka au lalamiko kuhusiana nalo liwe limepelekwa katika kipindi cha miezi kumi na mbili tangu muda wa kutokea kwa suala hilo linalohusu shtaka au lalamiko hilo.

Utaratibu kwa kosa
ambalo halifai kwa
uendeshaji wa
haraka

242. Iwapo katika **mtiririko wa mwenendo wa kesi** inaonekana kwa hakimu katika hatua yoyote ya mwenendo kwamba kesi hiyo ni moja wapo ya kesi ambazo inatakiwa iendeshwe na kusikilizwa na Mahakama Kuu, atasimamisha mwenendo wa kesi hiyo na kumuweka mtuhumiwa tayari kwa ajili ya mashtaka baada ya maelezo mbele ya Mahakama Kuu, na katika hilo atatumia utaratibu uliowekwa ndani ya Sheria hii unaohusiana na maandalizi ya mtuhumiwa kwa ajili ya mashtaka katika Mahakama Kuu..

Kupeleka Watuhumiwa kwa Ajili ya Mashitaka na Mahakama za Chini Kwenda
Mahakama Kuu

(a) Masharti Yanayohusiana na Kupelekwa Watuhumiwa kwa ajili ya Mashitaka

Mahakama Kuu

Uwezo wa kupeleka shauri Sheria Na. 12 ya 1987 kif. 25

243.-(1) Hakimu yeyote anaweza, isipokuwa kama amezuiwa kufanya hivyo na masharti ya ajira yake, kumwandaa mtu yoyote kwa ajili ya mashtaka mbele ya Mahakama Kuu.

Sura ya 200

(2) **Pale ambapo katika** muda wowote ndani ya kipindi cha **kusikilizwa kwa shauri** mbele ya mahakama ya chini lakini kabla ya kutiwa hatiani maelezo ya kesi yanaonyesha kwamba mtuhumiwa ametenda kosa ambalo ingebidi ashtakiwe chini ya Sheria ya Makosa ya Kuzuia Uhujumu Uchumi, hakimu atasimamisha mwenendo mzima, na kumwagiza mwendesha mashtaka kutengeneza shtaka jipya chini ya kifungu husika cha Sheria ya Kuzuia Makosa ya Uhujumu Uchumi na kisha ataendelea kumshughulikia kwa mujibu wa kifungu cha 29 na 30 cha sheria hiyo.

Mahakama kuendesha mashauri yaliyoletwa

244. Wakati wowote shtaka linapoletwa dhidi ya mtu yeyote kuhusu kosa ambalo haliwezi kusikilizwa na mahakama ya chini au ya kwamba mahakama imeshauriwa na Mkurugenzi wa Mashtaka kwa maandishi au vinginevyo kwamba si vizuri kesi ikamalizwa kwa utaratibu wa mwenendo wa haraka, mashauri yaliyoletwa yatafanyika kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na kwa mahakama ya chini zenye uwezo wa kusikiliza mashauri hayo.

Utaratibu wa kukamata

245.-(1) Baada ya mtu kukamatwa au baada ya kumalizika kwa uchunguzi na kukamatwa huko kwa mtu yeyote ni kuhusiana na kutenda kosa linalosikilizwa na Mahakama Kuu, mtu aliyekamatwa atatakiwa kuletwa ndani ya kipindi kilichoelezwa chini ya kifungu cha 32 cha Sheria hii mbele ya mahakama ya chini yenye uwezo wa kimamlaka ndani ya eneo la mipaka alilokamatiwa, pamoja na hati ya mashtaka ambayo inaonyesha wanataka kumshtaki, ili aweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria, na kwa kufuata Sheria hii.

(2) Wakati wowote mtu anapoletwa mbele ya mahakama ya chini kwa kufuata kifungu kidogo cha (1), hakimu anayehusika atamsomea na kumfafanulia mtuhumiwa shtaka au mashitaka kama yalivyoonyeshwa katika hati ya mashitaka ambayo anatarajiwa kushtakiwa nayo mshitakiwa lakini mshitakiwa hatatakiwa kujibu au kusema lolote kuhusu shtaka.

(3) Baada ya kumsomea na kumfafanulia mshtakiwa kuhusu shtaka au mashitaka hakimu atamweleza mshitakiwa katika maneno yafuatayo au maneno yenye maana kama hii:

“Hii si mahakama yako ambayo kesi yako itasikilizwa iwapo utasikilizwa baadaye katika Mahakama Kuu, na ushahidi dhidi yako utatolewa. Ndipo utakuwa na uwezo wa kuleta utetezi wako na kuwaita mashahidi kwa ajili yako”

(4) Baada ya mtu kupelekwa rumande au baada ya kuachiwa kwa dhamana na mahakama ya chini au baada ya uchunguzi

kukamilika lakini kabla ya mtuhumiwa kukamatwa , afisa polisi au mtumishi wa umma yeyote mwenye kusimamia uchunguzi huo wa kijinai chini ya Sheria hii, atatakiwa kuhakikisha kwamba maelezo yanawekwa katika nakala nne za watu anaotarajia kuwaita kama mashahidi katika kesi, zinachapwa vizuri, kutunzwa na kutumwa pamoja na faili la polisi kwa Mkurugenzi wa Mashtaka au mtumishi mwingine yeyote wa umma aliyemteua kwa niaba yake.

(5) Iwapo Mkurugenzi wa Mashtaka au mtumishi huyo mwingine wa umma aliyeteuliwa, baada ya kusoma faili la kesi la polisi na maelezo ya mashahidi watarajiwa, ana maoni kwamba ushahidi uliopo hautoshelezi kuruhusu kufungua kesi au haishauriwi kushtaki , atatakiwa ,kama mtuhumiwa ameshashtakiwa mara moja kuagiza kufuta kesi, isipokuwa akiwa na sababu ya kuamini kwamba uchunguzi zaidi utakaoendelea utabadilisha msimamo, kwahiyo katika mazingira hayo ataagiza uchunguzi zaidi ufanyike

(6) Iwapo Mkurugenzi wa Mashtaka au mtumishi huyo mwingine wa umma, baada ya kusoma faili la kesi la polisi pamoja na maelezo ya mashahidi watarajiwa , akiamua kwamba ushahidi uliopo au kesi yenyewe inapelekea mtuhumiwa kujibu shtaka, atatakiwa kuandika au kuhakikisha kwamba inaandikwa hati ya maelezo ya mashtaka kwa mujibu wa sheria, na akishaisaini, atapeleka pamoja na nakala tatu za kila maelezo ya mashahidi zilizopelekwa kwake chini ya kifungu kidogo cha (4) pamoja na waraka wenye ushahidi wa shahidi yoyote ambao haujawekwa kwenye maelezo ya maandishi.

(7) Baada ya hati ya maelezo ya mashtaka kupelekwa Mahakama Kuu, Msajili atatakiwa kuhakikisha kwamba nakala yake inapelekwa kwenye mahakama ya wilaya ambayo mtuhumiwa kwa mara ya kwanza alipelekwa au ndani ya mipaka ambayo mtuhumiwa anaishi.

Kupelekwa kwa ajili
ya kusilikizwa na
mahakama

246.-(1) Baada ya kupokea nakala ya hati ya maelezo ya mashtaka pamoja na notisi, mahakama ya chini itatakiwa kumwita mshtakiwa kutoka rumande au kama bado hajakamatwa kutoa amri ya kukamatwa na kuhudhuria mbele yake na kumpelekea yeye mwenyewe au wakili wake nakala ya hati ya maelezo ya mashtaka na notisi ya kesi iliyopelekwa kwake chini ya kifungu kidogo cha (7) cha kifungu cha 245 na kumuwezesha kuwepo mbele kwa mashtaka ya mahakama, na amri ya kupelekwa kwa mashtaka itakuwa mamlaka tosha kwa mtu aliyemfawidhi wa mahabusu husika kumtoa mshtakiwa kutoka magereza siku iliyopangwa na kuhakikisha anafika mbele ya mahakama.

(2) Baada ya kufika kwa mtuhumiwa mbele ya mahakama, mahakama ya chini itamsomea na kumwelezea au itahakikisha anasomewa mshtakiwa hati ya maelezo ya mashtaka iliyoletwa dhidi yake, pamoja na maelezo ya au vielelezo vyenye ushahidi wa mashahidi ambao Mkurugenzi wa Mashtaka anatarajia kuwaita wakati

wa usikilizaji wa kesi.

(3) Baada ya kufuata masharti ya kifungu kidogo cha(1) na cha (2) mahakama itamweleza mshtakiwa kwa maneno yafuatayo au kwa maneno inayofanana nayo:

"Sasa umesikia kiini cha ushahidi ambao upande wa mashtaka unatarajia kuuleta katika kesi yako hasa wakati wa usikilizaji. Unaweza kukaa na kuutunza utetezi wako, kitu ambacho ni haki na uhuru wako kufanya, au unaweza kusema chochote ambacho ni muhimu kwenye mashtaka dhidi yako. Chochote utakachosema kitaandikwa na kitatumika kama ushahidi katika kesi yako".

(4) Kabla ya mshtakiwa kusema chochote mahakama itatakiwa kumwambia na kumweleweshwa kwamba asitegemee chochote kutokana na ahadi ya kupendelewa na asiogope chochote kutokana na vitisho vilivyotolewa kwake kumfanya akubali kosa au akiri kufanya kosa, lakini chochote atakachosema kitatolewa kama ushahidi katika kesi yake bila kujali ahadi au vitisho..

(5) Kila kitu ambacho mshtakiwa anakisema kitatakiwa kuandikwa kama kilivyo na kitaonyeshwa au kusomwa kwa mhusika na atakuwa huru kueleza au kuongeza chochote katika kumbukumbu hiyo.

(6) Wakati kumbukumbu ya maelezo, kama ipo, iliyotolewa na mshtakiwa imethibitishwa naye kwamba huo ndio ukweli aliosema, kumbukumbu hiyo itasainiwa na hakimumu ambaye atathibitisha kwamba maelezo hayo yalichukuliwa mbele yake baada ya kumsikiliza na imebeba maelezo yote ya kweli yaliyotolewa na mshtakiwa, na mshtakiwa atasaini au atathibitisha kwa alama kumbukumbu hiyo kwa alama ya kidole chake lakini kama akikataa mahakama itatakiwa kuandika kukataa kwake na kumbukumbu hiyo itatumika kama vile mshtakiwa alisaini.

Mashahidi wa upande wa mashtaka na upande wa utetezi

247. Mara baada ya kufuata masharti ya vifungu vya 245 na 246, mahakama itaandaa orodha ya mashahidi ambao Mkurugenzi wa Mashtaka anatarajia kuwaita na kuwatumia na atamuuliza mshtakiwa kama anatarajia kuwaita mashahidi katika **kesi yake**, na kama ndivyo, kama yuko tayari kutoa majina na anuani ili ikiwezekana waweze kuitwa, na kama ataridhia, mahakama itayaandika majina na anuani za mashahidi ambao mshtakiwa amewataja.

Kuahirishwa kwa shauri.

248.-(1) Iwapo kwa sababu yoyote ya msingi, itakayorekodiwa katika mwenendo, mahakama inaona ni lazima au imeshauriwa kuahirisha mwenendo, inaweza kufanya hivyo mara kwa mara kwa hati, itampeleka mahabusu mshtakiwa kwa kipindi fulani, kisichozidi siku kumi na tano kwa mkupuo katika jela au sehemu nyingine yoyote ya usalama.

(2) Pale muda wa mahabusu si zaidi ya siku tatu, mahakama inaweza, kwa kusema, ikatoa amri kwa afisa au mtu ambaye

mshtakiwa yupo chini yake au afisa mwingine yeyote anayefaa au mtu, kuendelea kumweka mshitakiwa chini ya uangalizi na kumleta mbele ya mahakama katika muda atakoahitajika ili kuanza au kuendelea na uchunguzi.

(3) Wakati mshitakiwa akiwa mahabusu mahakama inaweza wakati wowote kutoa amri mshatakiwa apelekwe mbele yake.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 148 mahakama inaweza kumpatia dhamana mshtakiwa aliye mahabusu.

Mtuhumiwa ana haki ya kupewa nakala ya mwenendo wa kesi.

249.-(1) Mtu ambaye amepolekwa kwa ajili ya mashtaka kusikilizwa Mahakama Kuu ana haki wakati wowote kabla ya kesi yake kuanza kusikilizwa kupewa nakala ya kumbukumbu za mwenendo uliopo polekwa bila malipo yoyote.

(2) Mahakama itatakiwa katika muda wa kumpeleka mshitakiwa kwa kesi yake, impe taarifa mshtakiwa juu ya haki yake ya kupata nakala ya kumbukumbu za mwenendo uliopo polekwa bila malipo.

(3) Kila kumbukumbu ya mwenendo atakayopatiwa mshtakiwa kwa mujibu wa kifungu hiki itatakiwa iwe na nakala ya hati ya shtaka au mashtaka, nakala za maelezo na vielelezo vilivyotolewa mahakamani katika kipindi cha mwenendo wa mashtaka uliopo polekwa pamoja na nakala ya kumbukumbu za mwenendo mbele ya mahakama.

Mahakama inaweza kumlazimisha shahidi kuhudhuria kwenyekesi

250.-(1) Mwendesha mashtaka anaweza ndani ya muda wowote wakati wa kusikiliza kesi Mahakama Kuu, kuomba mahakama imwite mtu yeyote ambaye kufika kwake kunaweza kuhitajika wakati wa kusikilizwa **kwa kesi** ili kutoa ushahidi au kutoa waraka wowote na kumlazimisha mtu huyo kufika siku ya kusikilizwa kwa kesi.

(2) Baada ya ombi kufanyika chini ya kifungu kidogo cha (1) mahakama itamwita mtu huyo ambaye ombi linamtaka kufika mbele yake na pale anapofika, mahakama inaweza kumbana kwa kujidhamini yeye mwenyewe pamoja au bila ya wadhamini kama itakavyoonekana inafaa, kufika wakati wa kusikiliza wa kesi kufuatana na hati za wito zilizotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 263.

Kukataa kulazimishwa

251. Iwapo mtu ametakiwa ajidhamini mwenyewe kwa mujibu wa kifungu cha 250 na anakataa kujidhamini mahakama inaweza kumpeleka jela au chini ya uangalizi wa afisa yeyote wa mahakama, ambako anabakia hadi muda wa kusikilizwa kesi utakapofika au pale ambapo kesi dhidi ya mshtakiwa itakapomalizika au isipokuwa kama katika muda huo atakubali kujidhamini kama atakavyotakiwa na mahakama.

(b) Utunzaji wa Ushahidi katika Kesi Fulani.

Kuchukua ushahidi wa watu wanaoumwa sana na wasioweza kuhudhuria kesi.

252. Pale inapoonekana kwa hakimu kwamba mtu yeyote ambaye ni mgonjwa sana au kaumizwa sana na inaonekana kwamba hawezi kupona au kwamba kwa sababu zozote zile anaweza asiwepo kutoa ushahidi katika siku ya usikilizaji wa kesi lakini anaweza na yuko tayari kutoa ushahidi wa msingi kuhusiana na kosa, mahakama inaweza kuchukua kwa maandishi maelezo yake kwa kiapo au kwa kuthibitisha na atasaini na kuthibitisha kwamba imebeba maelezo yake ya kweli na hakimu anayechukua maelezo hayo atathibitisha sababu za kuchukua maelezo na ataeleza tarehe na mahali na ni lini na wapi yalipochukuliwa, atatunza maelezo hayo na kuyaweka kwenye faili kwa ajili ya kumbukumbu.

Isipokuwa kwamba pale ambapo maelezo ni ya mtu ambaye kwa sababu ya umri wake mdogo au kwa sababu ya imani yake ya kidini hatakiwi kwa maoni ya hakimu kuapa au kuthibitisha, maelezo yanaweza kuchukuliwa bila kiapo au kuthibitisha.

Taarifa kutolewa.

253.-(1) Pale mtu yeyote ameshtakiwa au amepelekwa kwa ajili ya mashtaka ambayo kosa lake linahusiana na maelezo ya maandishi yaliyoelezwa katika kifungu cha 252 inategemewa kuhusiana (katika vifungu vya 257 and 258 anatajwa kama “mshtakiwa”) notisi ya uhakiki itotolewa juu ya nia ya kuchukua maelezo ya maandishi ya mwendesha mashtaka na mtu huyo.

(2) Iwapo mtu huyo yupo chini ya ulinzi, anaweza, na kama atahitaji kuletwa na afisa ambaye yupo chini ya uangalizi wake kwa amri ya maandishi ya hakimu, sehemu ambayo maelezo yatachukuliwa..

Nafasi ya kuhoji ushahidi na kuhamisha maelezo

254. Pale ambapo maelezo yanachukuliwa mbele ya mshtakiwa au wakili wake (mwendesha mashtaka kama naye atakuwepo) watatakiwa wapewe nafasi ya kuuliza maswali kwa shahidi na maandishi na majibu ya shahidi na maandishi yatakuwa sehemu ya maelezo na kama mshtakiwa atapelekwa kwa ajili ya mashtaka, maelezo yatatakiwa kupelekwa kwa Msajili wa Mahakama Kuu na nakala yake itapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Matumizi ya maelezo ya ushahidi

255.-(1) Kila maelezo yaliyochukuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 252 na kuhakikiwa na kuthibitishwa na hakimu kwa namna ambayo inatakiwa na kifungu hicho itatakiwa bila ushahidi wowote mwingine kupokelewa katika ushahidi kwenye kesi yoyote, ama Mahakama Kuu au mahakama ya chini ambayo mshtakiwa anashtakiwa na kosa ambalo maelezo yanahusiana iwapo-

(a) mahakama inaridhika kwamba mtu aliyetoa maelezo hayo amefariki au kufika kwake mahakamani hakuwezekani bila kuchelewa kwa kiwango kikubwa, gharama au usumbufu ambao kwa mazingira ya kesi

utakuwa hauna msingi.

- (b) mshtakiwa alipata notisi au taarifa ya mahakama ya kuchukua maelezo kama ilivyoelezwa na kifungu cha 253 na alikuwa au angekuwa kama angechagua kuwepo . nafasi ya kutosha ya kumuuliza maswali shahidi wa maandishi.

(2)Wakati kesi yoyote mahakamani ambayo maelezo hayo yametumika katika ushahidi imemalizika, maelezo yatarudishwa kwa hakimu aliyeyaandika maelezo hayo kwa ajili ya kuyafaili kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 252.

(3) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachotafsiriwa kwamba kinapingana na masharti ya kifungu cha 34 cha Sheria ya Ushahidi.

Sura ya .6

(c) Mwenendo baada ya Kupelekwa kwa Ajili ya Mashtaka

Kupeleka
kumbukumbu
Mahakama Kuu.

256. Wakati mshtakiwa amepelekwa kwa ajili ya mashtaka yake kumbukumbu za mwenendo wa kupelekwa kwa mashtaka zilizosainiwa na kuthibitishwa na hakimu zitapelekwa bila kuchelewa na mahakama iliyopeleka mshtakiwa kwa Msajili wa Mahakama Kuu na nakala zilizothibitishwa za hati ya mashtaka na mwenendo zitapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kusikilizwa na
hakimu mkazi
mwenye mamlaka
ya ziada Sheria Na.
2 ya 1996 Jedwali.
17 ya 1996 Jedwali

256A.-(1) Mahakama Kuu inaweza kuagiza kwamba kitendo cha kusomewa na kujibu shtaka pamoja na usikilizaji wa kesi ya mshtakiwa aliyepelekwa kwa mashtaka Mahakama Kuu uhamishiwe na ufanywe na hakimu mkazi ambaye amepewa mamlaka ya **kupitiliza** kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 173.

(2) Ili kuzuia mgongano, mwenendo wowote au maamuzi yoyote yaliyofanywa na hakimu mkazi mwenye mamlaka ya kupitiliza kabla ya masharti ya vifungu hivi kuanza kufanya kazi, itachukuliwa kwamba vilifanyika au kufanywa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki..

(3) Masharti ya Sheria hii yanayohusu namna Mahakama Kuu inavyotekeleza mamlaka yake ya awali yatakuwa kama yalivyo, kwa namna ile yanavyohusika, yatumika pia kuendesha mwenendo wa kesi mbele ya hakimu mkazi katika kifungu hiki kwa namna ileile yanavyotumika kuendesha mwenendo wa kesi za namna hii mbele ya Mahakama Kuu.

Taarifa ya kesi.

257. Baada ya kupokea nakala za kumbukumbu za mwenendo wa upelekaji wa mashtaka Mahakama Kuu , Msajili au msaidizi wake ataweka au ataambatanisha katika kila hati ya maelezo ya kosa iliyo katika faili na katika kila nakala inayopelekwa kwa afisa wa mahakama au afisa wa polisi kwa kusambaza, notisi ya usikilizaji

wa kesi ambayo itaeleza vikao vya Mahakama Kuu ambapo mshtakiwa atashtakiwa kwa hati ya maelezo ya shtaka itakayokuwa kwa namna ifuatayo au inayokaribiana na hiyo:

"A.B.

Tunakupa taarifa kwamba utashtakiwa kwa mujibu wa maelezo ya shtaka na hii ni nakala halisi katika vikao maalum vya usikilizaji wa kesi wa Mahakama Kuu kitakachofanyika katika.....
.....siku ya20....."

Nakala ya maelezo
ya mashtaka na
taarifa
kuwasilishwa.

258. Msajili atapeleka au atahakikisha zinapelekwa kwa afisa wa mahakama au kwa afisa wa polisi anayepeleka hati ya maelezo ya mashtaka nakala yenye taarifa ya kusikilizwa kwa kesi na, iwapo kuna washtakiwa wengi wameandaliwa kwa mashtaka zaidi ya mmoja, nakala nyingi kuwatosha washtakiwa wote: na afisa wa mahakama au wa polisi kwa haraka sana baada ya kupokea nakala za hati ya maelezo ya mashtaka, taarifai za kusikilizwa kwa kesi, na angalau siku tatu kabla ya siku iliyoelezwa ya kuanza kwa usikilizaji wa kesi, yeye mwenyewe au msaidizi wake au afisa yeyote atapeleka kwa mshtakiwa au mtu yeyote aliyeandaliwa kwa ajili ya mashtaka nakala ya mashtaka au nakala za maelezo ya mashtaka pamoja na taarifa na atamwelezea aina na umuhimu wake, na wakati mshtakiwa mmojawapo yupo nje kwa dhamana na hawezi kupatikana kwa urahisi, ataacha nakala ya maelezo ya mashtaka na taarifa/notisi ya kusikilizwa kwa kesi kwa mmojawapo wa nyumbani kwake katika nyumba yake ya kuishi au kwa mmojawapo wa watu waliomdhamini na kama hakuna mmojawapo anayepatikana, ataweka karatasi ya nakala na notisi kwa kuibana nje ya mlango mkuu wa nyumba ya kuishi au nyumba za kuishi za mshtakiwa au za yeyote katika wadhamini wake.

Isipokuwa kwamba hakuna chochote kitakachozuia mtu yeyote aliyepelekwa kwa mashtaka, aliye katika uangalizi wakati wa ufunguzi wa au wakati wa usikilizaji wa kesi kuendelea kwa mashtaka dhidi yake kama atatoa ridhaa yake na hakuna pingamizi lolote limetolewa na upande wa Jamhuri.

Taarifa ya
uwasilishaji.

259. Afisa anayepeleka nakala ya au nakala za hati ya maelezo ya mashtaka na notisi ya au notisi za kesi atatakiwa kuleta kwa Msajili taarifa ya waliopelekewa na kupokea vielelezo vya kesi.

Kuahirishwa kwa
kesi.

260.-(1) Itakuwa ni halali kwa Mahakama Kuu baada ya maombi ya mwendesha mashtaka au mshtakiwa, kama mahakama itaona kuna sababu za kutosha za kuchelewa, kuahirisha usikilizaji wa kesi dhidi ya mshtakiwa hadi kipindi cha mahakama kitakachofanyika katika wilaya husika au sehemu nyingine yoyote itakayofaa au katika kipindi kingine kitakachofuata.

(2) Mahakama Kuu inaweza kutoa mwongozo wa marekebisho

ya hati ya maelezo ya mashtaka na namna ya kupeleka notisi kama mahakama itakavyoona inafaa kutokana na matokeo ya amri iliyoanywa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1)

Maelezo ya shtaka
Mkurugenzi wa
Mashtaka

261. Hati zote za maelezo ya mashtaka iliyoandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 257 zitakuwa katika jina na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 92, zilizosainiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

Muundo wa maelezo
ya shtaka

262 Kila hati ya maelezo ya mashtaka itawekewa tarehe ya siku iliposainiwa, pamoja na marekebishi yoyote kama yatakavyokuwa muhimu kuyaweka katika mazingira ya kila kesi, inaweza kuanza katika namna ifuatayo:

" Katika Mahakama Kuu ya Tanzania

Siku ya..... mwezi wa

..... 20.....

Katika kikao kitakachofanyika ndani ya siku ya 20..... Mahakama imepewa taarifa na Mkurugenzi wa Mashtaka kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano kwamba A.B. anashtakiwa na kosa (makosa) yafuatayo ".

Mashahidi kuitwa

263. Msajili wa Mahakama Kuu atahakikisha kabla ya kuanza kwa usikilizaji wa kesi anatoa hati za wito wa kufika mahakamani kwa ajili ya usikilizaji wa kesi kwa mashahidi wote ambao maelezo yao yalitolewa katika kipindi cha mwenendo wa upelekaji wa kesi na mashahidi wote ambao majina yao na anuani zao yaliyotolewa kwa hakimu aliyefanya upelekaji wa kesi na mshtakiwa.

SEHEMU YA NANE

UTARATIBU WA USIKILIZAJI KESI ZILIZO MBELE YA MAHAKAMA KUU

(a) Utendaji na Mfumo wa Usikilizaji wa Kesi

Utendaji
Mahakama Kuu
katika mamlaka
yake ya jinai.

264. Mahakama kuu inaweza, kwa kuzingatia vifungu vya Sheria hii na sheria zingine zozote, kudhibiti utendaji wake katika utekelezaji wa mamlaka yake ya kijinai.

Usikilizwaji wa
kesi mbele ya
Mahakama Kuu
utakuwa kwa
msaada wa Wazee
wa Baraza.

265. Usikilizaji wa kesi mbele ya Mahakama Kuu utafanyika kwa kusaidiana na wazee wa baraza ambapo idadi yao itakuwa wawili au zaidi kama mahakama itakavyoona inafaa.

(b) Wazee Wa Baraza

Wajibu wa
kutumikia kama
mzee wa baraza

266.-(1) Kwa kuzingatia misamaha chini ya masharti ya kifungu cha 267 na kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, watu wote wenye umri wa kati ya miaka ishirini na moja hadi miaka sitini wanaweza kutumikia kama wazee wa baraza.

(2) Mahakama kuu mara kwa mara itatengeneza kanuni zinazoeleza udhibiti wa eneo ambalo mtu anaweza kuitwa na kufanya kazi ya kusadia mahakama kama mzee wa baraza.

(3) Mtu atakuwa hana sifa za kufanya kazi kama mzee wa baraza ikiwa amewahi kupatikana na hatia na kufungwa kwa kipindi kisichozidi miezi sita kwa kosa linalohusiana na maadili.

(4) Hakuna mwenendo utakaokuwa batili kwa sababu tu mmoja wa wazee wa baraza hakuwa na sifa za kuwa au haruhusiwi kutumikia kama mzee wa baraza.

Misamaha.

267. Watu wafuatao hawaruhusiwi kutumikia kama wazee wa baraza:

- (a) mawaziri na wabunge
- (b) majaji na mahakimu;
- (c) watu ambao wanafanya kazi za kichungaji au za kidini kwa dini zao mbalimbali;
- (d) **tabibu, mpasuaji, daktari wa meno na mfamasia walioko kazini;**
- (e) wanasheria wanaojishughulisha na kazi za kisheria;
- (f) maofisa na watu wengine wote katika majeshi ya Jamhuri ya Muungano;
- (g) watu waliokatazwa kujiwakilisha mahakamani kwa mujibu wa vifungu vya Sheria ya Mwenendo wa Madai au kanuni zozote zile zilizotengenezwa kwa mujibu wa sheria hiyo;
- (h) watu ambao wana ulemavu wa akili sawasawa au wana ugonjwa wa mwili.;
- (i) maofisa wa polisi na magereza ;
- (j) maofisa wengine wowote wa Serikali na watu wengine ambao wanaweza **kukatazwa** na Jaji Mkuu kufanya kazi hiyo

Sura ya 33

Hakuna msamaha
kijinsia au kindoa
katika wajibu wa
kutumikia kama
mzee wa baraza

268. Mtu hatakatuzwa kwa sababu ya jinsia yake au ndoa kutumikia kama mzee wa baraza lakini jaji au hakimu anaweza kwa namna anavyoona inafaa kwa ombi litakaloletwa kwake kwa niaba ya mwendesha mashtaka au mshtakiwa au yeye mwenyewe, kutoa amri kwamba wazee wa baraza watakuwa wanaume tu au wanawake tu kwa namna mazingira ya kesi yatavyohitaji au anaweza kwa ombi likiletwa na mwanamke kwamba asiwe mzee wa baraza katika aina fulani ya kesi kwa sababu ya aina ya ushahidi utakaotolewa kwa mujibu wa masuala yanayotakiwa kusikilizwa, atatoa msamaha huo..

(c) Mahudhurio ya Wazee wa Baraza

Kuwaita wazee wa baraza

269.-(1) Msajili wa Mahakama Kuu atatakiwa ndani ya muda usiozidi siku kumi na nne kabla ya siku iliyopangwa ya kufanyika kikao chochote cha Mahakama Kuu , kumwagiza hakimu mkazi au hakimu wa wilaya ambaye ana mamlaka katika wilaya husika ambapo kikao kitafanyika kuita idadi fulani ya watu ili watumikie kama wazee wa baraza katika vikao husika kama Msajili atakavyoona inafaa, na Hakimu atalazimika kufuata maagizo ipasavyo.

(2) Pale ambapo kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) hakimu mkazi au hakimu wa wilaya ameagizwa kuwaita wazee wa baraza ,atachagua na kuwaita watu ambao anaona wanafaa na watawajibika kutumikia kama wazee wa baraza kwa mujibu wa kifungu cha 266.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya vifungu kidogo cha (1) na cha (2) , hakimu mkazi au hakimu wa wilaya akiagizwa na Msajili anaweza kukaimisha madaraka ya kuchagua wazee wa baraza kwa afisa tawala mwenye mamlaka katika wilaya au mkoa husika.

Muundo wa wito

270.Kila hati ya wito kwa mzee wa baraza itakuwa kwa maandishi na itatamtaka ahudhurie katika muda na mahali palipotajwa ndani yake. .

Pingamizi kwa wito wa kutumikia kama mzee wa baraza

271.-(1) Mtu yeyote ambaye amepokea hati ya wito wa iliyotolewa chini ya kifungu cha 269 cha kutumikia kama mzee wa baraza anaweza, kama ataona kwamba haruhusiwi chini ya kifungu cha 267 kutumikia kama mzee wa baraza, atafika bila kuchelewa mbele ya hakimu wa wilaya na hakimu mkazi kabla ya tarehe aliyotakiwa kufika kwa mujibu wa hati ya wito na atapinga hati hiyo ya wito na kama hakimu ataridhika kwamba mtu huyo hatakiwi kutumikia kama mzee wa baraza atatakiwa kufuta hati hiyo ya wito na kumuondolea mtu huyo amri ya kuhudhuria.

(2) Kufika mbele ya hakimu wa wilaya au hakimu mkazi chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) kutafanywa na mtu mwenyewe anayepinga isipokuwa katika mazingira ya mtu kupinga chini ya mashart ya aya ya (g) ya kifungu cha 267 ambapo mtu atakayemridhisha hakimu kwamba ameruhusiwa kufika kwa niaba anaweza kuruhusiwa kumwakilisha.

Udhuru wa kutofika

272. Mahakama Kuu inaweza, kwa sababu ya msingi kumpa udhuru mzee wa baraza yeyote kuhudhuria kikao fulani na itaweza kama ikiona inafaa, wakati wa kumaliza kusikiliza kesi yoyote, kuagiza kwamba wazee wa baraza waliotumikia katika usikilizaji wa kesi hawatakiwi kuitwa tena kutumikia kama mzee wa baraza kwa kipindi

cha miezi kumi na mbili.

Orodha ya wazee wa baraza wanaohudhuria

273. Katika kila kikao Mahakama Kuu itatahakikisha kwamba inatengenezwa orodha ya majina ya watu ambao walihudhuria na kutumikia kama wazee wa baraza katika vikao mbalimbali.

Adhabu kwa kutokuhudhuria kwa mzee wa baraza

274.-(1) Mtu yoyote aliyelitwa kuhudhuria kama mzee wa baraza, na ambaye bila sababu ya msingi anashindwa kuhudhuria kama alivyotakiwa na hati za wito au kama amehudhuria akaondoka bila kupata ruhusa ya Mahakama Kuu au akashindwa kuhudhuria baada ya kuahirishwa kwa kesi na mahakama pamoja na kutakiwa kuhudhuria atatakiwa kwa amri ya Mahakama Kuu kulipa faini isiyozidi shilingi mia tano.

(2) Faini iliyowekwa chini ya kifungu kidogo cha (1) itatozwa na hakimumu wa wilaya au hakimumu mkazi kutoka kwenye mali zinazohamishika zinazomilikiwa na mzee wa baraza zilizopo ndani ya mipaka ya kimamlaka ya hakimumu husika.

(3) Kwa sababu ya msingi iliyoonyeshwa, Mahakama Kuu inaweza kurudisha au kupunguza faini yoyote iliyowekwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1).

(4) Inaposhindikana kukusanya faini kwa njia ya kukamata na kuuza, mzee wa baraza anaweza kwa amri ya Mahakama Kuu kufungwa kama mfungwa wa madai kwa muda wa siku kumi na tano isipokuwa kama faini italipwa kabla ya kuisha kwa muda huo.

(d) Kuleta Mahabusu mbele ya Mahakama

Kujibu maelezo ya shtaka Sheria Na. 4 ya 1991 kif. 2

275.-(1) Mshtakiwa anayeshitakiwa mbele ya Mahakama Kuu kutokana na maelezo ya hati ya shtaka atawekwa kizimbani bila kufungwa, isipokuwa kwa amri ya mahakama pale itakavyoona vinginevyo, maelezo ya hati ya shtaka yatasomwa kwake na Msajili au afisa mwingine wa mahakama na kufafanuliwa kama itahijika na afisa au kutafsiriwa na mkalimani wa mahakama atatakiwa kujibu shtaka haraka isipokuwa pale mshtakiwa anapotakiwa kupatiwa nakala ya hati ya maelezo ya shtaka, anapopinga kwa kutaka kupatiwa hati hiyo na kama mahakama ikagundua ukweli kwamba mshtakiwa hakufikishiwa hati hizo.

(2) Baada ya mtuhumiwa kujibu mashtaka aliyosomewa mahakamani chini ya kifungu hiki, mahakama itatakiwa kupata kutoka kwake anuani yake ya kudumu na itaiandika na kuitunza.

Amri ya kurekebisha maelezo ya shtaka, usikilizaji tofauti na uahirishaji wa usikilizaji

276.-(1) Kila pingamizi kuhusiana na makosa na mapungufu ya wazi ya hati ya maelezo ya shtaka yatashughulikiwa haraka sana baada ya hati ya maelezo ya shtaka kusomwa kwa mtuhumiwa na siyo baadaye.

(2) Pale kabla ya usikilizaji wa kesi, baada ya hati ya maelezo

ya shtaka au katika hatua yoyote ya usikilizaji wa kesi imeonekana kwa mahakama kwamba hati ya maelezo ya shtaka ni mbovu , mahakama itatoa amri ya kurekebisha hati ya maelezo ya mashtaka itakavyoona inafaa katika kulingana na mazingira ya kesi isipokuwa tu kwa kuzingatia undani wa kesi yenyewe, marekebisho yaliyotakiwa hayawezi kufanyika bila kuleta uvunjifu wa haki na kila marekebisho hayo yatafanywa kwa mujibu wa masharti ambayo mahakama itaona yanafaa.

(3) Pale hati ya maelezo ya shtaka inapofanyiwa marekebisho, taarifa ya amri ya kufanya marekebisho itaingizwa katika hati ya maelezo ya shtaka na hati ya maelezo ya mshtaka itachukuliwa kwa madhumuni ya mwenendo wa kesi yote kwamba imefailiwa ikiwa katika muundo wa marekebisho.

(4) Pale , kabla ya usikilizaji wa kesi baada ya hati ya maelezo ya shtaka au katika hatua nyingine yoyote ,mahakama ina maoni kwamba mtuhumiwa ataumizwa au kuaibika katika utetezi wake kwa sababu ya kushtakiwa kwa zaidi ya kosa moja katika hati ya maelezo ya shtaka inayofanana au kwamba kwa sababu yoyote ile ni vizuri kuagiza kwamba mtuhumiwa ashtakiwe tofauti kwa kila kosa au kwa makosa mbalimbali aliyoshtakiwa katika hati ya maelezo ya shtaka, mahakama inaweza kutoa amri kwamba mashtaka yafanyike tofauti kwa kila shtaka au mashtaka yaliyopo katika hati ya maelezo ya shtaka

(5) Pale, kabla ya shtaka baada ya hati ya maelezo ya shtaka au katika hatua yoyote ya mashtaka , mahakama ina maoni kwamba kuahirisha kufanyika kwa mashtaka dhidi ya mtuhumiwa ni muhimu kulingana na matokeo ya matumizi ya madaraka ya mahakama kwa mujibu wa Sheria hii,mahakama itatoa amri hiyo ya kuahirisha kufanyika kwa usikilizaji wa kesi kama itakavyoonekana inafaa.

(6) Pale amri inatolewa na mahakama kwa mujibu wa kifungu hiki kwa ajili ya kufanyika kwa mashtaka tofauti au kwa ajili ya kuahirisha kufanyika kwa mashtaka-

(a) mahakama inaweza kutoa amri kwamba wazee wa baraza wanaondolewa katika majukumu ya kutoa maoni katika kosa au makosa ambayo usikilizaji wa kesi yake umeahirishwa kufanyika au katika hati ya maelezo ya shtaka, kama hali itakavyokuwa.

(b) utaratibu katika usikilizaji wa kesi za makosa tofauti utakuwa sawa kama vile kosa limetokana na hati ya maelezo ya shtaka tofauti na utaratibu katika kesi iliyoanzishwa utakuwa sawa alimradi kwamba wazee wa baraza kama wapo wameondolewa kama vile kesi haikuanza kusikilizwa; na

(c) Mahakama inaweza kutoa amri inayompa mtuhumiwa dhamana na pia kuongeza dhamana ya kujidhamini mwenyewe na vinginevyo kama mahakama itakavyoona

inafaa.

(7) Uwezo wowote wa mahakama kwa mujibu wa kifungu hiki utakuwa ni nyongeza tu na wala hautapunguza uwezo wa mahakama kwa mambo yanayofanana au kwa madhumuni sawa.

Kutupiliwa mbali
kwa kwa maelezo ya
shtaka

277.-(1) Iwapo hati ya maelezo ya shtaka haisemi, na haitasema, kwa rekebisho lililoruhusiwa kufanyika chini ya kifungu cha 276 ,itaifanyika kueleza kosa ambalo mtuhumiwa alikuwa na notisi , itafutwa kutokana na hoja iliyopelekwa kabla ya mtuhumiwa hajajibu shtaka au kwa hoja iliyopelekwa wakati wa kukamata kwa hukumu

(2) Maelezo ya maandishi ya kila hoja chini ya kifungu kidogo cha (1) yatapelekwa kwa Msajili au afisa mwingine wa mahakama na au kwa niaba ya mshtakiwa na itaingizwa katika kumbukumbu za mahakama.

Utaratibu kuhusu
kutiwa hatiani
kulikopita.

278.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), pale hati ya maelezo ya shtaka inapokuwa na kosa analoshtakiwa nalo mtuhumiwa kosa ambalo amewahi kupatikana nalo na kutiwa hatiani zamani, utaratibu utakuwa kama ufuatao:-

- (a) sehemu ya hati ya maelezo ya mashtaka inayoeleza kuhusu kupatikana na hatia zamani haitasomwa mahakamani, na wala mtuhumiwa hataulizwa kuhusu kama amewahi kupatikana na hatia zamani kama ilivyosemwa katika hati ya maelezo ya shtaka isipokuwa tu pale ambapo amekubali kosa au amepatikana na hatia ya kosa lingine.
- (b) iwapo atakubali kosa au atapatikana na hatia ya kosa lingine ndipo ataweza kuulizwa kama amewahi kupatikana na hatia zamani kama ilivyosemwa katika hati ya maelezo ya shtaka.
- (c) iwapo atajibu kwamba amewahi kupatikana na hatia zamani, jaji ataendelea kumpangia adhabu husika, au kama atakataa kuwahi kupatikana na hatia zamani ,au akakataa kujibu au kutojibu swali hilo, mahakama itabidi isikilize ushahidi kuhusiana na suala la kupatikana na hatia zamani.

(2) Iwapo katika usikilizaji wa kesi dhidi ya mtuhumiwa kwa kosa linalofuatia, anatoa ushahidi unaohusu tabia yake njema, itakuwa haki kwa wakili wa mashtaka ,katika kujibu hilo , kuleta ushahidi kuhusu kosa au makosa ya zamani kabla ya kupatikana na hatia kwa kosa linalofuatia na mahakama itatakiwa ichunguze kuhusiana na hatia ya au za zamani, wakati huo huo pia ikichunguza kuhusu kosa linalofuatia.

Kukataa shtaka

279. Kila mshtakiwa anayeletwa mbele ya mahakama ambaye

ameshtakiwa kwa hati ya maelezo ya mashtaka kwa kujibu hati hiyo kijumla kwa jibu la si kweli, atachukuliwa kwamba amejijweka tayari kwa ajili ya kesi yake.

Jibu kuhusu kuachiwa kulikopita au kutiwa hatiani kulikopita katika kosa lilelile.

280.-(1) Mshtakiwa yeyote ambaye hati ya maelezo ya shtaka imesomwa kwake anaweza kujibu-

- (a) kwamba amewahi kupatikana na hatia zamani au kuachiwa huru, kama itakavyokuwa, kwa kosa hilo hila au
- (b) kwamba alipata msamaha wa kisheria kwa kosa lake hilo.

(2) Iwapo mojawapo ya majibu yaliyoelezwa hapo juu katika kifungu kidogo cha (1) yamejibiwa au kutamkwa katika kesi yoyote na kupingwa na upande wa mashtaka kuwa na ukweli wowote, mahakama itaamua kama jibu hilo ni la kweli au hapana.

(3) Iwapo mahakama itaona kwamba yaliyosemwa na mtuhumiwa si ya uongo, mshtakiwa atatakiwa kujibu hati ya maelezo ya shtaka.

Kukataa kujibu

281.-(1) Iwapo mshtakiwa yeyote anayepelekwa mbele ya mahakama na anasomewa hati ya maelezo ya shtaka anakaa kimya kwa hila au hataki tu kujibu au bila sababu ya ulemavu, kujibu moja kwa moja hati ya maelezo ya shtaka, mahakama inaweza ikiona inafaa, kutoa amri kwa Msajili au afisa mwingine wa mahakama kujibu hati hiyo ya maelezo ya shtaka kwa jibu la siyo kweli kwa niaba ya mshtakiwa na jibu hilo lililoingizwa litakuwa na nguvu na madhara kama vile mshtakiwa amejibu mwenyewe au mahakama itatakiwa kuendelea kuangalia kuona kama mshtakiwa ana akili timamu au hana akili timamu, na kama ataonekana anazo akili timamu, itaendelea na shtaka na kama ataonekana hana akili na hivyo hana uwezo wa kufanya utetezi, itatoa amri kusimamisha au kuahirishwa kwa kesi na mshtakiwa atapelekwa mahali salama na kwa namna ambayo mahakama itakavyoona inafaa na itapeleka kumbukumbu za mahakama kwa Mwanasheria Mkuu, ili kuangaliwa na Waziri na Waziri anaweza kutoa amri kwamba mshtakiwa apelekwe katika hospitali ya wagonjwa wa akili au sehemu nyingine yoyote inayofaa ya uangalizi salama.

(2) Mwenendo wowote unapofuatia wa mashtaka dhidi ya mtuhumiwa utadhibitiwa kwa mujibu wa kifungu cha 217 na cha 218 cha Sheria hii.

Kukubali shtaka

282. Iwapo mshtakiwa atakubali kosa, jibu lake litaandikwa na anaweza kutiwa hatiani kwa hilo.

Mwenendo baada ya kukana shtaka

283. Iwapo mshtakiwa anakataa kosa au kama jibu la kukataa kosa litaingizwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 281, mahakama

itaendelea kuchagua wazee wa baraza kama ilivyoelekezwa na kifungu cha 285 na kusikiliza kesi hiyo.

Uwezo wa kuahirisha mwenendo wa kesi.

284.-(1)Iwapo , kutokana na kutofika kwa mashahidi au kwa sababu nyingine yoyote ya msingi itakayoandikwa katika mwenendo wa kesi , mahakama inaona ni muhimu au imeshauriwa kuahirisha kuanza kwa , au kuahirisha usikilizaji wa kesi , mahakama inaweza mara kwa mara kusimamisha au kuahirisha usikilizaji wa kesi kwa masharti kama itakavyoona inafaa kwa wakati huo na inaweza kwa hati rasmi, kumpeleka mahabusu mshtakiwa katika jela au sehemu nyingine ya usalama

(2) Katika kipindi cha kuwa mahabusu mahakama inaweza, wakati wowote kuamuru mshtakiwa kuletwa mbele yake.

(3) Mahakama inaweza mtuhumiwa akiwa mahabusu kutoa dhamana kwa mshtakiwa.

Kukoma kwa shtaka mbele ya Mahakama Kuu.Sheria Na. 9 ya 2002 Jedwali.

284A.Kila shtaka mbele ya Mahakama Kuu litakoma baada ya kifo cha mshtakiwa.

(e) Kuchaguliwa kwa Wazee wa Baraza

Kuchaguliwa kwa wazee wa baraza

285.-(1) Wakati shtaka linatakiwa kusikilizwa kwa msaada wa wazee wa baraza, wazee wa baraza watachaguliwa na mahakama.

(2) Mzee wa baraza anaweza kusaidia katika zaidi ya kesi moja, mfululizo.

Kutokuwepo kwa wazee wa baraza

286. Iwapo katika kipindi cha usikilizaji wa kesi kwa msaada wa wazee wa baraza , lakini wakati wowote ule kabla hawajatoa maoni yao, mzee wa baraza mmojawapo kutokana na sababu za msingi akashindwa kuhudhuria kipindi chote cha usikilizaji wa kesi au akashindwa kufika yeye mwenyewe na haiwezekani kwa njia za haraka kuweza kumlazimisha kuhudhuria usikilizaji utaendelea mbele ya wazee wa baraza waliobakia kama tu idadi yao haipungui wawili; na pale usikilizaji utaendelea wazee wa baraza waliobakia watachukuliwa kama ni idadi kamili kwa madhumini ya usikilizaji wa kesi na watakuwa na madaraka ya kufanya uamuzi kwa pamoja au kwa uwingi wao.

Wazee wa baraza kuhudhuria vikao vilivyoahirishwa

287.Iwapo kesi imeahirishwa ,wazee wa baraza watatakiwa kuhudhuria kikao kilichoahirishwa na kikao chochote kinachofuatia hadi mwisho wa kesi.

(f) Kesi kwa Upande wa Mashtaka

Kufungua kesi kwa upande mashtaka

288. Wakati wazee wa baraza wameshachaguliwa, wakili kwa

upande wa mashtaka atafungua kesi yake dhidi ya mshtakiwa na atawaita mashahidi na kupeleka ushahidi unaounga mkono hati ya shtaka.

Mashahidi wa ziada kwa upande wa mashtaka.

289.-(1) Hakuna shahidi yeyote ambaye maelezo yake au ushahidi wake haukusomwa wakati wa mwenendo wa upelekaji wa mashtaka utaletwa na upande wa mashtaka wakati wa usikilizaji wa kesi isipokuwa kama upande wa mashtaka umetoa notisi ya kutosheleza kwa maandishi kwa mshtakiwa au kwa wakili wake juu ya nia ya kuwaita mashahidi hao.

(2) Notisi itaeleza jina na anuani ya shahidi na kiini cha ushahidi ambao anatarajia kuutoa.

(3) Mahakama itafanya uamuzi kuhusu ni notisi gani ya kutosheleza ,mambo yatakayoangaliwa ni muda , aina na mazingira ya namna ambavyo upande wa mashtaka umepata aina ya ushahidi wa shahidi na ukaamua kumwita kama shahidi; lakini haitakuwa lazima notisi hiyo kutolewa iwapo upande wa mashtaka ulijua kwanza kuhusu ushahidi ambao atautoa shahidi siku na tarehe ambayo ameitwa.

Kuhojiwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka

290. Mashahidi watakaoitwa na upande wa mashtaka atatakiwa kuhojiwa na mtuhumiwa mwenyewe au wakili wake na baadaye kuhojiwa tena na wakili wa upande wa mashtaka.

Maelezo ya shahidi wa kitabibu

291.-(1) Katika usikilizaji wa kesi mbele ya Mahakama Kuu , kielelezo chochote kinachoonyesha kwamba ni taarifa iliyosainiwa na shahidi wa kitabibu kuhusu suala la kitaalamu la kitabibu au kiupasujaji litapokelewa katika ushahidi isipokuwa kwamba kifungu hiki kidogo hakitatumika hadi pale notisi ya kutosheleza ya nia ya kutoa kielelezo hicho wakati wa usikilizaji wa kesi, pamoja na nakala ya kielelezo hicho kutolewa kwa mshtakiwa au wakili wake.

(2) Mahakama inaweza kuamini kwamba saini katika kielelezo hicho ni halisi na kwamba mtu aliyesaini anayo nafasi katika ofisi au alikuwa na sifa alizotakiwa kuwa nazo wakati anasaini kielelezo hicho.

(3) Pale ushahidi unapokelewa na mahakama, mahakama inaweza kama ikiona inafaa, na itatakiwa, kama ,itaombwa na mshtakiwa au wakili wake kumwita na kumuuliza au kumleta kwa kuhojiwa mtu aliyeandaa taarifa; na mahakama itamjulisha mshtakiwa juu ya haki yake ya kumtaka mtu aliyeandaa taarifa kuitwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki kidogo

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (3), mahakama inaweza kuachana na mahitaji ya kifungu hiki kidogo pale inaporidhika kwamba mtu aliyeandaa taarifa hiyo amefariki au kufika kwake hakuwezekani bila kuchelewa sana au ni gharama.

Maelezo ya
ushahidi ya
mtuhumiwa.

292. Maelezo yoyote ya mshtakiwa ambayo yameidhinishwa na hakimu mpelekaji wa mashtaka kwa namna ambayo imeelezwa na kifungu cha 246 yanaweza, kama yamesainiwa au hayajasainiwa na mshtakiwa kutolewa kwenye ushahidi bila haja ya uthibitisho mwingine, labda tu ikionekana kwamba hakimu alitarajia kuidhinisha lakini alishindwa kuidhinisha.

Kufunga kesi kwa
upande wa
mashtaka
Sheria Na. 13 ya
1988 kif. 2

293.-(1) Wakati ushahidi wa mashahidi wa upande wa mashtaka umekamilishwa, na maelezo, kama yapo, ya mshtakiwa mwenyewe mbele ya mahakama iliyomuandaa yaliyotolewa kama ushahidi, mahakama, kama inaona inafaa, baada ya kuwasikiliza mawakili wa upande wa mashtaka na upande wa utetezi, kwamba hakuna ushahidi wa kwamba mshtakiwa au mojawapo ya washtakiwa ametenda kosa au kosa lingine lolote ambalo chini ya masharti ya vifungu vya 300 hadi 309 vya Sheria hii anaweza akapatikana na hatia, atatakiwa aandike kumbukumbu za uamuzi wa kutokuwa na hatia.

(2) Wakati wa ushahidi wa mashahidi wa upande wa mashtaka umekamilisha, na maelezo, kama yapo, ya mshtakiwa mwenyewe mbele ya mahakama iliyompeleka yaliyotolewa kama ushahidi, mahakama, kama inaona kwamba kuna ushahidi kwamba mshtakiwa alitenda kosa au kosa lolote ambalo chini ya masharti ya vifungu vya 300 hadi 309 vya Sheria hii anaweza akapatikana na hatia, atatakiwa amjulishe mshtakiwa mwenyewe juu ya haki yake-

(a) ya kutoa ushahidi yeye mwenyewe kwa niaba yake na

(b) ya kuita mashahidi kwa ajili ya utetezi wake.

na atamuuliza mshtakiwa au wakili wake kama anatarajia kutumia haki yoyote kati ya hizo na kuandika jibu lake, na baadaye mahakama itatakiwa kumwita mshtakiwa kwa ajili ya utetezi wake isipokuwa tu pale ambapo hataki kutumia haki yake yoyote.

(3) Iwapo mshtakiwa, baada ya kujulishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2), amechagua kukaa kimya mahakama itakuwa na uwezo wa kumuona ana nia mbaya dhidi yake na mahakama pamoja na upande wa mashtaka watakuwa huru kutoa maoni yao dhidi ya kitendo cha mshtakiwa kushindwa kutoa ushahidi.

(4) Bila kujali kwamba mshtakiwa amekubali au ametoa ushahidi wowote ambao si chini ya kiapo au kuthibitisha atatakiwa kuhojiwa na upande wa mashtaka.

(g) Kesi kwa Upande wa Utetezi

Kesi kwa upande wa
utetezi.

294.-(1) Mshtakiwa au wakili wake anaweza kufungua utetezi wake kwa kueleza mambo au sheria ambazo anatarajia kuzitumia katika utetezi na pia kutoa maoni anayoona yanafaa

katika ushahidi wa upande wa mashtaka.

(2) Mshtakiwa anaweza kutoa ushahidi kwa niaba yake mwenyewe na yeye mwenyewe au wakili wake anaweza kuwaongoza mashahidi wake kama wapo na baada ya kuhojiwa kwao na upande wa mashtaka au na kuhojiwa tena na upande wa utetezi kama kuna umuhimu, akakamilisha kesi yake.

Mashahidi wa
nyongeza upande wa
utetezi

295.-(1) Pamoja na mashahidi walioitwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 263 mshtakiwa ataruhusiwa kumuuliza shahidi yoyote ambaye ameitwa kuhudhuria

(2) Mshtakiwa hatastahili kama haki yake kumwita shahidi yeyote ukiondoa wale mashahidi ambao majina na anuani zao yalitolewa kwa hakimu wakati wa mwenendo wa upelekaji wa mashtaka yake lakini mahakama yoyote ya chini inaweza baada ya upelekaji wa mashtaka kwa usikilizaji na kabla ya mashtaka hayajaanza kusikilizwa, pamoja na mahakama ya usikilizaji wa mashtaka inaweza kabla au wakati wa usikilizaji wa mashtaka, kutoa hati ya wito wa kufika mtu yeyote kama shahidi wa upande wa utetezi kama mahakama itaridhika kwamba ushahidi huo ni muhimu sana kwa kesi.

Majibu ya
mwendesha
mashtaka

296.Iwapo mtu au mmojawapo kati ya watu kadhaa kati ya washtakiwa anatoa ushahidi wowote, mwendesha mashtaka atakuwa na haki ya kujibu kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 201.

Pale mshtakiwa
hatoi ushahidi

297.Iwapo mshtakiwa anasema kwamba asingependa kutoa au kuleta ushahidi na mahakama inaona kwamba kuna ushahidi kwamba alitenda kosa hilo, wakili wa upande wa mashtaka atatoa majumuisho ya kesi yake dhidi ya mshtakiwa na kisha mahakama itamwita tena mshtakiwa mwenyewe au wakili wake ili kuieleza mahakama.

(h) Ufungaji wa Kusikiliza kwa Kesi

Utoaji wa maoni ya
wazee wa baraza na
utoaji wa hukumu

298.-(1) Wakati kesi kwa pande zote imefungwa, jaji atatoa majumuisho ya ushahidi wa upande wa mashtaka na upande wa utetezi na atamtaka kila mzee wa baraza kutoa maoni yake kwa mdomo katika ujumla wake wa kesi na kwa kila suala mahususi aliloambiwa na jaji, na ataandika maoni hayo.

(2) Jaji atatoa uamuzi, lakini katika kufanya hivyo hatalazimika kufuata maoni ya wazee wa baraza.

(3) Iwapo mshtakiwa atapatikana na hatia, jaji atampa adhabu kwa mujibu wa sheria.

(4) Hakuna lolote katika kifungu hiki litatafsiriwa kama linamzuia au kuwazuia wazee wa baraza au yeyote kati yao kuondoka kwenda kuyafikiria maoni yao kama wakitaka, au wakati wa kipindi chochote cha mapumziko au muda wowote wakati wa usikilizaji wa

mashtaka, kushauriana baina yao wenyewe.

Kutiwa hatiani pale kesi ilisikilizwa na majaji wawili kwa nyakati tofauti

299.-(1) Pale jaji yeyote, baada ya kuwasikiliza na kuandika ushahidi wote au sehemu tu ya ushahidi katika kesi yoyote, na kwa sababu yoyote ile hawezi kumaliza kesi au hawezi kumaliza kesi ndani ya muda muafaka, jaji mwingine ambaye anayo na anatumia mamlaka, anaweza, kuichukua na kuendelea na kesi na jaji anayechukua anaweza kutumia ushahidi au mwenendo ulioandikwa na mtangulizi wake na anaweza katika usikilizaji wa kesi kuwaita upya mashahidi na akaanza kusikiliza upya kesi, ipokuwa tu katika usikilizaji wa kesi mshtakiwa anaweza wakati jaji wa pili ameanza mwenendo wake, kuhitaji kwamba kila mashahidi au mmoja wao aitwe upya na asikilizwe, na atatakiwa ajulishwe juu ya haki zake hizi na jaji wa pili atakapoanza mwenendo.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki kidogo hiki cha (1) kitatafsiriwa kwamba kinamzuia jaji ambaye ameandika ushahidi katika usikilizaji wa kesi yoyote na ambaye kabla ya kutoa hukumu na kupeleka kumbukumbu za mwenendo wa mashtaka pamoja na hukumu kwa jaji aliyembadili, hukumu inayotakiwa isomwe na iwapo kuna hatia adhabu itolewe na jaji huyo mwingine.

SEHEMU YA TISA

KUTIWA HATIANI, HUKUMU, ADHABU NA UTEKELEZAJI WAKE KATIKA MAHAKAMA ZA CHINI NA MAHAKAMA KUU

A. – Mashart ya Ujumla Kuhusiana na Kutiwa Hatiani

Wakati kosa lililohitibishwa limejumuishwa katika kosa lililoshtakiwa

300.-(1) Wakati mtu anaposhtakiwa na kosa lenye maelezo tofauti, ambayo muunganiko wake unaleta kosa moja dogo lililokamilika, na muunganiko huo unathibitishwa lakini maelezo mengine yaliyobaki hayathibitishwi anaweza kutiwa hatiani kwa hilo kosa dogo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

(2) Wakati mtu anashtakiwa na kosa na maelezo yanathibitisha kwa kupunguza kosa na kuwa kosa dogo, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo dogo japokuwa hakishtakiwa na kosa hilo.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki makosa yaliyoelezwa katika kifungu cha 222 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu itatumika pale mtu anashtakiwa kwa kosa la kujaribu kuua chini ya kifungu cha 211, yatachukuliwa kuwa ni makosa madogo.

Sura ya .16

Mtu aliyeshitakiwa kwa kosa anaweza kutiwa hatiani kwa kujaribu kufanya kosa hilo.

301. Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa la kujaribu kutenda kosa hilo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa la kujaribu.

Hukumu mbadala

302.-(1) Wakati mwanamke anashtakiwa kwa kosa la mauaji

katika mashtaka mbalimbali ya uuaji wa watoto

Sura ya.16

ya mtoto wake aliyemzaa na mahakama inaona kwamba kwa kitendo cha kudhamiria au kwa kutokutenda, amesababisha kifo chake lakini wakati wa tukio hilo au kutokutenda huko alikuwa bado hajatengamaa kabisa kutokana na madhara ya kutoka kujifungua kwa mtoto huyo na kwa sababu hiyo au kwa sababu ya madhara yatokanayo na kunyonyesha baada ya kuzaliwa kwa mtoto, uwezo wa akili yake ulivurugwa, anaweza, bila kujali mazingira yalivyokuwa isipokuwa kwa masharti ya kifungu cha 199 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu angeweza kutiwa hatiani kwa kuuu , atatiwa hatiani kwa kosa la kuuu mtoto mchanga japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

Sura ya.16

Sura ya.16
Sura ya.16

(2) Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa la mauaji au mauaji bila kukusudia ya mtoto yeyote au mtoto mchanga au kwa kosa chini ya kifungu cha 150 au kifungu cha 151 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu (kinachohusiana na usababishaji wa utoaji wa mimba au kuharibika kwa mimba) na mahakama ina maoni kwamba hana hatia ya kosa la mauaji, mauaji bila kukusudia au mauaji ya mtoto mchanga au kwa kosa chini ya kifungu cha 150 au kifungu cha 151 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, lakini ana kosa la kuharibu mtoto chini ya kifungu cha 219 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

Sura ya 16

(3) Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa la kuharibu mtoto na mahakama ina maoni kwamba hana hatia ya kosa hilo lakini anayo hatia ya kosa chini ya kifungu cha 150 au chini ya kifungu cha 151 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

(4) Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa la mauaji au mauaji ya mtoto mchanga au kwa kosa la kuharibu mtoto na mahakama ina maoni kwamba hana hatia ya kosa lolote kati ya hayo hapo juu, lakini anayo hatia ya kosa la kuficha kuzaa , anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo

Hukumu mbadala chini ya Sheria ya Usalama Barabarani kwa baadhi ya makosa ya kuuu bila kukusudia
Sura ya .168

303. Pale mtu anashtakiwa kwa kosa la mauaji ya bila kukusudia yanayohusiana na uendeshaji wake wa gari na mahakama inaona hana hatia ya kosa hilo, lakini anahatia ya kosa chini ya kipengele cha 50 cha Sheria ya Usalama Barabarani (kuhusiana na kuendesha kwa uzembe au kwa hatari, au kwa kutokujali), anaweza kutiwa hatiani kwa mojawapo ya makosa ya kipengele hicho japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

Hukumu mbadala katika mashtaka ya ubakaji na makosa yanayofanana nayo
Sura ya.16

304.-(1) Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa chini ya kifungu cha 130 au kifungu cha 132 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu na mahakama inaona kwamba hana hatia ya kosa hilo lakini ana hatia ya kosa chini ya kifungu cha 135,140, au 158 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

Sura ya .16

(2) Wakati mtu anashtakiwa na kosa chini ya kifungu cha 158

cha Sheria ya Kanuni za Adhabu na mahakama ina maoni kwamba hana hatia chini ya kosa hilo lakini anayo hatia chini ya kifungu cha 137 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, anaweza kutiwa hatiani chini ya kosa hilo hata kama hakishtakiwa kwa kosa hilo.

Sura ya.16

(3) Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa chini ya kifungu cha 136 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu na mahakama ina maoni kwamba mtu huyo hana hatia ya kosa hilo lakini anayo hatia ya kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) au kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 135 au cha kifungu cha 140 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

Mtu aliyeshtakiwa kwa uvunjaji nyumba, n.k, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa linalofanana na hilo. Sura ya.16

305. Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa chini ya mojawapo ya vifungu vya 294 hadi 298 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu na mahakama ina maoni kwamba hana hatia kwa kosa hilo lakini anayo hatia kwa kosa lingine lolote chini ya vifungu vingine vilivyotajwa anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo lingine japokuwa hakishtakiwa kwa kosa kosa hilo.

Hukumu mbadala kwa mashtaka ya wizi na makosa yanayofanana nayo Sura ya 16

306.-(1) Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa la kuiba kitu chochote na mahakama inamaoni kwamba hana hatia ya kosa hilo lakini analo kosa kuhusiana na kitu hicho chini ya mojawapo ya vifungu vya 302,304,311 na 312 vya Sheria ya kanuni za adhabu, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

Sura ya.16

(2) Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa chini ya kifungu cha 304 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu na mahakama inaona kwamba hana hatia ya kosa hilo lakini anayo hatia ya kuiba mali ambayo ameshtakiwa nayo, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

Sura ya .16

(3) Pale mtu anashtakiwa kwa kosa chini ya kifungu cha 302 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu na mahakama ina maoni kwamba hana hatia kwa kosa hilo aliloshtakiwa nalo lakini anayo hatia kwa kosa chini ya kifungu cha 304 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo; na pia pale mtu anaposhtakiwa kwa kosa chini ya kifungu cha 304 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu na mahakama inaona kwamba hana hatia kwa kosa hilo lakini anayo hatia kwa kosa chini ya kifungu cha 302 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

(4) Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa chini ya kifungu cha 311 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu kwa kosa la kupokea chochote na mahakama inamaoni kwamba hana hatia ya kosa hilo lakini anayo hatia ya kutunza kitu hicho na pia pale mtu anashtakiwa chiniya kifungu hicho kwa kosa la kutunza chochote na mahakama inamaoni kwamba hana hatia chini ya kosa hilo lakini analo kosa la kupokea mali, anaweza kutiwa hatiani chini ya masharti ya kifungu hicho cha

kutunza au kupokea kama itakavyokuwa ijapokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

Hukumu mbadala katika mashtaka ya kukutwa na mali zinazodhaniwa kuwa zimepatikana kwa rushwa Sheria Na. 11 ya 2007

307. Pale mtu yoyote anashtakiwa kwa kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) kifungu cha 10 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na mahakama ina maoni kwamba hakupata kwa rushwa au kupokea mali lakini analo kosa chini ya kifungu cha 312 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu kuhusiana na mali hiyo, mahakama inaweza kumtia hatiani kwa kosa hilo la mwisho japokuwa hakishtakiwa kwa kosa hilo.

Tafsiri ya vifungu vya 300 mpaka 307.

308. Masharti ya vifungu vya 300 hadi 307 vitatafsiriwa kama nyongeza ya na wala siyo kuondoa masharti ya sheria nyingine yoyote au masharti mengine ya sheria hii, na masharti ya vifungu vya 301 hadi 307 vitatafsiriwa bila kuathiri ujumla wa kifungu cha 300.

Mtu anayeshitakiwa kwa kosa la kibali kutokuachiwa kama kosa lisilo la kibali limethibitishwa

309. *Iwapo katika shtaka lolote la kosa la kibali mambo yaliyothibitishwa katika ushahidi yanaonyesha kwamba ni kosa lisilo la kibali, mshtakiwa hatatakiwa kwa sababu hiyo kuachiwa kwa kosa hilo la kibali, na hakuna mtu aliyeshitakiwa kwa kosa hilo lisilo la kibali atakayekuja kuwajibika baadaye kushtakiwa kwa kosa la kibali kwa mambo yenye kufanana nalo, katika hiari yake mahakama ikiona itaagiza mtu huyo ashtakiwe kwa kosa lisilo la kibali, hivyo mtu huyo anaweza kushughulikiwa kama vile amewahi kuwekwa katika usikilizaji wa kesi ya kosa la kibali.*

Haki ya mshtakiwa kutetewa

310. Mtu yeyote ambaye ameshtakiwa mbele ya mahakama ya jinai, tofauti na mahakama ya mwanzo, anayo haki ya kutetewa na wakili wa Mahakama Kuu kwa kuzingatia masharti ya sheria inayohusiana na utoaji wa huduma za kitaaluma na mawakili.

B. – Hukumu kwa Ujumla

Jinsi ya kutoa hukumu Sheria Na. 2 ya 2005 kif.46

311.-(1) Hukumu katika kesi yoyote ya jinai au suala lolote utatolewa mbele ya mahakama ya wazi mapema au haraka iwezekanavyo baada ya kumalizika kwa usikilizaji wa kesi, au katika wakati ujao, ambapo notisi itatolewa kwa wahusika au mawakili wao, kama wapo, lakini kama hukumu ipo kwa maandishi wakati wa kusomwa, jaji au hakimu anaweza, isipokuwa kama kutakuwa na pingamizi kuhusu utaratibu huo ukitolewa na upande wa mashtaka au upande wa utetezi, ataelezea kiini cha hukumu mbele ya mahakama ya wazi badala ya kusoma hukumu yote.

(2) Mshtakiwa kama atakuwa chini ya ulinzi, atatakiwa aletwe au kama hayupo chini ya ulinzi, atatakiwa na mahakama afike kusikiliza hukumu ikitolewa isipokuwa tu ikiwa ulazima wa kufika

kwake umeondolewa na adhabu yake ni ya faini tu au anaachiwa huru.

(3) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2) pale kunapokuwa na washtakiwa zaidi ya mmoja, na mmoja au zaidi ya mmoja hawajafika mahakamani siku na tarehe ya kutolewa hukumu, jaji au hakimu anaweza ili kuzuia ucheleweshaji wa muda mrefu katika kumaliza kesi, kutoa hukumu ya kesi bila kujali kutokuwepo kwa mshtakiwa au washtakiwa

(4) Hakuna hukumu iliyotolewa na mahakama yoyote itachukuliwa kuwa haifai kwa sababu tu imetolewa bila kuwepo kwa upande fulani au wakili siku ile au kutoka sehemu iliyoelezwa kutolewa hukumu, au kwa kutokupeleka hati za wito, au makosa katika kupeleka hati, kwa wahusika au kwa mawakili wao, au mmoja wao kati ya hao, notisi ya siku na mahali.

(5) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachotafsiriwa kwamba kinazuia kwa namna yoyote masharti ya kifungu cha 299.

Yaliyomo kwenye hukumu Sheria Na. 10 ya 1989 kif. 2

312.-(1) Kila hukumu chini ya masharti ya kifungu cha 311 itatakiwa, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo na Sheria hii, iandikwe na au iandikwe chini ya usimamizi na uangalizi wa jaji aliyesikiliza au hakimu katika lugha ya mahakama na itatakiwa iwe na hoja au hoja za kuamuliwa, uamuzi wenyewe na sababu za uamuzi, na itatakiwa iwekwe tarehe na kisha isainiwe na **afisa msikilizaji kwa tarehe iliyosomwa katika mahakama ya wazi.**

(2) Katika kesi ya kutiwa hatiani hukumu itatakiwa ionyeshe kosa ambalo, na kifungu cha Sheria ya Kanuni za Adhabu au sheria yoyote ambayo mshtakiwa anatiwa hatiani na adhabu ambayo anaadhibiwa.

(3) Katika kesi ambayo anaachiwa huru, hukumu itatakiwa ieleze kosa ambalo mshtakiwa anaachiwa kwalo na itaagiza kwamba aachiwe huru.

(4) Pale katika hatua yoyote ya kesi, mahakama inapomwachia mshtakiwa, itamtaka mshtakiwa atoe anuani yake ya kudumu kwa ajili ya kumpelekea vielelezo endapo kutakuwa na rufaa dhidi ya kuachiwa kwake na mahakama itaweka kumbukumbu au kusababisha kumbukumbu kuwekwa

Nakala ya hukumu, n.k, kutolewa kwa mshtakiwa au mtu mwingine mwenye maslahi kwa maombi

313.-(1) Kwa ombi la mshtakiwa nakala ya hukumu au pale anapotaka tafsiri kwa lugha yake mwenyewe, kama inawezekana, itatolewa kwake bila kuchelewa na bila malipo.

(2) Mtu yeyote mwenye maslahi au aliyeathiriwa na hukumu anaweza kupewa nakala ya hukumu kama akiomba na iwapo atalipa ada iliyoagizwa isipokuwa kama mahakama, ikiona inafaa kwa sababu zingine, itampatia bila malipo.

C. -Adhabu

(a)Utoaji wa Adhabu katika Mahakama Kuu

Kumwita mshtakiwa **314.** Iwapo jaji atamtia hatiani mshtakiwa au kama atakubali kosa, itakuwa ni jukumu la Msajili au afisa mwingine wa mahakama kumuuliza kama ana lolote la kusema kwanini adhabu isipitishwe dhidi yake kwa mujibu wa sheria, lakini kosa la kuacha kumuuliza halitakuwa na madhara kwenye usahihi wa mwenendo wa kesi

Mwenendo katika kuzuia kwa hukumu **315.**-(1) Mshtakiwa anaweza , wakati wowote kabla ya adhabu iwe kwa kukubali kosa au vyovyote vile, kuizua hukumu kwa sababu kwamba hati ya maelezo ya mashtaka haitoi au haionyeshi, baada ya marekebisho yoyote ambayo mahakama inapendelea na inao uwezo wa kufanya, kutaja kosa lolote ambalo mahakama ina uwezo wa kulisikiliza.

(2) Mahakama inaweza kwa hiari yake, kusikiliza na kuamua suala hilo wakati wa kikao hicho au kuahirisha usikilizaji hadi tarehe ya mbele itakayopangwa kwa dhumuni hilo.

(3) Iwapo mahakama inaamua kwa kumpendelea mshtakiwa, ataachiwa kutoka kwenye hati hiyo ya maelezo ya mashtaka

Adhabu **316.** Iwapo hakuna hoja ya kuzuia hukumu imetolewa au kama mahakama imeamua dhidi ya mshtakiwa juu ya hoja hiyo, mahakama inaweza kumwadhibu mshtakiwa muda wowote katika kikao hicho.

Uwezo wa kuweka kando maamuzi ya maswali yaliyojitokeza katika usikilizaji wa kesi. **317.** Mahakama ambayo mbele yake mtu anashtakiwa kwa kosa inaweza kuweka kando utoaji wa hukumu kwa suala lolote lililoibuliwa katika usikilizaji wa kesi na uamuzi pale unapotolewa utachukuliwa kama ulifikiriwa wakati wa usikilizaji wa kesi.

Uwezo wa kuweka kando maswali yaliyojitokeza wakati wa usikilizaji wa kesi **318.**-(1) Wakati mtu yeyote, akiwa katika kesi mbele ya Mahakama Kuu, amepatikana na hatia ya kosa ,jaji anaweza kuweka kando na kupeleka kwa ajili ya uamuzi wa mahakama yenye majaji wawili au zaidi wa Mahakama Kuu swali lolote lililoibuka wakati wa usikilizaji wa kesi na uamuzi ambao utaathiri matokeo ya kesi.

(2) Iwapo jaji ataweka kando swali hilo lolote, mtu aliyetiwa hatiani atatakiwa wakati akisubiri uamuzi , kupelekwa rumande gerezani au kama jaji akiona inafaa, atamwachia kwa dhamana na Mahakama Kuu itakuwa na uwezo kupitia upya kesi au sehemu ya kesi kama itakavyoona ni muhimu na baadaye kutoa uamuzi wa swali hilo na kisha kubadili adhabu iliyopitishwa na jaji aliyesikiliza kesi hiyo na kisha kupitisha hukumu au amri kama Mahakama Kuu itakavyoona inafaa.

Pingamizi **319.** Hakuna hukumu itakayosimamishwa au kuwekwa kando

zilizoponywa na hukumu

kwa sababu tu kuna pingamizi lolote ambalo lingesemwa baada ya hati ya maelezo ya mashtaka kusomwa kwa mshtakiwa au wakati wa kuendelea kwa usikilizaji wa kesi ,lingeweza kuponywa kwa marekekebisho na mahakama ,au kwa uapishaji wowote usio rasmi wa mashahidi au yeyote kati yao.

Ushahidi wa kufikia hukumu inayofaa.

320. Mahakama inaweza, kabla ya kupitisha hukumu,kupokea ushahidi kama itakavyoona inafaa ili kujiridhisha kuhusu adhabu inayofaa kutolewa.

Kuzingatia makosa mengine

321.-(1) Bila kuathiri ujumla wa kifungu cha 320 Mahakama Kuu inaweza, kwa kufuata masharti ya kifungu hiki, kwa dhumuni la kutathmini adhabu inayofaa kutolewa, kuzingatia kosa lingine lolote lililofanywa na mshtakiwa lakini ambalo hakutiwa nalo hatiani.

(2)Mahakama Kuu haitatakiwa kuzingatia kosa lolote isipokuwa kama:-

(a) imeelezwa na mahakama kwa mshtakiwa katika lugha ya kawaida kwamba adhabu itakayopitishwa kwake kwa kosa alilopatikana na hatia katika mwenendo huo linaweza kuwa kubwa ikiwa kosa jingine litazingatiwa; na

(b) baada ya ufafanuzi huo mshtakiwa:-

(i) anakubali kufanya kosa hilo lingine;na

(ii) anaiomba mahakama izingatie kosa jingine katika kutoa adhabu.

(3) Hakuna lolote katika kifungu hiki kitakachoipa mahakama uwezo,baada ya kuzingatia kosa jingine ,kutoa adhabu kwa mshtakiwa iliyozidi kiwango cha juu cha adhabu kilichowekwa kwa ajili ya kutolewa kwa kosa ambalo mtu amepatikana nalo na hatia katika mwenendo wa mashtaka.

(b) Hukumu ya Kifo

Hukumu ya kifo

322.-(1) Wakati mtu yeyote anapoadhibiwa adhabu ya kifo, atatakiwa kufa kwa kunyongwa.

(2) Wakati mtu yeyote anapoadhibiwa adhabu ya kifo, adhabu hiyo lazima iagize kwamba atakufa kwa kunyongwa.

Mshtakiwa kutaarifiwa kuhusu haki ya kukata rufaa.

323. Wakati mshtakiwa anahukumiwa adhabu ya kifo, mahakama itamtaarifu mshtakiwa kipindi ambacho atakiwa kukitumia kama anataka kukata rufaa, rufaa yake kufikiriwa katika kipindi hicho.

Mamlaka ya kumweka mtu kizuizini.

324. Cheti kilichosainiwa na Msajili au Afisa mwingine wa mahakama kwamba adhabu ya kifo imetolewa,na inamtaja mtu aliyehukumiwa, itatosha kuwa mamlaka ya kutosha kwa ajili ya kumweka kizuizini mtu huyo.

Taarifa na
kumbukumbu
kupelekwa kwa
Rais.

325.-(1) Haraka sana kama itakavyokuwa, baada ya adhabu ya kifo kutolewa, na kama hakuna rufaa dhidi ya adhabu ya kifo iliyotolewa na Mahakama Kuu imepelekwa au kama rufaa dhidi ya hukumu yoyote ya kifo ilipokelewa na adhabu iliyotolewa ikathibitishwa katika rufaa, kwa haraka kama itakavyoweze kana baada ya uamuzi wa rufaa, jaji au hakimu aliyesikiliza kesi hiyo kwa madaraka aliyopewa na kifungu cha 173 atapeleka kwa Rais nakala ya maandishi ya ushahidi iliyotolewa katika usikilizaji wa kesi pamoja na taarifa ya maandishi iliyosainiwa na yeye yenye mapendekezo au maangalizo juu ya kesi kama atakavyoona inafaa kutoa.

(2) Baada ya taarifa kuangaliwa, Rais atawasiliana na jaji au hakimu au aliyebadili nafasi yao ya ofisi, masharti juu ya uamuzi wowote alioufanya, na jaji au hakimu huyo atatakiwa utaratibu na kiini cha uamuzi huo uingizwe katika kumbukumbu za mahakama.

(3) Rais atatakiwa kutoa hati ya kifo au amri ya adhabu ya kifo ,au msamaha uliosainiwa naye na kuwekwa nembo ya Jamhuri ya Muungano kuupa nguvu uamuzi huo. Iwapo adhabu ya kifo inatakiwa itekelezwe, hati ya kifo itaeleza mahali na muda ambao adhabu ya kifo itatolewa na ataelekeza mahali ambapo mwili wa mtu aliyenyongwa utazikwa. Iwapo adhabu imepunguzwa kuwa adhabu ingine yoyote amri itaeleza adhabu hiyo. Iwapo mtu aliyehukumiwa adhabu amesamehewa, msamaha utaeleza kama ni msamaha huru au ni msamaha wa masharti, kama yapo, ufuatwe.

(4) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), hati ya kifo inaweza kuagiza kwamba utekelezaji wa hukumu ya kunyongwa ufanywe kwa muda na mahali fulani na mwili wa mtu aliyenyongwa utazikwa au utachomwa mahali fulani, kama itakavyochaguliwa na afisa aliyetajwa katika hati ya kifo.

(5) Hati ya kifo au amri au msamaha wa Rais vitakuwa mamlaka tosha ya kisheria kwa watu wote inakoelekezwa kutekeleza adhabu ya kifo au adhabu nyingine yoyote iliyotolewa na kutekeleza maagizo hayo kama yalivyotolewa kulingana na masharti yake.

(c) Adhabu Zingine

Kuachiwa kwa
masharti.

326.-(1) Pale mahakama yoyote inaona kwamba shtaka linamtia hatiani mshtakiwa na kwa maoni yake ikizingatia tabia, taarifa za nyuma juu ya makosa, umri, hali ya afya, hali ya akili ya mtu aliyeshtakiwa au asili ya udogo wa kosa lenyewe, au mazingira ya kufanyika kwa kosa lenyewe, si sawa kumpa adhabu yoyote au ni sawa kumwachia mkosaji kwa masharti kama yalivyo elekezwa hapa chini, mahakama inaweza, bila kuendelea kumtia hatiani ama:-

(a) kuamuru mkosaji aachiwe baada ya onyo kutolewa na mahakama kama itakavyoona inafaa; au

(b) kumwachia mkosaji kwa masharti ya kuweka dhamana yenye au isiyokuwa na wadhamini, kuwa wa tabia njema na kufika wakati wa kutiwa hatiani na kuadhibiwa atakapoitwa muda wowote wa kipindi hicho, usiozidi miaka mitatu, kama itakavyowekwa kwenye amri hiyo ya mahakama.

(2) Amri chini ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa kwa madhumuni ya kuweka au kurudisha mali iliyoibiwa au kuhusiana na masuala ya kurejesha au kupokelewa kwa mali na mmiliki, zitakuwa na athari sawa kama kupatikana na hatia.

(3) Dhamana iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu hiki inaweza kuwa na masharti kama mahakama inavyoweza, kwa kuzingatia mazingira ya kila kesi, kuamuru yaingizwe kuhusiana na yote au moja wapo ya masuala yafuatayo-

- (a) kwa kumkataza mkosaji kujumuika na watu wasiofaa au kwenda mara kwa mara sehemu zisizofaa;
- (b) kuacha kunywa pombe, pale kosa lenyewe linahusiana na ulevi au kama kosa lenyewe lilifanyika kutokana na kunywa kilevi;
- (c) kwa ujumla kuhakikisha kwamba mkosaji ataishi maisha ya uaminifu na ya kujishughulisha;
- (d) kuelezea kwamba mkosaji pamoja na mdhamini au wadhamini wake kama wapo watafika mahakamani mbele ya jaji wa mahakama kwa vipindi kama itakavyoelezwa katika amri.

(d) Utekelezaji wa Adhabu

Hati kwa adhabu ya kifungo

327. Hati iliyotiwa saini na jaji au hakimu kwamba mtu yeyote anatakiwa kuadhibiwa kwa kifungo gereza, ikiamuru kwamba adhabu itatendeka katika gereza lolote ndani ya Tanzania Bara, itatolewa na jaji au hakimu aliyetoa adhabu na itakuwa ni mamlaka kamili kwa afisa mfawidhi wa gereza hilo na kwa watu wengine wote wanaotakiwa kutekeleza kifungo hicho kilichoelezwa katika hati hiyo, isiyokuwa adhabu ya kifo; na kila adhabu itachukulia kuanza kutoka na itajumuisha siku nzima ya siku ya tarehe ambayo ilitajwa isipokuwa pale inapoelezwa vinginevyo katika Sheria hii au Sheria ya Kanuni za Adhabu

Hati kwa kulipa faini.

328.-(1) Pale mahakama imeamuru pesa ilipwe na mshtakiwa au mwendesha mashtaka au mlalamikaji kwa ajili ya faini au adhabu au malipo, gharama, matumizi au vyovyote vile, hizi fedha zinaweza kutozwa kutoka katika mali inayohamishika au isiyohamishika ya mtu alimyeamriwa kulipa kwa kukamata mali na kuuza chini ya hati, lakini kama ataonyesha mali ya kutosha inayohamishika ya kutosheleza amri ya mahakama, mali isiyohamishika haitauzwa.

(2) Mtu aliyeamriwa chini ya kifungu kidogo cha (1) kulipa pesa

anaweza kulipa au kuzabuni kwa afisa aliyepewa hati ya utekelezaji wa hati kwa kiasi kilichotajwa katika hati pamoja na matumizi ya ukamataji kutoka siku ya ukamataji hadi siku ya ulipaji au zabuni na baada ya hapo afisa muuzaji ataacha kutekeleza hati hiyo.

(3) Hati chini ya kifungu hiki inaweza kutekelezwa ndani ya mipaka ya mamlaka ya mahakama iliyotoa hati hiyo, na itaruhusu ukamataji na uuzaji wa mali yoyote ya mtu huyo wakati itakaporuhusiwa na hakimu wa wilaya au hakimu mkazi aliyeko ndani ya mamlaka ambayo mali hiyo inapatikana.

Pingamizi katika ukamataji.

329.-(1) Mtu yeyote anayedai kuwa na haki ya kisheria au haki nyingine katika jumla au sehemu tu ya mali iliyokamatwa kwa ajili ya utekelezaji wa hati iliyotolewa chini ya kifungu cha 327 anaweza katika muda wowote kabla ya kupata kwa mahakama mauzo ya mali hiyo, kutoa notisi ya maandishi kwa mahakama juu ya pingamizi lake la kukamatwa kwa mali hiyo na notisi hiyo itaeleza kwa kifupi asili ya madai ambayo mtu huyo (katika kifungu hiki ataitwa “mpingaji”) anayetoa kwa mali yote au sehemu ya mali iliyokamatwa na athibitisha thamani ya mali anayoidai, thamani hiyo ikisaidiwa na hati ambayo itawekwa kwenye faili la mahakama pamoja na notisi.

(2) Baada ya kupokea notisi halali iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha(1) mahakama, kwa amri ya maandishi itakayopelekwa kwa afisa aliyetaka kutekeleza hati ya kukamata na kuuza, kuagiza kusimamishwa kwa utekelezaji wa amri iliyotolewa.

(3) Baada ya kutolewa kwa amri chini ya kifungu kidogo cha (2) mahakama itatakiwa kwa notisi ya maandishi kuagiza mpingaji afike mbele ya mahakama hiyo na athibitisha madai yake katika tarehe itakayoelezwa katika notisi.

(4) Notisi itatumwa kwa mtu ambaye mali yake ilitakiwa ikamatwe kwa mujibu wa hati iliyotolewa chini ya kifungu cha 328, isipokuwa kama mali inabidi itumike kulipa faini, kwa mtu ambaye alistahili mapato yatokanayo na mauzo ya mali na itaeleza muda na mahali anapotakiwa kufika mpingaji na itamwagiza mtu ambaye notisi imetumwa kwake kufika mbele ya mahakama katika muda huohuo na mahali kama atapenda kusikiliza wakati wa usikilizaji wa pingamizi.

(5) Baada ya tarehe iliyopangwa ya kusikiliza pingamizi, mahakama itachunguza madai na kwa dhumuni hilo, inaweza kusikiliza ushahidi wowote ambao mpingaji ataotoa au ataleta na ushahidi wowote uliotolewa na mtu yeyote aliyetumiwa notisi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) .

(6) Iwapo, baada ya uchunguzi wa madai , mahakama itaridhika kwamba mali iliyokamatwa wakati imekamatwa haikuwa chini ya mtu aliyeamuriwa kulipa pesa , au kwa mtu aliyekuwa akimtunzia, au ilikuwa imekaliwa na mpingaji, au mtu mwingine

aliyekuwa akilipa kodi ya pango, kwake , au kuwa chini yake mtu aliyeamuriwa kulipa pesa kwa muda huo ilipokuwa chini yake japo siyo kwa kufikiri kwake au kama mali yake lakini kwa kufikiri kwa au kwa kumtunzia mtu mwingine au kwa sehemu kwa kufikiri kwake na sehemu kwa kufikiria kwa mtu mwingine, mahakama itatoa amri ya kuachiwa kwa mali hiyo yote au kwa kiwango fulani kama itakavyoona inafaa.

(7) Iwapo , katika tarehe zilizopangwa kwa ajili ya kufika ,mpingaji ameshindwa kufika au baada ya uchunguzi wa madai kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (5), mahakama ikiwa na maoni kwamba mpingaji ameshindwa kuthibitisha madai yake, mahakama itaamuru ukamataji na utekelezaji kuendelea na itatoa amri hiyo ya malipo ya gharama kama itakavyoona inafaa. .

(8) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitachukuliwa kumzuia mtu ambaye ameshindwa kufuata mahitaji ya kifungu kidogo cha (1) ya haki ya kuchukua utaratibu mwingine wowote ukiacha wa masharti ya kifungu hiki, unaweza kihalali kuchukuliwa na mtu anayedai manufaa katika mali iliyokamatwa chini ya hati ya kukamatwa.

Kusimamisha kwa utekelezaji wa adhabu ya kifungo kama faini haikulipwa.

330.-(1) Wakati mkosaji amehukumiwa kulipa faini tu na kutumikia kifungo, kama akishindwa kulipa faini, mahakama inaweza kusimamisha utekelezaji wa adhabu ya kifungo na inaweza kumwachia mkosaji akiweka dhamana, ikiwa na wadhamini au bila wadhamini, kama mahakama itakavyoona inafaa kwa sharti la kuhudhuria mbele ya mahakama katika tarehe ambayo si zaidi ya siku kumi na tano kutoka siku ya kuweka dhamana; na kama faini itakuwa bado haijawasilishwa mahakama inaweza kuagiza adhabu ya kifungo kutekelezwa mara moja au mara kwa mara kuongeza muda wa kutumika kwa dhamana kwa kipindi kingine kisichozidi siku kumi na tano tu.

(2) Katika kesi yoyote ambayo amri ya kulipa pesa imetolewa mahakama inaweza kumhitaji mtu aliyeamuriwa kulipa fedha hizo kuweka dhamana kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1), na akishindwa kulipa inaweza mara moja kutoa adhabu ya kifungo kama vile fedha hazikupatikana.

(3) Bila kuathiri masharti ya vifungu vidogo vya (1) na (2) katika kesi yoyote ambayo amri ya kulipa fedha imetolewa, na kama kuna au hakuna amri yoyote iliyotolewa ya kifungo kwa kushindwa kulipa, mahakama inaweza, katika maagizo yake, vyovyote katika muda wa amri hiyo inapotolewa au baadaye, kuagiza kwamba pesa ilipwe kwa awamu katika muda na wakati na kwa kiwango ambacho mahakama inaona inafaa.

4) Pale chini ya kifungu kidogo cha(3), mahakama inaagiza kwamba fedha inaweza kulipwa kwa awamu, kiasi chote kilichobaki kitatakiwa kiwe kimelipwa isipokuwa kama mahakama itaongeza muda ambao

Sura ya .16

inatakiwa awamu za malipo hayo zilipwe, zitakuwa tayari kwa ajili ya kulipwa na vifungu vyote vya Sheria hii na Sheria ya Kanuni za Adhabu vinavyotumika pale faini isipolipwa vitatumika kwa na kuhusiana na kiwango kisicholipwa .

Kushikiliwa kwa hati za kuuza mali za mtuhumiwa.

331. Iwapo afisa mwenye kutekeleza hati ya kukamata mali anatoa taarifa kwamba hajapata mali yoyote au hajapata mali ya kutosha ili kuweza kupata pesa hizo zilizotajwa katika hati pamoja na gharama zake ,mahakama inaweza kwa hati hiyohiyo au nyingine kuagiza mtu aliyeamuriwa kulipa aende jela kwa kipindi kilichoelezwa katika hati, isipokuwa kama fedha pamoja na gharama zote za ukamataji , kama ilivyo katika hati zimelipwa mapema.

Kushikiliwa kama mbadala wa kuuza mali za mtuhumiwa

332. Wakati ikionekana kwa mahakama kwamba ukamataji na mauzo ya mali ya mkosaji kutakuwa na madhara kwa mtu aliyeamuriwa kulipa au kwa familia yake, au (kwa ukiri wake au vinginevyo) kwamba hana mali yoyote ambayo itaweza kukamatwa au wakati sababu zingine za msingi zinaonekana kwa mahakama ,mahakama inaweza, ikiona inafaa badala ya kuagiza au baada ya kutoa hati ya kukamata mali kutolewa , itampeleka magereza kwa muda ulioelezwa katika hati japokuwa kama pesa pamoja na gharama za kumpeleka magereza,zilizotajwa katika hati zimelipwa mapema

Malipo yote baada ya kushikiliwa

333. Mtu yoyote aliyefungwa katika gereza kwa kushindwa kulipa fedha anaweza kulipa fedha hizo zilizoelezwa katika hati pamoja na gharama za matumizi zilizoidhinishwa , kama zipo kwa mtu ambaye yupo chini ya uangalizi wake na mtu huyo atamwachia mara moja ikiwa hayuko chini ya uangalizi kwa jambo jingine.

Malipo kidogo baada ya kushikiliwa

334.-(1) Iwapo mtu yeyote aliyefungwa katika gereza lolote kwa kushindwa kulipa kiwango chochote kilichoamuriwa na mahakama katika mamlaka yake ya kijinai kilichotakiwa kulipwa chini ya Sheria hii au sheria nyingine ,akilipa kiwango chochote kwa kupunguza sehemu ya deni hilo alilotakiwa kulipa, kipindi cha kifungo chake kitapunguzwa kwa siku zinazokaribiana na kiwango sawa na jumla ya siku alizofungwa mtu huyo na kiwango alicholipa.

(2) Afisa mfawidhi wa gereza ambalo mtu huyo amefungwa, ambaye anataka kutumia kifungu kidogo cha (1) kwa faida yake, baada ya maombi kufanyika kwake na mtu huyo atamchukua mhusika mbele ya mahakama na mahakama hiyo itathibitisha kupunguzwa kwa muda wa kutumikia gerezani kwa kiwango hicho cha malipo kilichofanyika pamoja na kutoa amri hiyo kulingana na mazingira. .

Nani anaweza kutoa hati

335. Kila hati ya utekelezaji wa adhabu yoyote inaweza kutolewa na jaji au hakimu aliyepitisha adhabu hiyo au na mtu aliyembadili ofisi au

mamlaka yake.

Mwisho wa kifungo
baada ya
kushikiliwa

336. Hakuna kufungwa kwa kushindwa kulipa kutakuwa zaidi ya miezi sita isipokuwa kama sheria ambayo imetumika kumtia hatiani inaruhusu muda mrefu zaidi.

D. – Masharti ya Mbalimbali ya Kushughulika na Wakosaji

(a) *Wakosaji wa Kwanza*

Uwezo wa
kumuachia kwa
matazamio badala
ya kuhukumu kwa
adhabu.

337.-(1) Katika kesi yoyote ambayo mtu amepatikana na hatia mbele ya mahakama yoyote kwa kosa ambalo haliadhibiwi kwa adhabu ya kifo na hakuna hukumu ya awali imethibitika dhidi yake, iwapo itaonekana kwa mahakama ambayo iliyomtia hatiani kwamba, kwa kuzingatia ujana, tabia, taarifa za nyuma za makosa, afya au hali ya kiakili, ya mkosaji au asili ya udogo wa kosa lenyewe au mazingira ya kufanyika kwa kosa lenyewe, ni jambo zuri kumwachia mkosaji kwa majaribio mahakama inaweza, badala ya kumuadhibu papo kwa papo kwa adhabu yoyote, kuagiza aachiwe kwa kusaini dhamana ikiwa na wadhamini au bila wadhamini, na katika kipindi hicho (kisichozidi miaka mitatu kama mahakama itakavyoagiza) **kuhudhuria** na kupokea adhabu atakapoitwa na katika muda huu kuhakikisha anatumia amani na kuwa mwenye tabia njema.

(2) Amri chini ya kifungu hiki inaweza kutolewa na Mahakama Kuu pale inapofanya marejeo.

Masharti kama
mkosaji atashindwa
kufuata masharti ya
dhamana.

338.-(1) Iwapo katika muda wowote mahakama iliyomtia hatiani mkosaji imejiridhisha kwamba mkosaji ameshindwa kufuata mojawapo ya masharti yoyote yale ya kujidhamini kwake, inaweza kutoa hati ya kumkamata

(2) Mkosaji anapokamatwa kwa hati ya kukamatwa chini ya kifungu kidogo cha(1) atapelekwa moja kwa moja mbele ya mahakama iliyotoa hati hiyo, na mahakama inaweza kumpeleka mahabusu hadi kesi itakaposikilizwa au kumwachia kwa dhamana kwa wadhamini wa kutosha pamoja na masharti ya kufika kwake kwa ajili ya adhabu na mahakama inaweza baada ya kusikiliza kesi, kutoa adhabu.

Masharti kuhusu
makazi ya mkosaji.

339. Mahakama, kabla ya kuagiza kuachiwa kwa mkosaji chini ya kifungu cha 338, itatakiwa kujiridhisha kwamba mkosaji au mdhamini wake kama anaye, awe na makazi ya kudumu, au ana shughuli zake za kikazi katika eneo ambalo mahakama ipo au iwe ni eneo ambalo mkosaji anatarajiwa kuishi katika kipindi kilichotajwa kwa ajili ya kuzingatia masharti.

Kumuachia mkosaji
kwa masharti ya
kuitumikia jamii.

339A.-(1) Katika kesi ambazo mtu anatiwa hatiani mbele ya mahakama kwa kosa ambalo adhabu yake si kifo, yenyewe kwa

Sura ya.291

uamuzi wake au kwa maombi ya mkosaji au mamlaka yoyote yenye uwezo kisheria, kama itaonekana kwa mahakama ambayo ilimtia hatiani, kwa kuzingatia ujana, tabia, taarifa za nyuma za makosa, afya au hali ya kiakili, ya mkosaji au asili ya udogo wa kosa lenyewe au mazingira ya kufanyika kwa kosa lenyewe, ni jambo zuri kumwachia mkosaji kwa ajili ya shughuli za kijamii chini ya Sheria ya Huduma za Jamii, mahakama inaweza badala ya kumpeleka mkosaji gerezani kuagiza achiwe kwa ajili ya huduma za kijamii kwa kuweka dhamana, bila au na wadhamini kwa kipindi kitakachoelezwa na mahakama katika amri ya kutoa huduma kwa jamii.

Sura ya .11

(2) Hakuna kitu chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kitakachoizua mahakama kutoa amri chini ya kifungu hiki kwa ombi ya mapitio chini ya Sheria hii au Sheria ya Mahakama ya Mahakimu.

Sura ya .291

(3) Amri chini ya kifungu hiki inaweza kutolewa na mahakama yoyote ingine katika kutekeleza mamlaka yake ya rufaa au marejeo kwenye kesi.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno “**mamlaka ya kisheria**” lina maana sawa na maana iliyopewa chini ya Sheria ya Huduma za Jamii.

Vifungu vya 337, 338 na 339 kutotumika katika mazingira fulani Sura ya .247

340. vifungu vya 337,338 na 339 vya sheria hii havitatumika katika eneo lolote la Tanzania Bara ambako Sheria ya Majaribio Kwa Wakosaji inatumika.

(b) Wakosaji Waliowahi Kuhukumiwa Huko Nyuma

Uwezo wa kuweka mtu chini ya uangalizi wa polisi Sura ya .16 Sura ya.337

341.-(1) Wakati mtu yeyote:-

(a) anapatikana na hatia ya kosa lolote dhidi ya vifungu vya 59 au 60 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu au kifungu cha 25,26, au 27 cha Sheria ya vyama vya Jamii; au

(b) baada ya kupatikana na hatia kwa kosa lolote linaloadhibiwa kwa kifungu cha muda wa miaka mitatu au zaidi au kwa kosa chini ya kifungu cha 343 cha Sheria hii, mahakama inaweza, ikiona inafaa, wakati wa kutoa adhabu ya kifungu kwa mtu huyo, pia ikaamuru kwamba atatakiwa awe chini ya uangalizi wa polisi kama ilivyoelezwa kwa kipindi kisichozidi miaka mitano kutoka tarehe ya kuachiwa kwake kutoka jela.

(2) Iwapo hukumu itatenguliwa katika rufaa au kwa sababu ingine yoyote, amri hiyo itakuwa batili.

(3) Amri chini ya kifungu hiki inaweza kutolewa na Mahakama Kuu wakati ikitekeleza uwezo wake wa marejeo.

(4) Kila amri itakayofanywa chini ya kifungu hiki itafanywa katika fomu maalumu na kwa kuongezea itatajwa katika hati ya utekelezaji.

Matakwa kwa mtu aliye chini ya uangalizi wa polisi

342.-(1) Mahakama inaweza wakati wowote kuagiza kwamba mtu awapo chini ya uangalizi wa polisi na Tanzania kwa ujumla , afuate matakwa yafuatayo yote au mojawapo na inaweza kubadilisha maagizo hayo wakati wowote-

- (a) kuishi ndani ya mipaka yeyote katika wilaya itakayotajwa;
- (b) kutohamishia makazi yake kwenda wilaya nyingine bila ruhusa ya maandishi ya Afisa Tawala au afisa polisi msimamizi wa wilaya anayoishi;
- (c) kutokuondoka katika wilaya anayoishi bila ruhusa ya maandishi ya Afisa Tawala au afisa polisi msimamizi wa wilaya hiyo;
- (d) wakati wowote kumpa taarifa afisa polisi au kama hakuna afisa polisi, afisa tawala mfawidhi wa wilaya anayoishi kuhusu nyumba au mahali anapoishi;
- (e) kwenda mwenyewe, wakati wowote anapoitwa na Afisa Tawala au Afisa Polisi msimamizi wa wilaya ambayo anaishi, mahali popote katika wilaya hiyo.

(2) Kwa madhumuni ya kutoa maagizo yoyote au kubadilisha maagizo yoyote chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mahakama inaweza ikatoa hati ya wito kwa mtu ambaye kifungu kidogo kinamhusu na ambaye yupo chini ya mamlaka ya mahakama hiyo, kumtaka ahudhuri mbele yake katika muda na mahali kama itakavyoelezwa; na masharti ya vifungu vya 143,144, 145,146, na 147 vya Sheria hii, vitatumika kwake sawa kama ambavyo vinatumika kwa shahidi.

(3) Waziri anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya kifungu hiki.

Kushindwa kukidhi matakwa chini ya kifungu 342

343. Iwapo mtu yeyote aliyechini ya uangalizi wa polisi Tanzania amekataa au anadharau kufuata masharti yoyote yaliyoelezwa na kipengele cha 342 au na kanuni zozote ziliyotengenezwa chini ya, atatakiwa isipokuwa akithibitisha kwa kuiridhisha mahakama ambayo yeye anashtakiwa, kwamba alifanya kila alichoweza kwa mujibu wa Sheria, atakuwa na hatia kwa kosa na atafungwa kwa kipindi kisichozidi miezi sita au akipatikana na hatia kwa kosa la pili au yanayofuatia atafungwa kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili.

(c) Dosari kwenye Amri za Hati

Makosa na upungufu kwenye amri na hati.

344. Mahakama inaweza wakati wowote kurekebisha dosari zozote za kiini au mfumo katika amri au hati na hakuna upungufu au kosa la kuhusu muda na mahali na hakuna dosari katika amri au hati iliyotolewa chini ya Sheria hii, itafanya kuwa batili au kinyume cha sheria kitu chochote kilichofanywa au kilichotarajiwa kufanyika kwa

mujibu wa amri hiyo au hati, isipokuwa kwamba imetajwa au inaweza kuunganishwa kwamba imetokana na kutiwa hatiani au hukumu ili **huhlalisha** amri au hati.

E. – Uwezo Mbalimbali wa Mahakama kuamuru Fidia, Gharama, Kutaifisha, n.k.

(a) Gharama na Fidia

Gharama dhidi ya mshtakiwa

345.-(1) Itakuwa ni halali kwa jaji wa mahakama kuu au hakimu yeyote kumwamuru mtu yeyote aliyekutwa na hatia mbele yake kwa kufanya kosa, kulipa kwa mwendesha mashitaka wa serikali au binafsi, kama itakavyokuwa, gharama stahili kama ile ambayo jaji au hakimu atakavyoona inafaa, ikiongezea kwenye adhabu yeyote ile iliyokwishatolewa; isipokuwa kwamba gharama hizo zisizidi shilingi elfu nne kwa shauri lililoko mahakama kuu na shilingi elfu mbili kwa shauri lililoko mahakama za chini.

(2) Itakuwa ni halali kwa jaji wa mahakama kuu au hakimu yeyote ambaye amemuachia au kumtoa mtu aliyeshitakiwa kwa kosa, iwapo mashtaka kwa kosa hilo mwanzoni yalifunguliwa kwa wito au hati iliyotolewa na mahakama kwa maombi ya mwendesha mashtaka binafsi, kumuamuru mwendesha mashtaka binafsi kumlipa mshtakiwa gharama stahili kama vile jaji au hakimu atakavyoona inafaa; isipokuwa kwamba gharama hizo zisizidi shilingi shilingi elfu mbili katika suala la kuachiliwa au kuondolewa na mahakama kuu au shilingi elfu moja katika suala la kuachilwa au kuondolewa na mahakama ya chini isipokuwa zaidi kwamba hakuna amri kama hiyo itakayotolewa iwapo jaji au hakimu ataona kwamba mwendesha mashtaka binafsi alikuwa na sababu za msingi kwa kufanya lalamiko lake.

(3) Gharama zilizotolewa chini ya kifungu hiki zinaweza kutolewa kama nyongeza kwenye fidia yoyote iliyotolewa chini ya kifungu cha 347.

(4) Katika kifungu hiki:-

“mwendesha mashtaka wa serikali” maana yake ni mtu yeyote anayeendesha mashtaka kwa ajili au kwa niaba ya Jamuhuri ya Muungano au kwa ajili ya au kwa niaba ya au kwa niaba ya mamlaka ya umma

“mwendesha mashtaka binafsi” maana yake ni mwendesha mashtaka yeyote tofauti na mwendesha mashtaka wa serikali.

Amri ya kulipa gharama inaweza

346. Rufaa lazima iwe dhidi ya amri yeyote ya gharama iliyotolewa

kukatiwa rufaa

chini ya kifungu cha 345 ikiwa ilitolewa na hakimu kwenda mahakama kuu na ikiwa na jaji, kwenda mahakama ya rufaa na mahakama ambayo rufaa imefanywa itakuwa na uwezo wa kutoa gharama hizo za rufaa kama itakavyoona ni za msingi.

Fidia katika kesi zisizo na msingi au usumbufu.

347. Iwapo katika kuachiliwa kwa mshtakiwa, mahakama ina maoni kwamba shitaka halikuwa na msingi na ni ya kijinga, mahakama inaweza kuamuru mlalamikaji kumlipa mtu mshtakiwa fidia ya kiasi stahili kwa usumbufu na matumizi ambayo aliyatumia kutokana na shtaka hilo, kama nyongeza katika gharama zake.

Uwezo wa kuamuru mshtakiwa alipe gharama Sheria Na. 2 ya 1979

348.-(1) Pale mshtakiwa anatiwa hatiani na mahakama yeyote kwa kosa lolote ambalo adhabu yake si kifo na inaonesha katika ushahidi kwamba mtu mwingine, ama au siyo mwendesha mashtaka au shahidi katika shauri, amepata hasara ya mali au maumivu ya mwili kutokana na kosa lililotendeka na kwamba fidia ni ya msingi, kwa maoni ya mahakama, mtu huyo anaweza kufidiwa katika shauri la madai, mahakama inaweza, kwa ridhaa yake na kama nyongeza ya adhabu yeyote ile halali, kuamuru mtu aliyepatikana na hatia kumlipa mtu mwingine fidia hiyo, kwa mali au fedha kama mahakama itakavyoona haki na msingi.

Sura ya 16

(2) Pale mtu yeyote ametiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sura ishirini na saba mpaka Sura thelathini na mbili ya Sheria ya Kanuni za Adhabu, uwezo uliotolewa na kifungu kidogo cha (1) utachukuliwa kujumuisha uwezo wa kutoa fidia kwa mnunuzi yeyote mwenye nia njema wa mali yoyote kuhusiana na kosa lililotendwa kwa hasara ya hiyo mali kama mali imerudishwa katika umiliki wa mtu yule mwenye kustahili.

(3) Amri yeyote ya fidia chini ya kifungu hiki itakatiwa rufaa iwapo amri ya malipo ya faini ya kiasi kinachofanana ingetakiwa kukatiwa rufaa na hakuna malipo yeyote ya fidia yatakayofanyika kabla ya kipindi kilichoruhusiwa kuwasilisha rufaa hakijaisha au kama rufaa imewasilishwa, kabla ya uamuzi wa rufaa.

Fidia katika kesi za kujamiana Sheria Na. 4 ya 1998 kif. 25

348A.-(1) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 348 cha Sheria hii, wakati mahakama inapomtia mtu hatiani kwa kosa la kujamiana, kama nyongeza ya adhabu ambayo itatoa amri inayomtaka aliyetiwa hatiani kulipa fidia inayotakiwa kama vile mahakama itakavyoamua kufidia hasara inayoweza kupatikana katika shauri la madai kwa aliyethirika wakati kosa linafanywa dhidi yake.

Sura ya 16

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki “kosa la kujamiana” maana yake ni kosa lolote lililoko chini ya Sura ya XV ya Sheria ya Kanuni ya za Adhabu.

Gharama na fidia kuonyeshwa kwenye amri na jinsi ya

349. Kiasi kilichoruhusiwa kama gharama au fidia lazima katika mashauri yote kuonyesha katika hukumu au amri, na ni lazima

kuzipata

zipatikane kwa namna sawa kama itakavyopatikana kama adhabu yeyote inavyoweza kupatikana chini ya Sheria hii; na kushindwa kulipa gharama hizo au fidia na kushindwa kama ilivyoelezwa hapa, mtu aliyeshindwa atawajibika kwa kifungo cha kipindi kisichozidi miezi sita labda kama gharama au fidia italipwa haraka.

Uwezo wa mahakama wa kutoa gharama au fidia nje ya faini

350.-(1) Pale mahakama inatoa faini au kuridhia katika rufaa, mapitio au vinginevyo, adhabu ya faini ,au adhabu ambayo faini inakuwa sehemu, mahakama inaweza, wakati inapitisha hukumu, kuamuru yote au sehemu yoyote ya faini iliyopatikana kutumika-

(a) katika matumizi sahihi yaliyotumika katika kuendesha mashtaka;

(b) katika kumlipa mtu yeyote fidia kwa hasara yeyote au maumivu yaliyosababishwa na kosa pale fidia halisi ni, kwa maoni ya mahakama, itapatikana kwa shauri la madai.

(2) Iwapo faini iliyowekwa katika shauri ambalo linapelekea rufaa, hakuna malipo kama hayo yatakayofanywa kabla ya kipindi kilichokubaliwa kwa kuwasilisha rufaa hakijaisha au, kama rufaa imewasilishwa kabla ya uamuzi wa rufaa..

(3) Wakati wa kutoa fidia yoyote kwenye shauri lolote la madai litakalofuata kuhusiana na swala lilelile, mahakama inayosikiliza shauri la madai lazima izingatie fidia yoyote iliyolipwa au iliyopatikana chini ya kifungu cha 348.

(b) Kutwaa

Uwezo wa kuamuru kutwaliwa kwa mali

351.-(1) Pale mtu ametiwa hatiani kwa kosa na mahakama iliyopitisha adhabu imeridhika kwamba mali yeyote ambayo iliyokuwa kwenye miliki yake au chini yake wakati wa kukamatwa kwake-

(a) imetumika kwa madhumuni ya kutenda au kusaidia utendaji wa kosa lolote; au

(b) ilikusudiwa nae kutumika kwa madhumuni hayo, mali hiyo itawajibika kutwaliwa na kutaifishwa na mali yeyote iliyotwaliwa chini ya kifungu hiki lazima **itolewe** kama mahakama itakavyoagiza.

(2) Pale mahakama inaamuru amri kutwaliwa au kutaifishwa mali yeyote kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki lakini haikutoa amri ya kuiharibu au kupelekwa kwa mtu yeyote, mahakama inaweza kuelekeza kwamba mali lazima iifadhiwe au kuuzwa na kwamba hiyo mali au, iwapo itauzwa, mapato yake baada ya hapo lazima yashikiliwe kama itakavyoelekeza mpaka mtu adhibitishe kwa kuiridhisha mahakama haki yake; lakini kama hakuna

mtu anayethibitisha haki hiyo ndani ya miezi sita toka siku ya kutwaliwa au kutaifishwa, mali au mapato yake yatalipwa na kufanya sehemu ya mfuko maalumu.

(3) Uwezo uliotolewa chini ya kifungu hiki kwa mahakama utajumuisha uwezo wa kutoa amri ya kutwaa au kutaifisha au kuharibiwa au kukabidhiwa kwa mtu yeyote mali hiyo, lakini utekelezwe kufuatana na masharti maalum yoyote kuhusiana na kutwaa, kutaifisha, kuharibu, kushikiliwa au kukabidhiwa kuliopo ndani ya sheria ambapo hukumu ilikuwepo au sheria nyingine yoyote ambayo inatumika kwa kesi hiyo.

(4) Pale amri inatolewa chini ya kifungu hiki katika kesi ambayo rufaa **imetokea**, amri haitakuwepo, isipokuwa pale ambapo mali hiyo ni mifugo au ina asili ya haraka, itachukuliwa mpaka muda ulioruhusiwa kwa kuwasilisha rufaa utakuwa umekwisha au, wakati rufaa itakuwa imeshawasilishwa, mpaka rufaa itakaposikilizwa.

(5) Katika kifungu hiki rejeo lolote kwa:-

- (a) “mali” inajumuisha, katika kesi ya mali kuhusiana na kosa linaloonekana kufanyika, siyo tu mali hiyo ilikuwa mwanzo kwenye miliki au chini ya uangalizi wa mhusika yeyote, lakini pia mali yeyote iliyopo au ambayo kwa kubadilishana na kitu chochote kilichopatikana kwa aina hiyo ya na kwa kubadilishana huko, au haraka iwezekanavyo au vinginevyo
- (b) kusaidia utendaji wa kosa ukijumuisha uchukuaji wa hatua zozote baada ya kufanyika kwa dhumuni la kuhamisha mali yeyote ambayo inahusisha au inakwepa kutiwa kizuizini.

Hati ya upekuzi wa vitu vilivyotwaliwa au vilivyotaifishwa

352. Pale mahakama imetoa amri ya kutwaliwa au kutaifishwa kwa kitu mahakama au mlinzi yeyote wa amani anaweza, kama atajiridhisha kwa maelezo ya kiapo-

- (a) kwamba kuna sababu za msingi za kuamini kwamba kitu kitapatikana mahali popote au katika majengo; na
- (b) kwamba kuingia mahali au katika majengo kumekataliwa au kwamba kwa kuingia huko kunahofiwa,

itatoa hati ya upekuzi ambayo inaweza kutekelezwa kufuatana na sheria.

(c) Kuondolewa kwa Vielelezo

Kuondolewa kwa vielelezo

353.-(1) Pale kitu chochote ambacho kimetolewa au kuwekwa kama ushahidi katika mwenendo wowote wa jinai mbele ya mahakama yeyote hakijadaiwa na mtu yeyote anayejitokeza mahakamani kwamba ana haki nacho ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili baada ya

mwisho wa mwenendo au kama rufaa yeyote itapitishwa kuhusiana na hilo, kitu hicho kinaweza kuuzwa, kuharibiwa au vinginevyo kuondolewa kwa namna ambayo mahakama inaweza kwa amri kuelekeza na mapato ya mauzo yake yatalipwa kwenye kodi za jumla za Jamhuri.

(2) Iwapo kitu chochote ambacho kimetolewa au kuwekwa kama ushahidi kwenye mwenendo wowote wa jinai mbele ya mahakama yoyote kina asili ya kuharibika haraka, mahakama inaweza, katika hatua yoyote ya mwenendo au muda wowote baada ya kumalizika kwa mwenendo, kuamuru kwamba kiuzwe au vinginevyo kutolewa lakini itashikilia mapato ya mauzo na, iwapo hakijadaiwa baada ya kumalizika kwa kipindi cha miezi kumi na mbili baada ya kumalizika kwa mwenendo huo au rufaa yeyote iliyopitishwa juu ya hilo, italipa mapato hayo kwenye mapato ya jumla ya Jamhuri.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha

(1), mahakama inaweza, kama imejiridhisha kwamba itakuwa haki kufanya hivyo, kuamuru kwamba kitu chochote kilichotolewa, au kuwekwa kama ushahidi kwenye mwenendo ya jinai mbele yake itarudishwa kwenye hatua yeyote ya huo mwenendo au wakati wowote baada ya mwisho wa mwenendo huo kwa mtu ambaye anaonekana kustahili, kufuatana na masharti kama vile mahakama itakavyoonelea ni sahihi kuweka.

(4) Amri yoyote iliyotolewa na mahakama chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) au (2) itakuwa ya mwisho na itatumika kama zuio kwenye madai yeyote au kwa manufaa yeyote katika hicho kitu kwa kufuatia **umiliki** wowote unaojitokeza kabla ya tarehe ya amri.

(5) Pale amri inatolewa chini ya kifungu hiki katika shauri ambalo rufaa imeshawasilishwa amri (isipokuwa pale mali ni mifugo au ipo katika asili ya kuoza haraka) itachukuliwa mpaka pale kipindi cha kupeleka rufaa kimepita au pale rufaa imepelekwa, mpaka rufaa itakapomalizika.

(6) Katika kifungu hiki neno “mali” inajumuisha, katika shauri la mali ambapo kosa linaonekana limefanyika, siyo tu mali hiyo iliyokuwa mwanzoni kwenye milki, au chini ya uangalizi wa sehemu yeyote lakini pia mali yeyote kwenye au ambayo imebadilishwa au kubadilishana huko na kitu chochote kilichopatikana kwa kubadilishwa au kubadilishana ama **hapohapo** au vinginevyo.

Kutupwa kwa machapisho yanayodhalilisha au, yanayoshusha hadhi ya au vyakula visivyofaa, n.k..

354.-(1) Hukumu inayotokana na maneno yeyote machafu au machapisho ya kashfa, mahakama inaweza kuamuru kuharibiwa kwa nakala zote ya hicho kitu kutokana na hukumu ilivyokuwa na vile vilivyo katika uangalizi wa mahakama au vilivyobaki katika umiliki au uwezo wa mtu aliyehukumiwa.

(2) Mahakama inaweza kwa namna sawa na hukumu inayohusiana na madhara yeyote, au chakula kilichochanganywa,

kinywaji, dawa au maandalizi ya tabibu kuamuru kitu kinachoendana na hukumu kuharibiwa.

Mtu aliyenyang'anywa mali anaweza kurudishiwa.

355.-(1) Pale mtu yeyote anahukumiwa kwa kosa lolote lililofanywa kwa **nguvu ya jinai** na inaonekana mahakamani kwamba kwa nguvu hiyo mtu yeyote amenyang'anywa mali yeyote inayohamishika mahakama inaweza, kama ikiona inafaa, kuamuru mali hiyo kurudushwa kwenye milki ya huyo mtu mwingine..

(2) Hakuna amri iliyotolewa chini a kifungu kidogo (1) itakaathiri haki yeyote au manufaa katika mali inayohamishika ambayo mtu yeyote anaweza kudhibitisha kwenye shauri la madai.

Afisa wa umma anayehusiana na uuzwaji wa mali kutonunua au Kujinadi kwa nia ya kununua mali Sheria Na. 9 ya 1996 Jedwali.

356.-(1) Hakuna afisa wa umma mwenye jukumu lolote linahusiana na mauzo ya mali yeyote chini ya Sheria hii atafanya moja kwa moja au kwa kupitia, ununuzi au kujinadi kwa mali hiyo.

(2) Afisa wa umma ambaye amefanya kinyume na kifungu kidogo cha (1) ananunua au anajinadi kwa mali yoyote ana hatia ya kosa atawajibika kulipa faini isiyozidi laki tano au kifungu cha miaka miwili au vyote.

F. – Kurudishiwa kwa Mali

Mali iliyokutwa kwa mshtakiwa.

357. Pale, kukamatwa kwa mtu aliyeshitakiwa kwa kosa, mali yeyote imechukuliwa kutoka kwake, mahakama ambayo anashitakiwa inaweza kuamuru:-

- (a) kwamba mali au sehemu yake irurudishwe kwa mtu yule anayeonekana an mahakama anastahili na, iwapo yeye ni mtu aliyeshitakiwa, kwamba irudishwe aidha kwake au kwa mtu mwingine kama itakavyoelekeza; au
- (b) iwapo mali ni yake, kwamba mali au sehemu yake itumike kwenye malipo ya faini yeyote au gharama zozote au fidia iliyoelekezwa kulipwa na mtu aliyeshitakiwa..

Mali iliyoiwiwa Sura ya 16

358.-(1) Iwapo mtu yeyote amepatikana na kosa lililotajwa katika Sura ya XXVII mpaka XXXII ya Sheria ya Kanuni za Adhabu inayohusisha kuiba, kuchukua., kupata, toza kwa nguvu, kubadilisha au kukomesha au kupokea ukifahamu mali yeyote, atapelekewa kwenye hatia na au kwa niaba ya mmiliki wa mali hiyo, mali itarudishwa kwa mmiliki au mwakilishi wake.

(2) Katika kila kesi iliyorejewa kwenye kifungu hiki mbele ya mahakama ambayo mtuhumiwa ametiwa hatia itakuwa na uwezo wa kumpa mara kwa mara amri ya kurejeshewa kwa mali au kuamuru irejeshwe kwa namna fupi. isipokuwa kwamba:-

Sura ya 214

- (a) pale bidhaa, kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mauzo Ya Bidhaa, itakuwa imepatikana kwa udanganyifu au

njia nyingine zisizo halali zisizo sawa na wizi, mali katika bidhaa hizo hazitarudisha kwa mtu ambaye alikuwa mmliki wa bidhaa au kwa wakilishi wake binafsi kwa sababu tu ya kuhukumiwa kwa mtuhumiwa; na

- (b) hakuna kitu katika kifungu hiki kitatumika katika kesi ya thamani yeyote ya ulinzi ambayo kwa nia njema imelipwa au kutolewa na mtu mwingine anayewajibika kufanya malipo au kwa vile ni yenye uwezo wa kubadilishwa kwa fedha kwa nia njema imechukuliwa au imepokelewa kwa kuhamishwa au kukabidhiwa mtu mwingine kwa haki na thamani yake bila taarifa yeyote au bila sababu za msingi kushuku kwamba imeibiwa.

(3) Katika kurudisha mali yoyote iliyoibiwa iwapo itaonekana na mahakama kwa ushahidi kwamba mtuhumiwa ameuza mali iliyoibiwa kwa mtu yeyote na kwamba mtu huyo mwingine hakuwa anafahamu kwamba mali iliibiwa, na kwamba pesa zimekutwa kwake na zimechukuliwa kutoka kwa mtuhumiwa wakati wa kukamatwa kwake mahakama inaweza, kwa maombi ya mnunuzi, kuamuru kwamba kutokana na fedha hizo, kiasi cha fedha kisichozidi mapato ya mauzo kilipwe kwa mnunuzi.

(4) Matumizi ya amri yoyote chini ya kifungu hiki lazima, isipokuwa kwamba mahakama ambayo hukumu ilitolewa inaelekeza vinginevyo, katika kesi yoyote ambayo umiliki wa mali sio tatizo, isimamishwe:–

- (a) katika kesi yoyote, mpaka hapo muda wa kuwasilisha rufaa utakapoisha; na;
- (b) katika kesi yoyote pale rufaa imewasilishwa, mpaka rufaa itakapoamuliwa na, katika kesi ambazo matumizi ya amri yamesimamishwa, mpaka rufaa itakapoamuliwa, amri haitatumika kuhusiana na mali inayohusishwa iwapo hukumu itafutwa kwenye rufaa. Mahakama Kuu inaweza kuweka masharti kwa taratibu za kuhakikisha usalama wa mali yeyote, kusubiri kusimamishwa kwa matumizi ya amri yoyote hiyo.

(5) Mtu yeyote asiyeridhika na amri iliyotolewa chini ya kifungu hiki anaweza kukata rufaa mahakama kuu na katika usikilizwaji wa rufaa hiyo mahakama inaweza, kwa amri kufuta au kubadili amri yoyote iliyotolewa katika kusikilizwa kwa kurudisha kwa mali yeyote kwa mtu yoyote, ingawa hukumu haijatenguliwa; na amri, iwapo itafutwa, haitatekelezwa na, iwapo itabadilishwa, itatekelezwa kama ilivyobadilishwa.

SEHEMU YA KUMI RUFAA

(a) Rufaa kwa Ujumla

Rufaa kwenda
Mahakama Kuu.

359.-(1) Isipokuwa kama ilivyoelezwa hapa chini, mtu yeyote ambaye hakuridhika na matokeo yoyote, adhabu au amri iliyotolewa au kupitishwa na mahakama ya chini tofauti na ile inayofanywa kwa mamlaka iliyoongezwa kupitia amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 173 cha Sheria hii, anaweza kukata rufaa mahakama kuu na mahakama ya chini lazima katika muda ambao matokeo, adhabu au amri ilitolewa au kupitishwa, kumtaarifu mtu huyo kuhusu kipindi ambacho, kama ataamua kukata rufaa atahitajiwa kutoa taarifa ya nia yake ya kukata rufaa na kuwasilisha sababu zake za rufaa.

(2) Rufaa yoyote kwenda mahakama kuu inaweza kuwa ya jambo la hakika na hata jambo la kisheria.

Hakuna rufaa katika
kukiri kosa.

360.-(1) Hakuna rufaa itakayokubaliwa katika kesi ya mtuhumiwa yeyote ambaye amekiri kosa na ameshatiwa hatiani kwa ukiri huo na mahakama ya chini isipokuwa kwa kiwango au uhalali wa adhabu.

(2) Isipokuwa kwa ruhusa ya mahakama kuu tu, hakuna rufaa itakayokubaliwa katika kesi ambazo mahakama ya chini imeshapitisha adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu moja tu, au adhabu ya viboko iliyopitishwa tu kwa mtu wa chini ya miaka kumi na sita, au kutoka adhabu ya kifungo iliyokwishapitishwa kwa kutolipa faini iwapo hakuna adhabu ya msingi ya kifungo imepitishwa.

(3) Hakuna adhabu tofauti na inavyotakiwa kwa kukatiwa rufaa itakatiwa rufaa kwa sababu kwamba mtu aliyetiwa hatiani ameamriwa kutafuta ulinzi wa kutunza amani.

Kikomo
Sheria Na. 9 ya
2002

361.-(1) Kufuatana na kifungu kidogo cha (2), hakuna rufaa kutoka kwenye matokeo, adhabu au amri iliyorejewa katika kifungu cha 359 kitazingatiwa isipokuwa kama mrufani-

(a) ametoa taarifa kuhusu nia yake ya kukata rufaa ndani ya siku kumi toka tarehe ya matokeo, adhabu au amri au, kwenye swala la adhabu ya kuchapwa viboko tu, ndani ya siku tatu za tarehe ya adhabu hiyo; na

(b) amewasilisha sababu zake za rufaa ndani ya siku arobaini na tano toka tarehe ya matokeo, adhabu au amri,

isipokuwa kwamba katika kuhesabu kipindi cha siku arobaini na tano muda unaotakiwa wa kupata nakala ya mwenendo, hukumu au amri dhidi ya rufaa hautahesabiwa.

(2) Mahakama kuu inaweza, kwa sababu za msingi, kupokea rufaa hata kama ukomo wa muda uliowekwa chini ya kifungu hiki umekwisha.

Ombi la Rufaa
Sheria Na. 9 ya
2002 Jedwali.

362.-(1) Kila rufaa itafanywa katika muundo wa maombi kwa maandishi yaliyowasilishwa na mrufani au wakili wake, na kila maombi yatakuwa, isipokuwa kama mahakama kuu itakavyoelekeza vinginevyo, iambatanishwe na nakala ya mwenendo wa hukumu au ya amri inayokatiwa rufaa.

(2) Maombi lazima yawe na masuala ya kisheria au mambo ya hakika kwa kuzingatia vile rufaa inaona vimekosewa na mahakama ya chini.

Muomba rufaa aliye
gerezani

363. Iwapo mrufani yupo gerezani, anaweza kuwasilisha maombi ya rufaa na nakala zikiambatanishwa pamoja kwa afisa msimamizi wa gereza, ambaye baadaye atapeleka maombi na nakala kwa Msajili wa Mahakama Kuu.

Kukataliwa kwa
rufaa kwa haraka.

364.-(1) Katika kupokea maombi na nakala zinazohitajika na kifungu cha 362, mahakama kuu itazipitia na:-

- (a) iwapo rufaa ni dhidi ya adhabu na imeletwa kwa sababu kwamba adhabu ni zaidi na ikaonekana na mahakama kwamba hakuna kitu cha msingi katika mazingira ya kesi ambacho lingepelekea kufikiria kwamba adhabu ilitakiwa kupunguzwa;
- (b) iwapo rufaa ni dhidi ya hukumu na mahakama imezingatia kwamba ushahidi mbele ya mahakama ya chini haukuacha mashaka yoyote ya msingi juu ya kosa la mtuhumiwa na kwamba rufaa ni hafifu au haina msingi; au
- (c) iwapo rufaa ni dhidi ya hukumu na adhabu na mahakama inazingatia kwamba ushahidi mbele ya mahakama ya chini haijaacha mashaka kuhusiana na kosa la mtuhumiwa na kwamba rufaa ni hafifu au haina msingi na kwamba hakuna kitu cha msingi kwenye hukumu ambacho adhabu ilitakiwa kupunguzwa,

mahakama inaweza hapohapo kufuta rufaa kwa amri inayothibitisha kwamba kwa kupitia kumbukumbu, mahakama imejiridhisha kwamba rufaa iliwasilishwa bila sababu yoyote ya msingi ya lalamiko.

(2) Taarifa ya amri yoyote iliyotolewa chini ya masharti ya kifungu hiki itapelekwa maramoja kwa Mkurugenzi wa Mashitaka .

Taarifa ya muda na
mahali pa kusikiliza
rufaa
Sheria Na. 10 ya
1989 kif. 2

365.-(1) Iwapo Mahakama Kuu haikufuta rufaa hapohapo, itatoa taarifa kwa mrufani au wakili wake, na kwa Mkurugenzi wa Mashtaka katika muda na mahali ambapo rufaa itasikilizwa na atapatiwa Mkurugenzi wa Mashtaka nakala ya mwenendo pamoja na sababu za rufaa; isipokuwa kwamba taarifa haihitajiki kupewa mrufani au wakili wake kama imeshaelezwa kwenye sababu za rufaa kwamba mrufani hana nia ya kuwepo na hokusudii kumtafuta wakili kumuwakilisha katika usikilizaji wa rufaa.

(2) Pale taarifa ya muda, mahali pa kusikiliza haiwezi kutumwa kwa mtu yeyote kwa sababu hawezi kupatikana kupitia anwani iliyotolewa naye mahakamani chini ya kifungu cha 228 au 275, taarifa lazima itolewe kwa kufahamishwa kwa namna iliyoelezewa na kifungu cha 381.

Uwezo wa
Mahakama Kuu
kwenye rufaa na
haki ya mrufani
kuhudhuria.

366.-(1) Katika kusikiliza rufaa, mrufani au wakili wake ataelezea mahakama kwa kutetea taarifa zilizoelezwa kwenye sababu za rufaa na mwendesha mashtaka, iwapo atatokea, anaweza kuelezea mahakama na baada ya hapo, mahakama inaweza kumualika mrufani au wakili wake katika kujibu masuala yoyote ya kisheria au jambo la hakika lililoanzishwa na mwendesha mashtaka katika maelezo yake na mahakama inaweza iwapo itazingatia kuwa hakuna sababu ya msingi ya kuingilia, kufuta rufa au inaweza:-

(a) katika rufaa kutoka katika hukumu:-

(i) kubatilisha matokeo naadhabu na kumuachia mtuhumiwa au kumtoa chini ya kifungu cha 38 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu au kuamuru ashitakiwe tena na mahakama yenye mamlaka au kuielekeza mahakama ya chini kufanya uchunguzi wa awali.

(ii) kubadilisha matokeo, kuishikilia adhabu au ikiwa au bila kubadilisha matokeo, kupunguza au kuongeza hukumu;

(iii) ikiwa au bila mapunguzo hayo au kuongezwa kwa adhabu na ikiwa au isipokuwa na kubadilisha matokeo, kubadilisha asili ya adhabu;

(b) katika rufaa dhidi ya adhabu,kuongeza au kupunguza adhabu au kubadilisha asili ya adhabu;

(c) katika rufaa kutokana na amri nyingine yoyote, kubadili au kugeuza, amri hiyo na katika jambo kama hilo, inaweza kufanya badiliko lolote au amri yoyote inayotokana na au amri inayojitokezaa kwamba zinaweza kuonekana ya haki na sahihi..

(2) Mrufani, ama yuko chini ya ulinzi au hapana atastahili kuwepo wakati wa kusikiliza rufaa yake..

(3) Haki ya mrufani ambaye yupo chini ya ulinzi kuwepo katika kusikiliza rufaa itatokana na yeye kulipa gharama zote zitakazotokea katika kumhamisha kwenda na kurudi kwenye mahali ambapo mahakama itakaa kuamua rufaa; isipokuwa kwamba mahakama inaweza kuelekeza kwamba mrufani apelekwe mbele yake katika jambo lolote ambalo, kwa maoni ya mahakama, kuwepo kwake kunahitajika kutokana na kuamuliwa kwa rufaa, ambazo gharama hizo zitatolewa na serikali.

(4) Hakuna kitu katika kifungu hiki litatafsiriwa kama kuizua

Sura ya.16

mahakama kutoa adhabu kubwa zaidi ya adhabu ile ambayo ingetolewa na mahakama iliyotoa adhabu.

Amri ya Mahakama Kuu kuthibitishwa mahakama za chini.

367.-(1) Wakati shauri limeamuliwa kwenye rufaa na Mahakama Kuu, itathibitisha hukumu yake au amri kwenye mahakama ambayo hukumu,adhabu au amri iliyokatiwa rufaa iliandikwa au kupitishwa.

(2) Mahakama ambayo Mahakama Kuu imethibitisha hukumu yake au amri itatoa amri zinazoendana na hukumu au amri ya Mahakama Kuu na, iwapo ni muhimu, kumbukumbu zitabadilishwa ipasavyo.

Kusimamishwa kwa adhabu na kupatiwa dhamana kusubiri rufaa

368.-(1)Baada ya kupitisha rufaa na mtu anayestahili kukata rufaa, mahakama kuu au mahakama ya chini ambayo ilimhukumu au kumuadhibu mtu huyo inaweza, kwa sababu za msingi kuwekwa katika kumbukumbu kwa maandishi:-

(a) Katika jambo la mtu aliyepewa adhabu ya kifungo, kuamuru:-

(ii) kwamba utekelezaji wa adhabu iliyokatiwa rufaa usimamishwe mpaka rufaa yake isikilizwe ambapo atachukuliwa kama mfungwa aliye rumande hadi rufaa yake itakaposikilizwa; na

(b) katika jambo lingine lolote ,kuamuru utekelezaji wa adhabu au amri iliyokatiwa rufaa usimamishwe mpaka kusikilizwa kwa rufaa.

(2)Iwapo mwishoni rufaa inafutwa na adhabu ya mwanzo (ikiwa ni adhabu ya kifungo) imepitishwa au adhabu nyinginezo za kifungo zimebadilishwa , muda ambao mrufani alikuwa ameachiwa kwa dhamana au kipindi ambacho adhabu imesimamishwa kitatolewa katika kuhesabu kipindi cha kifungo ambacho mwishowe ataadhibiwa .

Ushahidi wa ziada.

369.-(1) Katika kushughulikia rufaa kutoka mahakama ya chini, Mahakama Kuu iwapo itaona inafaa ushahidi wa ziada ni muhimu, itaandika sababu zake na inaweza aidha kuchukua ushahidi huo ama kuagiza uchukuliwe na mahakama ya chini.

(2)Wakati ushahidi wa ziada unachukuliwa na mahakama ya chini mahakama hiyo itadhibitisha ushahidi kwa Mahakama Kuu ambayo baada ya hapo itaendelea kusikiliza rufaa.

(3) Isipokuwa kama Mahakama Kuu itaelekeza vinginevyo, mrufani au wakili wake anatakiwa kuwepo wakati ushahidi wa ziada unachukuliwa..

(4) Ushahidi unaochukuliwa kutokana na kifungu hiki

utachukuliwa kama ushahidi uliochukuliwa wakati wa shauri lililokuwa mbele ya mahakama ya chini.

Idadi ya majaji katika rufaa ya mrufani.

370.-(1) Rufaa toka mahakama za chini utasikilizwa na jaji mmoja wa Mahakama Kuu isipokuwa pale katika suala fulani jaji mkuu anaelekeza rufaa isikilizwe na majaji wawili au zaidi wa Mahakama Kuu na maelekezo hayo yatatolewa kabla ya kusikiliza rufaa au muda wowote kabla hukumu haijatolewa.

(2) Iwapo katika kusikiliza rufaa Mahakama Kuu imelingana katika utofauti wa maoni rufaa itatupwa.

Kuondolewa kwa rufaa Sheria Na. 9 ya 2002 Jedwali.

371.-(1) Rufaa inaweza kuondolewa muda wowote kabla ya kusikilizwa kwa taarifa ya maandishi kwa Msajili na kusainiwa na mrufani au wakili wake, na wakati rufaa inatolewa rufaa itawekewa alama kwamba imeondolewa.

(2) Wakati rufaa yoyote imeondolewa, Msajili hapohapo atamjulisha mjiburufaa na mahakama ya chini ambapo kesi ilianzia.

(3) Rufaa ambayo imeondolewa inaweza kurejeshwa kwa ruhusa ya mahakama kwa maombi ya mrufani iwapo mahakama itajiridhisha kwamba kuna sababu za msingi kwamba rufaa isikilizwe.

Ukomo wa rufaa baada ya kifo cha mrufani Sheria Na. 9 ya 2002 Jedwali.

371A. Kila rufaa kutoka mahakama ya chini (isipokuwa rufaa toka kwenye adhabu ya faini) itakoma iwapo mrufani atafariki.

(b) Mapitio

Uwezo wa Mahakama Kuu kuita kumbukumbu

372. Mahakama Kuu inaweza kuitisha na kuchunguza kumbukumbu ya mwenendo wowote wa kesi ya jinai iliyoko mahakama ya chini kwa madhumuni ya kujiridhisha yenyewe kwenye usahihi, uhalali au uhakika wa matokeo, adhabu, au amri iliyoandikwa au iliyopitishwa na kwenye usahihi wa mwenendo wowote wa mahakama yoyote ya chini.

Uwezo wa Mahakama Kuu katika mapitio Sheria Na. 4 ya 1998 kif. 26

373.-(1) Katika suala la mwenendo wowote katika mahakama ya chini kumbukumbu ambazo ziliitishwa au kutaarifiwa kwa amri au vinginevyo vimekuja kufahamika, Mahakama Kuu inaweza-

(a) katika suala la hukumu, kutekeleza uwezo wowote iliyopewa kama mahakama ya rufaa na kifungu cha 366,368 na 369 na inaweza kuongeza adhabu; au

(b) katika suala la amri nyingine yoyote tofauti na amri ya kuachiwa, kubadili au kugeuza amri hiyo, isipokuwa kwamba kwa madhumuni ya aya hii matokeo maalumu chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 219 cha Sheria hii itachukuliwa kuwa si amri ya kuachiwa.

(2) Hakuna amri chini ya kifungu hiki itakayofanywa kwa kumuathiri mshtakiwa isipokuwa kama alipata fursa ya kusikilizwa

yeye binafsi au kupitia wakili wake kwenye utetezi wake; isipokuwa kwamba amri inayobadili amri ya hakimu iliyotolewa chini ya kifungu cha 129 itachukuliwa kutofanywa kwa kumuathiri mshtakiwa kwa maana iliyo katika kifungu hiki kidogo.

(3) Pale adhabu iliyoshughulikiwa chini ya kifungu hiki imepitishwa na mahakama ya chini, isipokuwa kama jambo hilo lilihusisha kosa la kujamiana, Mahakama Kuu haitapitisha adhabu kubwa kwa kosa hilo, ambayo kwa maoni ya Mahakama Kuu mshtakiwa alitenda, zaidi ingeweza kupitishwa na mahakama iliyotoa hukumu.

(4) Hakuna kitu katika kifungu hiki litachukuliwa kuzuia Mahakama Kuu kubadilisha matokeo ya kuachiliwa kuwa ya hukumu pale inaona ni muhimu kufanya hivyo kwa manufaa ya haki.

(5) Pale Mahakama Kuu inapopitia kumbukumbu ya mwenendo wa mahakama ya chini iliyohusiana na makosa ya kujamiana, inaweza kama itaona kwamba haki katika shauri inahitaji kutoa adhabu kubwa zaidi ya mahakama iliyotoa hukumu ingeweza kutoa lakini Mahakama Kuu ingeweza kutoa iwapo jambo lingekuja mbele yake kwa rufaa kama vile jambo hilo lilikuwa katika rufaa.

(6) Katika kifungu hiki neno “kosa la kujamiana” maana yake kosa lolote lililo kwenye Sura ya XV ya Sheria ya Kanuni zaAdhabu.

Sura ya.16

Ridhaa ya Mahakama katika kuwasikiliza wahusika wa kesi.

374. Hakuna mhusika mwenye haki ya kusikilizwa aidha binafsi au kupitia wakili mbele ya Mahakama Kuu wakati inatekeleza uwezo wake wa mapitio; isipokuwa kwamba mahakama inaweza, kama itaona sahihi pale inapotekeleza uwezo huo, kumsikiliza mhusika yeyote iwe binafsi au kupitia wakili na kwamba hakuna kitu katika kifungu hiki kitakachochukuliwa kuathiri kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 373.

Idadi ya majaji katika mapitio.

375. Mienendo yote ya Mahakama Kuu katika kutekeleza mamlaka ya mapitio inaweza kusikilizwa na hukumu yoyote au amri hapo inaweza kutolewa au kupitishwa na jaji mmoja;

Isipokuwa kwamba wakati mahakama ina idadi ya zaidi ya jaji mmoja na imegawanyika kiusawa katika maoni,adhabu au amri ya mahakama ya chini itasimama.

Amri ya Mahakama Kuu kuthibitishwa mahakama ya chini.

376. Wakati kesi imepitiwa na Mahakama Kuu itathibitisha uamuzi wake au amri kwenda mahakama ambayo adhabu au amri iliyopitiwa iliandikwa au kupitishwa, na mahakama ambayo uamuzi au amri vimethibitishwa itatoa amri hizo zinazoendana na uamuzi uliothibitishwa na, iwapo ni muhimu, kumbukumbu zitabadilishwa ipasavyo.

(c) Rufaa za Mkurugenzi wa Mashtaka

Tafsiri.

377. Katika kifungu kifuatacho cha Sehemu hii labda kama kitahitaji vinginevyo

“Mkurugenzi wa Mashtaka” inajumuisha afisa yeyote wa chini yake anayetenda kufuatana na maelekezo ya jumla au maalumu; “mrufaniwa” maana yake ni mtu ambaye alikuwa mtuhumiwa kwenye mwenendo ambao rufaa yake chini ya kifungu cha 378 inahusiana na ambae anaweza kuathirika kwa amri yoyote ya Mahakama Kuu katika rufaa hiyo.

Rufaa za
Mkurugenzi wa
Mashtaka.

378.-(1) Pale Mkurugenzi wa Mashitaka hajaridhika na kuachiwa, matokeo, adhabu au amri iliyotolewa au kupitishwa na mahakama ya chini, tofauti na ile mahakama ya chini inayotekeleza uwezo wa nyongeza ya mamlaka kufuatia amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 173 cha Sheria hii, anaweza kukata rufaa kwenda Mahakama Kuu.

(2) Rufaa ya kwenda Mahakama Kuu chini ya kifungu hiki inaweza kuwa juu ya jambo la uhakika na vilevile juu ya masuala ya kisheria.

Kikomo Sheria Na.
5 ya 1988 kif. 11; 10
ya 1989 kif. 2; 9 ya
2002 Jedwali;
.27
ya 2008

379.-(1) Kufuatana na kifungu kidogo cha (2), hakuna rufaa chini ya kifungu cha 378 itazingatiwa isipokuwa kama Mkurugenzi wa Mashtaka

(a) ametoa taarifa ya nia yake ya kukata rufaa kwenda mahakama ya chini ndani ya siku thelathini kuachiwa, matokeo, adhabu au amri ambayo dhidi yake anatarajia kukata rufaa; na

(b) ameshapeleka sababu zake za rufaa ndani ya siku arobaini na tano toka tarehe ya kuachiwa, matokeo, adhabu au amri; isipokuwa kwamba katika kuhesabu hicho kipindi cha siku arobaini na tano muda uliotumika kupata nakala ya mwenendo, hukumu au amri iliyokatiwa rufaa au kumbukumbu za mwenendo wa shauri utaondolewa..

(2) Mahakama kuu inaweza, kwa sababu za msingi, kupokea rufaa bila kujali kipindi cha kikomo kilichoelezwa katika kifungu hiki kimeisha.

Ombi la rufaa
Sheria Na. 9 ya
2002 Jedwali.

380.-(1) Kila rufaa chini ya kifungu cha 378 itakuwa katika muundo wa maombi kwa maandishi iliyowakilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na isipokuwa kama Mahakama Kuu inaelekeza vinginevyo, yataambatanishwa na nakala ya mwenendo, hukumu au amri iliyokatiwa rufaa.

(2) Maombi yatakuwa na masuala ya kisheria na mambo ya uhakika kwa kuzingatia vile ambavyo rufaa toka mahakama ya chini inadaiwa kukosea.

Taarifa ya muda na
mahali pa kusikiliza

381.-(1) Pale ambapo maombi ya rufaa yamepelekwa

kesi
Sheria Na. 9 ya
2002 Jedwali.

Mahakama Kuu kufuatia kifungu cha 380 Mahakama Kuu itatoa taarifa itakayopelekwa kwa mjibu rufaa au wakili wake, na kila taarifa itaonyesha muda na sehemu ambapo rufaa itasikilizwa na itaambatanishwa na nakala ya maombi ya rufaa na nakala ya mwenendo, hukumu au amri iliyokatiwa rufaa.

(2) Pale taarifa ya muda, mahali na kusikilizwa haitamfikia mjibu rufaa kwa sababu hawezi kupatikana kupitia anwani iliyopata mahakama chini ya kifungu cha 228 na 275 taarifa itatolewa kumfahamisha kupitia chapisho katika gazeti mara tatu, na mwisho wa utumaji huo mahakama itaendelea na rufaa bila kuwepo mjibu rufaa.

Mkurugenzi wa
Mashtaka anaweza
kutoa hoja mbele ya
mahakama

382.-(1) Katika kusikiliza rufaa chini ya kifungu cha 378 Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuelezea mahakama kwa kutetea mambo yaliyoandikwa kwenye maombi ya rufaa na mjibu rufaa au wakili wake anaweza baadaye kuelezea mahakama na baadaye mahakama inaweza kumualika Mkurugenzi wa Mashtaka kutoa jibu kwa jambo lolote la kisheria au jambo la uhakika lililoanzishwa na mjibu rufaa au wakili wake na mahakama tena inaweza kama itaona kuna sababu za msingi za kuingilia, kutupilia mbali rufaa au inaweza:—

- (a) katika rufaa kuachia:—
 - (i) kubadili matokeo, kumtia hatiani mrufaniwa kwa kosa ambalo angeweza kutiwa hatiani na mahakama ya chini, na ama iendelee na kutoa adhabu au kurudisha shauri mahakama ya chini kwa kutoa adhabu;
 - (ii) kuamuru mjibu rufaa kushitakiwa na mahakama yenye mamlaka; au
 - (iii) kuelekeza mahakama ya chini kufanya upelekaji wa mashtaka;
- (b) katika rufaa dhidi ya adhabu, kuongeza au kupunguza adhabu au kubadilisha asili ya adhabu; au
- (c) katika rufaa kutokana na amri nyingine yoyote, kubadili au kugeuza hiyo amri na, katika jambo lolote, inaweza kufanya badiliko lolote au amri yoyote ya matokeo au yenye kujitokeza ambayo inaweza kuonekana ya haki na sahihi.

Kutofika kwa
wahusika.

383.-(1) Pale ambapo tarehe, siku iliyopangwa kwa kusikiliza rufaa chini ya kifungu cha 378 au tarehe nyingine yoyote ambayo inaweza kuahirishwa kusikilizwa Mkurugenzi wa Mashtaka hajatokea pale rufaa ilipoitwa kwa kusikilizwa, Mahakama Kuu inaweza kutoa amri kwamba rufaa itupiliwe mbali.

(2) Pale Mkurugenzi wa Mashtaka anatokea na mjibu rufaa au wakili wake hajatokea na Mahakama Kuu imejiridhisha kwamba mjibu rufaa au wakili wake walipewa taarifa ya rufaa, Mahakama Kuu inaweza kuendelea kusikiliza rufaa upande mmoja au unaweza

kuahirisha kusikiliza mpaka tarehe nyingine na kutoa taarifa kwa mjibu rufaa au wakili wake.

(3) Wakati rufaa inapotupiliwa mbali chini ya kifungu kidogo cha (1) Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuomba mahakama kupokea upya rufaa na, pale atakapoiridhisha mahakama kwamba alizuiwa kwa sababu zozote za msingi kutokutokea rufaa ilipoitwa kwa kusikilizwa Mahakama Kuu inaweza kupokea upya rufaa.

(4) Pale wakati wa kusikiliza rufaa mjibu rufaa hajatokea yeye mwenyewe Mahakama Kuu inaweza kutoa amri kuhitaji mahudhurio ya mjibu rufaa na, kama mjibu rufaa atashindwa kufuata amri hiyo, inaweza kutoa hati ya kukamatwa na kuletwa kwa mjibu rufaa mbele ya Mahakama Kuu siku na muda maalumu uliowekwa katika hati.

Ushahidi wa ziada.

384.-(1) Katika kushughulikia rufaa chini ya kifungu cha 378 Mahakama Kuu, kama itaona ushahidi wa ziada ni muhimu, itaandika sababu na inaweza ama kuchukua ushahidi yenyewe au kuelekeza uchukuliwe na mahakama ya chini.

(2) Wakati ushahidi wa ziada umechukuliwa na mahakama ya chini mahakama hiyo itathibitisha ushahidi kwa Mahakama Kuu ambayo baadaye itaendelea na rufaa.

(3) Hakuna ushahidi wa ziada utakaochukuliwa chini ya kifungu hiki kidogo isipokuwa katika uwepo wa mjibu rufaa au wakili wake na ushahidi huo utachukuliwa kana kwamba ulikuwa ushahidi uliochukuliwa wakati wa usikilizaji wa kesi mbele ya mahakama ya chini.

385. Masharti ya kifungu cha 370 yatatumika katika rufaa chini ya kifungu cha 378.

Kuondolewa kwa rufaa na Mkurugenzi wa Mashtaka. Sheria Na. 9 ya 2002 Jedwali.

386.-(1) Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza katika muda wowote kabla ya kusikiliza rufaa kuondoa rufaa kwa taarifa ya maandishi kwa Msajili na baada ya taarifa hiyo kutolewa rufaa itakuwa imeondolewa.

(2) Wakati rufaa imeondolewa, Msajili atamtaarifu mjibu rufaa na mahakama ya chini ambapo shauri lilianza.

(3) Rufaa iliyoondolewa chini ya kifungu kidogo cha (2), inaweza kurudishwa kwa rufaa ya mahakama kwa maombi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kama mahakama itaridhika kuna sababu za msingi kwamba rufaa isikilizwe.

Ukomo wa rufaa anapokufa mjibu rufaa Sheria Na. 9 ya 2002 Jedwali.

386A. Kila rufaa chini ya kifungu cha 378 itakoma anapokufa mjibu rufaa.

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA
MASHARTI YA ZIADA**

(a) Mwenendo Usiofuata Utaratibu

Mwenendo mahali pasipo sahihi.

387. Hakuna matokeo, adhabu au amri ya mahakama yoyote ya jinai itawekwa pembeni kwa sababu tu kwamba uchunguzi, kutatua au mwenendo mwingine katika kupitishwa kwake yaliyopitishwa, yalitokea katika mkoa, wilaya au eneo lingine kimakosa, isipokuwa kama inaonekana kwamba kosa hilo limesababisha ukosefu wa kutokutenda haki.

Matokeo au adhabu, inapogeuzwa kwa sababu ya kosa au upungufu katika hati ya mashtaka au mwenendo.

388. Kufuatia kifungu cha 387, hakuna matokeo, adhabu au amri iliyotolewa au kupitishwa na mahakama yenye mamlaka, itageuzwa au kubadilishwa kwenye rufaa au mapitio kwa ajili ya kosa, lolote au kutokuwa sahihi katika lalamiko, wito, hati, shtaka ,tangazo, amri, hukumu au uchunguzi wowote au mienendo mingine chini ya Sheria hii; isipokuwa kwamba kwenye rufaa au mapitio, mahakama ikiridhika kwamba kosa hilo upungufu, kutotenda au kutokuwa sahihi kiuhalisia hakukuwa na haki, mahakama inaweza kuamuru kusikilizwa upya au kutoa amri nyingine kama itakavyoona ni haki na sawa.

Uchukuaji wa vitu kinyume na sheria mchukuaji kutokuwa mvamizi kutokana na makosa au kwa ajili ya muundo katika mwenendo

389. Hakuna uchukuaji wa vitu iliyofanywa chini ya sheria hii utachukuliwa kuwa si halali, au mtu anayefanya atakuwa ameingilia au kutokana na kasoro yoyote au kukosekana kwa fomu ya wito, hatia, hati ya uchukuaji wa vitu au mienendo mingine inayohusiana hapo.

(b) Maelekezo kuhusiana na asili ya amri ya kumfikisha mfungwa na hati mahakamani

Uwezo wa kutoa maelekezo ya amri ya kumfikisha mfungwa mahakamani .

390.-(1) Mahakama kuu, itakavyoona inafaa itaelekeza

- (a) Kwamba mtu yeyote ndani ya eneo la Tanzania Bara ataletwa mbele ya mahakama na kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.
- (b) Kwamba mtu yeyote kinyume na sheria au visivyo sahihi atazuiwa na Jamhuri au chini ya kizuizi binafsi katika eneo hilo kuachiwa huru.
- (c) Kwamba mfungwa yeyote aliyeshikiliwa kwenye magereza yoyote katika eneo hilo kuletwa mahakamani kuulizwa maswali kama shahidi katiaka swala lolote lililowekwa kando au kutakiwa kuchunguzwa na mahakama hiyo.
- (d) Kwamba mfungwa yeyote aliyeko kizuizini atafikishwa mbele ya mahakama ya kijeshi au kamishna yeyote anayekaimu chini ya mamlaka au tume yoyote kutoka

kwa Rais kwa kusikilizwa au kuhojiwa ukigusa jambo lolote lililowekwa kando mbele ya mahakama ya kijeshi au kamishna.

- (e) Kwamba mfungwa yeyote ndani ya mipaka hiyo kutolewa kutoka kizuizi kimoja kwenda kingine kwa madhumuni ya kusikiliza; na
- (f) Kwamba mwili wa mdaiwa ndani ya mipaka hiyo uletwe kwa amri ya kukamatwa.

(2) Mahakama kuu inaweza mara kwa mara kutengeneza kanuni kushughulikia utaratibu wa kesi chini ya kifungu hiki.

Nguvu ya Mahakama Kuu kutoa hati.

391. Mahakama kuu inaweza kwa kutumia mamlaka yake ya jinai, ya kutoa amri yeyote kutoa amri ambayo engeweza kutolewa na mahakama hiyo.

(c) Mengineyo

Watu ambao viapo vinaweza kuapwa mbele yao

392. Viapo na vidhibitisho vitakavyotumika mbele ya mahakama kuu vinaweza kuapwa na kuthibitishwa mbele ya jaji wa mahakama kuu au hakimu au msajili au msajili msaidizi wa mahakama kuu au mlinzi yeyote wa amani au kamishna wa viapo.

Nakala za mienendo ya kesi.

393. Iwapo mtu yeyote aliyeathirika na hukumu yeyote au amri iliyopitishwa katika mwenendo wowote chini ya sheria hii atapenda kuwa na nakala ya hukumu au kiapo chochote au kuwekwa kokote au sehemu nyingine ya kumbukumbu atatakiwa, kwa maombi ya nakala hiyo, kupewa; itakapoonekana, kuhusiana na kiapo chochote au sehemu ya kumbukumbu zaidi ya hukumu au amri, atalipa kwa hiyo, isipokuwa mahakama kwa sababu maalumu itaona sahihi kutoa bila gharama.

Fomu.

394. Fomu hizo kama mahakama kuu mara kwa mara itahakiki, pamoja na tofauti hizo kama inavyoweza kuhitajika na mazingira hayo, inaweza kutumika kwa madhumuni yaliyotajwa na kama imetumika yatakuwa yamejitosheleza.

Gharama za wazee wa baraza, mashahidi, n.k.

395. Kufuatia kanuni zozote ambazo zinaweza kutengenezwa na waziri, mahakama yoyote inaweza kuamri malipo kwa upande wa serikali kwa matumizi ya msingi ya mzee yeyote wa baraza, mlalamikaji au shahidi anayehudhiria mbele ya mahakama kwa madhumuni ya uchunguzi, usikilizwaji au mienendo mingine chini ya sheria hii.

[Imefutwa.]

396. [Inafuta Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Akiba.]

Sheria Na: 2 ya 1972; 3 ya 1976	<p>_____</p> <p>JEDWALI LA KWANZA</p> <p>_____</p> <p>(Chini ya Vifungu Na. 2, 164, 165 na 225)</p>
<p>SEHEMU A.</p> <p>MAKOSA CHINI YA SHERIA YA KANUNI ZA ADHABU</p>	
<p><i>Taarifa ya ufafanuzi-</i> Yaliyoingizwa katika safu ya pili na ya nne ya jedwali hili, yenye kichwa “Kosa” na “Adhabu chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu” hayakusudiwi kuwa ni maana ya kosa na adhabu zilizotolewa katika vifungu husika katika Sheria ya Kanuni za Adhabu au kama ufupisho wa vifungu hivyo, lakini kama rejea ya kilichoko kwenye kifungu, namba ambayo imetolewa katika safu ya kwanza..</p>	

SURA YA TANO – WAHUSIKA KWENYE MAKOSA

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Iwapo afisa wa polisi anaweza au hawezi kukamata bila hati</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni za Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni za Adhabu)</i>	<i>Mahakama (pamoja na Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
22	Kusaidia, Kushawishi, Kushauri au Kuchukuliwa katika utendaji wa kosa.	Anaweza kukamata bila hati iwapo ukamataji wa kosa lililosaidiwa, shawishiwa, shauriwa au chukuliwa utafanywa bila hati lakini si vinginevyo..	Adhabu inayofanana kwa kosa la kusaidiwa, kushawishiwa, kushauriwa au kuchukuliwa.	Mahakama yoyote ambayo kosa lililosaidiwa, shawishiwa, shauriwa au chukuliwa linaweza kusikilizwa.

Divisheni ya I. – Makosa dhidi ya Usakama wa Umma

SURA YA SABA. – UHAINI NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA JAMHURI

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Iwapo afisa wa polisi anaweza au hawezi kukamata bila hati</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni za Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni za Adhabu)</i>	<i>Mahakama (pamoja na Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

39 ..	Uhaini	Anaweza kukamata bila hati.	Kifo.	
40 ...	Kosa dogo la uhaini	Anaweza kukamata bila hati	Kifo.	
41 ...	Kuficha uhaini	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha maisha	
43 ...	Kuendeleza vitendo vya kivita.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha maisha	
45 ...	Kuchochea uasi.	Anaweza kukamata	Kifungo cha maisha	

		bila hati		
46 ...	Kusaidia katika matendo ya uasi.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.
47 ...	Kushawishi kutoroka.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miezi sita.	Mahakama ya chini.
48(a)	Kumsaidia mfungwa wa kivita kutoroka.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	
(b)...	Kuruhusu wafungwa wa kivita kutoroka.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.
59 ...	Kusimamia au kuchukua kiapo cha kutenda kosa la kuua.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	Mahakama ya Chini.
60 ...	Kusimamia au kuchukua viapo vingine vilivyopo kinyume na sheria.	anaweza kukama bila hati	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
62(1)..	Kwata isiyo halali	anaweza kukama bila hati	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
(2)..	Kupigishwa kwata kusikokuwa halali	anaweza kukama bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	
63 B...	Kuanzisha kutoridhika na nia mbaya kwa madhumuni yasiyohalali kisheria.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miezi kumi na mbili.	

**SURA YA NANE. – MAKOSA YANAYOATHIRI MAHUSIANO NA NCHI ZA NJE
NA AMANI NA UTULIVU WA NJE**

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Iwapo afisa wa polisi anaweza au hawezi kukamata bila hati</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni za Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni za Adhabu)</i>	<i>Mahakama (pamoja na Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

65 ...	Uandikishaji wa askari wa kivita kwa nchi za kigeni	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya chini
66 ...	Uharamia.	Anaweza kukamata bila hati.	kifungo cha maisha	Mahakama ya chini

**SURA YA TISA . – MIKUSANYIKO ISIYO HALALI ,, MIGOMO NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA
UTULIVU WA NCHI**

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Iwapo afisa wa polisi anaweza au hawezi kukamata bila hati</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni za Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni za Adhabu)</i>	<i>Mahakama (pamoja na Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa</i>

74 ...	Mikusanyiko	Anaweza kukamata bila	Kifungo cha mwaka	Mahakama ya chini.
--------	-------------	-----------------------	-------------------	--------------------

	isiyokuwa halali	hati..	mmoja.	
74 ...	Mgomo	Anaweza kukamatabila hati..	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
79 ...	Mgomo baada ya utoaji wa ilani	Anaweza kukamatabila hati	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini
80 ...	Kupinga utoaji wa ilani	Anaweza kukamatabila hati	Kifungo cha miaka mitano au kumi.	Mahakama ya chini
81 ...	Wafanya ghasia kuharibu majengo.	Anaweza kukamatabila hati	Kifungo cha maisha.	
82 ...	Wafanya ghasia kuhasiri majengo.	Anaweza kukamatabila hati	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
83 ...	Kuyaingilia kwa ghasia reli, n.k.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.
84 ...	Kutembea na silaha hadharani	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya chini
86....	Kuzuia kwa nguvu.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya chini
87 ...	Kufanya fujo hadharani.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miezi sita.	Mahakama ya chini
88 ...	Kuchochea mapigano ya wawili	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
89(1)..	Lugha ya matusi na ugomvi.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miezi sita.	Mahakama ya chini
89(2)..	kutishia utumiaji wa nguvu .	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha mwaka mmoja	Mahakama ya chini
	Iwapo kosa limetendeka usiku.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini .
89 (A)	Kuvinjari au kuzonga	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miezi sita	Mahakama ya chini
89B ...	Vitisho	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha mwaka mmoja.	Mahakama ya chini
89C ...	Kushawishi watu kutokusaidia miradi ya kujitolea	Hawezi kukamata bila hati	Faini ya shilingi elfu moja au kifungo cha miezi sita au vyote.	Mahakama ya chini
90 ...	Kukusanyika kwa lengo la magendo.	Hawezi kukamatabila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini

Divisheni ya II. – Makosa dhidi ya Usimamiaji wa Mamlaka Halali Kisheria
SURA YA KUMI . – KUTUMIA VIBAYA OFISI

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Iwapo afisa wa polisi anaweza au hawezi kukamata bila hati</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni za Adhabu)</i>	<i>Mahakama (pamoja na Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

94 ...	Afisa anayetokeleza majukumu kuhusiana na mali ambayo ana maslahi maalumu.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha mwaka mmoja	Mahakama ya Chini
95 ...	Madai ya uongo ya maafisa.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya Chini
96 ...	Kudharau ofisi.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya Chini
	(kama ni kwa lengo la faida).	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya Chini
97 ...	Cheti cha uongo na afisa wa umma.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya Chini
98 ...	Kusimamia kiapo bila idhini.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha mwaka mmoja.	Mahakama ya Chini
99 ...	Kujichukulia madaraka ya uongo.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili..	Mahakama ya Chini
100 ...	Kujifanya maafisa wa umma.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili...	Mahakama ya Chini.
101 ...	Vitisho vya kuwadhuru watu walioajiriwa kwenye utumishi wa umma.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili....	Mahakama ya Chini

SURA YA KUMI NA MOJA – MAKOSA YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA HAKI

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Iwapo afisa wa polisi anaweza au hawezi kukamata bila hati</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni za Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni za Adhabu)</i>	<i>Mahakama (pamoja na Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

103 ...	Maelezo ya uongo na mkalimani.	Hawezi kukamata bila hati	Adhabu sawa na ile ya kudanganya mahakama.	Mahakama ya chini.
104 ...	Kutoa ushahidi wa uongo au kutegemea ushahidi wa uongo.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
106 ...	Uzushi wa ushahidi..	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba	Mahakama ya chini
107 ...	Kuapa uongo.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
108 ...	Mashahidi wanaodanganya.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
109	Kuharibu ushahidi	Hatakamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya chini

110 ...	Kula njama kupinga haki na kuingilia mashahidi	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini
111 ...	Kuunganisha makosa.	Hawezi kukamata	Kifungo cha miaka	Mahakama ya chini .

		bila hati	miwili.	
112 ...	Kuunganisha matendo ya jinai.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili .	Mahakama ya chini .
113 ...	Kutangaza kwa mali iliyoibiwa.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili .	Mahakama ya chini .
114(1).	Kudharau mahakama.	Hatakamata bila hati	Kifungo cha miezi sita au faini ya shilingi elfu hamsini.	Mahakama ya chini .
114(2).	Kudharau mahakama (iwapo ilitendeka mbele ya mahakama).	Anaweza kukamata bila hati.	Faini ya shilingi elfu nne au akishindwa kulipa kifungo cha mwezi mmoja.	Mahakama ya chini .
114A ..	Kuzuia au kupinga wito au utekelezaji wa hukumu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha mwaka mmoja.	Mahakama ya chini.
SURA YA KUMI NA MBILI – KUOKOA, KUTOROKA NA KUWAZUIA MAAFISA WA MAHAKAMA				
1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Iwapo afisa wa polisi anaweza au hawezi kukamata bila hati</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni za Adhabu)</i>	<i>Mahakama (pamoja na Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
115 ...	Kuokoa–			
(a) ..	Iwapo mtu aliyeokolewa yuko chini ya adhabu ya kifo au kifungo cha maisha au ameshitakiwa kwa kosa linaloadhibiwa kwa kifo au kifungo cha maisha;	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	
(b) ..	Iwapo mtu aliyeokolewa amefungwa kwa mashitaka au chini ya adhabu kwa kosa lolote lingine.	Anaweza kukamata bila hati .	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
(c) ..	Katika kesi nyingine. yoyote	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini .
116 ...	Kutoroka.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
116A(1)	Kutokuhudhuria kwenye kazi ya kifungo cha jela .	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili au faini au vyote.	Mahakama ya chini
117 ...	Kusaidia wafungwa kutoroka.	Anaweza kukamata bila hati .	Kifungo cha miaka saba	Mahakama ya chini
	Uondoshaji n.k wa mali yoyote	Anaweza kukamata bila	Kifungo cha miaka	Mahakama ya chini

118	iliyokamatwa kihalali	hati	mitatu	
-----	-----------------------	------	--------	--

SURA YA KUMI NA TATU – MAKOSA MADOGO MADOGO DHIDI YA MAMLAKA YA UMMA

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, Punishment under the Penal Code, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
120 ...	Uongo na kukosa uaminifu kwa maafisa wa umma.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
121 ...	Kupuzia wajibu wa kiofisi.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba	Mahakama ya chini
122 ...	Taarifa za uongo kwa watu walioajiriwa katika utumishi wa umma.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miezi sita au faini ya shilingi elfu moja.	Mahakama ya chini
123 ...	Kutoheshimu wajibu wa kisheria.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
124 ...	Kutoheshimu amri halali kisheria.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
Divisheni ya III. – Makosa yanayodhuru umma kwa ujumla				
SURA YA KUMI NA NNE. – MAKOSA YANAYOHUSIANA NA DINI				
1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
125 ...	Kufedhehesha dini aina yoyote	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini..
126 ...	Kuvuruga mikusanyiko ya dini.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya chini.
127 ...	Kuingilia sehemu za mazishi au sehemu nyingine bila idhini	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini...
128 ...	Kuzuia kuzikwa	Anaweza kukamata	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya chini...

	kwa maiti n.k.	bila hati		
129 ...	Kutamka maneno kwa nia ya kuudhi imani ya dini	Hairuhusiwi kukamata bila hati	Kifungo cha mwaka mmoja.	Mahakama ya chini...
SURA YA KUMI NA TANO. – MAKOSA DHIDI YA MAADILI				
1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
131 ...	Kubaka.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha na au bila adhabu ya viboko.	Mahakama ya chini.
132 ...	Kujaribu kubaka.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha kipindi kisichozidi miaka thelathini na au bila adhabu ya viboko	Mahakama ya chini.
133 ...	Kuteka nyara.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
134 ...	Kumteka nyara msichana wa chini ya miaka kumi na sita.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.
135(1)	Udhalilishaji wa kujamiiana na shambulio la aibu kwa mwanamke.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo kisichozidi miaka mitano au faini isiyozidi shilingi laki tatu.	Mahakama ya chini.
(3).....	Kufedhehesha utu wa mwanamke	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha mwaka mmoja	Mahakama ya chini.
137 ...	Kunajisi majuha au punguani.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne na au bila adhabu ya viboko.	Mahakama ya chini.
138(1)	Mume kumnajisi mkewe aliye chini ya umri wa miaka kumi na tano	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka mitano.	
(2)...	mzazi au mlezi anayemruhusu msichana wa miaka chini ya miaka kumi na mbili ili kujamiiana na mume wake.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.
138A	Vitendo vya shambulio kubwa la aibu baina ya watu.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi, adhabu ya viboko na fidia.	Mahakama ya chini.
138B	Kuwatumia Watoto kwa Ngono	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano na kisichozidi	Mahakama ya chini.

			miaka ishirini.	
138C	Matumizi mabaya ya ngono	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini na kisichozidi miaka thelathini.	Mahakama ya chini.
138D	Bugudha katika ngono	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au faini isiyozidi shilingi laki mbili au vyote faini na kifungo na fidia.	Mahakama ya chini.
139 ...	Ukuwadi kwa ukahaba	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi na kisichopungua miaka ishirini au kwa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu.	Mahakama ya chini.
(3)....	Kumkuwadia mtoto wa kike wa chini ya miaka kumi na mbili ili aweze kujamiiana na mume wake.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini na kisichozidi miaka thelathini au kwa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au faini na fidia.	Mahakama ya chini
139(A)	Usafirishaji watu	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini na kisichozidi miaka thelathini au faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au faini na fidia	Mahakama ya chini.
140 ...	Kukuwadia unajisi.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi na kisichozidi miaka ishirini au kwa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au kwa vyote na fidia.	Mahakama ya chini
141 ...	Mwenye nyumba kuruhusu kunajisiwa kwa mtoto wa kike wa chini ya miaka kumi na mbili ndani ya majengo yake.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini
142 ...	Mwenye nyumba kuruhusu kunajisiwa kwa mtoto wa kike wa chini ya miaka kumi na sita ndani ya majengo yake.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
143 ...	Kizuizi kwa dhamira isiyo halali au katika	Anaweza kukamata bila hati..	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini

	danguro			
145 ...	Mwanamume kuishi kwa pato la la ukahaba au ukuwadi	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
146 ...	Mwanamke anayesaidia, n.k. ukahaba wa mwanamke mwingine kwa kipato.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
148 ...	Kumiliki danguro.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
149 ...	Kula njama kunajisi.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya chini
150 ...	Kujaribu kutoa mimba.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na minne.	Mahakama ya chini
151 ...	Mwanamke anayejaribu kutoa mimba yake mwenyewe.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba..	Mahakama ya chini
152 .	Kutoa madawa au vifaa kwa ajili ya kutoa mimba.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya chini
(2)...	Kutoa madawa au vyombo kwa ajili ya kutoa mimba.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	Mahakama ya chini
154 (1)	Makosa ya kinyume cha maumbile	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha na wakati mwingine kifungo kisichopungua miaka thelathini jela.	Mahakama ya chini
(2)	Makosa ya kinyume cha maumbile	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha maisha	Mahakama ya chini
	155 ... Kujaribu kutenda kosa kinyume na maumbile.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka thelathini	Mahakama ya chini
	156 (1) ... Shambulio la aibu kwa mtoto wa kiume chini ya miaka kumi na nne.	Anaweza kukamata bila hati..	Kifungo cha maisha.	Mahakama ya chini
	(2) ... Shambulio la aibu kwa mtoto wa kiume chini ya miaka kumi na nne.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na tano	Mahakama ya chini.
	157 ... Matendo ya aibu baina ya wanaume.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini

Sheria Na. 4 ya 2004 Jedwali.	158(1)(a)	kujamiiiana kwa maharimu (iwapo mwanamke ana umri chini ya miaka kumi na nane).	Anaweza kukamata bila hati..	Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka thelathini.	Mahakama ya Chini.
	(1)(b) ...	kujamiiiana kwa maharimu (iwapo mwanamke ana umri wa miaka kumi na nane na zaidi).	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo kisichopungua miaka ishirini au faini isiyozidi shilingi mia tatu au vyote kwa pamoja na fidia.	Mahakama ya chini
	(2)....	Iwapo mwanamke ana umri chini ya miaka kumi na mbili.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha	
	(3)....	Kujaribu kutenda kosa la kujamiiiana baina ya maharimu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	
	160 ...	Kujamiiiana kwa mharimu wa kike.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha au kifungo kisichopungua miaka thelathini na fidia.	Mahakama ya Chini.

SURA YA KUMI NA SITA- MAKOSA YANAYOHUSIANA NA NDOA NA MAJUKUMU YA KIFAMILIA

1	2	3	4	5
Kifungu	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
163 ...	Ndoa ya hadaa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi	
165 ...	Kwa udanganyifu au kwa ulaghai kuingia kwenye sherehe ya ndoa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	
166 ...	Kuwatelekeza watoto.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	
167 ...	Kupuuzwa kutoa	Hawezi kukamata	Kifungo cha miaka	Mahakama ya Chini.

	chakula, nk. kwa watoto.	bila hati	miwili.	
168	Tajiri kutompatia mtumishi wake au mwanagenzi wake mahitaji	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya Chini.
169...	Kuiba mtoto.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
169A.	Ukatili kwa watoto.	Anaweza kukamata bila hati..	Kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano na isiyozidi miaka kumi na tano.	Mahakama ya chini

SURA YA KUMI NA SABA – ADHA NA MAKOSA DHIDI YA AFYA NA RAHA

1	2	3	4	5
Kifungu	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

170 ...	Adha za kawaida	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha mwaka mmoja.	Mahakama ya Chini..
171(3).	Kumiliki nyumba ya kamari	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
(4) ...	Kukutwa katika nyuma ya kamari.	Hawezi kukamata bila hati	Faini ya shilingi elfu moja kwa kosa la kwanza, na kwa kila kosa linalofuata faini ya shilingi mia nne au kifungo kwa miezi mitatu au vyote.	Mahakama ya chini
172 ...	Kumiliki au kuruhusu umiliki wa nyumba ya kupingiana	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka mmoja.	Mahakama ya chini
173B..	Barua za mnyororo	Hawezi kukamata bila hati	Faini ya shilingi mia nne au kifungo cha miezi sita au vyote.	Mahakama ya chini
175 ...	Usafirishaji wa Machapisho Machafu	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili au faini ya shilingi elfu mbili.	Mahakama ya chini

176 ...	Kuwa bila kazi au kuwa mtu asiye na mpango.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miezi mitatu au faini isiyozidi shilingi mia tano au vyote.	Mahakama ya chini.
176A..	Kuwahifadhi Makahaba.	Hawezi kukamata	Faini ya shilingi mia	Mahakama ya chini

		bila hati.	tano kwa kosa la kwanza, na shilingi elfu moja kwa mimosa yanayofuata.	
177 ...	Kuwa mhuni au mzururaji.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miezi mitatu kwa kosa la kwanza na kwa kila kosa linalofuata kifungo cha mwaka mmoja.	Mahakama ya Chini.
177 (A)	Kushindwa kutoa hesabu ya fedha iliyokusanywa kwa michango ya Umma	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili kwa kosa la kwanza na kwa kila kosa linalofuata kifungo cha miaka mitatu	Mahakama ya Chini
178(1)	Uvaaji wa sare bila mamlaka.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha mwezi mmoja au faini ya shilingi mia mbili.	Mahakama ya Chini.
(2) ...	Kudharau sare.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miezi mitatu au faini ya shilingi mia nne.	Mahakama ya chini
(3) ...	Kuingiza au kuuza sare bila mamlaka.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miezi sita au faini ya shilingi mia mbili.	Mahakama ya chini
179 ...	Kufanya kitendo chochote ambacho kinaweza kusababisha kuenezwa kwa ugonjwa wa hatari.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
180 ...	Kuchanganya kitu kisichofaa katika chakula au kinywaji kinachokusudiwa kuuzwa.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
181 ...	Kuuza au kujaribu kuuza au kuweka tayari kwa kuuza, chakula au kinywaji chenye madhara.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya chini
182 ...	Kuchanganya kitu kisichofaa katika madawa yanayokusudiwa kuuzwa.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya chini
183 ...	Kuuza madawa yaliyodhuriwa	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya chini
184 ...	Kuchafua chemichemi au bwawa la umma.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
185 ...	Kuchafua hewa.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya chini
186 ...	Kufanya biashara kimakosa.	Hawezi kukamata bila hati	Kifungo cha mwaka mmoja.	Mahakama ya chini.

Divisheni ya IV. – Makosa dhidi ya mtu
SURA YA ISHIRINI. – KUUA KWA KUKUSUDIA NA KUUA BILA KUKUSUDIA

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

197 ...	Kuua kwa kukusudia	Anaweza kukamata bila hati..	Kifo.	
	Kuua kwa kukusudia (iwapo mwanamke atatiwa hatiani akiwa mja mzito).	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	
198 ...	Kuua bila kukusudia.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	
199 ...	Kosa la uuaji wa mtoto mchanga.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	

SURA YA ISHIRINI NA MOJA. –MAKOSA YANAYOHUSIANA NA MAUAJI NA KUJIUA

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

213 ...	Kuwa msaidizi baada ya kosa kwa kosa la mauaji.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	
214 ...	Kitisho cha kua kwa maandishi.	Anaweza kukamata bila hati..	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya Chini.
215 ...	Kula njama kua.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo kwa miaka kumi na nne.	
216 ...	Kusaidia kujiua	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	
217 ...	Kujaribu kujiua	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya Chini.
218 ...	Kuficha kuzaliwa kwa mtoto.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili	Mahakama ya Chini.

219 ...	Kuharibu mtoto.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha	
SURA YA ISHIRINI NA TATU. – MAKOSA YANAYOHATARISHA MAISHA AU AFYA				
1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
220 ...	Kulemaza kwa nia ya kutenda kosa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha	
221 ...	Kupumbaza mtu kwa nia ya kutenda kosa	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha maisha	
222 ...	Vitendo vinavyokusudiwa kusababisha madhara makubwa au kuzuia ukamataji	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha maisha	
223 ...	Kuzuia kuponyoka kwenye chombo kilichovunjika.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha	
224(1)	kuhatarisha kwa makusudi usalama wa watu wanaosafiri kwa reli.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha maisha	

(2) ...	Kuhatarisha bila kukusudia.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya Chini.
225 ...	Kutenda madhara makubwa.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya Chini.
226 ...	Kujaribu kuuu kwa vitu vya mlipuko.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka kumi na nne.	
227 ...	Kulisha sumu kwa nia ya kuuu.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka kumi na nne	
228 ...	Kujeruhi na matendo kama hayo.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya Chini.
229 ...	Kushindwa kutoa mahitaji muhimu ya maisha.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miaka mitatu	Mahakama ya chini

SURA YA ISHIRINI NA NNE – JINAI KWA KUTOJALI NA UZEMBE

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
233 ...	Matendo ya pupa na uzembe.	Anaweza kukamata	Kifungo cha miaka	Mahakama ya chini.

		bila hati.	miwili. .	
234 ...	Matendo mengine ya kizembe yanayosababisha madhara.	Anaweza kukamata bila hati	Kifungo cha miezi sita.	Mahakama ya chini
235 ...	Kushughulikia vitu vyenye sumu kizembe.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miezi sita au faini ya shilingi elfu mbili.	Mahakama ya chini
237 ...	Kuonyesha mwanga, alama, au boya la uongo.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
238 ...	Kusafirisha mtu kwa njia ya maji kwa chombo cha kukodi katika hali isiyo salama au chombo kilichojaa sana.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
239 ...	Kusabisha hatari au kizuizi katika njia ya umma au katika usafiri wa maji.	Hawezi kukamata bila hati.	Faini.	Mahakama ya chini

SURA YA ISHIRINI NA TANO. – SHAMBULIO

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

240 ...	Shambulio la kawaida.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha mwaka mmoja.	Mahakama ya chini.
241 ...	Shambulio linalosababisha madhara ya mwili.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini
242 ...	Kushambulia watu wanaozuia kuvunjika kwa chombo.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
243 ...	Mashambulio mbalimbali	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini

SURA YA ISHIRINI NA SITA. – MAKOSA DHIDI YA UHURU WA MTU

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

247 ...	Kuteka nyara	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
248 ...	Kuteka nyara au	Anaweza kukamata bila	Kifungo cha miaka kumi.	

	kutorosha kwa nia ya kuua	hati.		
249 ...	Kuteka nyara au kutosha kwa nia ya kumficha.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
250 ...	Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kujeruhi, utumwa n.k	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	
251 ...	Kumficha mtu aliyetekwa au aliyeporwa kinyume na sheria	Anaweza kukamata bila hati.	Adhabu sawa na kuteka au kutorosha	
252 ...	Kumteka nyara au kumtorosha mtoto wa chini ya miaka kumi na nne kwa nia ya kumwibia	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
253 ...	Adhabu kwa kuzuiliwa kimakosa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha mwaka mmoja au faini ya shilingi elfu tatu.	Mahakama ya chini
254 ...	Kununua au kumweka mtu yeyote kama mtumwa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	
255 ...	Kuwa na mazoea kushughulika na watumwa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	
256 ...	Kazi ya lazima kinyume cha sheria.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.

**Divisheni ya V. – Makosa yanayohusiana na mali
SURA YA ISHIRINI NA SABA. – WIZI**

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

258 ...	Wizi.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya chini.
266 ...	Kuiba wosia.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	Mahakama ya chini
268 ...	Kuiba baadhi ya wanyama.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na tano.	Mahakama ya chini

269 ...	Kuiba kutoka kwa mtu, katika nyumba ya kuishi, safarini, n.k.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	Mahakama ya chini .
270 ...	Kuiba kwa watu waliopo katika	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	

	utumishi wa umma.			
271 ...	Kuiba kwa makarani na watumishi.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	Mahakama ya chini
272 ...	Kuiba kwa wakurugenzi au maafisa wa makampuni.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
273 ...	Kuiba kwa mawakala ,n.k.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	Mahakama ya chini
274 ...	Kuiba kwa wapangaji wa kudumu wapangaji wa muda	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
275 ...	Kuiba baada ya kutiwa hatiani kulikopita.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini

SURA YA ISHIRINI NA NANE. – MAKOSA YANAYOENDANA NA KUIBA

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
276 ...	Kuficha rejista.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	
277 ...	Kuficha wosia.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	
278 ...	Kuficha hati.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	
279 ...	Kuua wanyama kwa kusudi la kuiba.	Anaweza kukamata bila hati.	Adhabu sawa kama vile mnyama ameibiwa.	Mahakama yoyote ambayo wizi wa mnyama unaweza kusikilizwa.
280 ...	Kuvunja kwa nia ya kuiba.	Anaweza kukamata bila hati.	Adhabu sawa kama vile kitu kimeibiwa.	Mahakama yoyote ambayo wizi wa kitu unaweza kusikilizwa.
281 ...	Uhamishaji wa udanganyifu wa bidhaa iliyowekwa rehani.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.
282 ...	Kujihusisha kiudanganyifu na mawe yenye madini au madini katika machimbo.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini
283 ...	Kujipatia kwa udanganyifu mashine za makenika au umeme.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini.
284 ...	Kubadilisha kitu cha mtu mwingine ambako sio wizi	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miezi sita au faini ya shilingi elfu moja.	Mahakama ya chini

284A .	Hasara kwa serikali au shirika la umma na wafanyakazi	Hawezi kukamata bila hati.	Faini isiyozidi shilingi laki tano au kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.
--------	---	----------------------------	---	--------------------

SURA YA ISHIRINI NA TISA. – UNYANG’ANYI NA KUPATA MALI KWA NGUVU

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
286 ...	Unyang’anyi.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka ishirini.	Mahakama ya chini.
286 ...	Unyang’anyi kwa kutumia nguvu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha, na au bila adhabu ya viboko.	Mahakama ya chini
287 ...	Kujaribu kunyang’anya.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo kisichopungua miaka saba na kisichozidi miaka ishirini.	Mahakama ya chini
287 ...	Kujaribu kunyang’anya kwa kutumia nguvu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha, au kifungo cha miaka isiyozidi kumi na tano na adhabu ya viboko.	Mahakama ya chini
288 ...	Kuchambulia kwa nia ya kuiba.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka isiyopungua miaka mitano na isiyozidi miaka kumi na nne na adhabu ya viboko.	Mahakama ya chini
289 ...	Kutaka mali kwa vitisho vya maandishi.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
290 ...	Kutishia kwa nia ya kupata mali kwa nguvu	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
290 ...	Katika kesi maalumu na katika kesi nyingine yoyote.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya chini.
291 ...	Kulazimisha kutekelezwa kwa hati, n.k, kwa vitisho.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
292 ...	Kudai mali kwa kutishia kwa kusudi la kuiba	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini.

SURA YA THELATHINI- UVUNJAJI WA NYIMBA USIKU, UVUNJAJI WA NYUMBA MCHANA NA MAKOSA SAWA NA HAYO.

		3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza</i>

		<i>hawezi.</i>	<i>na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>kusikilizwa.</i>
294 (1)	Kuvunja nyumba mchana	Anaweza kukamata bila hati..	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahaka ya chini.
(2)	Kuvunja nyumba usiku.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka ishirini.	Mahakama ya chini
295 ...	Kuingia Nyumba ya kuishi kwa nia ya kutenda kosa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	Mahakama ya chini
295 ...	Iwapo kosa limetendeka usiku.	Anaweza kukamata bila hati..	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
296 ...	Kuvunja nyumba na kuingia na kutenda kosa .	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	Mahakama ya chini.
297 ...	Kuvunja nyumba na kuingia kwa nia ya kutenda kosa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini
298 ...	Kukutwa na silaha, n.k., kwa nia ya kutenda kosa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini
298 ...	Iwapo mkosaji aliwahi kutiwa hatiani kwa kosa linalohusiana na mali.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
299 ...	Jinai ya kuingia bila idhini	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miezi mitatu.	Mahakama ya chini
299 ...	Iwapo mali ambayo kosa lilitendeka ni jengo linalotumika kama makazi ya watu au sehemu ya ibada au kama sehemu ya kutunzia mali.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha mwaka mmoja.	Mahakama ya chini

SURA YA THELATHINI NA MOJA. – UDANGANYIFU

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

302 ...	Kupata mali kwa njia ya udanganyifu	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
303 ...	Kupata dhamana ya utekelezaji kwa njia ya udanganyifu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba	Mahakama ya chini
304 ...	Kudanganya.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya chini.
305 ...	Kupata mkopo,n.k., kwa njia ya	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	

	udanganyifu.			
306 ...	Kula njama kwa nia ya kudanganya.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini.
307 ...	Udanganyifu katika kuuza au kuweka rehani mali.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini

308 ...	Kujifanya mtabiri	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
309 ...	Kupata usajili, n.k, kwa njia ya udanganyifu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
310 ...	Tamko la uongo kwa hati ya kusafiria.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	

SURA YA THELATHINI NA MBILI. – KUPOKEA MALI LIYOIBIWA AU ILIYOPATIKANA KINYUME NA SHERIA NA MAKOSA YANAYOFANANA

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

311 ...	Kupokea au kutunza mali iliyoibiwa au iliyopatikana kinyume cha sheria.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi.	Mahakama ya chini.
312 ...	Kushindwa kutoa maelezo kwa mali aliyokutwa nayo mtu na inayodhaniwa kuibwa au kupatikana kinyume cha sheria.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya chini.
312A(2)	Kuhodhi kinyume cha sheria ghala ya serikali au reli.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
(3) ...	Kuhodhi kinyume cha sheria huduma ya ghala.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
313 ...	Kupokea mali zilizoibiwa nje ya Tanzania.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini

SURA YA THELATHINI NA TATU. – UDANGANYIFU WA WADHAMINI NA WATU WA KAZI ZA

MUAMANA NA HESABU ZA UWONGO

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
314 ...	kutoa mali iliyodhaminiwa kwa udanganyifu	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
315 ...	Wakurugenzi na maafisa wa mashirika wanaojipatia mali kwa udanganyifu, au kutunza mahesabu ya kidanganyifu, kughushi vitabu au mahesabu	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
316 ...	Maelezo ya uongo na maafisa wa shirika	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
317 ...	Kutunza hesabu za uongo kwa karani au mtumishi.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini

318 ...	Kudanganya kwa Kutoa maesabu ya udanganyifu maafisa wa umma.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
---------	--	-----------------------------	-------------------------	-------------------

**Divisheni ya VI. – Madhara ya Makusudi kwa Mali.
SURA YA THELATHINI NA NNE. – MAKOSA YANAYOSABABISHA MADHARA KWA MALI**

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
319 ...	Kuchoma nyumba moto.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	Mahakama ya chini.
320 ...	Kujaribu kuchoma Nyumba.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
321 ...	Kuchoma moto mazao au mazao yanayokua.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
322 ...	Kujaribu kuchoma moto mazao au	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.

	mazao yanayokua.			
323 ...	Kutelekeza chombo cha maajini.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	
324 ...	Kujaribu kutelekeza chombo cha maajini	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
325 ...	Kujeruhi wanyama.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
326(1)	Kuharibu au kuvunja mali kwa makusudi.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
(2)...	Kuharibu nyumba ya kuishi au chombo cha majini kwa mlipuko.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	
(3)	Kuharibu au kuvunja kingo za mto au ukuta au njia ya maji, au madaraja.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	
3(c)	Kuvunja au kuharibu bomba la mafuta ya Tanzania- Zambia au mali zinginezo.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha	Mahakama ya chini
(4) ...	Kuharibu wosia au rejesta.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini.
(5) ...	Kuharibu au kuvunja vyombo vilivyoharibika..	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
(6) ...	Kuharibu kuvunja reli.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
(7) ...	Kuvunja au kuharibu mali zinazotumika kusambazia umeme.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne iwapo kosa linaweza kusababisha hatari kwa maisha ya binadamu, vinginevyo kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
(8) ...	Kuvunja au kuharibu mali zenye thamani maalumu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
(9) ...	Kuvunja au kuharibu hati au kumbukumbu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba	Mahakama ya chini
327 ...	Kujaribu kuvunja au kuharibu mali kwa kutumia mlipuko.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka kumi na nne.	Mahakama ya chini
328 ...	Kueneza ugonjwa wa kuambukiza kwa wanyama.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
329 ...	Kuondoa alama za mipaka kwa nia ya kudanganya.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya chini.
331 ...	Kudhuru au kuzuia kazi za reli, n.k.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miezi mitatu au faini ya shilingi mia nne.	Mahakama ya chini.
332 ...	Kutishia kuchoma jengo lolote, n.k., au kua au kujeruhi mfugo wowote.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
332A..	Kuharibu noti za	Hawezi kukamata	Faini ya shilingi elfu tano	Mahakama ya chini.

	benki.	bila hati.	kwa kila noti iliyoharibiwa au ikishindikana faini kulipwa kwa kifungo cha mwaka mmoja.	
Divisheni ya VII. - Kughushi,, Utengenezaji Sarafu, Kubuni Sarafu na Makosa sawa na hayo SURA YA THELATHINI NA TANO – ADHABU ZA KUGHUSHI				
1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
337 ...	Kughushi (iwapo hakuna adhabu maalumu iliyotolewa)	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
338 ...	Kughushi wosia, waraka wa umiliki, dhamana, cheki, n.k.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	Mahakama ya chini
339 ...	Kughushi nyaraka za mahakama au kiofisi.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
340 ...	Kughushi, n.k., kwa stempu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba	Mahakama ya chini
341 ...	Kutengeneza au kuhodhi karatasi au vifaa vya kughushi noti za benki. nk.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
342 ...	Kuwasilisha nyaraka za kughushi.	Anaweza kukamata bila hati.	Adhabu sawa na ya kughushi nyaraka.	Mahakama yoyote ambayo kughushi nyaraka kunaweza kusikilizwa.
343 ...	Kuwasilisha waraka uliofutwa au uliopitwa na wakati..	Anaweza kukamata bila hati.	Adhabu sawa na ya kughushi nyaraka	Mahakama ya chini
344 ...	Kusababisha kutekelezwa kwa waraka kwa udanganyifu	Anaweza kukamata bila hati.	Adhabu sawa na ya kughushi nyaraka	Mahakama ya chini
345 ...	Kufuta au kubadili mistari kwenye cheki.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
346 ...	Kutengeza au kutekeleza waraka bila mamlaka.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba	Mahakama ya chini
347 ...	Kutaka mali kwa kutumia waraka ulioghushiwa.	Anaweza kukamata bila hati.	Adhabu sawa na ya kughushi hati.	Mahakama yoyote ambako kughushi hati kunaweza kusikilizwa.
348 ...	Kununua au kupokea noti za benki	Anaweza kukamata bila hati. .	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.

	zilizoghushiwa.			
349 ...	Kughushi hati ya fedha inayolipwa chini ya mamlaka ya umma.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba	Mahakama ya chini
350 ...	Kuruhusu kughushi rejesta au kumbukumbu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba	Mahakama ya chini
351 ...	Kutuma cheti cha ndoa kilichoghushiwa kwa msajili.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini
352 ...	Kutoa maelezo ya uongo kwa kuingizwa kwenye rejesta ya vizazi, vifo na ndoa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya chini.
352A ..	Kutoa noti kimakosa.	Anaweza kukamata bila hati. .	Kifungo cha miaka mitano.	Mahakama ya chini.

SURA YA THELATHINI NA SITA. – MAKOSA YANAYOHUSIANA NA SARAFU

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaaweza kusikilizwa.</i>
354 ...	Kughushi sarafu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha.	
355 ...	Kufanya maandalizi kwa ajili ya kughushi sarafu.	Anaweza kukamata bila hati. .	Kifungo cha maisha	
356 ...	Kukata sarafu	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.

359 ...	Kukukutwa na makala ya sarafu iliyokatwa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha maisha	Mahakama ya chini
360 ...	Kuwasilisha sarafu zilizoghushiwa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
361 ...	Kurudia kuwasilisha sarafu zilizoghushiwa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka mitatu.	Mahakama ya chini
362 ...	Kuwasilisha kipande cha chuma kama sarafu.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha mwaka mmoja.	Mahakama ya chini
363 ...	Kupeleka nje ya nchi sarafu zilizoghushiwa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini

SURA YA THELATHINI NA SABA. – STEMPU ZILIZOGHUSHIWA

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
365 ...	Kukutwa, nk., wino au karatasi zinazotumika kutengenezea stempu za ushuru.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
366 ...	Kukutwa nk., wino au karatasi zinazotumika kutengeneza stempu za posta.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha mwaka mmoja au faini ya shilingi elfu moja.	Mahakama ya chini
SURA YA THELATHINI NA NANE. – KUGHUSHI ALAMA ZA BIASHARA				
367 ...	Kughushi, n.k., alama ya biashara.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.

SURA YA THELATHINI NA TISA. – KUJIFANYA

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>
368 ...	Kujifanya	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.
	Iwapa kujifanya ni kwamba mkosaji ni mtu anayeruhusiwa kwa wosia au kwa mujibu wa sheria kwa mali yoyote iliyotajwa na akatenda kosa kupata mali hiyo	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
370 ...	Kukubali kwa udanganyifu hati, ahadi za mahakama n.k.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.
371 ...	Kujifanya ni mtu aliyetajwa kwenye cheti.	Anaweza kukamata bila hati.	Adhabu sawa kama ya kughushi cheti.	Mahakama yoyote ambayo kughushi cheti kunaweza kusikilizwa.
372 ...	Kuazimisha n.k., cheti kwa lengo la kujifanya.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.
373 ...	Kujifanya kuwa ni mtu	Anaweza kukamata bila	Kifungo cha miaka	Mahakama ya chini

	alijetajwa kwenye waraka wa tabia.	hati.	miwili.	
374 ...	Kuazimisha n.k., waraka wa tabia kwa lengo la kujifanya.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini

Divisheni ya IX. – Kujaribu na kula njama kutenda kosa na washiriki baada ya kosa.

SURA YA AROBAINI NA MOJA. – KUJARIBU

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

381 ...	Kujaribu kutenda kosa.	Inatokana na labda au siyo kosa ni lile ambalo polisi anaweza kukama bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama yoyote ambayo kosa lililojaribiwa linaweza kusikilizwa.
382 ...	Kujaribu kutenda kosa linaloadhibiwa kwa adhabu ya kifo, kifungo cha miaka kumi na nne au zaidi.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama yoyote ambayo kosa lililojaribiwa linaweza kusikilizwa.
383 ...	Kuzembea katika kuzuia kutendeka au kumalizika kwa kosa.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.

SURA YA AROBAINI NA MBILI – KULA NJAMA

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kosa linaweza kusikilizwa.</i>

384 ...	Kula njama kutenda kosa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama yoyote inaweza kusikiliza kosa.
385 ...	Kula njama kutenda kosa.	Inatokana na labda au siyo kosa ni lile ambalo polisi anaweza kukama bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama yoyote ambayo kosa linaweza kusikilizwa.
386 ...	Kula njama kutekeleza malengo Fulani yaliyotajwa.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini.

SURA YA AROBAINI NA TATU. – WASHIRIKI BAADA YA KOSA

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kos linaweza kusikilizwa.</i>
388 ...	Kuwa mshiriki baada ya kosa kutendeka.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka saba.	Mahakama ya chini.
389 ...	Kuwa mshiriki baada ya kosa kutendeka.	Hawezi kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini
390 ...	Kuchawishi kutendeka kwa kosa.	Anaweza kukamata bila hati.	Kifungo cha miaka miwili.	Mahakama ya chini

**SEHEMU B. – MAKOSA KWENYE SHERIA NYINGINE TOFAUTI NA SHERIA YA KANUNI ZA ADHABU
Sheria Na. 13 ya 1972 kif. 9**

1	2	3	4	5
<i>Kifungu</i>	<i>Kosa</i>	<i>Kama afisa wa polisi anaweza kukama bila hati au hawezi.</i>	<i>Adhabu chini ya Sheria ya kanuni ya Adhabu, (N.B. Kupitia. Vilevile vifungu 27 na 35, Sheria ya Kanuni ya Adhabu)</i>	<i>Mahakama (kuongezea kwenye Mahakama Kuu) ambayo kos linaweza kusikilizwa.</i>
	Iwapo inaadhibiwa kwa adhabu ya kifo au kifungo cha zaidi ya miaka kumi na tano.	Anaweza kukamata bila hati.		
	Iwapo inaadhibiwa kwa kifungo cha miaka miwili au zaidi, lakini si zaidi ya miaka kumi na tano.			Mahakama ya chini.

Iwapo inaadhibiwa kwa kifungo cha miaka chini ya miwili au na faini tu.

Hawezi kukamata bila hati isipokuwa kama sheria inayounda kosa inasema vinginevyo.

Mahakama ya chini.

JEDWALI LA PILI

**FOMU ZA KUELEZA KOSA KATIKA TAARIFA
(Kifungu 135)**

1. – KUUA KWA KUKUSUDIA

Kuua kwa kukusudia, kinyume na kifungo cha 196 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B. katika tarehe.....mwezi.....mwaka.....katika mkoa wa....., alimuua bila kukusudia J.S.

2. – MTU ANAYESAIDIA KUTENDEKA KWA KOSA LA KUUA KWA KUKUSUDIA

Mtu anayesaidia kutendeka kwa kosa la kuua kwa kukusudia, kinyume na kifungu cha 213 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., kwa kujua kuwa H.C., alifanya tarehe.....siku ya.....20..... katika mkoa wa..... alimuua kwa kukusudia C.C alifanyasikuya20.....katika mkoa wana siku nyingine baada ya hapo alipokea au alimsaidi mtajwa H.C. ili kumfanya kutoroka adhabu.

3. – KUUA BILA KUKUSUDIA

Kuua bila kukusudia, kinyume na kifungu cha 195 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehesiku ya.....,20.....katika mkoa wa.....alimuua kinyume na sheria J.S.

4. - UBAKAJI

Ubakaji, kinyume na kifungu cha 130 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya..... 20.....katika mkoa wa.....alimwingilia kimwili E.F., bila ya ridhaa yake.

5. - KUJERUHI

Kosa la kwanza. – Kujeruhi kwa kukusudia, kinyume na kifungu cha 22 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

A.B., tarehe.....siku ya....., 20.....katika mkoa wa.....alimjeruhi C.D, kwa nia ya kumfanya bubu, kumharibu umbo, kumlemaza, au kumsababishia madhara makubwa au kupinga ukamataji halali kisheria wa huyo A.B.

Kosa la pili. – Kujeruhi, kinyume na kifungu cha 228 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya....., 20..... katika mkoa wa.....kinyume na sheria alimjeruhi C.D.

6. - WIZI

Kosa la kwanza. – Kuiba, kinyume na kifungu cha 265 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya....., 20.....katika mkoa wa.....aliiba mfuko.

Kosa la pili. – Kupokea vitu vilivyoibiwa, kinyume na kifungu cha 311 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya....., 20.....katika mkoa wa..... alipokea mfuko akijua kuwa mfuko huo umeibiwa.

7. – WIZI WA KARANI

Kuiba, kwa karani na watumishi, kinyume na vifungu vya 265 na 271 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya.....,20.....katika mkoa wa.....akiwa karani au mtumishi wa M.N., aliiba kutoka kwa M.N. yadi 10 za nguo.

8. – UNYANG’ANYI

Unyang’anyi kwa kutumia nguvu, kinyume na kifungu cha 285 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya.....,20.....katika mkoa wa.....aliiba simu na hapohapo au baada ya hapo kabla au baadaye baada ya muda wa wizi huo alitumia nguvu kwa C.D.

9. – WIZI WA KUINGIA NDANI YA JENGO USIKU

Wizi wa kuingia ndani ya jengo, kinyume na kifungu cha 294, na kuiba, kinyume na kifungu cha 269 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., usiku wa tarehe.....siku ya.....,20.....katika mkoa wa.....alivunja na kuingia ndani ya nyumba ya kuishi ya C.D., kwa lengo la kuiba ndani yake, na aliiba ndani yake saa moja, mali ya S.T., saa hiyo ikiwa na thamani ya shilingi mia mbili.

10. - KUTISHIA

Kuhitaji mali kwa vitisho vilivyoandikwa, kinyume na kifungu cha 289 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya.....katika mkoa wa.....akiwa na nia ya kupora fedha kutoka kwa C.D., alisababisha huyo C.D. kupokea barua yenye vitisho vya madhara au hasara kusababishwa kwa E.F.

11. – KUJARIBU KUPORA

Kujaribu kupora kwa vitisho, kinyume na kifungu cha 290 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya.....20.....katika mkoa wa.....akiwa na nia ya kupora fedha kutoka kwa C.D., alimtuhumu au alitishia kumtuhumu kwa kosa la kunyume cha maumbile.

12. – KUJIFANYA KWA UONGO

Kupata bidhaa kwa kujifanya kwa uongo, kinyume na kifungu cha 302 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B.,tarehe.....siku ya.....,20.....katika mkoa wa.....akiwa na nia ya kudanganya, alipata kutoka kwa S.P. mita 5 za nguo kwa uongo kwa kujifanya kuwa huyo A.B. alikuwa mtumishi wa J.S. na huyo, mtajwa A.B., alikuwa ametumwa na mtajwa J.S. kwa S.P., kwa nguo hizo, na kwamba yeye, mtajwa A.B. wakati huo aliidhinishwa na mtajwa J.S. kupokea nguo hizo kwa niaba ya mtajwa J.S.

13. – KUPANGA NJAMA KUDANGANYA

Kupanga njama kudanganya, kinyume na kifungu cha 306 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., na C.D. tarehe.....siku ya.....,20.....na katika siku zote kati ya siku hiyo na siku ya.....katika mkoa wa.....walipanga njama pamoja kwa lengo la kudanganya kwa njia ya tangazo lililoingizwa na wao, mtajwa A.B. na C.D., katika gazeti la H.S., kwa uongo wakijifanya kuwa A.B. na C.D. walikuwa wakifanya biashara halali kama masonara mahali.....katika mkoa na kwamba wakati huo walikuwa na uwezo wa kugawa bidaa fulani za usonara kwa mtu yeyote ambaye atapeleka kwao jumla ya shilingi arobaini.

14. – KUCHOMA NYUMBA

Kuchoma nyumba, kinyume na kifungu cha 319 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya.....katika mkoa wa.....kwa makusudi na kinyume cha Sheria alichoma moto nyumba.

15. - UHARIBIFU

Kuharibu miti, kinyume na kifungu cha 326 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya.....katika mkoa wa.....kwa makusudi na kinyume cha Sheria aliharibu mti wa mwembe uliokuwa unakuwa.

16. - KUGHUSHI

Kosa la kwanza. – Kugushi, kinyume na kifungu cha 338 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya.....katika mkoa wakwa lengo la kudanganya au kusema uongo, alighushi wosia fulani akisema ni wosia wa C.D.

Kosa la pili. – Kuota nyaraka ya kughushi, kinyume na kifungu cha 342 cha Sheria ya kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku yakatika mkoa wakwa kujua na kwa kudanganya alitoa wosia fulani ulioghushiwa akisema ni waosia wa C.D.

17. – KUTOA SARAFU BANDIA

Kutoa sarafu bandia, kinyume na kifungu cha 360 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku yakatika soko lakatika mkoa waalitoa shilingi ya kughushi, akijua kuwa hiyo ni ya kughushi.

18. – KUDANGANYA MAHAKAMA

Kudanganya mahakama, kinyume na kifungu cha 102 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya.....katika mkoa waakiwa shahidi katika shauri katika Mahakama Kuu ya Tanzania Dar es Salaam ambayo mtajwa.....alikuwa mshitaki na mmoja.....alikuwa mshitakiwa, kwa kujua alitoa ushahidi wa uongo kwamba alimuona M.W. katika mtaa unaoitwa.....tarehe.....siku ya.....

19. – KASHFA YA MAANDISHI

Kuchapisha mambo ya kashfa, kinyume na kifungu cha 187 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

[Iliachwa: kifungu cha 187 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu kilichofutwa na Sheria Na. 3 ya 1976.]

20. – MAHESABU YA UDANGANYIFU

Kosa la kwanza. – Mahesabu ya udanganyifu, kinyume na kifungu cha 317 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya.....katika mkoa waakiwa karani au mtumishi wa C.D., akiwa na lengo la kudanganya, alifanya, au alikuwa mmojawapo katika kuingiza hesabu za udanganyifu katika kitabu cha fedha taslimu kinachomilikiwa na C.D., mwajiri wake, kikionyesha kuwa siku hiyo shilingi elfu mbili zililipwa kwa L.M.

Kosa la pili – Sawa na kosa la kwanza.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku yakatika mkoa wa , akiwa karani au mtumishi wa C.D., akiwa na lengo la kudanganya au akiwa mmojawapo katika kuacha kuingiza maelezo ya muhimu katika kitabu cha fedha taslimu kinachomilikiwa na C.D., hii ni kusema, upokeaji katika siku hiyo wa shilingi elfu moja kutoka kwa H.S.

21. – KUIBA KWA UWAKALA

Kosa la kwanza – Kuiba kwa uwakala na wengine, kinyume na kifungu cha 273 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B., tarehe.....siku ya.....katika mkoa wa....., aliiba shilingi elfu mbili ambazo alipewa na H.S. kwa ajili yake, mtajwa A.B., kutunza katika mahali pa usalama.

Kosa la pili. – Kuiba kwa uwakala na wengine, kinyume na kifungu cha 273 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

MAELEZO YA KOSA

A.B.,tarehe.....siku ya.....katika mkoa wa ,aliiba shilingi elfu mbili ambazo alizipokea, kwa ajili na kwa niaba ya L.M.

22. – KUTIWA HATIANI KULIKOPITA

(Kifungu cha 275 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu).

Kabla ya kutenda kosa hilo, huyo A.B. hapo awali alikuwa ametiwa hatiani kwa.....tarehe.....siku ya.....katika mahakama ya.....iliyoketi.....

JEDWALI LA TATU

CHETI KUHUSIANA NA ALAMA ZA PICHA SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI (Kifungu cha 202)

Mimi, wa nikiwa afisa aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 202 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya jinai, hapa nathibitisha kama ifuatavyo:

(1) Tarehe.....siku ya20.....mahali.....nilipokea paketi iliyofungwa kwa mkono wayenye namba.....ikionekana kutumwa naambayo ilijumuisha picha za wazi na mikanda ya picha iliyosafishwa, chini ya bahasha ya barua Na.....ya tarehe.....ikionekana kusainiwa na.....ikiomba kwamba nisafishe mikanda hiyo na au kutayarisha kutokana na hizo picha alama za picha na zilizokuzwa

(2) Barua hiyo na paketi kila kimojawapo kilisainiwa na kuwekwa tarehe na mimi na vimeambatanishwa hapa kama viambatanisho.....na..... kila kimoja.

(3) katika kushughulikia ombi hilo nilisafisha mikanda hiyo na kutayarisha kutoka humo alama za picha na kuzikuza kila mojawapo ambayo nimesaini na kuambatanisha hapa kama viambatanisho.....na.....

(4) Alama za picha na picha zilizokuzwa zilizoambatanishwa hapa kama viambatanisho.....ni, kwa karibu inavyowezekana, uzao halisi kutoka kwenye picha zilizo wazi na mikanda iliyosafishwa iliyoletwa kwangu kama ilivyoelezwa na hazijaguswa kwa njia yoyote, kubadilishwa au kuharibiwa vinginevyo katika hatua za kutayarisha.

Imetolewa chini ya mkono wangu tarehe.....siku ya.....20.....
Imesainiwa.....

JEDWALI LA NNE

TAARIFA YA MTAALAMU WA MWANDIKO SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI (Kifungu cha 205)

Mimi, wa nikiwa ni afisa niliyeteuliwa chini ya kifungu cha 154(c) cha sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai chini ya taarifa ya serikali Na.....ya.....20....., hapa nathibitisha kama ifuatavyo:

(1) Tarehe.....siku ya20.....mahali..... nilipokea paketi iliyofungwa, yenye nambailiyoonekana kutumwa naambayo ilijumuisha.....chini ya bahasha ya barua Na.ya tareheiliyoonekana kusainiwa na Bahasha hiyo, barua nakila moja ilisainiwa na kuwekwa tarehe na vimeambatanishwa hapa kama viambatanisho....., nakila moja.

(2)Tarehe.....sikuya20.....mahali.....nilipokea (1) paketi moja iliyofungwa, yenye namba.....iliyooneka kutumwa naambayo ilijumuisha (2) katika mfuko mmoja(3) chini ya bahasha ya barua yenye namba.....ya tarehe.....iliyoonekana kusainiwa na (4) na paketi hiyo na barua kila moja ilisainiwa na kutumwa na mimi na vimeambatanishwa hapa na viambatanishona

(3) Nimechunguza na kufananisha mwandiko kwenye viambatanisho hivyo.....na mwandiko katika kiambatanisho hicho.....na kiambatanisho katika kiambatanisho hicho..... na nimetayarisha kama kiambatanisho viwakilisho vya picha - jedwali) ya ufananisho na ufanano kati ya mwandiko katika viambatanisho hivyo.....na.....pamoja na maoni yangu .

Na hapa naeleza kwamba, kwa maoni yangu,

.....
Imetolewa chini ya mkono wangu tarehe.....siku ya.....20.....
Imesainiwa.....
